Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA NANE

### Kikao cha Thelathini na Tano – Tarehe 28 Julai, 2012

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

## HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2012/2013 - Wizara ya Nishati na Madini**

*Majadiliano yanaendelea*

**SPIKA***:* Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Kama nilivyowaambia, leo tutajadiliana mpaka saa tano na nusu tutakuwa tumemaliza Orodha ya waliomba kuchangia. Halafu saa tano na nusu hadi saa sita tutatoa dakika 15 kwa Manaibu Waziri, saa sita mpaka saa saba atapewa mtoa hoja Waziri, saa saba mpaka saa nane Kamati ya Matumizi. Kwa hiyo, nitawaita waliochangia mara moja.

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mwongozo wakati hatuna kitu kilichotokea hapo awali tumeomba Dua tu, naomba matumizi ya mwongozo yawe sahihi kwa sababu tumesoma Dua tu basi.

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Aya ya 68 (7) inazungumzia jambo ambalo limetokea wakati uliopita Bungeni ambalo jana wakati Mheshimiwa Kafulila anachangia alitumia neno kwamba nchi hii imebakwa na mafisadi. Mwenyekiti aliyekuwa anaongoza Bunge alimtaka Mheshimiwa David Kafulila neno aliondoe kwamba neno hilo ni matusi na la kufedhehesha Bunge.

Mheshimiwa Spika, mimi nimesoma *literature* neno moja linapotumika kuna *dictionary meaning* na *contextual meaaning.* Ukienda kwenye *dictionary* ya *contextual meaning* neno kubakwa siyo tusi. Nimesoma usiku nimetafakari sana, na nimeona kubakwa maana yake nini katika *dictionary* ya *contextual meaning* neno kubakwa ni kupokwa, ni kuzidiwa na kulemewa.

Kwa matumizi haya Mheshimiwa Kafulila alikuwa sahihi na ukitazama michango ya Wabunge humu ndani wote kwa pamoja jana kwa mara ya kwanza matendo yetu, maneno yote yalikuwa yanaashiria kwamba nchi hii imebakwa na mafisadi.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba mwongozo wake, maana itafika mahali sasa Wabunge wataogopa maneno ambayo yanamanisha yanataka kutupatia uzito wa kauli zao. (*Makofi*)

**SPIKA:** Usinihutubie mwongozo unaniomba nifanye nini?

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Ndio mwongozo wangu, kwa maana neno hili linatumika tunasikia Demokrasia imebakwa na tunalitumia kila siku tunaomba mwongozo wako mimi nataka neno hili lirudi.

**SPIKA:** Basi ukae mdogo wangu imeshatosha.

Waheshimiwa Wabunge sifa ya mtu yeyote mwenye hulka ya kuitwa mtu ni kile kinachotoka mdomoni kwake kisichokuwa na nidhamu ndio kinachomfanya mtu aonekane. Unaweza kuwa mtu umevaa vizuri kabisa, unapendeza lakini kinachotoka mdomoni ndio kinakufananisha na wewe unavyoweza kusema.

Kuna maneno mengine hapa ukisema ni sawa sawa wewe umejivua nguo unaona hiyo. Kwa hiyo, ninachokisema hulka ya kiongozi hata kama neno hilo lina tafsiri nyingi lakini angalia unamwambia nani?

Huyo atakayesoma *dictionary* unayosema ni nani atakayesoma na humu *dictionary* hazipo na mbaya zaidi ni kwamba Mwenyekiti anapotoa maamuzi kuna tabia watu wanasimama na kuanza kubisha, jamani kanuni zetu ni kali mno.

Tunapenda sana kuelimishana lakini ni kali mno. Ubishani na Mwenyekiti siyo tabia ya Bunge lolote duniani kote. Kwa hiyo, mimi nasema neno lile hata kama umesoma *dictionary*, hatuna *dictionary* hiyo lakini linamweleza mtu mwenyewe. Tunaendelea. (*Makofi*)

**MHE. SUBIRA KHAMIS MGALU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi asubuhi ya leo kuweza kuchangia hoja hii ya Wizara ya Nishati na Madini. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuweza kusimama ndani ya Bunge lako Tukufu na mimi kuweza kutoa mchango wangu.

Napenda niwatakie kheri ya mwezi wa Ramadhani Waislam wote nchini. Pia napenda kuwashukuru sana wananchi wa Mkoa wa Pwani hasa wanawake kwa kuweza kuendelea kuniunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kuipongeza Wizara hii pamoja na viongozi wake kuanzia Waziri, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa maandalizi mazuri ya Hotuba ambayo imewasilishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia niipongeze Wizara kwa utekelezaji wa shughuli mbalimbali za mwaka 2011/2012 hasa ambazo zimefanyika katika Mkoa wetu wa Pwani. Kwa mfano kukamilika kwa msongo wa umeme wa kV 33 kwa Kata ya Mbwewe.

Lakini sambamba na hilo kwa mara ya kwanza Makao Makuu ya Wilaya ya Rufiji yamepata umeme. Lakini pamoja na hayo pia niipongeze Wizara na niiombe iendelee kutekeleza miradi ambayo inaendelea ya kusambaza umeme katika Kata ya Magindu Wilaya ya Kibaha katika Kata ya Kimanzichana Wilaya ya Mkuranga mradi huu uendelee.

Pia katika Kata ya Kiwangwa wananchi wa Kiwangwa walimpa kura nyingi za Udiwani wa CCM kutokana na imani ya kwamba mradi ule wa kusambaza umeme na nguzo zimefika. Kama tunavyofahamu eneo lile linaongoza kwa uzalishaji wa matunda, tunategemea wadau mbalimbali baada ya

kufika nishati ya umeme wanaweza wakajenga viwanda na hatimaye wananchi nao wa Mkoa wa Pwani hususan katika maeneo niliyoyataja waweze kufanya shughuli za kujiletea uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia niipongeze *REA* kwa kuweza kutangaza *tender* ya kusambaza umeme unaokwenda katika Kijiji cha Nyamisati Kata ya Salale ambako kuna shughuli mbalimbali za uchumi kule. Kuna shule inayosomesha watoto yatima, kwa hiyo, ninadhani kufika kwa nishati hiyo itatusaidia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tumeshuhudia na jana Bunge lilijielekeza zaidi katika kutetea maslahi ya Watanzania. Jana Bunge lako Tukufu lilikwenda sambamba na dhamira yako ambayo wakati tunakuchagua ulisema una nia ya kujenga Bunge moja jana dhamira hiyo imeanza kuonekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jana yamejitokeza makundi mbalimbali yanayoona sheria ya manunuzi ya Umma katika mkataba wa kusambaza mafuta kwa ajili ya *IPTL* wako wanaona kwamba Wizara imekiuka kanuni, wako wanaona kwamba mtazamo ule ulikuwa sawa sawa.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba niunge mkono na nina uhakika hakuna kanuni ya manunuzi iliyovunjwa. Nasema hivyo kwa sababu gani, kwamba katika Serikali yako manunuzi ambayo unatakiwa kwa mfano sekta ya madawa lazima dawa ununue *MSD,*

Pia utengenezaji wa magari lazima utengeneze kwenye karakana ya Serikali (TEMESA).

Lakini pia hii *PUMA (BP)* ni kampuni ya Serikali ina asilimia 50. Hivi ni ubaya gani Serikali kuiwezesha taasisi yake inayomiliki asilimia 50 na ambayo taasisi hiyo Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa *PUMA* ni Mtanzania Ndugu Kelvin Felix ni dhambi gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kinachosikitisha hata wale waliokuwa wanasema kanuni imevunjwa viongozi wawajibike hawataji kanuni gani ndani ya sheria ya manunuzi iliyovunjwa. Taifa limepata hasara ya kiasi gani. Lakini kwa wale ambao tunaona kanuni haijavunjwa tunaambiwa taifa limeokoa kiasi cha bilioni tatu (3) kwa muda wa wiki mbili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, inasikitisha imefika wakati Bunge letu linatumika ndivyo sivyo. Tabia hii imeanza kuota mizizi tumeona Bunge la mwezi wa nne wakati tunajadili namna gani viongozi wawajibike, tulifanya maamuzi. *(Makofi)*

Lakini leo anaposimamishwa mtendaji kamati zinatumia mamlaka yake vibaya wanataka wakutane wajadili, alivyoteuliwa huyo mtendaji mbona hawakukutana.

Kwa nini tunaingilia muhimili wa Serikali leo, alipopewa nafasi alivyoteuliwa hatukukutana kujadili kwa nini ameteuliwa kuwa Mkurugenzi wa shirika hilo. Lakini Serikali inapoamua hebu simama pisha

uchunguzi tujiridhishe Kamati zinaitana ili wajadili kuna nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumechoka na ujasiri huu wa kifisadi. Tunaomba Mheshimiwa Spika, utumie mamlaka yako, tunaomba ifike wakati tuzi-*review* hizi kanuni kama unaunda Kamati na endapo inatokea Kamati hizo hazitimizi wajibu wake, zivunjwe. Leo Kamati zingine hazina heshima, zipo Kamati zinatuhumiwa Watanzania hawaelewi zinatuhumiwa lakini watu wanaendelea na kazi.

Hivi imani ya Watanzania itatoka wapi? Watu wanateuliwa kwenye Kamati wanaonekana kabisa ushahidi upo, wanakwenda kuomba rushwa eti Bajeti tupitishe Katibu Mkuu amewataja ushahidi anao kwa nini wasichukuliwe hatua? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, usitulee Wabunge, chukua hatua hata kama ni sisi tunahusika, tuchukulie hatua haiwezekani kanuni hii iseme eti kamati iliundwa ikae miaka miwili na nusu hata kama kamati hiyo ikivurunda ikae tu, tuzi-*review* hizo kanuni za Wabunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nchi hii ina changamoto nyingi, Serikali kila siku inatuhumiwa inanyanyasika kumbe kwa maslahi binafsi, leo tumewagundua. Waheshimiwa Wabunge wenzangu nawaomba watu ambao wametajwa na hata kwenye vyombo vya habari vimetajwa, sasa tuwasusie michango yao kwenye *part caucus* zetu kwenye Bunge, tujue michango yao itakuwa ya maslahi binafsi.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani kumbe watu tunawaona wanapata sifa wanachangia wanaonyesha uchungu kumbe wanachangia wanakumbuka maslahi yao. Hivi ni binadamu gani umechaguliwa na wananchi kuja kuisimamia Serikali, Serikali gani unayosimamia hiyo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Watanzania wamesikitika, lakini baya zaidi vinanunuliwa mpaka vyombo vya habari havizingatii weledi vinaandika taarifa tu Mkataba wa PUMA lakini hawatupi upande mwingine wa shilingi, nini kimeokolewa zingetumika kwa ajili ya kununulia madawa, madawati, kujenga zahanati na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nasema naunga mkono hoja lakini ninawaomba Waheshimiwa Wabunge, tusitumike tuache kuwa na ma-*agent* wa mafisadi. Nawaomba watendaji wa Wizara hii waendelee kuziba mianya hiyo hata kama kwa kuvunja Kanuni ili mradi taifa hili linafaidika. Sisi Wabunge tutawaunga mkono na wale ambao tumewagundua kwanza tutawasusia mkichangia tutawazomea, kwenye *part caucas* tutawazomea. Hamna chenu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MHE. MOZA ABEDI SAIDY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara ya Nishati na Madini.

Kwanza kabisa napenda kuungana na Waislam wenzangu wote katika mfungo huu wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla ulivyovaa siyo. Naomba ujiangalie, huruhusiwi kuwa na baraghashia na koti na kanzu hiyo inaruhusiwa. Lakini vingine ulivyovaa hapana. Endelea Mheshimiwa Moza. (*Makofi*)

**MHE. MOZA ABEDI SAIDY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pia napenda kutoa pole kwa wale wote ambao waliokutwa na maafa kwa namna moja ama nyingine Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi na marehemu wote waliotutangulia mbele ya haki.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa mchango wangu mimi katika suala moja la ardhi kwani ni suala mtambuka na juu ya ardhi kuna watu chini ya ardhi kuna vingi vilivyomo hata mali ambazo ni madini.

Mheshimiwa Spika, nije moja kwa moja kwenye suala la madini. Kuna kitu kimoja ambacho kinatushangaza kidogo. Katika harakati nzima za kuweza kufambua madini haya wanavumbua vijana wetu ambao ni wazawa katika eneo husika ambao wanayagundua madini, wakishavumbua madini hayo basi wanakuja wawekezaji wengine, Serikali inawaondoa wao inawaweka wawekezaji, wenyewe wazawa halisi wanakuwa hawana kipato chochote wanakuwa kama vile watumishi katika eneo lao. Mifano tunayo mingi katika nchi hii.

Mfano huko Arusha katika uchimbaji wa madini ya *Tanzanite,* tumegundua kwamba sasa hivi mkataba ule uko na Makaburu. Hata madini haya yanauzwa kwa nembo ya Makaburu. Tuangalie katika nchi yetu ya Tanzania uchumi huu ni wa kwetu wenyewe wananchi wa Tanzania, ardhi ni ya kwetu Tanzania, vijana wa kwetu Tanzania, lakini wananyanyaswa vibaya mno vijana wetu ambao ndio wazawa wanaogundua madini haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningependa kuuliza Serikali ina mpango gani ya kuwaweka katika hali nzuri ya kimaisha inayoweza kustawisha katika kupata uchumi mzuri katika nchi yao na madini yao? Tunao wasomi wakubwa katika nchi hii kwa mfano Profesa Ibrahim Lipumba ambaye anaweza akasimamia uchumi huu wa nchi kama iwapo kuna sehemu ipo kunalegalega. Tusiwe wachoyo wa fadhila tuwe pia watu ambao tuna uwezo wa kuwatumia watu ambao wana elimu na ambao wanaweza wakaiongoza pia nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia suala la mapato ya madini, kwa kweli katika mapato ya madini hivi karibuni tumeona madini ya dhahabu na madini mengineyo yamepanda bei kitaifa. Lakini siamini kama kweli sisi tunaweza tukawa tunanufaika katika hali hiyo. Yapo mashaka makubwa tokea huko mwanzo. Pia tuna wasiwasi na Hati Miliki. Hati Miliki hizi kwa nini Serikali haitoi kwa hawa wawekezaji wadogo wadogo? Inatoa kwa wawekezaji wakubwa, kwa nini inakuwa wawekezaji ambao wanatoka nje, ambao siyo Watanzania wanapewa nafasi kama hizi wanakuja

kuendelea kututawala na wanasomba mpaka udongo wetu.

Hivi tufikirie wananchi tuliopo hapa Tanzania tutabaki maskini mpaka sehemu ya kukaa katika maeneo yetu tutakuja kubaki na mashimo tu. Hebu Serikali sasa ifikie hatua ya kufikiria kwamba kama kuna uwezekano watalaam tunao hapa hapa nchini Tanzania hii kazi ifanyike hapa hapa katika nchi yetu ya Tanzania na tusingoje kwamba tusubiri watu kutoka nje ili wao wawe na uwezo mkubwa wa kuweza kutufanyia shughuli hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nihame moja kwa moja na suala ambalo ni la umeme, nije kwenye suala la *TANESCO.* Kwa kweli ni hali ambayo inasikitisha huko nyuma tulipotokea. Lakini sasa hivi naona kwamba shaka inakuwa inaondoka. Maadam tunao Mawaziri wetu ambao walioteuliwa juzi tu na Mheshimiwa Rais kwamba wasimamie suala hili la Nishati na Madini. Tunajua kwamba Tanzania tutanufaika kwa ajili yao wao. Wametutoa shaka, wasi wasi na mimi sina wasi wasi nawaunga mkono *percent* mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tumegundua kwamba Serikali imeweza kugundua kwamba kuna njama nyingi ambazo zimejitokeza za hujuma nyingi za mafuta, haya mafuta ya umeme yanakuwa yanahujumiwa na watu wengi hata na wafanyakazi wenyewe na inasadikiwa mafuta haya yanapikiwa hata chipsi, samaki yanakaangiwa. Sasa sijui kama

Serikali ina taarifa hii na kwamba inawezekana yakawa na athari gani katika maisha ya wanaadamu.

Tunalo suala la ajira kwa vijana, *TANESCO* imekuwa na ubaguzi mkubwa kwa huyu Mkurugenzi Mtendaji huyu Ndugu William Muhando. Kwa kweli ukiangalia familia nzima ya *TANESCO* imekuwa imejikita katika sehemu kubwa imekuwa ni ya kifamilia. Hakuna watoto wa kimasikini ambao wanaweza pale hata kama wamesoma waende pale wakafanye kazi na hata wakifanya kazi ndani ya siku mbili, tatu utakuta kwamba wanabambikizwa kesi, hii imetokea maeneo mengi, haya yalianzia kwenye maeneo ya Mpwapwa, Kiteto na maeneo mengine hali kadhalika vitu kama vilishawahi kujitokeza, hii yote ni mtu Meneja anamtaka kuwa Ndugu yake asimamie yeye kuwa Mhasibu au yeye ndiyo kila shughuli ambazo za umeme anazotaka yeye wawe wao tu kifamilia, kiukoo. Kwa kweli tumegundua mambo mengi ambayo kweli yanaweza kujitokeza katika suala la umeme.

Bili za umeme zimekuwa kubwa mno. Utakuta mtu anabambikizwa kesi ya bili aende akalipie ya mtu ambaye anaesaga mashine au ya mtu ambaye anapasua mbao wakati ni mkazi tu anaekaa katika nyumba.

Je, kwa mtindo huu si tunahamisha sisi wenyewe wateja? Kwa hiyo, suala hili kwa kweli lifikiriwe kwa undani zaidi. Mita za umeme zimekuwa zinalipiwa kwa gharama kubwa mno na nashukuru sasa hivi Serikali imetangaza kwamba bei hiyo sasa hivi itakuwa imeshapungua na ipungue kwa asilimia kutoka kwenye

hiyo asilimia iliyopo mpaka ikifike hata asilimia tatu (3) angalau tuwe tunapata hata wateja wawe wengi.

Kwa kuwa suala la umeme ni suala ambalo kwamba linatakiwa liwe mbadala kwa sababu wananchi wengi huko Vijijini wanatumia kuni, gesi, huenda ikawa basi na hata umeme pia wawe wanatumia. Bei ya umeme ipunguzwe, iwe chini ya hapo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuyaongea haya, kwa kweli kuna suala ambalo linasikitisha mno kuona kwamba mwananchi wa kawaida kuambiwa kwamba alipie nguzo ya umeme kwa bei ya shilingi laki tano au mita ya umeme. Hivi ile bili tu ya shilingi elfu mbili au elfu moja inamshinda, hivi kweli huko tunakokwenda kweli tutafika katika nchi yetu ya Tanzania?

Mimi nalaani kitendo kikubwa kinachotokea cha mafisadi wa *TANESCO* ambao wamejilimbikizia mali na wakawa wanawafanya wananchi kama watumishi wao, naomba mali zao zote wale wote ambao wamegundulikana na suala hilo, wataifishiwe mali zao ili suala lirudi katika nchi yetu ya Tanzania kwamba liwe na msimamo na haki iwe sawa kwa wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru. (*Makofi*)

**MHE. JOHN SHIBUDA MAGALLE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata fursa hii ili na mimi niweze kuchangia katika hoja ya Wizara ya Nishati na Madini. Jambo la kwanza ni kwamba nina masikitiko makubwa sana, tusipoangalia umoja wa fikra kati ya

Bunge na Serikali usipoimarishwa, Taifa hili litakuwa limeathirika sana kupata faida kuwepo Mihimili hii kwa ustawi na maendeleo ya jamii, kwa ustawi na maendeleo ya uchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo una deni kubwa sana la kuhakikisha ya kwamba Bunge letu hili pamoja na sisi Wabunge tunakuwa ni watu waadilifu kwa maslahi ya nchi hii. Kama pana shutuma, pana kusutwa Wabunge, ni vyema hawa wanaosutwa wakatolewa majina yao, wakafahamika kuliko kukaa tunanung'unika, tunalalamika. Kama tutaendeleza mchezo wa kusutana na kutuhumiana kwa hisia, nadharia, vionjo, porojo ni hatari kubwa sana kama tunaweza tukaoneana pale ambapo hakuna ukweli na pale palipo na ukweli basi ukweli utekelezeke, mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni.

Mheshimiwa Spika, sekta ya nishati na madini ni sekta muhimu sana katika kuhakikisha kwamba panakuwa na ustawi na maendeleo ya uchumi. Sekta ya uchumi inategemea sana kuhakikisha kwamba pana nishati ya kutosha. Kipindi hiki CCM naishauri ielekeze Serikali yake kuhakikisha kwamba nishati inaimarishwa na kama Serikali ilivyotangaza kupitia Wizara hii, vitendo vionekane vya kutuhakikishia ya kwamba kuna mabadiliko yanayotarajiwa. Serikali ihakikishe ya kwamba inatunga taratibu za kuhakikisha inaondoa mfumo batili wa kuagiza mafuta katika maeneo ambako ndiko kwenye mazalio ya shutuma na rushwa.

Mheshimiwa Spika, tuhakikishe ya kwamba umuhimu wa nishati una faida kubwa sana kwa uchumi wetu pamoja na kuhakikisha ya kwamba palipo na uchumi endelevu, hapo hapo pia hata mapato ya Taifa yanakuwepo, wajasiliamali wanapata rasilimali na wanapata nguvu ya kuendelea. CCM na Serikali yake itambue ukweli wa kwamba utangulizi wa kuhakikisha kwamba nishati inayopatikana na iliyokuwa ikipatikana, ulikuwa ni udhaifu mkubwa kwa sababu ya shutuma za rushwa, basi mfanye upembuzi, msiwe kifuniko, mhakikishe ya kwamba mnapambanua na Watanzania mnawaambia dhuluma ya hujuma iliyotendeka kutokana na fikra hasi za watumishi hasi wasio na uzalendo na uaminifu kwa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, ahadi ya Serikali ya kwamba mgao hautokuwepo, naomba Serikali hii ijiimarishe. Je, Mheshimiwa Waziri umekaa na Waziri wa Fedha akakuakikishia kwamba atakusaidia kukupa mashirikiano? Je, mtandao uliokuwa ni batili kwa usatwi na maendeleo ya nchi haupo katika Wizara ya Fedha hivyo ukapata kikwazo, tafakari, chunguza, make pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu atoe mashirikiano yakinifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri aielekeze *TANESCO* ihakikishe inakagua nguzo zilizooza katika kipindi hiki cha kiangazi na ihimarishe mfumo wa kusafirisha umeme wa njia kutoka Shinyanga hadi Maswa, Meatu, Bariadi.

Maswa kila siku tuna mgao kipindi cha masika, ninaomba, nakuomba Mheshimiwa Waziri, kama kauli hiyo wananchi wa Maswa waienzi, ni wewe uhakikishe ya kwamba sasa unasimamia *TANESCO* la sivyo huo ni mradi wao wa *over time*.

Mheshimiwa Spika, asiejua maana, hajui maana. Waziri na Katibu Mkuu mmerithi majambo ambayo hayakuwa yenu. Kama mmerithi watu wabovu, hakikisheni mnatumia JIK sugueni muaondoe wale wote ambao ni watu hatarishi kwa ustawi na maendeleo, msioneane aibu. La sivyo mtakuja kujikuta kwamba hao watu ambao mtawaacha, watakapobainika ya kwamba wamepona, watajiimarisha na watakuwa ni vichugu na watakuwa ni dhoroba ya kuwamaliza nyinyi kwa sababu alieumia lazima anakuwa na makovu ya hasira na anakuwa na tabia ya kusigana.

Mheshimiwa Spika, katika jamii yetu, lazima mjue kwamba kuna makuwadi wa mabwenyenye ambao hutafuta madalali wa kutia kitanzini waadilifu na waaminifu wa watumishi. Waziri lazima atambue ya kwamba kuna watu wa mbegu za ubadhilifu, watu mbegu ubadhilifu, huwa hawakomi ndiyo maana wahenga wakasema kunguru hafugiki, sasa tambueni na muyaondoe yote ambayo ni makunguru kwa sababu kunguru hata ukimpa ubwabwa, hawezi akakaa akafugika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, viharifu na vihusisho vina shutuma kwamba baadhi ya Wabunge ni najisi kwa masilahi ya nchi yetu. Hao Wabunge ambao ni najisi,

naomba ili Watanzania wajue basi watambulishwe kwamba hawa ni najisi na kwa utukufu wa Bunge la Tanzania, lakini tusiichi kwa hisia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, natambua ya kwamba kuna watu ambao wanapendwa kuitwa watwana, vibarua na maboi ya unyonyaji.

Kwa hiyo, napenda kusema ya kwamba lazima tuhakikishe ya kwamba tunapambana na watu ambao ni makandarasi wa fitna na ni wataalam elekezi wa Itifaki za kubadilisha utu wa binaadamu. Hakikisheni hawa wanaondoka.

Je, Serikali itawaambia nini Watanzania wajenge suluhu na Serikali ya CCM kuhusu kwamba kuna watu ambao wamedhulumu mabilioni ya fedha.

Je, kama hii basi ndiyo ninyi mmekuwa maabara ya kutambulisha dhuluma hizo, basi nawaomba mhakikishe kwamba ninyi mnakuwa ndiyo Bima ya kuthaminika Serikali na ninyi ndiyo mnakuwa Bima ya kusadikika kwa Serikali. Mheshimiwa Waziri utukufu wako na Katibu Mkuu pamoja na timu yako, hivi sasa nyie mnaonekana ni watu ambao mmekuja na utukufu. Kwa hiyo, kabla watu hawajawatengua udhu wa maadili yenu hakikisheni ya kwamba mnawamaliza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tembo hubeba viroboto, lakini viroboto haviwezi kubeba tembo.

Je, wale tembo wanaobeba viroboto mna hakika ya kwamba mmewapiga risasi wakafa? Maana yangu mazalia ya hao vimelea ambao ni watu dhulumati, kwa masilahi ya nchi. Je mmehakikisha ya kwamba mmewajua wote na kama mmewajua wote. Je, mnataka kuatamia funiko la vundo ambalo kwa Watanzania wamekuwa wakiumia nalo? Je, hasara ngapi Tanzania imepata?

Naomba shutuma hizo mzifanyie kazi kwani Viongozi ambao wanakataliwa hata na Imani ya madhehebu yao mkiwastiri sijui hao mnataka kufanya nini. Ikiwa Viongozi wa madhehebu ambayo ni batili huumbuliwa na madhehebu yao. Naomba na Serikali iwaumbue, iwatangaze hao watu ambao ni najisi kwa Serikali. Imani bila matendo mema, imani hufa. Kwa hiyo, naomba Bunge hili vile vile lifanye hivyo hivyo. Natambua ya kwamba Bunge hili hivi sasa linataka kuwa kama *butcher* ya kuchinjia ubadhilifu wa watu. *(Makofi)*

Kuna mtu mmoja ambaye amechinjwa humu ndani kupitia Wabunge ambao walistiri watu wanaodaiwa na Bodi ya Pamba, naiomba Serikali itangaze makosa ya Mheshimiwa Mtunga, *DG* wa Bodi ya Pamba, Bunge lako hili na watu ambao wamejigeuza kuwa watwana wa mabwenyenye, makuwaidi wa naizesheni tuhakikishe ya kwamba wanachukuliwa hatua na wanaposema humu, wawe wanatambulisha ushahidi sio kuzusha maneno ya jumla jumla na kubambikiza watu naomba na Bunge lisiwe na dhana hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba Wabunge tutumie vyema na dhamana tulizonazo kwa sababu tusipoangalia utakaso na utukufu wa Bunge utakua umeingia shari na wananchi wataanza kushangaa. Je, tukimbile wapi? Naomba wafanyabiashara wahalifu wa madeni ya kudhulumu sekta ya pamba washughulikiwe.

Mheshimiwa Spika, hakuna dini inayosema dhulumati iitikiwe amen. Kwa hiyo, naomba na kushauri kwamba hivi sasa Serikali ijielekeze na mhakikishe ya kwamba mnashindanisha uhadilifu kwani ujinga na ujinga tukiushindanisha, uzaliwa chizi. Kwa hiyo, naomba hilo tuliondoe na siasa isiwe gulio la kuuza vionjo vya maneno ambayo ni batili kwa mstakabali tu kujitafutia umaarufu binafsi.

Mheshimiwa Spika, ni kitu gani kinaunda sumaku ya kuvutia Wabunge wako waanze kuwa na vitendo ambavyo si sahihi. Fanya utafiti, uchunguzi, ujue kuna matatizo gani yanayokabili sekta yako ya Wabunge, hatimaye wanaingia katika masuala ya rushwa na kutuhumiwa. Wewe la sivyo utaonekana Bunge lako limeacha *legacy* mbovu. Malighafi ya uwoto wa umanamba ni vitendo ambavyo vinasababisha mtu uwe mtwana. Kwa hiyo, naomba uhakikishe ya kwamba wananchi ambao walikuwa wanaamini kwamba Uongozi wako utajenga *legacy* au urithi mzuri kwa masilahi ya vijana, basi tuhakikishe ya kwamba tunashinda vizuri.

Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Katibu Mkuu upatanyifu wa matendo yenu unahitajika na utaheshimika sana pale mtakapoendeleza vita hiyo hata kwenye mikataba ya madini. Watu wanaoishi katika maeneo ya madini Kahama , Geita na kadhalika, ni watu dhalili, lakini Katiba inasema rasilimali ya Tanzania itumike kwa masilahi ya nchi na Watanzania wote. Katiba ya nchi inazungumzia hivyo hivyo pamoja na Katiba ya CCM, mbona ninyi wana-CCM ambao ni asilia yangu hamtaki kuhakikisha Serikali yenu inatii Katiba pamoja na Katiba ya CCM?

Ndugu zangu nawashauri, vyombo vya dola vitoe mashirikiano ya kuhakikisha ya kwamba Katiba ya nchi inaheshimika, CCM ongezeni kasi ya uadilifu ili mhakikishe kwamba Serikali yenu sasa inayoitwa imeokoka baada ya kuwa katika tingatinga na matetemo ya kushtumiwa kisiasa.

Mheshimiwa Spika, hakuna mabaya yanayoweza kumfikia mtenda mema. Kwa hiyo, nahakikisha kwamba Mheshimiwa Waziri pamoja na Katibu Mkuu na timu yako, Mwenyezi Mungu yuko pamoja nanyi mtastirika na naomba Imani ya dini zenu muiendeleze na nawaomba kila mtu ambaye ana Imani ya dini hususani mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani, tuhakikishe matendo yetu basi yanakuwa na uzalendo, uaminifu na utiifu kwa masilahi ya Taifa. Aidha, udhibiti wa dhuluma uliopo ndani ya jamii yetu hivi sasa unanyima hakika kuthaminika wongozi wa Serikali.

Vile vile naomba kusema ya kwamba ikiwa wananchi wanapata ruzuku katika umeme, basi na bei ya pamba vile vile ambayo pia ni nishati na madini, tuhakikishe kwamba bei ya pamba Serikali inapewa.

Mheshimiwa Rais Kikwete, sikiliza kilio cha wakulima wa pamba kwa sababu pia ni madini na ni nishati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na kunipa fursa ya kuzungumza Bungeni leo hii katika mazingira ambayo Mwenyezi Mungu amejidhihirisha na kweli naomba sasa tukumbuke na tukubali kwamba Mwenyezi Mungu na aitwe Mungu. (*Makofi*)

Niliwahi kusema hapa Bunge kwamba tumwogope Mungu, nakushukuru Mungu umeanza kujidhihirisha. Hii tabia iliyokwisha kuanza kujengeka ingeiyumbisha sana Serikali. Hawa waliokaa hapa mbele wanafanya maamuzi, hakuna Waziri asie amua na kwa vyovyote vile unapoamua, wako watakaokubali, wako ambao hawatakubali.

Kwa kawaida tunategemea mtu ambaye amekuwa *aggrieved* na maamuzi yaliyofanyika na watendaji wa Serikali, kuna mkondo ambao umewekwa na wakati mwingine imetajwa kabisa

kwamba mtu ambaye hajaridhika aende Mahakamani, amekosa tenda, amekosa hili.

Mtindo ambao ulikwishakuanza kujengeka kwamba mtu anakosa jambo fulani, anakwenda kwa Wabunge baadhi yao, anawarubuni, anawa- *mobilize*, wanakwenda Bungeni kusema vitu sasa tumeanza kuona kwamba si wote wanaopaza sauti kwamba kuna jambo fulani limefanyika kwamba wanakuwa wana dhamira ya kweli.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukienda hivyo, Mheshimiwa Kaimu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Rais wananisikia hakuna Serikali au hakuna Waziri ambaye atakuwa salama kama pale ambapo wanaamua, halafu watu wanakuja ku- *mobilize* Wabunge, wana-*pile up pressure* na mambo yanakwenda ambavyo yanaweza yakaenda. (*Makofi*)

Nampongeza sana sana Ndugu yangu Maswi, Mheshimiwa Waziri Prof. Muhongo kwa kufanya maamuzi mazuri ya kijasiri ya kuhakikisha kwamba wanaokoa rasilimali za nchi hii.

Mheshimiwa Spika, nakuomba Ndugu yangu Maswi jipe moyo na tumia kitabu cha Wafalme, kitabu cha kwanza, mlango wa nane (8) mstari wa 44-45; watashindwa na watakuwa wanaumbuka mmoja baada ya mwingine. Leo hawatajwi na naomba msiwataje, Mwenyezi Mungu ana namna yake ya kuwataja, *time will tell.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie manufaa ya wananchi wanaoishi kwenye maeneo ya migodi, tumekuwa tukilalamikia sana suala hili, ninawaomba sana wawekezaji ambao tunao kwenye maeneo yetu kwamba sasa muda umefika wa kukaa chini na niwaombe sana *serioulsly* kampuni ya *Africa Barrick Gold,* tumekuwa na changamoto nyingi, wao ndiyo wawekezaji wakubwa kwenye sekata hii, lakini kwa bahati mbaya sana wao ndiyo wamekuwa wamwisho kwenye kila jambo ambalo linalenga kunufaisha wananchi.

Mwaka 2008 Mheshimiwa Rais aliteuwa Kamati ya Bomani na mimi nilikuwa Mjumbe, yalikuja mapendekezo mengi mazuri, moja wapo ni lile linalosema kwamba mrabaha uongezwe kutoka asilimia 3 hadi asilimia 4, kampuni zingine zimekubali lakini kampuni iliyokuwa inasuasua kukubali ni hii kampuni ya *Barrick.*

Sehemu zote tulizozunguka duniani kampuni hizi za migodi zimefanya uwekezaji mkubwa, tulikwenda Kalgurie, Australia, kule Barrick wamejenga barabara ya lami kutoka Perth kilomita 720, leo tunawaambia katika mazingira haya ambayo wako Kahama kwa zaidi ya miaka 30 ijayo, washirikiane na Serikali kujenga barabara ya lami kutoka Kahama Mjini hadi Kakola wanasema hilo ni jukumu la Serikali. Mbona Australia wamefanya? Umefika wakati sasa wa mikataba hii tuitizame. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala la *Service Levy*, Sheria ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 inaziruhusu Halmashauri kutengeneza *by- laws* itakayoziwezesha kutoza ushuru wa 0.3 asilimia ya *gross turn over*. Mikataba ya Migodi, Mgodi wa Bulyanhulu, Buzwagi ambayo ilifungwa baada ya Sheria hiyo kuwepo.

Mheshimiwa Spika, sheria inazuia Halmashauri kutoza ushuru huo, badala yake inasema zitalipwa dola 200,000. Sheria hiyo au Mkataba huo au Mikataba hiyo, imevunja Sheria ya Serikali Tawala, Kamati ya Bomani ililiona na tukaishauri Serikali, irekebishe. Tunashukuru Serikali, ililiona na ikaliingiza kwenye Sheria ya Madini ya Mwaka 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana *Resolute,* wamekubali kuanza kurekebisha suala hilo. Sisi tunawadai *Africa Barrick Gold,* dola za Kimarekani milioni 11.7 ambazo zinatokana na *Service Levy,* toka Mgodi wa Bulyanhulu ulipoanza uzalishaji mwaka 2001 na toka Mgodi wa Buzwagi ulipoanza uzalishaji mwaka 2009. Wamekuwa wakilipa dola 200,000 ambazo ni *far lesser than what we real deserve.* Niwaombe *Barrick,* waoneshe sasa kweli *spirit* kwamba, wao ndio *industry leader* kwenye nchi hii na wanapoendelea kuwa wakaidi kama ambavyo wamekuwa, niiombe Serikali, Profesa Mhongo na Timu yako kwamba, endeleeni kuwa wakali dhidi ya watu hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananyemelea kuanza Mgodi mpya pale Mwakitolyo na wameshaanza kunyemelea kuanza Mgodi mpya pale Nyanzaga. Endapo hawatakubali kufanya marekebosho ya mapungufu yaliyokuwepo toka zamani, kulipa *Service Levy,* kusaidia wananchi wanaoishi jirani na migodi, musiendelee kuwapa leseni za kufanya kazi watu hawa, wapeni wengine.

Tunategemea kwa sababu wao ndio wako kwenye *industry* ndio waliwekeza kuliko wengine, wawe mfano. Tunawaambia rekebisheni mikataba, lipeni *service levy,* hawataki. Tunawaambia rekebisheni mikataba, lipeni ushuru au *royalty* kutoka 3 kwenda 4 wanakuwa wazito. Katika mazingira hayo wananchi wetu wataendelea kuteseka. Mimi ninaiomba Serikali, iendelee kusimama imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mahusiano ya migodi na wananchi, limekuwepo tatizo kubwa sana la maeneo ya wachimbaji wadogowadogo, nilisema wakati fulani mwaka 2007, enzi zile Waziri ni Karamagi kwamba, haiwezekani nchi nzima Kampuni moja, *directly* au *indirectly,* ikawa na leseni za utafiti nchi nzima. Wilaya ya Kahama, ambayo ina madini karibu kila sehemu, haina eneo hata moja la wachimbaji wadogowadogo. Maeneo yote yameachiwa wawekezaji wakubwa, wakifanya utafiti na hakuna wanachokifanya. Nakupongeza sana Mdogo wangu Mheshimiwa Masele, juzi nilipokuwa nyumbani Segese, walikuwa wananiuliza kwamba. *“Kaliza nanalia kamasele?”* yaani wakimaanisha Masele anakuja lini kwetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wamesikia kazi nzuri aliyoifanya Ng'anzo, wamesikia kazi nzuri aliyoifanya Geita. Naomba mdogo wangu Mheshimiwa Naibu Waziri, simama hivyo hivyo, njoo na Kahama. Tunaomba eneo letu la Mwazimba, tunaomba eneo letu la Masabi, tunaomba eneo letu la Nyangalata, tunaomba eneo letu la Nyamakwenge, ambayo yote yametolewa leseni kwa wachimbaji wakubwa na wachimbaji wadogo kila wakisogea, wanatimuliwa. Ila nikuombe tu, uwe na tahadhari, maamuzi haya ya kuwanyang'anya wakubwa au kuwanyima wakubwa ukawapa wadogo, yana hatari zake. Ushahidi upo na wewe ni mtu mzima, nafikiri umenielewa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la umeme vijijini. Nawashukuru sana *REA,* wamefanya kazi nzuri, mwaka jana wamepeleka umeme kwenye vijiji vya Ntunguru,Mwakata, pamoja na Mpera. Sasa hivi nashukuru kwamba, wamekubali kupeleka umeme kwenye vijiji vingine. Nikuombe Mheshimiwa Waziri na bahati nzuri umesema uko *transparent,* haujataja vijiji ambavyo vitapatiwa umeme kwa Mwaka huu wa Fedha tunaouanza. Tunajua vijiji vipo, lakini hujavitaja. Kweli, umetoa ramani, lakini pamoja na macho yangu kuwa mazuri, ile ramani ilikuwa haioneshi vijiji vyangu. Tunaomba utupe orodha, usipofanya hivyo, unatoa nafasi ya kuchakachua, atakuja mtu mwenye nguvu pale *REA* ataondoa kijiji hiki ataweka kijiji kingine. Lakini ukishalitoa likajulikana kwamba, Wilaya ya Kahama, Jimbo la Msalala, Vijiji vinavyopata umeme ni hivi, haitakuwa rahisi kuchakachua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini naomba pia, Wizara ya Nishati na Madini, Mradi wa Umeme wa kwenda Bukombe, ambao ni wa siku nyingi sana, ambao unapita kwenye Vijiji vyangu, Vijiji vya Longuya, Vijiji vya Ikinda, Vijiji vya Shilela, Vijiji vya Segese, mradi huo uanze. Umechelewa sana na ninaamini kwamba, wananchi kwa kweli, wamefika mahali wanaelekea kukata tama. Niombe Serikali, kama mlivyokwisha kuanza, muoneshe ujasiri huo huo.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, nizungumze suala lile lile la mahusiano kati ya Mgodi na wananchi. Kumekuwepo na malalamiko ya wananchi walioondolewa eneo la Kakola, eneo la Bulyanhulu, mwaka 1996. Wananchi hao wamekuwa na madai, wananchi 4,176 wanadai nyumba 2,330, mashamba zaidi ya hekta 34, visima 72, mialo 31 na mali zingine. Walikwenda Mahakamani, Mahakamani kule kutokana na kutokuwa na uwezo kesi imeendelea milele, hadi leo haijakwisha. Mwaka 2009 wakaomba kwamba, tuzungumze tulimalize suala hili nje ya Mahakama; na bahati nzuri, tulizungumza na Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na aliyekuwa Waziri wa Madini wakati ule na mazungumzo yakawa yameanza. Niwaombe, kama walivyoonesha nia njema watu wa *Resolute* kule Nzega, kulimaliza suala hili, hebu tukae pamoja tulizungumze, tuweze kuona namna ya kulimaliza. Ni kwa njia hiyo tu, huu mzimu, hili bundi, litaondoka.

Mheshimiwa Spika, kutokulitatua suala hili, *Barrick* atakapokuwepo pale na wananchi watakuwepo pale, manung'uniko yatakuwepo milele. Na kwa vyovyote

vile, hayatakuwa na manufaa kwa mgodi wala kwa wananchi. Ikumbukwe, dawa ya deni ni kulilipa. Wako watu walifanya mambo ya ajabu kule Kenya, miaka ya 1800 sasa wanadai fidia.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na mimi kuweza kupata nafasi kuweza kuchangia hoja katika Wizara hii. Kwanza kabisa, napenda kuipongeza Wizara na uongozi wake wote kwa ujumla, kwa namna ambavyo imejiwekea mikakati ya kuweza kuwapunguzia wananchi matatizo.

Mheshimiwa Spika, lakini pili, kwa masikitiko makubwa napenda kueleza kwamba, Bunge letu hili na Wabunge wote walioko humu ndani, tumesahau majukumu yetu ya msingi ambayo tunapaswa humu ndani, kuja kusimamia Serikali na kutetea hoja za Serikali, au kuchangia katika hoja za Serikali, ili tuweze kuona ni namna gani tunaweza tukawasaidia wananchi, ambao kwa imani yao kubwa wametuchagua kuja kuwatetea na kuwakilisha mawazo yao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, nalisema hili kwa sababu, Bunge hili, limekuwa ni Bunge la kujadili Muongozo, limekuwa ni Bunge la kujadili Taarifa na mambo mengineyo yanayohusu Kanuni; sasa tunakuwa kana kwamba, hatukupata Semina wakati tunaingia humu

Bungeni. Kwa kweli, ni aibu, ni vema tukawawakilisha vyema wananchi katika kujadili matatizo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pili, nasikitika sana maana naogopa wanasema samaki mmoja akioza, huenda wote wakaoza. Sasa ninaogopa hili lisije likatokea katika Bunge hili, kwa Wabunge wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama kweli, hizi tuhuma zinazotolewa na wapo Wabunge waliohusika, basi Sheria ifuate mkondo wake. Hawa ni sawa na akina Yuda, kama akina Yuda waliomsaliti Yesu. Sasa hawa ni akina Yuda, wanaowasaliti wananchi waliowachagua. Wananchi, wamewachagua kwa imani kubwa kabisa kwamba, waje kuwakilisha mawazo yao na kuweza kusaidiana katika kuleta maendeleo katika jamii tunazoishi.

Lakini sasa, kama kiongozi, maana Mheshimiwa Mbunge ni Kiongozi; ukirudi Kijijini kule, ni Mheshimiwa, Mheshimiwa, Mheshimiwa, kila unakopita. Sasa kama utakuwa unaitwa Mheshimiwa, Mheshimiwa, utakuwaje Mheshimiwa ambaye, unakubali kabisa kweli kweli, kupoteza mwelekeo wako, kupoteza dira yako, kupoteza *vision* yako uliyowaambia wananchi, unakuja kuchukua rushwa kwa ajili, ya kukwamisha miradi ya maendeleo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli, ni aibu, aibu, aibu sana.  Waliofanya hivyo, kwa kweli, hapa sasa hivi najua nafsi zao zinawasuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunakemea rushwa, tunakemea nini. Je, tunategemea kweli, Mkurugenzi wa *TAKUKURU,* Mzee Dkt. Hosea, atafanya kazi yake vizuri kweli? Kama sisi wenyewe Viongozi, ndio tunakuwa vyanzo vya kuchukua rushwa? Kwa kweli, ni aibu sana. Wananchi huko kwa kweli, wanapiga simu, wanasikitika mno. Kwa hiyo, ninaomba kabisa katika hilo kwa kweli, ulivalie njuga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niende kwenye hoja moja kwa moja. Napenda kuongelea suala la wachimbaji wadogowadogo. Wachimbaji wadogowadogo wamekuwa wakinyanyasika sana. Wachimbaji wadogowadogo ni masikini, wachimbaji wadogo wadogo hawana vifaa vya kutendea kazi. Katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, inaonesha kuna pesa na kuna vitu ambavyo vinatakiwa kupewa hawa wachimbaji wadogo wadogo. *(Makofi)*

Sasa sielewi ni utaratibu upi kwa sababu, hata Bajeti ya mwaka jana ilisomeka hivyo hivyo, lakini hivi ninavyoongea wachimbaji wadogowadogo, hasa wanaotoka eneo la Mpanda, Ibindi, Machimboni, Katesunga, hawajapata vifaa hivi hata siku moja. Sasa ninaomba, katika majumuisho yako Mheshimiwa Waziri, uwaeleze wananchi wa Ibindi, Katesunga, Machimboni, Magamba, ni namna gani wanaweza wakapata hiyo mikopo na ni namna gani wanaweza kupata vifaa hivyo vya kutendea kazi.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine napenda kuongelea kuhusu hili suala la mrahaba wa 4%.

Napendekeza, hii pesa ya mrahaba, itengewe akaunti yake maalum, ili iweze kuelekezwa hasa katika kutatua matatizo ya jamii, kwa mfano, ikaelekezwa kwenye mashule, ikaelekezwa mahospitalini ambako ndiko sisi wote tunakotegemea kwamba, bila kurekebisha afya, ina maana kwamba, huyu mtu hataweza kufanya kazi yake vizuri, hataweza kujiletea maendeleo. Kama hatutaweza kuboresha shule zetu vizuri ni wazi kabisa kwamba, hatutakuwa na *product* nzuri hapo baadaye. Kwa hiyo, ninaomba hii pesa kama inawezekana ikatengewa akaunti yake maalum, ili iweze kujulikana inafanya kazi gani hasa katika kuleta maendeleo kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine katika hilohilo, Mheshimiwa aliyetoka kuzungumza, ameongelea kwamba, kuna makampuni ambayo yanagoma kulipa. Inakuwaje kampuni imekuja hapa, ikasaini mkataba, leo Serikali, inaiambia ifanye hivi, inakataa *and then* mnaanza *negotiation?* Sheria ziko wapi? Makampuni kama haya yanayokataa kushiriki katika shughuli kama hizo ama kama mmejiwekea mkataba ni wazi kwamba, hafai aondoke, hakuna sababu ya kumbembeleza mtu, madini yetu hayaozi. Kwa hiyo, tunaomba kabisa kama mtu anashindwa ku-*comply* na Sheria za nchi na mikataba hiyo mnayoiweka, kama ni mizuri kama ni mibovu, basi muipitie upya ili kila kitu kijulikane na huyo anayekataa atoke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naongelea suala la malipo ya leseni kwa wenye viwanja vidogo, ambao ni wachimbaji wadogowadogo. Hivi karibuni nimekuwa nikisikia kwamba, kuna Waraka umeandaliwa kwa ajili

ya kupandishwa kodi ya leseni kwa wachimbaji kutokana na eneo alilonalo. Kodi hii ilianza, ilikuwa kama 80,000/= ikapandishwa ikaja kama laki moja na kidogo, ikapanda tena ikawa kama laki mbili.

Sasa hivi, inasemekana kwamba, watalipa milioni moja kwa mwaka. Sasa huyu mchimbaji mdogo ambaye hujamwezesha katika vifaa vya kuchimbia, vifaa vya kjutafutia yale madini. Atapataje hiyo milioni moja, ili aweze kulipia ile leseni yake? Hii si njama ya kutaka kuwanyang'anya viwanja vyao? Kama ndivyo, je, mnafanyaje kuhusu hilo?

Kwa kweli, katika kodi hiyo, naomba muangalie upya na muangalie ni namna gani, huyu mchimbaji mdogomdogo mtakavyoweza kumsaidia.

Mheshimiwa Spika, katika hilohilo la leseni, kumekuwa na makundi nimeongelea sana hili. Baadhi ya wafanyabiashara, ambao ni *investors,* wanakuja moja kwa moja Wizarani, mnawapatia leseni kwa kuangalia ramani. Mnasema hapa Katesunga hapa, Mpanda, kuna hii *plot,* unampatia yule mtu leseni, anakwenda kule. Anafika kule kwa Afisa Madini, anamwambia leseni yangu ni hii. Kwa kweli, tunataka sasa, leseni zote zianzie kwa wananchi kule chini na si kutoka Wizarani kwenda kule kwa wananchi. Hii yote ni kujaribu kuleta migogoro na kuwafukuza wananchi katika maeneo yao, ili muwape hao *investors,* wakati wao ndio wamezaliwa katika hayo maeneo na wana haki kabisa ya kuendelea kuchimba katika yale maeneo. Suala la msingi ni kuwawezesha, kuwapa vifaa, ili waweze kujiongezea vipato.

Mheshimiwa Spika, suala la nguzo za kusambaza umeme. Kwa kweli, kama tutamwambia mwananchi alipie nguzo, kutoka *point* moja kwenda nyingine, tunamwonea. *TANESCO* ilifanye hili suala yenyewe, *TANESCO* inajiendesha kibiashara, mwananchi huyo kila mwezi analipia umeme, sasa ni kwa nini napo kutoa nguzo kutoka pale kuileta hapa, mnamwambia mtu ailipie, kazi ya *TANESCO* ni nini? Sisi tunasema tunataka mwananchi awe na maisha bora? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba hilo nalo lizingatiwe na liangaliwe upya namna ambavyo tunaweza tukampunguzia mwananchi wa kawaida, gharama za kuvuta umeme, ili aweze na yeye kuwa na umeme nyumbani kwake, kwani tunaelewa faida za umeme katika kujiletea maisha bora. Kwa hiyo, ni vema hasa wananchi wa vijijini, tukawafikiria mara mbili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa na mimi nafasi kuchangia mchango huu. Naomba niwapongeze Mheshimiwa Waziri na Manaibu Waziri na Katibu Mkuu na Maafisa wote wa Wizara hii, kwa kufanya kazi yao vizuri na kuandaa vizuri Bajeti yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi, wamezungumzia hapa kwa uchungu mambo mengi, Wataalamu wa kutumbua majipu ya majungu ya siasa wametumbua vyakutosha. Lakini jambo hili, wengi wamelizungumza katika hotuba hii ya Waziri, lakini lazima tulitafutie wakati kwa sababu, limedhalilisha sana Bunge letu, jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (2), kinasema, naomba kunukuu: *"Bila kuathiri masharti ya Katiba na ya Kanuni hizi, Waziri au Mbunge mwingine, anaweza kutoa hoja na kupendekeza kwamba, suala lolote lijadiliwe Bungeni na hoja hiyo, itaamuliwa kwa mujibu wa masharti ya Kanuni hizi."*

Mheshimiwa Spika, naomba Wabunge wenzangu mniunge mkono, kwamba, nitoe Hoja, baada ya Bunge, utafutwe wakati muafaka, tulijadili suala hili, ili kama tuamue waliohusika wachukuliwe hatua au Kamati ivunjwe au iendelee kama ilivyo, kwa muda muafaka. Naomba kutoa Hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, naafikiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa, naomba niwaambieni, huyu anachangia hoja, hajatoa hoja. Mheshimiwa Vita Kawawa, huo siyo utaratibu… *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuendelea baada ya kuungwa mkono.

**SPIKA:** Naomba munisikilize basi. Sasa hivi, unachangia tu, utaratibu wa kutoa hoja hauko hivyo. Kwa hiyo, tunaendelea. Endelea kuchangia. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nawashukuru Wabunge wote, waliounga mkono hoja yangu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee kwa kutoa shukrani sana kwa Serikali. Kama ilivyozungumzwa katika Hotuba ya Bajeti, umeme wa jenereta katika Wilaya yetu ya Namtumbo na tunategemea wakati wowote umeme huo utaanza.

Mheshimiwa Spika, lakini pia, jenereta lile walituambia ni la muda. Tunategemea umeme wa gridi, ambao utaunganishwa kutoka Makambako. Lakini, katika umeme huo naishukuru sana Serikali, ulikuwa umeme wa *KV* 132, lakini nimefanya mapitio na sasa kuna makaa ya mawe Ngaka, ambayo yanategemea kuzalisha mpaka *Mega Watts* 400. Kwa hiyo, wameona waweke msongo wa *Kilo Volt* 220. Tunaishukuru sana Serikali kwa kufanya maamuzi hayo.

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Serikali, sasa. Kwa kuwa, Namtumbo ulikuwa unakuja umeme wa gridi, baada ya kuwa umeshafika Songea, wa msongo wa *Kilo Volt* 33, tunaomba nao uongezwe *transmission*

yake kwa sababu, kutakuwa na mradi wa *urani* ambao peke yake tu, utahitaji matumizi ya *more than 20 Mega Watts* za umeme. Kwa hiyo, tunaomba nayo Serikali iongeze uwezo wa msongo huo utakaokuja Namtumbo.

Mheshimiwa Spika, Waziri, ametueleza hapa makaa ya mawe ya Ngaka na kampuni ile ambayo inategemewa kuzalisha umeme wa makaa ya mawe wa *Mega Watts* 400, ambayo wataanzia kwa *Mega Watts* 200, yenye thamani kwa kuanzia dola za marekani 400.

Sasa nilikuwa nataka kujua pia kwa Wizara *investment* hii ya dola 400 pia imechanganya na *transmission line* kuja mpaka Songea, au laah na kama sivyo tunaomba Serikali mpango wake ukoje wa kuweka Bajeti ya kuweka transmission line?

Kama hawa wenzetu ambao ni wawekezaji watawekeza dola hizo milioni 400 kwa kuweka mtambo wa kuzalisha umeme sisi kama Serikali tumejipangaje kuweka fedha za kuweka *transmission line* mpaka kutawanya na *distribution line* katika wilaya ya Mbinga Songea, Namtumbo na Tunduru, tunaomba Serikali Waziri anapokuja kujumuisha aje atueleze mpango huo ukoje.

Mheshimiwa Spika, lingine nilikuwa nataka kuzungumza nchi yetu tuna miradi mikubwa hii ya gesi inayokuja na yurani. Sasa nilikuwa nataka tujiulize na tutafute majibu tumejiandaa vipi kusomesha vijana wetu zaidi watakaofanya kazi moja kwa moja katika

kazi ya usimamizi wa kitaalam katika machimbo na usafirishaji wa yurani, tumejiandaa vipi tunaomba Waziri aje atueleze na tuangalie pia wataalam tulionao.

Lakini pia tumejiandaa vipi kusomesha zaidi wataalam wa kusimamia uzalishaji wa gesi asilia kusimamia mitambo yake vituo vya usafirishaji, na pia usambazaji katika mtandao wa gesi katika vituo na majumbani.

Tumesomesha vipi vijana wetu na je, tuna data za wataalam wangapi wa Kitanzania tulionao nchini katika sekta hii na walio nje, na je, sasa hivi kwa miradi hii mikubwa wataalam hao watatutosha katika kipindi hiki tulichonacho?

Lazima tufanye kazi hiyo kwa nguvu zote tumeanza lakini pia tuongeze nguvu kwa haraka tuwapeleke vijana wetu katika nchi ambazo zenye vyuo zoefu za kusomesha wataalam wa gesi na yurani ili waweze sisi tusijekuwa watazamaji tu, tuweze kufanya kazi hiyo sisi wenyewe hapa nchini na Watanzania vijana wetu waweze kufanya kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awamu ya kwanza ya mwalimu Nyerere tulipopata uhuru ilikuwa haina wasomi hata kidogo, lakini wao waliamua kwa makusudi kabisa ku-*invest* kwenye *human capital* walisomesha sana, mpaka leo tunao wakina Prof. Mhongo leo tunampigia makofi na sifa zote. *(Makofi)*

Kwa hiyo na sisi lazima tufanye maamuzi ya makusudi ya kusomesha vijana wetu hawa, lazima kwa sababu ya hali halisi tuliyonayo na teknolojia tuliyonayo sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kufahamu nimesikia kwamba katika haya makampuni ambayo yamegundua gesi hii ujazo wa *cubic feet trillion 25* mpaka 28 ni kwamba wana *lessen* walikuwa na lessen au wana lessen za pamoja za utafiti na uchimbaji kwa ajili ya kwenda sokoni. Kwa sheria ile ya mwaka 1980 nasema hivyo kwanini sheria ya uchimbaji gesi na mafuta kama ni hivyo je, kwa sera na sheria tunayotaka kuitunga sasa hivi ya gesi makampuni haya yatahusika kwa sheria hii mpya na gesi au wataendelea na sheria ile ya zamani ya mwaka 1980. Na kama wataendelea na sheria ile ya mwaka 1980 itakuwa ni kifo kingine cha kwetu kwenye madini haya. *(Makofi)*

Naomba sana tufahamu hili Mheshimiwa Waziri anapokuja kwamba je, au tutaanza ku-*negotiate* nao kama tulivyoanza ku-negotiate nao kama tulivyoanza ku-*negotiate* na wale wanaochimba madini ya dhahabu. Wana mikataba ipi kwamba tutakapotunga sera na sheria hii mpya na wao watakuwa ndani yake au watasimamia ile sheria ya zamani. Tunaomba sana Mheshimiwa Waziri anapokuja atueleze hivyo, tusianze tena kulumbana na kama tulivyokosea katika mikataba ya nyuma.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka kumwunga mkono Mheshimiwa Zungu juzi alizungumza kuhusiana na mradi wa gesi kuweka kwenye *stock market* hasa wa bomba hili, ili wananchi na wao waweze kuchangia, hili ni suala jema sana tukiwezesha wananchi kuwa na *share* katika mtandao wa bomba la gesi basi pia tunawezesha pia mapato kwa Serikali.

Naomba hii mtandao wa gesi tufikirie pia bomba hili kuwa *public entity* Watanzania wenyewe waweze kuwa na *share* angalau asilimia 60, Serikali asilimia 30, lakini mtu yeyote wa nje asilimia zao zisizidi kumi tunaomba sana hili Serikali iweze kulifikiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na mchango wangu ni huo lakini naomba ufikirie ile hoja ili niweze kuunga mkono ili tuweze kulifanyia kazi ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Usije ukafikiria ulikuwa na hoja soma kanuni ya 54 na 55 ndiyo inakupa ruhusu wewe kuleta hoja. Sasa nitamwita Said Mussa Zuberi na Mheshimiwa Wambura ajiandae kwa sababu hawa ndiyo wachangiaji wa kwanza. Mwongozo wa Spika kuhusu nini.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, nimesimama kwa mujibu wa kanuni ya 68(7) nikitaka kuomba mwongozo wako kuhusiana na jambo lilitokea hapo awali, wakati Mheshimiwa Ezekiel Maige akichangia na hata aliyemfuatia Dkt. Pudenciana Kikwembe akichangia walisema kwamba migodi hailipi ushuru wa huduma.

Lakini ninavyofahamu mimi kwa mujibu wa sheria iliyotengeneza Halmashauri ya mwaka 1982 sheria namba saba na ile sheria ya fedha za Halmashauri ya mwaka 1982 namba tisa ambazo zote zinatoa *precedence* kwa Halmashauri kukusanya ushuru wa huduma kwenye *Business Enterprises* ambazo ziko kwenye maeneo husika. Mikataba ya midini imekuja kuingia miaka ya 90 na kuendelea…

**SPIKA:** Usijadili Mwongozo hatujadili kwa sababu unajadili sasa nataka mwongozo siyo kujadili.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Sasa mwongozo wangu ni kwamba sheria zilitungwa miaka ya mwanzoni ya 80 mikataba ya madini imekuja kusainiwa baadaye sheria zikiwepo na zikitaka Serikali yaani Halmashauri husika zikusanye ushuru wa huduma.

Sasa mwongozo wangu ni kwamba naomba unipe mwongozo kama sheria mama ambayo ilitungwa tena kabla ya mikataba kusainiwa inaweza ikawa *over redden* na mkataba tu ambao umesainiwa baina ya pande hizi mbili. Huo ndiyo mwongozo ninao utaka kwako Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

**MHE. SAIDI MUSSA ZUBERI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na afya njema, la pili ni kuunga mkono hoja asilimia mia moja. *(Makofi)*

Tatu niwapongeze Waziri pamoja na Manaibu wake wawili na Katibu wake Mkuu niwaambie *you are doing well carry on*. *(Makofi)*

Nimpongeze tena Waziri na Wizara yake kwa utandikaji wa bomba la gesi kuelekea kule kwetu Zanzibar. Tunaomba hili suala lifanyike ikiwezekana haraka iwezekanavyo ili na sisi tuweze kupata matunda haya.

Mheshimiwa Spika, nije moja kwa moja kwenye suala la sakata la umeme, uwezo wa TANESCO na umeme ambao kwamba tunaupata. *Totally capacity* ni *megawatt* 1,327, kama ile mitambo inafanya kazi sawasawa. Matumizi yetu ni *megawatt* 800 ili tuwe na mgao tunatakiwa chini ya 800 yaani 600 na kuendelea. Kwa maana hiyo kama alivyosema Waziri kwamba hakuna sababu ya Tanzania kuwa na mgao wa umeme, hili mimi nimelikubali kufuatana na takwimu zinavyoonyesha. Sasa tunachotakiwa tujiulize kwanini kipindi hicho cha nyuma tulikuwa na tatizo hili. *(Makofi)*

Nashukuru sasa hivi tuna mwezi wa pili tangu kuingia hawa hali imekuwa nzuri isipokuwa hali ya hewa ilitaka kuchafuka kidogo tu. Lakini tunamshukuru Mungu kwamba bado tunaendelea vizuri kwa sababu vyombo vya habari vilishaanza kuandika kwamba mgao unakuja lakini vyombo hivyo vikaweka mambo sawa kwamba hakuna mgao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nilikuwa nataka niende moja kwa moja kwenye haya masuala ya

uhujumu uchumi, hii inaonekana dhahiri kwamba katika Taifa letu tuna wadudu sijui tuwaite mchwa au watu wa aina gani ambao hawa kazi yao wao kuharibu kila kinachotengenezwa kwa maslahi yao. *(Makofi)*

Wamewaweka wananchi katika hali ya unyonge katika muda mkubwa sana uliopita, hawa ni watu wachache na mimi niwashauri tu wananchi kwa kuwa sasa hivi tuko kwenye suala la Katiba basi ni wakati muafaka baada ya kuzungumzia vizuri suala la Muungano na Serikali mbili basi wasisahau kuweka sheria ipitishwe sheria ya kuhakikisha hawa watu wahujumu uchumi tunatakiwa sasa tuwaue tena kwa risasi. *(Makofi)*

Wapitishe na nafasi hiyo wananchi wanayo wakati ndiyo huu, hatuna muda mwingine na lazima twende kufuatana na hali za nyakati, wakati wa mwalimu Nyerere umeshapita, wakati ule ilikuwa watu wakiambiwa tu kwa maneno wanasikia lakini sasa hivi watu wanaambiwa walikuwa wakiambiwa kwenye maandamano mpaka wanapelekewa washawasha pamoja na mabomu sasa tujue kwamba hali imeshabadilika lazima tuwe na sheria ya uhakika kwamba hawa wanapigwa risasi na zile risasi wanazinunua. *(Makofi)*

Kama hilo haliwezekani kama ni kitanzi basi hiyo kambana ya kunyongewa nao wanainunua na wafanyaji wa kazi hizo wanawalipa na fedha wanazo wamezichukua fedha nyingi fedha za kufanyia hivyo zipo. Mimi naona wakati umefika na wala tusije

tukashawishiwa sijui wakaja *Amnesty International* haki sijui za binadamu haki za nani wasije wakatusumbua hawa. *(Makofi)*

Juzi hapa Waziri wa Mambo ya Nje alisimama pale na akazungumza kuhusu suala la ushoga, ulimwengu mzima umesikia au mabwana wakubwa ambao kama wanasema wanaongoza ulimwengu wamesikia kwamba hatulitaki na tumesema kwamba tutafunga mikanda kuhakikisha kwamba hili jambo lisifanyike huku kwetu hata kama watatuzuilia misaada. *(Makofi)*

Basi na hili tuje tuwaambie kufuatana na hali tunayokwenda nayo na nyakati tulizonazo sasa hivi tunastahiki kuwa na sheria hii ya kuua waambiwe na vigezo vipo na kama watashindwa kuwaeleza mimi nitawaambia kwa sababu hawa ni wahujumu uchumi mimi nasema moja kwa moja wao wenyewe ni wauaji au kwa kuwa hawaandikwi kwenye magazeti? Wao wenyewe ni mauaji.

Sasa mimi naona labda nitoe rai tu kwamba ni wakati sasa wa kukusanya *data* na kuwaelekeza kwamba sasa tunakwenda tunakuelezeni kwanini tunazungumza hivi unapozimwa umeme labda kwa masaa mawili tu au matatu hasara gani na watu wangapi wanapoteza maisha kwenye nchi hii au kwa kuwa magazeti hayaandiki? *(Makofi)*

Kuna watu wanakuwa wako kwenye mashine kule Muhimbili, umeme unapozimwa watu wanakufa kule kwa kuwa hawaandikwi kwenye vyombo vya habari, kuna dawa zinazohitajika zipate aidha joto la wastani

au baridi ya wastani zisitetereke, umeme ukizimwa zinakosekana ina maana kuna watu wanapata injection au vipi kwa kufikiriafikiria kwamba labda zimeharibika au hazijaaribika na kuna nyingine zinaharibika kabisa.

Umeme huu unapozimwa viwanda vina *collapse,* kuna kuwa hakuna ajira na wanaofanya kazi viwandani ni watu wa hali ya chini, kipato chao kinatetereka na kinapotetereka kipato chao hata nyumba zao zinatetereka na kusababisha watoto aliokuwa nao kuanza kuwa na utapiamlo, watoto nao wanakufa hawa. *(Makofi)*

Wapewe *data* kama hizi waambiwe halafu sasa watueleze na nahakika wakiambiwa wanaweza wakasema hao watu wa haki za binadamu wakisema kweli kumbe sasa kuna lazima ya kuweka sheria hii kwa sababu wanakufa wengi na wala hatujamalizia hapo. Huo umeme wenyewe unapozimwa ukienda kama Dar es Salaam pamekaa kama kwenye hekalu la mfalme nani huyu...

**MBUNGE FULANI:** Solomoni.

**MHE. SAIDI MUSSA ZUBERI:**Anakuwa urooo! Unasikia ni mivumo ni *noise* (makelele) yanakuwa mengi, kiasi kwamba hata watu nao wanataka kupokea simu mjini pale unatafuta uchochoro wapi ujifiche kwa ajili ya yale majenereta.

Sasa tutizame nao masuala ya mazingira yanavyoharibika na wakisemwa watu wa pale wakapimwe wale wote wale wameathirika na umeme wa majenereta wao, au kwa kuwa haziwekwi takwimu hizi, mimi naona ni afadhali kuepusha kuuwa maelfu ya watu lakini tukawauwa watu wasizidi 200. *(Makofi)*

Halafu hawa watakaa sawa hawa, tukianza nao watano kumi mpaka kumi na tano basin chi hii itatulia na inawezekana ikarudia kule kule kwa mwalimu Nyerere. Lakini sasa hivi wanachezea tu sheria kwa sababu wanajua tena sio wao tu peke yao na zamani hawa mwalimu Nyerere hawa aliwaita wahujumu uchumi, baadaye wakaitwa maghabacholi halafu wakaitwa mafisadi, au sasa hivi tuwaite mafia, kwa sababu sasa hivi wana dalili zote walishakuja mpaka humu Bungeni ni mafia hawa. Wanataka sasa hivi mpaka kuturubuni mpaka Wabunge walishafika Bungeni sasa hawa ni mafia hawa kitu ambacho kwamba wao hawajakifanya sasa jamani bado tuendelee tu kukaa nao basi mimi naishauri kama Serikali tunapoweka sheria hiyo tusiwaandike kwenye magazeti, wakifikia wakati wa hukumu tunawahukumu tu kisailensa hivyo hivyo kwa sababu wao wenyewe ni sailensa *killer* hawa tunawauwa tu tusiwaeleze. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mhh!

**MHE. SAID MUSSA ZUBERI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge naomba pia niwatambue wageni waliopo hapa ndani kwanza kabisa ni wageni wa Mheshimiwa Samuel Sitta, Waziri wa Afrika Mashariki, ambao ni Waheshimiwa Madiwani yuko Mheshimiwa Jafari Kanikila, yuko Mheshimiwa Diwani Ahmed Mohamed, huyu siyo diwani huyu ni hakimu Nduguta ambaye ni mgunduzi wa dhahabu Urambo, karibu sana na tumefurahi kuwaoneni. *(Makofi*)

Tuna wageni wengine wa Mheshimiwa Stephen Masele Naibu Waziri wa Nishati na Madini, kutoka Shinyanga Mjini, ambao ni Waheshimiwa Madiwani kutoka Manispaa ya Shinyanga wanaoongozwa na Katibu wao Mheshimiwa Shella Mashaneti, Waheshimiwa Madiwani karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Chama cha Mapinduzi wilaya na sekretarieti ya wilaya wakiongozwa na Mwenyekiti Ndugu Alhaji Salum huko huko Shinyanga nadhani karibuni. Kuna afisa Elimu manispaa ya Shinyanga Honorata Yuhubika ameambatana na Kamati ya shule maalum Luhachija na wawakilishi wa wanafunzi walemavu, karibuni sana. Wapo na wanafunzi wenye ulemavu, ahsante sana karibuni sana. *(Makofi*)

Halafu anacho kikundi cha madereva *taxi* wa Manispaa ya Shinyanga wakiongozwa na Ndugu Kennedy Nyangi Mwenyekiti wa hawa madereva yuko wapi? Ahsante sana. *(Makofi)*

Halafu yupo na mjomba wake Masele ambaye ni Mr. Bonda Kinga na Mrs. Elizabeth Bonda wasimame hawa walipo. *(Makofi)*

Pia ile *club* ya kulenga shabaha wale wanaambiwa kwamba kesho mabasi yataondoka tarehe 29 yatakuwepo saa mbili mabasi ya kuwachukuwa wale ma-*club* *rangers* wale wa Makutopora. Kwa hiyo, wale wanachama wa kulenga shabaha wa kulenga shabaha basi saa tatu mabasi yanaondoka yatakuwepo saa mbili hapa. Na kama mnalenga shabaha basi msichelewa.

Waheshimiwa sasa namwita Mheshimiwa Anastazia Wambura halafu atafuatiwa heshimiwa Prof. Peter Msolla na Mheshimiwa Naomi Kaihula pia ajiandae.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia asubuhi ya leo ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nishati na Madini.

Awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia uhai kwa sababu ni wengi walipenda waione siku ya leo lakini hawakuweza. Lakini vilevile si kwamba tunastahili sana sisi kuwepo hapa lakini Mwenyezi Mungu ameweza kutujaalia uhai.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kumpongeza Waziri Mhongo ambaye ni Waziri wetu wa Nishati na Madini, Manaibu Waziri Simbachawene pamoja na Mheshimiwa Masele pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini kwa kazi nzuri ambayo wameifanya katika kipindi kifupi sana cha kuwepo kwao katika nyadhifa zao. Nawapongeza sana. (*Makofi*)

Lakini pamoja na pongezi hizi kuna salamu za pekee kabisa kutoka Mkoa wa Mtwara. Salam hizi ni shukrani kwa mambo makubwa matatu, kwanza ni uzinduzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara kupitia Songosongo kuja Dar Es Salaam lakini vilevile wanashukuru sana kwa mgao wa Transformer 37 ambazo zitapelekwa katika Wilaya za Mkoa wa Mtwara yaani Wilaya ya Nanyumbu ambayo ilikuwa haina umeme kabisa, Wilaya ya Tandahimba, Masasi, Newala, Mtwara Vijijijini pamoja na Mtwara. Wanashukuru sana kwa hilo lakini vilevile wanashukuru sana kwa kuhakikisha kwamba sasa hivi *TANESCO* imeboresha miundombinu ya Umeme na kwamba jambo hili limepelekea sasa umeme haukatikikatiki hovyo.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na tatizo kubwa sana, Mtwara na Lindi tulikuwa na Umeme wa gesi lakini tatizo kubwa lilikuwa ni kukatika mara kwa mara kutokana na miundombinu ambayo ni chakavu. Wananchi wanashukuru sana na wanawaombea baraka tele kwa Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, uzinduzi wa bomba la gesi ulifanyika tarehe 21 Julai, 2012 katika Kata ya Madimba. Lakini ajabu ni kwamba kuna vikundi au kikundi tusema ambacho kimezuka na sasa hivi kimeanza kuwarubuni wananchi kwamba waukatae huu mradi.

Tulielezwa wazi na ni jambo ambalo ni la ziada ambalo Wizara ililifanya siku hiyo ya kuelimisha wananchi kuhusu faida kubwa sana za mradi wa bomba la gesi na faida mojawapo ambayo tulielezwa ni kwamba Serikali itakuwa inaokoa trilioni 1.5 shilingi za Kitanzania kila mwaka na ni dhahiri kwamba hizi pesa zitakwenda kusaidia katika sekta ya Nishati, Elimu, Maji, Afya na kadhalika.

Lakini sasa kinachoshangaza ni hiki kikundi ambacho kinapita kuwarubuni watu wakatae. Ninawaomba sana wananchi wa Mtwara ambao waliupokea mradi huu kwa mikono miwili na wamekubali kabisa kutoa ushirikiano wao wasikubali kurubuniwa. Naomba kikundi hiki kikiwafikia waseme hatudanganyiki na wakumbuke kwamba mkataa pema pabaya panamwita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna faida nyingine ambazo tulielezwa kwamba zitakuwepo, mojawapo ni ile ya kupunguza gharama za uzalishaji viwandaji kwa kutumia umeme wa gesi lakini pia hata magari yatakapokuwa yakitumia nishati ya gesi, gharama za nauli kwa wananchi au kwa abiria zitapungua na nitaafurahi sana kwa hili na ninaomba tu wananchi watambue kwamba maisha bora ambayo

tunaambiwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi huu ndiyo mwanzo wake.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii tena kuipongeza Serikali kwa jitihada ambazo imeonyesha, jitihada za kuondoa kabisa mgao wa umeme katika nchi yetu na tumeona wazi kwa sababu kipindi kama hiki mwaka jana kulikuwa na matatizo makubwa na kulikuwa na mgao mkali sana katika nchi yetu na hii ilipelekea hata kukwamisha Bajeti ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, mimi naiomba sana Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi, chonde chonde kwamba ule muda wa kuwafurahisha watu sasa umekwisha na sasa hivi tumebaki na muda wa kuwa-*surprise* watu na kwa kweli wananchi wanashangaa na wanapiga simu sana wakiuliza hivi ni kweli mgao utakwisha? Hawaelewi na hawaamini! Kwa hiyo, ninachotarajia ni kwamba hivi karibuni pengine tutakuwa na *surprise* nyingine katika kuhakikisha kwamba tunaboresha mapato yanayotokana na Nishati na Madini na pia tunapunguza migogoro au kuimaliza kabisa katika maeneo ya migodi. Lakini vilevile tuhakikishe tunaboresha hali za wachimbaji wadogo wadogo. Hizi ndizo *surprise* ambazo tunatakiwa tuwape wananchi wetu.

Ninaomba niungane na wenzangu kuwalaani wale wote ambao hawaitakii nchi yetu mema kwa mambo mazuri yanayofanyika, wale ambao wanajitahidi sana kuipeleka nchi yetu katika mwendo wa kasi. Kiongozi anapojitahidi kukimbia utashangaa

mmoja anamtega kwa kamba ili kumwangusha. Na mimi nachukua nafasi hii kuwalaani sana wanaofanya hivi.

Lakini kwa upande wa hili suala ambalo watu wanalilalamikia la kuhusiana na sheria ya manunuzi, naomba kurejea maandiko matakatifu ambayo yanamsimulia Bwana Yesu kipindi kile alipomponya mgonjwa siku ya Sabato na Mafarisayo na Walimu wa Sheria wakaanza kumtuhumu kwamba amefanya kazi siku ya Sabato. Lakini aliwaeleza yafuatayo na akawaambia kwamba hivi ni nani kati yenu ambaye Punda wake atatumbukia shimoni siku ya Sabato asiweze kumtoa eti kwa sababu tu ni siku ya Sabato?

Ni kengele ya pili?

**SPIKA:** Ya kwanza!

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, hiki kitendo ambacho viongozi wetu wa Wizara wamekifanya cha kuwasaidia wananchi wetu kuondokana na giza bila kuitisha *tender*, mimi nikifananishe na kitendo cha kumponya mgonjwa siku ya Sabato na pia kitendo cha kumwokoa Punda siku ya Sabato. Kwa kweli hawana makosa na ninaomba tuwaunge mkono kwa nguvu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijamalizia mimi niiombe Serikali iangalie mambo yafuatayo kupitia Wizara ya Nishati na Madini. Kuna tatizo kubwa sana la bili bandia kwa wananchi, wananchi wengi wanapelekewa bili ambazo si halisi ni kubwa kuliko

matumizi. Naomba sana Serikali ilifuatilie hili ili wananchi waweze kulipa kulingana na walichotumia.

Lakini kingine ni kwamba hili wimbi la vifaa bandia vya umeme ambavyo vimezagaa zagaa madukani vinapelekea mioto na hasara kubwa....

**MBUNGE FULANI:** Ni moto!

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, nasikia ni moto na siyo mioto.

Moto na hasara kubwa kwa wananchi wetu na kinaturudisha nyuma sana kimaendeleo, naomba Serikali au Wizara ishirikiane na *TBS* ili kusudi kuweza kudhibiti matatizo haya ya vifaa bandia vya umeme.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ambalo naliomba ni umeme unaotolewa wakati mwingine na hata juzi nadhani tumeona hapa, umeme ulikatika na tukaahirisha Bunge, sijui sababu ilikuwa ni nini lakini kuna maeneo ambayo nyumba moja utaona nyingine ina umeme na nyingine haina. Lakini kumbe uwezo wa zile mita ni tofauti na umeme unaopelekwa pale ni kidogo kwa hiyo, naomba sana *TANESCO* wanapo-*supply* umeme wa-*supply* umeme ambao unatosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ni la uzembe kwa wafanyakazi wa *TANESCO*. Mara nyingi zinakuwa zikitokea hitilafu lakini wanapoitwa wafanyakazi wa *TANESCO* wanakuwa ni wazito sana na utakuta yanatokea maafa bila sababu yoyote.

Mheshimiwa Spika, kabla sijamalizia naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wanawake wa Mtwara kwa kuniunga mkono siku zote na kushirikiana na mimi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Peter Msola atafuatiwa na Mheshimiwa Naomi Mwakyoma Kaihula na Mheshimiwa Mikidadi ajiandae.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Kilolo kwanza napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwako wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hoja hii iliyowasilishwa jana na hoja ambayo ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu.

Pili, napenda kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote bila kumsahau Dkt. Mwakahesya wa *REA* ambaye sisi watu wa Kilolo kwa kweli tumenufaika sana na kazi ambazo amezifanya.

Tatu, napenda kuipongeza sana Wizara kwa kupunguza gharama za kuunganisha umeme ambayo ilikuwa ni tatizo kubwa kwa watu wengi sana. Gharama za kuunganisha umeme kwa kweli zilianzia juu sana zilikuwa zaidi ya shiilngi 700,000/= na hatimaye zikaja shilingi 455,000/= na kwenye hotuba ya juzi kwa

vijijini kwamba gharama hizi sasa zimepunguzwa hadi kufikia shilingi 177,000/=.

Tunaipongeza sana Wizara kwa sababu hii itawezesha watu wengi na hasa walio vijijini ambao ni maskini kuunganishiwa umeme ikizingatiwa kwam ba sehemu nyingine hata kuni sasa hivi hazipatikani kutokana na kuharibika kwa mazingira. Hii ni nyenzo nzuri kwa utunzaji wa mazingira lakini vilevile kwa kuwawezesha wananchi walio wengi ili waweze kupata nishati ya uhakika.

Punguzo hilo kama mlivyoanzia juu kutoka shilingi 700,000/= mpaka shilingi 455,000/= na baadaye shilingi 177,000/= ni matarajio yangu kwamba mtaendelea kuliangalia jambo hili na kuzidi kupunguza ili kusudi watu wengi zaidi waweze kunufaika kwa sababu hata hiyo shilingi 177,000/= kwa vijijini bado ni gharama kubwa.

Katika maeneo ya sehemu za Kilolo watu wengi sana walipoona umeme umefika wamejiandikisha. Maeneo waliyojiandikisha ni Ruaha Mbuyuni, Mtandika, Mahenge na sehemu nyingine mbalimbali lakini tatizo lao limekuwa ni uwezekano wa kuweza kulipa hiyo gharama kubwa ambayo ilikuwepo awali kabla ya kutangaza tangazo hili juzi na ndiyo maana nasema kwamba tuendelee kuangalia hili ili kusudi tuweze kuendelea kupunguza gharama za kuwafikishia umeme wananchi walio wengi sehemu za vijijini.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana tulipitisha mpango wa maendeleo wa miaka mitano kama sehemu ya *Tanzania Development Division 2025* na lengo kubwa la mpango wa miaka mitano mwaka 2011/2012 hadi mwaka 2015/2016 ilikuwa ni kuweka jitihada za makusudi za kukuza uchumi ili hatimaye tufikapo mwaka 2025 Tanzania iwe ni nchi yenye uchumi wa kati na iondokane na kutegemea uchumi wa kilimo na badala yake itegemee zaidi viwanda yaani *a shift from an agriculture based economy to an industrial based economy* na hivi ndiyo nchi nyingi zilivyofanya, hazikukwepa kilimo lakini hatimaye wakaingia kwenye viwanda vidogovidogo na baadaye vikubwa na uchumi wa nchi ukaendelea.

Lakini hili liliwezekana tu pale ambapo walikuwa na nishati ya kuaminika na kwa kufuatana na mwenendo tunaokwenda nao inawezekana kwamba nishati inaanza kuwa ya kuaminika na kama tulivyohakikishiwa na Mheshimiwa Waziri kwamba mambo ya kukatakata umeme sasa yatakuwa ni historia. Kwa hiyo, hii sasa ni fursa ya sisi kukuza viwanda vyetu. Tuanze na viwanda vidogovidogo vya kusindika mazao yetu ili kuongeza thamani na hatimaye tuweze kupata masoko mazuri.

Najua tuliwahi kufanya semina na Wizara katika ukumbi wa Pius Msekwa juu ya *Power System Master Plan* ya nchi hii, mengi yalizungumzwa. Lakini mimi ningeomba Wizara ipitie tena hii *Power System Master Plan* ili kusudi waweze kuona ni namna gani wanaweza kuiboresha ili kusudi tuweze kuwa na umeme au nishati ya kuaminika kwa muda wote. *(Makofi)*

Tuna vyanzo vingi sana sana lakini hatujavitumia vizuri, ni matarajio yangu kwamba hii *Power System Master Plan* na itakuwa vizuri kama Waheshimiwa Wabunge ambao wanazungumza na wananchi wengi waweze kupata nakala hiyo ili kusudi waweze kujua ni nini nchi yetu inajitahidi kufanya ili kuboresha nishati katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa nirejee kwenye Jimbo langu la Kilolo, kwanza nishukuru kwa jitihada kubwa zilizofanywa na Wizara hii kwa kutupatia umeme katika baadhi ya maeneo.

Mwaka 2009 umeme ulivutwa kutoka Iringa Tagamenta ukapelekwa Kilolo na hatimaye kufika mpaka Kidabaga na umeme huu ulizinduliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Jakaya M. Kikwete tarehe 27 Oktoba, 2009. Toka wakati huo umeme huu umepita katika vijiji saba na shule za sekondari tatu bila kushushwa na watu hawajanufaika bado, ukianzia kijiji cha Ihimbo, Utengule, Luganga Kibaoni, Luganga, Lulanzi, Lusinga, Ilamba, Maria *Consolata Secondary School, Udzungwa Secondary School,* na *Dabaga Secondary School,* wote hawa wanaziangalia waya zikiwa zimepita juu bila kunufaika nao. *(Makofi)*

Lakini vilevile mwaka 2011/2012 umeme umevutwa kutoka mji mdogo wa Ilula kuelekea Ruaha Mbuyuni mpakani na Morogoro. Umeme huu toka umevutwa umepita Vijiji vya Ikokoto, Kitonga,

Mahenge, Mtandika, Kidika, Ruaha Mbuyuni na jirani kijiji cha Msosa bila wananchi kuweza kunufaika na umeme huo.

Ombi langu, baada ya kazi kubwa hii ambayo imefanywa na umeme huu tayari gharama za kuunganisha zimeteremshwa, naomba sasa Wizara itupie jicho la huruma katika vijiji hivyo ambavyo nimevitaja ili vinufaike na umeme huu unaopita kwenye vijiji hivi. Upatikanaji wa umeme huo utahamasisha ujasiriamali na usindikaji wa vyakula na mazao mbali mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache napenda kutamka kwamba naunga mkono hoja hii nikiwa na matumaini makubwa kwamba watu wa Kilolo watanufaika na mpango uliopo na Bajeti iliyowasilishwa na Wizara hii ya Nishati na Madini. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana, sasa nitamwita Mheshimiwa Naomi Kaihula, atafuatiwa na Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi na Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kahigi ajiandae.

**MHE. NAOMI M. KAIHULA:** Mheshimiwa Spika na Wabunge wote ahsanteni sana.

Mimi nina machache ambayo napenda kuzungumzia kuhusu hii Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini.

Kwanza kabisa napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwamba kweli Mwenyezi Mungu huwa anajibu na majibu yenyewe tumeanza kuyaona hapa hapa duniani kabla ya kufa, kama ambavyo mara nyingine nilisema hapa kwamba tunahitaji kuombewa na kusudi Mungu atuongoze jinsi ya kufanya kazi za wananchi waliotutuma humu Bungeni.

Kwa yaliyokuwa yakizungumziwa kuanzia jana na leo naona kabisa mkono wa Mungu upo. Tunaanza kuzungumzia mambo ambayo tunataka na ambayo Mungu anataka tufanye kazi ambayo tulipewa na wananchi kwa heshima na taadhima. Namshukuru Mungu kwa ajili ya jambo hili.

Pia napenda sasa hivi tumekwishaanza kuelewana kwamba Upinzani siyo ugomvi na kwamba Upinzani upo hapa kwa ajili ya kuwasukuma na kuwachokonoa wale watawala, upande mwingine ili waweze kufanya yale mambo ambayo wananchi wanayataka. Nimeona sasa tupo pamoja tunaendelea. Kwa hiyo, napenda niwapongeze pia Wapinzani wote wakiongozwa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo, kwamba sasa tunakwenda pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kuchangia katika Bajeti hii. Nina mambo mawili, matatu ambayo nilikuwa napenda kuyazungumzia zaidi. Jambo la kwanza moja ambalo pia ningependa kulisisitizia ninawapongeza kwa kweli Wizara hii ya Nishati na Madini, uongozi uliochaguliwa mpya na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt.

Jakaya Mrisho Kikwete, kwa sababu wameonekana kwamba wamekuwa na ujasiri na wakaweza kufanya kazi hiyo. Nawapongeza sana sana kwa hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa kwa upande wa umeme kama mlivyofanya ni kweli tunawashukuru mmepunguza bei za umeme kwa faida ya wananchi. Lakini pia tungekuwa tunawaomba kwamba mngeenda hatua nyingine kubwa zaidi.

Baada ya kupunguza hizo bei za kuunganisha umeme majumbani, tulikuwa tunaomba sasa mfikirie suala la umeme wenyewe upo juu sana, kiasi kwamba hata watu wengi wa kawaida wanashindwa hata kuutumia umeme wenyewe, na huenda pia ndilo linalopelekea watu wengine wakaanza kujiunganishia umeme isivyo halali.

Kwa hiyo, nilikuwa nawaomba sana mkae chini tena kwa maarifa na hekima kabisa kama mlivyofanya kupunguza bei za kuunganisha umeme majumbani mfanye hili suala muone jinsi ambavyo mtaweza kufanya kuweza kuwafikia watumiaji mmoja mmoja na wale wa chini kupunguza hizi bei za umeme. Lakini pia ninawapongeza kwa dhati na ninaomba Mungu awabariki kwa hilo mwendelee.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba *TANESCO* limekuwa Shirika letu na limekuwa na matatizo mengi, na kwa kweli katika majadiliano yetu tumeona kwamba limetetereka. Lakini pia kuna jambo nzuri ambalo Mungu ametuonyesha kwamba lilikuwa linatetereka

kwa ajili ya mambo ya ufisaidi. Sasa kwa ajili ya mambo hayo ya ufisadi ambayo sasa hivi yanaelekea kuwa wazi na yataendelea kuwa wazi. Tulikuwa tunaomba hivi Wizara haya mambo ya *IPTL* kwa kweli sisi watu ambao ni wa kawaida *layman* hatujaona vizuri, hatujui yameishia wapi, wataendelea kutuibia fedha mpaka lini. Hawa watu wa *DOWANS* mpaka leo hatujajua wameishia wapi? Mambo ya *Richmond* hatujaelewa yataishia wapi?

Tulikuwa tunaomba kwa vile mmekuwa na hekima mkafanya mambo mazuri mpaka tukafikia hapo tulipo sasa. Tunaomba tujulishwe wazi wazi je, *DOWANS* imeishia wapi, *IPTL* itaishia wapi, *Richmond* iliishia wapi? Ili kusudi tuweze kufuatana na nyie tunapokwenda kuweka sawasawa suala hili la umeme kupitia hawa *TANESCO.* Hili tunaliomba sana mtusaidie kuweka mikakati mizuri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo ningependa kuzungumzia pia suala nzima la nishati kuhusu gesi. Kweli tunafurahi kuhusu gesi lakini pia bado hatujafanya masuala mengi ya msingi, masuala kama ya sera, masuala kama ya sheria hizo. Lakini ninachoomba sasa hivi tusiende haraka sana kwamba mimi niweke gesi hapa hilo kweli litakuja.

Lakini kwanza nilikuwa nafikiri tungeomba hizo sera zije. Lakini hizo sera pia Serikali ihakikishie kwamba watu wengi ambao wana *experience* wameona katika sehemu nyingine duniani waweze kuchangia kwa uwazi kabisa hata kama ni kuweka kwenye magazeti, kwenye *TV* na kadhalika ili watu waletewe

waone ni jinsi gani gesi inaweza ikawa laana ama gesi inaweza kuwa na faida. Baada ya hapo ndiyo tuanze sasa kulizungumzia kama Katiba. Kwa sababu tusifanye makosa yale yale tuliyofanya kwenye madini.

Kwa hiyo, naomba sana tutakapokuja kutunga sera ya gesi tuwe wazi, tusiikimbize kimbize na mwisho ikawa ni sheria imepita halafu inakuja kutokea kama masuala ya *NSSF* na wafanyakazi. Kwa hiyo, tunaomba kwamba sera ya gesi ije haraka na vitu vingine ili tuweze kuona jinsi gani tutakwenda mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo ningependa kuzungumzia suala la lingine la madini. Napata utata sana inasemekana kwamba haya madini karibuni nchi nzima yamekwishauzwa. Inasemekana kwamba wajanja kama huko walikotoka walikwishajipangia sehemu za madini na wengine wenyeji wa hapa nchini na wengine wakapeana hizo *forty percent*, au *ten percent*. Sasa kama wamekwishapeana au imekwishagawiwa yote na sasa wana leseni zao pengine ni za miaka 90 au 99. Maana yake tunachekesha sana vitu vingine tukianza kufikiri.

Sasa tunazungumzia suala la wachimbaji wadogo wadogo, hawa wachimbaji wadogo wadogo tutawagawia nini na inaelekea kama tunawarubuni tu yaani hatusemi ya ukweli. Kwa sababu kama sehemu zote za madini wanazo watu, wengine wanazo wapo nje wamekaa, wale wachimbaji wadogo wanavyokwenda kule kuchimba anakuja mtu

anasema hii ni sehemu yangu kama kawaida wanawaambia waende mahakamani.

Mheshimiwa Spika, lakini tujue kwamba Mahakama yenyewe ni watu, mahakama nao wanaweza wakala rushwa na mara nyingi wanashinda wenye fedha. Tumeona kabisa, sasa hili tutalifanyaje? Naomba hili pia tulifikirie siyo kwa Wizara tu, hata sisi tunavyokwenda ku-*move* tufikirie itafika wakati ambapo itabidi Bunge hili kwa makusudi kabisa lilete sheria ya kuvunja hata sheria yake. Kwa sababu kama ni hivyo inaelekea kwamba hakutakuwa na ufumbuzi kwa sababu vita vitatokea daima milele.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu wale wachimbaji wakubwa hawatakubali kuachia yale watakimbilia Mahakamani, na wachimbaji wadogo ndiyo nchi yao Mungu aliwapa ardhi yao, madini yao ndivyo ambavyo wataishia. Kwa hiyo na wenyewe watakwenda kuchimba lazima sivyo watakuwa wanapiga risasi kama walivyokuwa wanaapigwa huko Bulyakhulu na huko mahali pengine. Kwa hiyo, hili suala pia naomba tuambiwe.

Je, inakuwaje ile mikataba iliyowekwa ambayo wameng'ang'ania wale wakubwa wenye fedha ili tuweze kuweka sawa mtafanya namna gani? Tungependa pia hili tupate jibu na tuone tunaendaje nalo.

Mheshimiwa Spika, sasa naona kwamba mambo muhimu ambayo nilikuwa nataka kuzungumzia ni hayo. Mwishowe, napenda nizungumze hivi kutokana

kwamba tumepata mafisadi wengi wapo, wengine humu humu wengine sehemu nyingine.

Mimi nilikuwa nasema hivi, kusema kuwaua itakuwa siyo kweli kama tunataka kufanya kweli tuwafilisi. Hatua ya kufanya kweli ni kuwafilisi halafu mnawatangaza, mkishawafilisi hata watu wengine wataona hawatafanya kile kitendo kwa sababu ukiwaachia zile mali wanatumia zile mali kuharibu *system*, wanatumia zile zile mali kwa ufisaidi kufanya nini, kwa hiyo mnakuwa hamwendelei.

Kwa hiyo, kinachohitajika hapa ambapo wengine tunawafahamu, mnawafahamu na *system* ipo kwa ajili hiyo ihakikishie inawapata wote na kuwafilisi na hizo mali zao kutumika kwa ajili kurekebisha madhara na makosa waliyofanya. Mimi hilo ndilo pendekezo langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninashukuru, napenda kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nitamwita Mheshimiwa Fatuma Mikidadi na Mheshimiwa Prof. Kahigi ajiandae na Mheshimiwa Josephat Kandege.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia mada hii ambayo ipo mezani petu leo. Mimi ninaungana na wenzangu wote waliosema kwamba suala hili tulichunguze likoje, tupate jibu. Siwezi kurudia tena maneno waliyoyasema, lakini ninasema

ninaungana nao na ninaunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, ninaanza na kusema kwamba lazima twende na wakati na tusingoje wakati utubadilishe. Kwa nini niseme hivyo, nimesema hivyo kwa sababu Tanzania tumegundua gesi. Sasa kwa nini tuendelee kupata tabu wakati Tanzania tumegundua gesi. Hatuwezi kukaa tukangojea masuala ya mvua inyeshe ili tupate umeme. Masuala ya Mtera sasa basi gesi imegunduliwa na ndiyo maana nimesema twende na wakati tusingoje wakati utubadilishe.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tuna vyanzo vingi vya gesi, tuna vyanzo vya nishati, nchi nzima sasa tufumbuke, vyanzo vile vya gesi tuanze kuvitumia.

Mheshimiwa Spika, tunayo gesi asilia Lindi, tunayo gesi asilia Mtwara, tunayo gesi asilia Kinyerezi hivi vyote ni vyanzo vya gesi tu. Si hilo tu tunayo makaa ya mawe Kiwira, tunao umeme wa upepo Singida, Makaa ya Mawe Ludewa, tunacho Chuma cha Liganga. Hivi vyote ni vyanzo vya gesi kwa nini tunakuwa na giza miaka yote hii? Tangu umeme umeanza mwaka 1908 Tanzania ambao uliletwa na Wajerumani mpaka leo hatujafika popote kuhusu umeme.

Mheshimiwa Spika, tunaomba sana sasa twende na wakati tusingoje wakati utubadilishe tutumie hivi vyanzo tulivyokuwa navyo kupata umeme Tanzania. Hilo lilikuwa suala la umeme.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, ni suala la madini. Tanzania tunayo madini mengi sana. Kuna Mikoa ambayo imepata ufadhili, kuna Mikoa ambayo imepata kuwezeshwa, lakini Mkoa wa Lindi hatujawezeshwa, Mkoa wa Lindi nao una madini kadhaa, lakini hatujawezeshwa, kuna wachimbaji wadogo wadogo tu wamejaa lakini Mkoa mzima una madini. Kila Wilaya ina madini, kwa nini na sisi Mkoa wa Lindi hatuwezi kuwezeshwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikikwambia hapa utashangaa Wilaya ambazo zina madini katika Mkoa wa Lindi. Wilaya ya Liwale kuna dhahabu, Wilaya ya Nachingwea kuna dhahabu, Wilaya ya Ruangwa kuna *green Tome line*, kuna *green garnet* kuna dhahabu Rungwa, lakini wachimbaji hawa hawasaidiwi. Kuna rangi mbalimbali za kujengea nyumba zipo Rungwa, lakini hawawezeshwi.

Mheshimiwa Spika, siyo hayo tu Lindi yenyewe kama Lindi kuna *Gypsum*, kuna chumvi, kuna gesi hatuwezeshwi. Kwa hiyo, naomba ile sera ya kuwawezesha wachimbaji wadogo wadogo Tanzania, naomba ifike Lindi iwasaidie wananchi wa Lindi ili waweze na wao kunufaika kidogo.

Mheshimiwa Spika, lingine madini ya chumvi, madini ya chumvi yasifananishwe na madini ya vito au madini mbalimbali kama dhahabu, kwa sababu chumvi kama chumvi ambayo inachimbwa Mikoa yote ya Pwani ni chakula. Sasa tunaomba wakulima hawa wa chumvi waweze kusaidiwa kwa sababu wanapata shida sana kwanza hawana soko. Pili, wanatozwa bei

kubwa sana ya ushuru. Sasa hivi haijulikani huyu mkulima wa chumvi anaenda katika ofisi ya madini au ofisi ya kilimo au ofisi ya ardhi yaani yupo yupo tu. Tunaomba sana waliangalie suala la wakulima wa chumvi itamkwe kabisa wapo katika Wizara gani, wawajibike katika Wizara gani? Kwa sababu huku wanaitwa ardhi wamekata mikoko, huku wanaitwa Ofisi ya Madini leta fedha, sasa shughuli zimekuwa nyingi mpaka watu hawaelewi. Tunaomba shughuli zote za madini ziwekwe pamoja, madini ya chumvi ili tujue sasa inahusika na Wizara gani badala ya kuitwa huku na kule.

Vilevile watafutiwe soko, chumvi sasa hivi haina soko, imekaa tu kwenye *godown* Mtwara, Lindi, Tanga na wapi huko naomba sana muwatafutie soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, madini hayo hayo ya chumvi inabidi kabla haujayauza uwe umeweka madini joto. Sasa madini joto haya yaliwekwa na Serikali ili wananchi waweze kula ndani ya mwili yao ili kusaidia kuondoa magonjwa mbalimbali. Sasa tunaomba sisi haya madini joto basi Serikali iwawezeshe wakulima wa chumvi ili waweze kuyapata bure au ipunguzwe bei ya madini joto. Kwa sababu bei sasa hivi ni aghali mno, haiwezi kununuliwa. Tunaomba mliangalie suala la madini joto na ushuru mbalimbali upunguzwe katika madini ya chumvi.

Mheshimiwa Spika, *TPDC: TPDC* walipewa uwezo wa kufanya kazi mbalimbali za gesi na kadhalika. Lakini vilevile walipewa kazi kwa ajili ya shughuli za umeme

vijijini. Sasa kwa nini hawafanyi hivyo au wanapata fedha kidogo? Kama walikabidhiwa shughuli za umeme vijijini basi Serikali iwawezeshe, waongezewe Bajeti yao ili wao waweze kuendeleza umeme vijijini. Tunaomba sana Serikali iwaangalie *TPDC* waweze kupewa msaada zaidi ili waendeleze umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, umeme wa *grid,* umeme ambao haupo katika *grid* kwa maana Mikoa ile ambayo haipo katika *grid* inakuwaje, kwa sababu mpaka sasa kuna Mikoa kadhaa ambayo haipo katika umeme wa *grid* Tanzania. Tunaomba sana hiyo Mikoa ninaijua ipo Kigoma, Rukwa, Ruvuma Kagera, Mtwara na Lindi wanatumia gharama kubwa sana kuweka mafuta kwenye *generator*. Tunaomba hapa baada ya kugundulika umeme wa gesi na wao waingizwe katika *grid*.

Mimi sikushangaa kwa nini Mkoa wa Lindi na Mtwara haupo katika umeme wa *grid* ni kwa sababu Lindi na Mtwara kuna gesi na hao wenzetu ni jirani zetu gesi imeonekana tatizo ni nini? Tunaomba sana mtusaidie ili na sisi tuweze kunufaika. Hilo lilikuwa kuhusu umeme wa *grid*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nimalizie moja tu kwamba, sheria ya marekebisho mpya ya Nishati, Ibara ya 4(39) ilielekeza kwamba bomba likipita katika kijiji fulani basi wananchi wale waweze kupatiwa umeme mpaka sasa sielewi bomba hili lililotoka Kilwa kwenda Dar es Salaam hivi vijiji vya katikati vimepatiwa umeme au bado nataka kupata jibu.

Kwa mfano, kuna Kilwa, kuna Jenga, Somanga, njia nne, Tingi, Nangukuru, Rufiji, Mkuranga na Songosongo penyewe. Tunataka kufahamu ni vijiji vingapi tayari vimepatiwa umeme na vingine ni vipi ambavyo ni bado na lini sasa hao watapatiwa umeme? Kwa sababu sheria ipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hilo lilikuwa la mwisho, nasema tena kwamba ninaunga mkono hoja mia kwa mia, mengine yote siwezi kuyarudia wenzangu wameyasema vya kutosha na imeeleweka. Sasa tunangoja tu tuelezwe wahalifu ni nani?

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mimi nimekwishachangia kwa maandishi, lakini nitasema machache ambayo nitayasema kwa msisitizo. La kwanza, linahusu madini mimi ninavyoona kuna udhaifu katika sera ya madini, kuna udhaifu katika sheria ya madini, na kuna udhaifu katika mikataba ya madini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Wizara lazima irejee hizo sera, sheria na mikataba. Kuna udhaifu hata katika kiwango cha kodi. Twende katika nchi nyingine kama Botswana, Zimbabwe, Guinea, Namibia na kadhalika tuangalie ni kiwango gani hasa ambacho wawekezaji wanatozwa. Maana hapa tunasikia ilikuwa asilimia tatu; sasa katika sheria ya mwaka 2010 wakapandisha kidogo ikawa asilimia nne, lakini je

hicho ndicho wawekezaji wanatozwa kule Botswana au Guinea? Kwa hiyo, inafaa tulifanyie kazi hilo.

Mheshimiwa Spika, nimesema kwamba kuna matatizo katika sera na sheria. Tatizo la kwanza linahusu utaratibu wa kugawa leseni za maeneo ya migodi. Toka mwanzo kabisa watu waliruhusiwa kuchukua maeneo kiasi wanachotaka. Sasa hivi ninavyoongea huko Bukombe, Bukombe nzima imeshachukuliwa. Nimesikia Mbunge wa Msalala amesema kwamba kule Kahama nako kumechukuliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, toka mwanzo kulikuwa na makosa yaliyofanyika. Maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo hayakutengwa. Hilo ndilo tatizo la msingi na hilo ndilo tatizo ambalo Wizara lazima ilishughulikie. Wakishalishughulikia hilo watakuwa wametatua tatizo kubwa sana, watakuwa wameondoa mgogoro ambao upo sasa hivi baina ya wachimbaji wakubwa na wachimbaji wadogo wadogo na pia watakuwa wameipatia sifa Serikali yao kwamba imetatua mgogoro mkubwa. Lakini hali ilivyo sasa kuna mgogoro mkubwa huko Bukombe.

Mheshimiwa Spika, kuna makundi ambayo yameungana, yakaunda ushirika, yamekwenda kuomba leseni yakaambiwa kwamba hayo maeneo yameshachukuliwa. Sasa hivi wanahangaika wananipigia simu, wanasema Mbunge wetu tufanye nini? Pia kuna kundi lingine moja linaitwa Mkombozi lilipeleka maombi ya kupata leseni, likapewa eneo

ambalo liko kwenye Ziwa Victoria, yaani mambo ya ajabu sana yanafanyika katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ndugu yangu Profesa bado ana kazi kubwa sana. Wizara hii imejaa ufisadi, imejaa ujanja ujanja. Sisi ambao tunakaa kwenye maeneo ya madini hayo, tunafahamu hilo na wananchi kule wanafahamu. Kwa hiyo, naomba kama ameanza hivi na watu wanamsifia sawa na mimi namsifia, amefanya kazi nzuri na aendelee hivyo, lakini bado changamoto ni nyingi.

Mheshimiwa Spika, kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri, kwenye ukurasa wa 91, amesema kwamba: "Natoa rai kuwa Serikali haitasita kufuta mikataba kwa Kampuni zitakazoshindwa kutekeleza mpango kazi kwa muda uliopangwa kwa mujibu wa sheria". Naomba atoe agizo sio rai liwe ni agizo, kwa sababu hizi kauli za rai za kubembeleza bembeleza hazitatufikisha kule tunakotaka kwenda na ndizo zilizotufikisha hapa tulipofika.

## TAARIFA

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpa taarifa baba yangu Professa Kahigi, Wizara hii imeacha kubembeleza na ndiyo maana wanapigwa vita kwa mambo ambayo wanayafanya. Kwa hiyo, hawabembelezi tena wanafuata taratibu, wameziba mianya ya wala rushwa na ndiyo maana tunakwenda nao sambamba na ndio maana wanapigwa vita. Kwa hiyo, mambo ya kubembeleza walishaacha.

**SPIKA:** Profesa Kahigi naomba uendelee.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Taarifa hiyo…

**SPIKA:** Nimesema endelea tu, achana na hiyo, endelea.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa taarifa, lakini sidhani kama imeongeza chochote nilichokuwa nasema.

Mheshimiwa Spika, nimeshamsifu kwa hatua ambazo amechukua, lakini ninachotaka ni kwamba, achukue hatua zaidi kwa sababu kusema kwamba ameziba mianya ya rushwa sidhani kama amefanya hivyo, rushwa ni kitu kigumu sana kukishughulikia. Mifano, iko mingi hapa duniani sitaki kuitoa. Mimi naendelea na mazungumzo yangu.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 106, namsifu Profesa anasema hivi, anatoa rai tena: "Kuwa migodi yote ianze kulipa kodi ya mapato bila ya kuleta visingizio." Naomba asitoe rai, atoe agizo na ni vizuri, anapokwenda huko mbele anaagiza katika ukurasa unaofuata. Ni kwamba ule ukurasa wenye rai haukuwa na sababu yoyote kwa sababu huku mbele anaagiza na ni hatua sahihi sasa hivi aagize na asimamie, kwa sababu tatizo kubwa ni usimamizi.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie nishati. Nishati kama sekta ya madini pia imegubikwa na tuhuma nyingi sana za rushwa na tunampongeza na

wenzake kwa jinsi walivyolishughulikia hili ambalo limekuwa likizungumzwa hapa Bungeni. Sitaki kuzungumza zaidi kuhusu hilo, lakini ni kwamba kushughulikia kitu kidogo sio kwamba umeziba nyufa kama anavyosema Mheshimiwa binti yangu pale, hapana. Hiki ni kitu kidogo tu, rushwa ni kitu kikubwa; ukiondoa tu pingili moja, ni kwamba hujaimaliza hiyo rushwa.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kuongelea ni kwamba, watu hapa Bungeni walikuwa wakililia umeme katika maeneo yao na mimi nimekuwa ni mmojawao kwa sababu Bukombe kwa miaka 50 toka tupate uhuru haijawa na umeme mpaka leo. Angalau nashukuru Serikali kwamba kuna mpango wa kupeleka umeme Bukombe na barua nimeshapata kutoka kwa Naibu Waziri anayeshughulikia Nishati Mheshimiwa Simbachawene.

Mheshimiwa Spika, lakini tunachoomba ratiba itekelezwe kama ilivyopangwa maana Bukombe wamesubiri sana umeme kwa muda mrefu na ninavyodhani sababu mojawapo kwa nini Bukombe iko nyuma kimaendeleo, ni kwa sababu haijawa na umeme katika kipindi chote cha miaka 50 toka tupate uhuru. Tunaomba hiyo ratiba itekelezwe.

Mheshimiwa Spika, halafu pili, vile vijiji ambavyo vinapitiwa na hizo nguzo, naomba vyenyewe viteremshiwe umeme na hasa katika maeneo ya zahanati, shule za sekondari na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo ningependa kuzungumzia kuhusu umeme ni kwamba, mwaka jana katika bajeti kulikuwa na miradi ambayo iliahidiwa na Serikali na kulikuwa na Mradi wa Taa za Mwanga Bora Vijijini ambao ulikuwa utekelezwe Bukombe, Kahama, Biharamulo na Chato. Swali, mradi huu umefikia wapi katika utekelezaji wake kwa sababu hatujauona na wala hatujausikia tena toka wakati huo. Kuna mradi wa *Tanzania Affordable Rural Electrification Plan* ambao ulikuwa utekelezwe Bukombe na Kibondo. Mradi huo umefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, nakushukuru kwa kunipatia hii nafasi, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Josephat Kandege na Mheshimiwa Yusuph Abdallah Nassir ajiandae.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hoja iliyo mbele yetu. Awali ya yote naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kwa namna ambavyo ameonesha Watanzania tukiamua tunaweza kwa dhati na hasa pale ambapo tukiamua kusimamia haki. Pia naomba niwapongeze Manaibu Waziri, Mheshimiwa George Simbachawene pamoja na ndugu yangu Masele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwapongeza, naomba nijielekeze katika mambo machache, kwa sababu kimsingi mengi yameshasemwa na

nisingependa nianze kurudia yale ambayo yalishasemwa.

Mheshimiwa Spika, ukipitia hotuba yake inaonesha nuru mpya kwa Tanzania, inawezekana tukiamua. Lakini pia ameonesha jinsi ambavyo ile mikoa ambayo iko pembezoni inaweza ikafunguka kwa kuhakikisha kwamba gridi ya Taifa inawafikia. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri ahakikishe kwamba ule umeme wa kutoka Nyakanazi kwenda Kigoma, Kigoma kwenda Katavi, Katavi/Sumbawanga, Sumbawanga/Tunduma, Tunduma/Njombe Makambako kule kwa Mheshimiwa Spika, halafu narudi Iringa maana yake ni nini? Kwa ajili ya wawekezaji tutakuwa tumefungua mikoa yote hiyo na uwekezaji ambao tunatarajia kwa ajili ya maendeleo ya nchi utawezekana.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nilikuwa napitia kwa haraka haraka, bahati nzuri Profesa amechora mpaka ramani kuonesha sehemu ambako miradi inatekelezwa. Namwomba ajaribu kurudia, atazame sehemu zipi ambazo zinaonesha kwamba bado hazijapelekewa msukumo wa kutosha. Siku zote nilikuwa nikisema kwamba, ni vizuri Tanzania tukaendelea kwa pamoja, ile biashara kwamba sehemu zingine bado zionekane Profesa usikubaliane na hii, wote twende kwa pamoja, maendeleo yawe kwa Watanzania wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, pia nimepitia nimekuta kuna sehemu ambako Mheshimiwa anakiri kabisa kwamba, kuna vyanzo vingine vya umeme ambavyo lazima

tuvitumie na kila nikipata nafasi nitapiga kelele kweli kweli kwa sababu najua vyanzo hivi na Profesa naye anajua makaa ya mawe ni chanzo ambacho ni rahisi sana katika kuzalisha nishati hii.

Mheshimiwa Spika, ukienda kule Rukwa kuna chanzo kile cha Namwele ambacho yupo Mtanzania mzalendo, yupo tayari kuzalisha anachotaka ni *guarantee* kwamba *TANESCO* watanunua umeme huo na kuingiza kwenye *grid* ya Taifa. Kwa hiyo, ni vizuri tukawaunga mkono Watanzania wazalendo wenye nia thabiti ya kuhakikisha kwamba nchi hii tunaendelea.

Mheshimiwa Spika, siku mbili tatu naamini ikiwezekana kwa Mheshimiwa Waziri kama siku sita hakupata usingizi. Hakupata usingizi kwa sababu ya kile ambacho kilikuwa kikiendelea hapa. Lakini bado ukifuatilia hawa ambao walikuwa wanataka kumkosesha usingizi ni wale ambao siku zote wamekuwa wakisema posho hawataki, kumbe wana posho nzito wanazozitaka na sisi wengine wote ni mashahidi. Hatuna posho nzito humu na ndiyo maana tumekuwa tukihangaika tupate posho hiyo ndogo kwa sababu ndiyo halali. Watu wamekuwa wakisema, lakini wamejipambanua kwamba waadilifu, lakini Mwenyezi Mungu akitaka kukuangaza unaonekana dhahiri, huyu muadilifu kweli huyu, nyie mashahidi. Nadhani ujumbe utakuwa umefika kwa uzito nilioutarajia.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kuhusiana na urani. Kuna maneno mengi sana yamesemwa na

inawezekana ni katika wale wenye nia mbaya kuhakikisha kwamba Tanzania tunarudi nyuma badala ya kusonga mbele. Mtu akikwambia kuhusiana na hadithi ya urani utaona kama jambo baya kweli kweli. Kwenye Kamati yangu nimepata nafasi, nimetembelea kule Namtumbo. Ukiambiwa kwamba eti ni madini hatari kama vile ukisogelewa tayari yatalipuka, si sahihi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba ndugu Wabunge kwa ujumla wetu naomba tuunge mkono, tuhakikishe kwamba uchimbaji wa urani kwa ajili ya manufaa ya Taifa hili unafanyika na tusije tukaanza kupigana vita wenyewe kwa wenyewe. Ni Mwenyezi Mungu ametujalia, tuna kila sababu ya kuhakikisha kwamba rasilimali hii tunaitumia kwa ajili ya manufaa ya Watanzania walio wengi na si kwa wachache.

Mheshimiwa Spika, nichangie kuhusiana na usambazaji wa umeme. Nimepitia katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri, ametaja sehemu kama mbili kwa Mkoa wa Rukwa na hasa Jimbo la Kalambo. Napeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya na Kasanga basi. Lakini ukija kutazama sehemu zingine naanza kusema ni hii Tanzania ambayo bado tunaondoka kwa pamoja, stahili hii ipo au haipo. Kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Waziri, bado inawezekana huu sio msahafu hebu watazame namna ambavyo watapeleka miradi ya kutosha kwa mikoa hii ambayo ilikuwa imeachwa nyuma na sisi tunataka tuinuke, *we are sleeping quite for a long,* ni wajibu wetu, ni hakika tutasimama, hebu tupeni uwezo. Msije mkatushika mikono halafu mkasema tunaendelea haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, kwa jirani yangu Mheshimiwa Mipata pale, Makao Makuu ya Jimbo Mheshimiwa Mbunge hana umeme na wala siioni kama imeandikwa sehemu yoyote. Haiwezekani Mheshimiwa Profesa ni vizuri akakaa tena akatazama sehemu zipi ambazo zinaonekana kuwa bado hazijapewa hizo nafasi, fursa hii tuitumie na tufaidike na namna ambavyo ameturahisishia ameshusha bei ya kuunganisha umeme.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana kwa sababu mara ya mwisho nilisema hapa kwamba, hivi leo sisi tunashindwa kuunganisha umeme baada ya miaka miwili bei ya kuunganisha umeme imepanda, tunataka mwananchi alipie kiwango cha juu, kosa lake nini ambalo linamsababisha mpaka aje alipie bei kubwa? Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kuwa ameliona kosa hili. Naamini ungekuwa utaratibu mzuri, tukiamua kwamba mwananchi kama inawezekana akaweka fedha leo kwa kiwango cha leo, abaki anaidai *TANESCO* kupeleka umeme. Kwa hiyo, ile hadithi kwamba itafika kipindi bei ya umeme itapanda isiwepo. Ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kwamba huduma inatufikia sisi wote.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kutambua kwamba tukitegemea chanzo kimoja hatuwezi kufika. Ni wajibu wa Wizara kuendelea kutafiti vyanzo vingine. Tanzania tuna vyanzo vingi sana na tuutumie umeme kama biashara ya kuweza kuuza baada ya kwamba tumeshajitosheleza sisi wenyewe. Kwa hiyo, wataalam

waendelee kutafiti vyanzo viko vingi. Pale Kalambo *Falls* maporomoko ya pili Afrika, wengi hawajui. Ukienda pale *its amazing, you cannot imagine.* Lakini tumeitumiaje fursa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atume wataalam wake wakatazame kama kuna uwezekano wa kufua umeme, pale utapata mwingi sana kwa ajili ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hoja kwa mara nyingine na nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Msemaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Yussuph Abdallah Nassir.

**MHE. YUSUPH A. NASSIR:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, sikuwa na uhakika kama ningepata fursa ya kuchangia leo, lakini niishukuru meza yako kwa utaratibu ulioutumia. Kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa siku hii ya leo. Nitumie fursa hii pia kuwatakia funga njema wale ambao hatujaonana, lakini pia niwashukuru Wanakorogwe Mjini.

Mheshimiwa Spika, kipindi cha wiki mbili zilizopita tumekuwa tuna kazi kubwa kuhusiana na Kamati ile ya Kisekta ya Nishati na Madini kuangalia tasnia nzima ya Wizara hii na kwa kuiangalia kwa dhati kabisa bila unafiki, bila ya *influence* na hata bila ya kushawishiwa kwa namna yoyote ile. Tulifanya kazi kubwa sisi wengine tuliobaki wakati Wajumbe wengine wakiwa China kwa safari ya kikazi. Hotuba ya Kamati ya Nishati na Madini tuliifanyia kazi na tukairidhia wote, ni bahati mbaya mengi yaliyoandikwa mle ndani hayakupata

kusomwa hadharani, lakini kama ambavyo nilimshauri Mwenyekiti wa Kamati akufahamishe kwamba hotuba yake iingie kama ilivyo.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii pia kuupongeza uongozi mpya wa Wizara ya Nishati na Madini. Nimpongeze Katibu Mkuu aliyekaimu wakati wa *turbulence* ya kipindi kilichopita na hatimaye akapata *confirmation* ya kuwa Katibu Mkuu sasa. Nichukue fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Manaibu wake, lakini nataka niweke msisitizo na nitakuwa na upendeleo hasa mdogo wangu Stephen Maselle kwa kazi kubwa na umakini alioufanya wa kuweza kutudhihirishia sisi ndani ya Kamati kuhusiana na yale yalikuwa yakiendelea.

Mheshimiwa Spika, tulipata kukaa vikao vingi, si vema nikayasema yale yaliyojiri kwenye vikao. Lakini aliyesikia kasikia na mkubwa amekanyika. Inawezekana wengi tukafikiria utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ni kuimba *iyena iyena*. Wakati wa *iyena iyena* umekwisha, sasa ni wakati wa kuchapa kazi na kuangalia misingi ya utendaji kazi iliyokuwa sahihi. Tuache watu waimbe *iyena iyena* kwa nyakati zilizokuwa sawa, za uchaguzi na kampeni, lakini sasa tuchape kazi. Mheshimiwa Waziri, Manaibu pamoja na Katibu Mkuu nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nijielekeze katika maeneo yanayohusiana na mafuta. Katika kipindi cha Januari mpaka sasa Watanzania walipata bahati mbaya ya kupata nishati ya mafuta kwenye vyombo vyao vya usafiri ambavyo kwa kiasi fulani hayakuwa ya viwango

vile ambavyo nchi ilielekeza. Kukawa na vuta nikuvute baina ya wafanyabiashara wadogo, wafanyabiashara wakubwa na hata na mwagizaji. Lakini tukajiuliza sisi kama Kamati, nafasi ya mdhibiti iko wapi? Sasa wakati Mheshimiwa Mwenyekiti alipokuwa akisoma hotuba yetu alishindwa kwa sababu ya wakati kuzungumzia yale yaliyojiri katika malumbano yaliyokuwa yakitokea baina ya Bodi ya waagizaji mafuta pamoja na Mamlaka inayosimamia udhibiti kwa maana ya *EWURA*.

Mheshimiwa Spika, kwa hesabu za haraka haraka, inawezekana kukawa kuna *wind fall profit* kubwa ambayo aidha mwagizaji au msambazaji ameipata. Ni vema basi tutumie fursa hii kwa kuangalia zile *import ratios* na *standard* yetu ya mafuta, basi tuangalie ni kodi kiasi gani ambayo tutaweza kuipata ili angalau wananchi waipate ile nafuu kwa kutumia mlango mwingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka nijikite kwenye suala la gesi. Tumewekeza kiasi cha rasilimali gesi tulichonacho ni kikubwa, uwekezaji umeanza kujitokeza na kwa mujibu wa taarifa na hotuba ya Mheshimiwa Waziri imetueleza wazi kabisa, umiliki wa bomba la gesi kutoka Mtwara mpaka Dar es Salaam na kuelekea litakakoelekea litakuwa chini ya Shirika la Maendeleo ya Petroli. Tuipongeze sana Wizara pamoja na taasisi hii. Lakini kubwa kwenye hotuba yake hakuelezea pale ambapo bomba hili litakapofanya kazi *TPDC* ni taasisi kubwa je, tumeishauri ianzishe kampuni tanzu?

Mheshimiwa Spika, nakumbuka kuna mahali wamezungumzia cha kuwepo kwa *GASCO*, basi kwa nini kuanzia sasa tusiipe uwezo ile *GASCO* tukaanza sasa kuwapa vijana wa Kitanzania fursa ya kuanza kuajiriwa kule, tukaanza sasa kuondoa lile kundi la tukale wapi pale Mtwara kwa kuwafunza kazi ndogondogo angalau kwa kupitia kile chuo cha *VETA* pale Mtwara, hata za kupita *red oxide* kwenye ma-*pipe* haya, washiriki hata kazi za kufunga *pig* kwa sababu ni kazi zinazohitaji ujuzi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, gesi tumekuwa tukisema inaweza ikawa ni baraka au laana. Tumeshuhudia *resources* na kwenye nchi nyingi kama Nigeria, Ogon Land, tumeshuhudia pia vita vinavyoendelea kule DRC Congo vyote vinahusiana na rasilimali na kwa sababu tuna matatizo ya kimpaka pale. Mashariki tuna mpaka wa bahari na kusini tuna mpaka wa mto. Jambo lolote ambalo linaweza kutokea Msimbati au Mnazi Bay ni rahisi wale wafanya vurugu wakavuka mto na wakaenda upande wa pili. Ni vema sasa uwekezaji huu tuupe sura mpya ya ulinzi na usalama wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ipo haja ya kuwa na naomba nitumie neno kachero, tuwe na makachero wengi sana kwenye maeneo haya ya kusini na tuwe na makachero wengi sana kwenye maeneo haya ya gesi.

**SPIKA:** Ni kengele ya pili, ahsante sana.

**MHE. YUSUPH A. NASSIR**: Mheshimiwa Spika, hiyo ni kengele ya kwanza!

**SPIKA:** Basi malizia dakika hizo mbili.

**MHE. YUSUPH A. NASSIR**: Mheshimiwa Spika ahsante. Suala la ulinzi na usalama halitakuwa na mjadala. Lakini kadhalika pia ni kwa mara ya kwanza nimeweza kushuhudia muungano wa Vyama Visivyo vya Kiserikali vingi ambavyo sasa vinaelekeza nguvu zake kusini. Tunajua Vyama Visivyo vya Kiserikali umuhimu wake kwa jamii zetu, lakini ni vyema mtaala mahususi uwekwe na Serikali au hata Sheria itungwe na Bunge letu. Kwamba vyama vitakavyojihusisha na uchochezi katika maeneo ambayo tuna rasilimali basi vipigwe marufuku na hata ikiwezekana viongozi wake wafungwe.

Nisingependa kuona Wamatumbi kule Mtwara wanashika pinde na mishale kwa ajili ya kuwamaliza wenzao au wawekezaji ambao tunahangaika nao halafu ifikie mahali bomba lipigwe pancha, hatutakuwa tumeitendea haki nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niguse kidogo suala la umeme vijijini. Katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa saba na wa nane amelizungumzia sana. Ameeleza wazi kabisa ni asilimia 6.5 ya Watanzania walioko vijijini ndiyo wanaopata umeme wakati wakazi wa vijijini, Tanzania nzima ni asilimia 75. Kama tulivyosema anatekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi, basi aende kwa mchakamchaka ili kuhakikisha angalau asilimia 26 inafikiwa kabla ya 2015.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, nisipoteze muda mwingi, naunga mkono hoja hii. Nawapongeza sana viongozi na watendaji wakuu wa Wizara. Naomba kaka asafishe tutamwombea aongeze idadi ya wafanyakazi kupunguza ombwe lililopo la watendaji ndani ya Wizara yake na wale tunaokuunga mkono kwa dhati tutaendelea kukuunga mkono ndani ya Kamati ya kisekta kwa maana ya Chama ndani ya Bunge na hata ile Kamati ya Bunge ambayo inasimamia Wizara yako.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama ilivyo ada wote mngependa kuzungumza na ningependa kuwapa nafasi, lakini kila kitu sharti kifikie mwisho. Mpaka sasa hivi waliochangia mara mbili wamebaki karibu 36, waliochangia mara tatu na hawakufikiwa ni 15 na aliyechangia mara nne ni mmoja tu. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba wapo wengine wangeachwa tu.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja na nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kwa uadilifu wake mkubwa na umakini mkubwa anaoufanya na ambao ameuonesha katika kipindi hiki kufupi cha uongozi wake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niende katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri

wa Nishati na Madini ukurasa wa 57, Mheshimiwa Waziri ametamka kwamba madini ya *Uranium* yanapatikana maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Mto Mkuyu, ulioko Wilaya ya Liwale, Namtumbo na Tunduru. Ukurasa wa 136 jedwali linaonesha kwamba Mkuju *Uranium project* iko Wilaya ya Namtumbo peke yake.

Mheshimiwa Spika, naomba binafsi kujiridhisha, je, ni kweli *project* hii ya Mkuju *Uranium Project,* Wilaya ya Liwale na Tunduru haihusiki? Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kutuonesha mpaka au mwisho wa eneo hilo la Mkuju *Project* ni wapi ili nasi Liwale tujiridhishe kwamba hatumo? Kumeshaanza kutokea malalamiko katika Wilaya ya Liwale. Hata Mheshimiwa Waziri hataweza kutoa jibu leo, naomba nimtafute kwa wakati mwingine ili niweze kupata majibu ya utata huu.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kuipongeza Serikali kwa kupunguza gharama za kuunganisha umeme kwa wateja wadogo wadogo, wakati na wateja wakubwa. Ninachoomba kwa Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini ni kwamba, punguzo hili la gharama za kuunganisha umeme, liende sambamba na upatikanaji wa vifaa vya kufanyia kazi hiyo, kama vile nguzo, nyaya za umeme, vikombe, *transformers* na kadhalika kwa sababu kumekuwa na tatizo sana la upatikanaji wa vifaa hivyo na hivyo hulifanya zoezi la kuwapatia wananchi wanaokusudiwa kupatikana umeme kukwama.

Mheshimiwa Spika nimeshuhudia tatizo la upatikanaji wa nguzo, nyaya za umeme, vikombe na kadhalika. Katika Wilaya ya Liwale na mara nyingi

niliwasiliana na wafanyakazi wa *TANESCO* bila mafanikio. Wilaya ya Liwale ina wateja wengi sana kwa sasa ambao hawana umeme na wanataka kuunganishiwa umeme lakini kuna tatizo hilo la njaa. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri alishughulikie na hili.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niongelee suala la kuwaendeleza wachimbaji wadogo wadogo wa madini. Wilaya ya Liwale ina fursa kubwa sana ya madini na katika Mkoa wa Mtwara na Lindi, Wilaya ya Liwale ni Wilaya pekee ambayo ina aina ya madini nyingi na kwa wingi na katika maeneo ambayo yanaonekana kuwa na madini, tayari kuna vitalu vya watafiti na wachimbaji mbalimbali wakubwa na vinaonekana kuwa na leseni za utafiti na uchimbaji. Sasa namwuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati, wachimbaji hawa wadogo wadogo ni maeneo gani watatengewa ndani ya Wilaya hiyo? Kama yapo maeneo bado hayana leseni za utafiti na uchimbaji, naomba Mheshimiwa Waziri atupe taarifa ili eneo hilo litengwe kwa ajili ya wachimbaji hawa wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, ni muda mrefu nimeomba kuwa na Ofisi Ndogo ya Madini Wilayani Liwale, wananchi wale wanateseka sana, kushughulikia masuala yao ya leseni, uuzaji wa madini yao na kadhalika. Tunaomba sana tupate Ofisi ya Madini, Wilaya ya Liwale. Kwa sasa Ofisi za Madini ziko Mtwara na Tunduru na kumekuwa na urasimu mkubwa sana katika Ofisi ya Madini Mtwara, katika kuwashughulikia wachimbaji hawa wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji hawa wadogo wadogo wana matatizo mengi ikiwa ni pamoja na kucheleweshwa leseni zao na *documents* nyinginezo, lakini pamoja na kuomba tupatiwe Ofisi Ndogo ya Madini ndani ya Wilaya ya Liwale ili na sisi tupunguziwe adha ya kushughulikiwa matatizo yetu, namuomba Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini aiangalie sana Ofisi ya Madini Mtwara kuna matatizo pale, ni kwa nini leseni zinachelewa? Ni kwa nini Ofisi hii ina-*facilitate* kuwanyang'anya wachimbaji wadogo wadogo maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie sasa masuala ya gesi. Gesi inatoka Mkoa wa Lindi na Mtwara na gesi hiyo sasa inachimbwa na kusafirishwa kuja Dar es Salaam kwa ajili ya uzalishaji wa umeme na matumizi mengine. Ni huruma sana na itakuwa ni uonevu mkubwa kama wananchi wa Mikoa hii ya Lindi na Mtwara, Wilaya zote za Mkoa wa Lindi na Mtwara hazifaidiki na matunda ya gesi hii.

Mheshimiwa Spika, Mikoa hiyo na Wilaya zake zote zinapaswa zifaidike na matunda ya gesi hiyo, ni aibu sana Wilaya yoyote ile ya Mkoa wa Lindi na Mtwara kukosa umeme na huku gesi ikisafirishwa kwenda Dar es Salaam, kuzalisha umeme na matumizi mengine huku ndani ya Mkoa wa Lindi kuna Wilaya ya Liwale ambayo haina umeme wa uhakika na ikiendelea kuhangaika na umeme wa *generators*, huku gesi ikitokea ndani ya Mkoa huo wa Lindi. Sio umeme tu

hata mazao na manufaa yoyote yanayotokana na gesi hiyo, Wilaya zote zinapaswa kufaidika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Spika, kwanza namwomba Mheshimiwa Waziri apokee pongezi zangu za dhati kabisa yeye mwenyewe, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara yake na Watendaji wake wote kwa ujumla. Kwa hotuba nzuri yenye kuleta matumaini makubwa ambayo yatapelekea kumaliza tatizo la mgao wa umeme na kuhamasisha Watanzania wengi waweze kuingiza umeme kwenye majumba yao kwa kupunguza gharama za kuingiza umeme majumbani, mijini na vijijini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi namwomba afanyie kazi watumishi wanaohujumu na wanaolalamikiwa kuhusika kwenye tuhuma mbalimbali ambazo zimethibitika wachukuliwe hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kuwafukuza kazi kabisa ili wasije wakakuingiza katika matatizo, kumbuka mficha maradhi kifo kitammaliza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Mheshimiwa Waziri kujitahidi kuweka mkakati mzuri na kupunguza gharama za kuingiza umeme, bado tatizo la kulipia nguzo inakuwa ngumu sana. *TANESCO* ni shirika linaloendesha shughuli zake kibiashara, kitendo cha kulipisha nguzo kinawafanya wakose wateja na hatimaye kupelekea shirika kufanya kazi kwa hasara. Ili biashara ichanganye ni kufutilia mbali gharama za kulipia nguzo za umeme. Pia nampongeza sana kwa

hotuba yake iliyopelekea nitambue ameguswa sana na matatizo ya Wachimbaji wadogo wadogo, kitendo cha kuamua kukutana nao na kuweka utaratibu endelevu wa kukutana kila mwaka naamini ni mwanzo mzuri sana. Namwomba aendelee na utaratibu huo.

Sambamba na hilo ajitahidi kuyafanyia kazi malalamiko atakayoyaona kuwa ni ya msingi na yana ukweli, akifanya hivyo amani itadumu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, namshukuru Mheshimiwa Waziri, amenifariji sana katika hotuba yake pale uliposema hakutakuwepo tena na usiri katika mambo yote yatakayohusu Wizara yake. Naamini ataweka kila jambo bayana ikiwa ni pamoja na mikataba yote ya madini ambayo imekuwa ikilalamikiwa sana. Naamini kabisa akitekeleza kama alivyoahidi atamaliza manung'uniko na atakuwa na amani katika kutekeleza mipango ya Wizara yake na akiwa na amani hakika ufanisi utakuwepo kwani akiwa na amani ataipa akili yake motisha na ubunifu, atapata nafasi ya ubunifu na ubunifu utasaidia sana kuleta ufanisi katika kazi yake.

Mheshimiwa Spika, naomba punguzo la kuingiza umeme lianze mara moja, huo mwezi wa kwanza uko mbali sana na ajue kitendo cha kuweka hadi mwakani mwezi wa kwanza atakuwa amesimamisha biashara, wananchi wote wataona wasubiri hadi mwakani ndipo waombe kuingiziwa umeme hata wakiomba na kukubaliwa hawatakwenda kulipia hadi punguzo litakapoanza. Nafikiri ataona uzito wake miezi zaidi ya mitano (5) ni hasara kubwa sana kibiashara.

Mheshimiwa Spika, namtakia Mheshimiwa Waziri kila la kheri katika utendaji kazi na mafanikio mema, wameanza vizuri Mwenyezi Mungu awasaidie waendelee vizuri.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya, kuifanya Wizara hii ifikie matarajio ya Watanzania. Kwa namna maalum niupongeze uongozi mpya chini ya Waziri Muhongo kwa kufichua madudu yaliyokuwa yanaikwaza Wizara hii, tunategemea baada ya kudorora kwa muda mrefu Wizara hii sasa itakuwa na matumaini ya Watanzania, pamoja na matumaini hayo, naomba nichangie yafuatayo:-

Kwanza ni kuhusu madini, Tanzania imebarikiwa kuwa na madini mengi, lakini wingi wake haujawanufaisha Watanzania hata mahali pale panapochimbwa. Mirahaba inayotolewa bado haikidhi haja, Watanzania wanaobahatika kugundua madini hawaaachwi kuendelea kuchimba na kufaidi badala yake haraka haraka wanaletwa wachimbaji wakubwa wao wanabaki manamba. Hii ni dhuluma kubwa. Serikali lazima iwasaidie wagunduzi hawa kwa kuwapa mitaji na utaalam ili nao wafaidi matunda ya uhuru.

Pili ni umeme; umeme ni muhimu kwa maendeleo, bila ya umeme wa uhakika hatutakuwa na wawekezaji makini, lakini hata wajasiriamali wetu wa ndani

watakuwa wakikatishwa tamaa na umeme usiotabirika. Hivi sasa tumeanza kujenga imani baada ya tamko la Wizara kuwa hapatakuwa na mgao tena wa umeme. Tunawapongeza kwa hili, hata hivyo bei ya umeme bado ni kubwa hasa kwa Watanzania wa kipato cha chini na kipato cha kati. Naiomba Serikali ieleze ni namna gani bei ya umeme itapungua ili Watanzania wengi waweze kuunga umeme ikitiliwa maanani kuwa ni asilimia ndogo tu ya Watanzania wenye umeme majumbani kwao.

Tatu, nichangie kuhusu umeme Zanzibar; Zanzibar inapata umeme, lakini kwa muda mrefu sasa Zanzibar kuna mgao wa umeme kila siku kwa maeneo kwa muda wa saa moja moja. Je, ni kwa sababu gani Tanzania Bara hakuna mgao, lakini Zanzibar kuna mgao wa umeme? Naomba ufafanuzi.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na maoni na mapendekezo niliyowasilisha kupitia hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kutoa mchango ufuatao wa nyongeza hususan kuhusu masuala yanayohusu Jimbo la Ubungo:-

Mheshimiwa Spika, mosi, kuhusu maombi ya umeme ya wananchi wa Mtaa wa Msakuzi juu ya mradi wa umeme Kibamba Luguruni, Mtaa wa Msamakuzi *including* Maswet Mosha ambao eneo lao lilifanyiwa *survey* mwaka 2008 na kuahidiwa kusambaziwa umeme ambapo alama au vizingiti vya nguzo viliwekwa. Mpaka sasa mradi huo

haujatekelezwa au hata baada ya *TANESCO* ngazi zote husika kukumbushwa kwa miaka mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pili, maombi ya kupewa umeme kwa wananchi wa Goba Matosa ambapo umeme ulipelekwa katika shule ya Lilian Kibo *High School*. Hata hivyo, wakazi wa maeneo husika umeme umepita mbali yao. Pamoja na kupeleka barua za maombi *TANESCO* kuanzia Julai, 2007 (*GB/MT/U/VOL*.6/07) na Machi, 2010 (*KIN/S/RM/P/S*) na mwaka 2011 nilikabidhi vielelezo vyote kwa *TANESCO* Makao Makuu.

Mheshimiwa Spika, tatu, wananchi wa eneo la Mringwa katika Mtaa wa Temboni (kwa Msuguri) ambao Kaya zaidi ya 1,000 zinaishi gizani. Mnamo mwaka 2007 *TANESCO* ilituma wataalam na kufanya *Survey* katika eneo hilo na kuweka *pegs* maeneo ambayo nguzo zilipita. Baada ya *survey* hiyo wananchi waliahidiwa kuwa umeme umepangwa kufanywa na Kampuni binafsi, mradi unaojulikana kama Kimara-Msigwa.

Mheshimiwa Spika, nne, katika Kata ya Kwembe kuna mradi wa maji unaofadhiliwa na *BYC* pamoja na Taasisi zingine ambazo zinashindwa kufanya kazi kwa kuwa umeme ni mdogo. *TANESCO* wameshaandikiwa kwa ajili ya kuweka Transfoma kubwa zaidi. Hata hivyo, majibu yamekuwa mpaka tusubiri eneo hilo lipangiwe mradi. Ni muhimu *TANESCO* ikaharakisha kuwezesha wananchi wa eneo husika kupata maji kwa kuweka transfoma yenye kuwezesha pampu kubwa ya maji kufanya kazi. Aidha, Wizara ya Nishati na Madini ifahamu kuwa eneo husika linahitaji kuongezewa

nguvu kubwa ya umeme kwa kuwa kuna miradi mikubwa imeanza kutekelezwa katika eneo husika mfano ujenzi wa Chuo Kikuu Muhimbili *(MUHAS)* Kwembe na Mloganzila na ujenzi wa Mji wa Viungani *(satellite town)* na Luguruni Kibamba.

Mheshimiwa Spika, tano, Wizara imefikia hatua gani kwenye kusimamia upelekaji wa umeme katika miradi ya Maji ya King'ongo, Saranga, Kilungule na Mavurunza iliyotolewa na ahadi ya Rais Kikwete ya Mei, 2010. Izingatiwe kwamba mwaka 2011, niliomba Wizara ingilie kati kwa kuwa nguzo za umeme zilisambazwa, lakini miradi ilisimama kutokana na kile kilichoelezwa kuwa ni uhaba wa vifaa na kuchelewa kwa malipo ya Wakandarasi husika.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, hongereni sana, bajeti yetu imepita kiulaini na kwa kishindo kuliko ilivyotarajiwa. Mmeanza kwa huruma ya Mungu na kuihurumia nchi endeleeni hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, napendekeza yafuatayo:-

Kwanza, leteni mapendekezo ya mapitio ya Sheria ya Madini ili yafuatayo yafanyiwe kazi:-

(a) Kuondoa uwezekano wa uwepo wa *fiscal stability clauses"* kwenye mikataba ya madini;

(b) M-*introduce* kodi mpya za *windfall gains tax na ring fencing (for tax purposes)* ya miradi ya makampuni yanayochimba madini Tanzania;

*(c) Ku-charge capital gains* na kubana mianya yote ya *tax Avoidance strategies;*

(d) Ondoa *exemptions* kwenye sekta hii;

(e) Weka lazima ya *free carried interest* na pia ya *share* za Serikali kwenye kila mradi uliopo nchini Tanzania; na

(f) Badili au tafuteni namna nzuri ya kutwaa ardhi toka kwa wananchi bila kuwaacha maskini na pia bila fidia ama radhi nyingine.

Pili, hakikisheni mnawabana wawekezaji wote watekeleze maelezo ya Sheria ya Madini ya mwaka 2010, kuwa waweke *environmental rehabilitation bond* ili tuwe na uhakika kuwa watu wetu hawapati madhara yatokanayo na uharibifu wa mazingira utokanao na shughuli za uchimbaji wa madini

Mheshimiwa Spika, Tanzania *must go beyond EITI*, kwamba tutakapokuwa tunafanya marekebisho ya Sheria ya Madini (kama nilivyopendekeza hapo juu) (tuongeze *accountability* na *transparency* zaidi kwenye sekta za madini, gesi na mafuta, tuweke kipengele cha *publicity* kwenye mikataba (ili mchakato mzima wa kuondoa, kukabiliana na kusaini uwe wazi zaidi) pia wawekezaji wawe wanalazimika kisheria kufanya yafuatayo:-

- Ku-*publish* taarifa zao za mahesabu hapa ndani;

- Kuwekeza kwenye soko la hisa la ndani;

- Kuingiza fedha zao za mauzo yote hapa ndani na kufanya manunuzi yote kutokea ndani ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kama hawatokubali haya wasipewe maeneo ya kuwekeza miradi mipya waondoke na badala yake Serikali imiliki maeneo hayo mapya na kupitia *STAMICO* ambaye atamiliki hisa nyingi zaidi na atatafuta wabia kuongeza mtaji, ujuzi (*technology*) na *management*. Leo hii *Resolute* Tanzania *Limited* kwa mfano, imelipa *Cumulative taxes* zisizozidi TZS 150 bilioni toka imeingia Nzega na kuanza kuzalisha madini na kuuza. Uwekezaji wao ulikuwa TZS 58 bilioni tu na baadaye wali-*upgrade* mitambo yao kwa kuongeza TZS Bil 26 nyingine. Walichovuna wao ni zaidi ya *ounce* 1.99 milioni ya dhahabu yenye thamani (*conservative rates*) ya pesa isiyopungua trilioni mbili! Kweli tunaweza tukasema tunafaidika namna hii?

Mheshimiwa Spika, Serikali imepewa dhamana ya kuokoa nchi hii na wizi, dhuluma na ukandamizaji wa mabeberu na kusaidia kuipaisha nchi hii kiuchumi kwa faida ya ndugu zetu, okoeni nchi hii!

Mheshimiwa Spika, nashukuru na naunga mkono hoja.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Muhongo kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Wizara hii muhimu. However, *I saw it coming ever since he came back from the big post in* South Africa. Aidha nimpongeze kwa kazi nzuri anayofanya katika mazingira mengi tata aliyoyakuta najua ataweza kurekebisha. Ninawapongeza Mawaziri wako wawili, Mheshimiwa Simbachawene na Mheshimiwa Masele kwa kuteuliwa kuwa Manaibu Waziri. *My belief is given that team nothing will go asunder*.

Vile vile kama Maswi *is an asset*, napenda muelewe kwa muda mrefu utendaji ndani ya Wizara hiyo na Serikali ulikuwa hautekelezi ipasavyo au kutoa maamuzi ya ukweli na uadilifu, kama mnavyofanya sasa kwa uwazi na kwa maslahi ya wasema kweli tupo pamoja nanyi na Mungu yupo mbele yenu. Nataka kuchangia, lakini nimeona licha ya muda kuwa mchache, naweza kuja kuwaona na kupata majibu yote nitakayo, hivyo naomba mpokee hoja zangu chache.

Mheshimiwa Spika, Kilindi ni moja ya Wilaya ambapo zaidi ya asilimia 70 ni maeneo ya uchimbaji madini takribani miaka mitatu iliyopita, tuliahidiwa kuwa na Ofisi ya Madini ya Wilaya badala ya kutegemea Ofisi ya Handeni ambayo ni takriban kilomita 110 toka Makao Makuu. Pamekuwepo na matatizo mengi yakiwemo malalamiko mengi ambapo yangetatuliwa endapo tungekuwa na Ofisi Wilayani. Ofisi tunayo, ningeomba sana sasa muangalie uwezekano wa kukamilisha suala hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha zilizotengwa kwa ajili ya kuwaendeleza wachimbaji wadogo, naomba sana angalau awamu hii, basi wachimbaji wadogo wa kilindi wafikiriwe, nimekuwa nikifuatilia sana bila mafanikio, wengi wana maeneo lakini wanashindwa kwani hawana vifaa (zana) na uelewa stahiki. Naomba sana sana elimu ya Sheria ya Madini itaondoa dhana ya kufikiria kuibiwa kila mara na kupunguza kero ambazo hazina msingi.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze kwa *reshuffle* zilizofanywa na Katibu Mkuu za watumishi kumuacha mtumishi katika Ofisi ya Madini zaidi ya miaka mitano ni tatizo kubwa kwani anajenga mazingira kuwa yeye ndiye *Alpha* na *Omega* katika eneo husika. Inaumiza unapoona Afisa *(RM)* ana viwanja vya wachimbaji wadogo zaidi ya 80 kwa majina tofauti. Katika Ofisi ya Handeni napongeza sana mabadiliko, lakini bado yupo mmoja Elias wa muda mrefu ndiye anayesimamia maslahi ya hao waliopita. Ukiua mende kwenye nyumba maliza wote, ukibakiza kidogo watazaliana tena".

Mheshimiwa Spika, suala la umeme, nashukuru kuwa kupitia Umeme Vijijini *REA*, tulipata umeme hadi Makao Makuu ya Kilindi Songe. Naishukuru Serikali kwa niaba ya watu wa Kilindi kwa hilo. Umeme umepita kuelekea Makao Makuu, njiani transfoma hakuna ambapo nadhani pia wangenufaika na kazi hiyo nzuri ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, aidha Mashule hasa ya Sekondari, Zahanati na vituo vya Afya vingepata umeme, nimejitahidi kufuatilia tangu mwaka 2010, ahadi ni nyingi bila mafanikio, kila mara nimekuwa nikijibiwa kuwa transfoma zipo Mkoani, naomba nisaidiwe kwa hili ili vijiji vyangu vifaidike kwani:-

- Kukosa umeme kila mara kutokana na kuungua transfoma na vifaa mbalimbali, ni vyema sasa kuangalia ubora wa vifaa vinavyoletwa, aidha wengi wanatoa fedha kufungiwa umeme lakini vifaa hakuna.

- Niliahidiwa kuanzia mwaka 2012 umeme kuendelea toka Songe Makao Makuu hadi Gairo, Makao Mkuu ya Wilaya, vipi?

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Spika, ni jambo la faraja na la kutia moyo kuona Serikali yetu ina mipango kabambe ya kutandika bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam. Dhamira hiyo ni kuhakikisha kwamba mbali na kuunganisha umeme, lakini gesi hiyo itafikishwa majumbani na kutumika kwa matumizi ya kupikia.

Mheshimiwa Spika, hii itasaidia sana kwa kupunguza gharama za matumizi ya kuni na hasa mkaa, wazo hili vile vile litapelekea kunusuru mazingira yetu ambapo watu wengi hukata miti na kutengeneza mkaa kwa matumizi ya majumbani hongera kwa hilo, lakini vile vile ieleweke kuwa hiyo ni asilimia ndogo tu ya matumizi ya gesi majumbani ukilinganisha na ukubwa wa nchi yetu. Hivyo ni vyema katika miji mingine mikuu au hata vijijini nao wanaweza kufaidika

na mradi huu, ni dhahiri kuweka bomba na kusambaza nchi nzima ni gharama kubwa nmo.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, ni vyema Serikali ikatafuta njia mbadala nayo si nyingine ila kuuza gesi hii ikiwemo ndani ya majiko ya gesi au mitungi ya gesi. Hapa watafaidika watu wote wa nchi nzima, hivyo ni vyema Serikali ikaweka bei nafuu kwa majiko na mitungi hii ili watu hasa wa vipato vya chini waweze kumiliki au kununua mitungi hii na kuanza kutumika hadi vijijini na sio vibaya mitungi ikapunguzwa bei kwa asilimia 50 na gesi yenyewe kuwa bei chini. Vile vile mitungi hii ifikishwe hadi Zanzibar, kwani kutandikwa kwa bomba kwenda Zanzibar ni gharama kubwa ila nao wapate mitungi hii kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, hii italeta faraja na Serikali itaona faida zake katika suala zima la uhifadhi wa mazingira na hii itapelekea hata kuweza kutunza maeneo yenye vianzio vya maji kwa vile ukataji miti kiholela utapungua. Matumizi ya gesi ni bora kwa hizi *gas cylinder*, kwa kuwa utatumia moto kwa mujibu wa matumizi yako, unapika chakula kikishawiva unazima jiko lako pale pale, ila mkaa utaendelea kuteketea mara baada ya upishi wako kwa vile hauzimwi kama jiko la gesi.

Mheshimiwa Spika, mwisho tuwe makini na uvumbuzi wa *uranium* ni vyema tuwe makini na suala zima na uzito wa suala zima Kimataifa, sio vibaya ni utajiri ambao Mungu ametujalia, ila naona tuwe makini, ni bora tujikite na gesi kwanza hadi tujue tija yake. Nchi ipo, watu wapo na tuanze kusomesha

vijana wetu ili tuwe na wataalam wa kutosha na watayarishwe vyema na wao ndio watakaoweza kumudu uchimbaji wa *Uranium*. Hatuna wataalam wa kutosha kwa sasa, sio vibaya kwenda kidogo kidogo *is better to be sure than to be sorry*.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Wafanyakazi wote kwa kazi nzuri inayoleta matumaini, aidha hotuba ya Wizara imetengeneza njia ya matumaini kwa Taifa letu, naomba kusisitiza yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme, *transmission* ni muhimu, umeme ni nguzo muhimu katika Taifa kufikia nchi kuwa ya uchumi wa kati katika muda mfupi, nchi yetu ni kubwa na naona pamoja na kupata njia za uhakika kama vile kutumia gesi na makaa ya mawe, juhudi za kuzalishwa umeme lazima ziendane na kuimarisha *transmission*. Kinachoonekana uzalishaji uko upande mmoja *southern corridor* mpaka Dodoma, lakini mahitaji makubwa yako Kanda ya Ziwa. Nashauri mikakati ya *transmission* iwekwe wazi ili nasi tulio Kanda ya Ziwa tupate matumaini mapya. Nasisitiza jambo hili ukizingatia kazi na nia nzuri ya kufikisha umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme vijijini, napongeza *REA* kwa kazi nzuri inayofanywa hata Wilaya mpya yetu ya Itilima imekumbukwa na katika Jimbo langu vijiji vingi vimetajwa ingawa vimetajwa Bungeni, basi vingebaki katika *hansard*. Natumaini atakupa taarifa rasmi kwa Wabunge wote, hakika Jimbo langu nasisitiza umeme. Nywalushu-Nkoma

wapewe kipaumbele ili tupate *power* ya kuvuta maji kutoka bwawa la Nkoma, kwenda Kituo cha Afya Nywalushu ambacho kwa Wilaya mpya hii ya Itilima, hii ndio hospitali ya Wilaya mpya Itilima. Jambo hili linajulikana kwa Mheshimiwa Rais aliyezindua lile bwawa mwaka 2006, Mheshimiwa Waziri Mkuu pia katika ziara yake mwanzo wa mwaka huu alishuhudia umuhimu wa kuwa na umeme kwenye Kituo kipya cha Afya na kuwa na pampu ya maji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini, Tanzania tumetunukiwa madini mengi sana nchi nzima, nami ni mmoja wa wanakamati ya Bomani pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara Ndugu Maswi na changamoto katika *sector* hii ni nyingi na chanzo chake ni mtazamo hasi kwamba anayegundua madini yanakuwa yake *mineral right*. Mgunduzi asiruhusiwe kuinyang'anya nchi hayo madini kwa kisingizio analeta fedha ya kuyachimba, ni ukweli usiopingika kwamba gharama si mali ya mwekezaji bali ni mkopo. Dhamana yake ikiwa madini yetu *The mineral right deposit certificate* jambo hili ni sawa na kumpa mtu vyumba vyako aweke rehani mawe unachopata ni kiduchu. Mtazamo huu naomba upya na kila mwekezaji lazima atoe hisa si chini ya asilimia 50 kwa Serikali itakayoshikilia kwa niaba ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, urani ni madini yenye upekee maalum, maoni yangu ni kwamba, tumeharakisha mno kukubali kwani ichimbwe na kuhamishiwe nchi nyingine. Kwa nini tunawapa watu wengine *nuclear capability,* madini haya ni *defence material*. Nashauri

sera maalum itumiwe na tusichimbe sana, tusubiri Mataifa yanaelekea wapi katika madini haya.

Mheshimiwa Spika, pamekuwa na mtindo wa kukubali kutenga fedha lakini fedha haitolewi ni lazima, aidha, kisingizio kimekuwa fedha inatolewa kufuatana na mikataba ya ujenzi wa miundombinu ya umeme au gesi, mikataba au michakato ya ununuzi ikichelewa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa mwaka huo nazo zinachelewa na kwa kawaida muda wa bajeti ukiisha nazo fedha zinatoweka na kuanza tena katika mwaka wa bajeti. *And eventually we remain with unfunded or under funded projects*, matokeo ya utaratibu huu wa bajeti unafanya miradi mingi isitekelezwe kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, nashauri fedha yote iliyotolewa kwa mwaka husika ziwe *ring formed* na zitolewe kwa Wizara na ziwekwe kwa *deposit A/C* ya mradi au miradi. Tukifanya hivyo basi, miradi itakuwa *fully funded* katika uhai wote wa utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Spika, aidha, nashauri ukaguzi ufanyike kama migodi yote inachimbwa tu katika maeneo yaliyoruhusiwa, ni wazi kwamba uchimbaji wa chini ya ardhi siyo rahisi kuona kama *mining* inafanyika kwa eneo tu lile lililoruhusiwa na lina *license,* ikigundulika mwekezaji amevuka basi madini hayo yarudishwe kwa Watanzania au thamani ya fedha ya madini hayo ilipwe *with interest*.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Simiyu tu umepata *nickel* na uchimbaji karibu umeanza, lakini kuna utata

mkubwa juu ya watu waliokutwa na mradi huu. Kama inavyojulikana Wilaya ya Busega, Wilaya ya Bariadi na Itilima, mfano, Zanzui ina watu wengi sana na watu wana wasiwasi. Sheria inataka *resetlement* kabla ya kuchimba, tunaomba mipango ya kuwapa watu hawa makazi mapya na sisi Wabunge tuelezwe kiuwazi.

Mheshimiwa Spika, uongozi mpya wa Wizara hii, Mawaziri wote na Katibu Mkuu wanafanya kazi nzuri na nawapongeza na kuwaomba waendelee kwa ujasiri na kwa kujua kwamba Bunge letu litaunga mkono mafanikio katika Wizara hii muhimu, Mungu awabariki.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nashauri kwa kuwa tumefanikiwa kupata asilimia kubwa ya fedha za maendeleo ya ndani, basi fedha hizi zitolewe kwa wakati.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, nawapa hongera sana Mheshimiwa Waziri Mhongo, Naibu Mawaziri Simbachawene na Mheshimiwa Masele, pamoja na ndugu Maswi Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini kwa kazi nzuri mliyofanya kwa kipindi kifupi cha nyadhifa zenu. Naipongeza Serikali kwa kuzindua mradi wa bomba la gesi na kwa dhamira njema ya kumaliza mgao wa umeme.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri wanayoifanya naomba nichangie yafuatayo:-

(1) Serikali ifuatilie suala la bili bandia kwa maana ya bili kubwa kuliko matumizi;

(2) Wizara ishirikiane na *TBS* kudhibiti vifaa bandia vya umeme vinavyoingizwa nchini ili kuzuia hasara na majanga ya moto;

(3) Umeme unaosambazwa ulingane na uwezo wa mita kwani unapokuwa mdogo zaidi ya mita hauwaki kabisa au unakatikakatika; na

*(4) TANESCO* wakiitwa panapotokea hitilafu wafike mapema ili kuzuia maafa yasiwe yanatokea.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuwawezesha wachimbaji wadogo kuanzisha vituo vya kisasa vya kuchimba madini katika maeneo ya Rwamgasa-Geita, Londoni Manyoni na Pongwe:-

(a) Je, ni vigezo vipi vimetumika kuchagua maeneo hayo tu?

(b) Ni kwa nini vituo hivyo visiwepo maeneo yote yenye madini kwa mfano Mpanda?

Mheshimiwa Spika, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 8.9 kwa ajili ya kuwaendeleza wachimbaji wadogo wadogo ikiwa ni pamoja na kuwapa mikopo kwa mwaka 2012/2013 na je, ni lini na kwa utaratibu gani fedha hizo zitagawiwa?, Je fedha hizo zitagawiwa

kwa namna gani? Je, ni kwa maeneo yaliyotajwa tu kwa mfano, maeneo ya Nyakuguru, Goronga, Gibaso na Mogaviri, Kapalmsenga Mpanda, Ilagala, Ibaga na Mpambaa, Isenyela (Chunya) na Makanya (Same), ama ni kwa maeneo yote yenye machimbo Tanzania nzima?

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ya Mheshimwa Waziri, ukurasa 107, ameagiza Kampuni zote zilizochimba madini kwa miaka mitano na kuendelea, zianze kulipa kodi ya mapato bila kuleta visingizio? Je, agizo hilo linaanza lini? Je, mikataba na sheria hazipo mpaka makampuni hayo yawe na visingizio?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Naipongeza sana Serikali kwa kutupatia umeme wa Jenereta Makao Makuu ya Wilaya ya Ngorongoro-Loliondo. Ahadi ya Mheshimiwa Rais ya mwaka 2007 imetimia, naomba kufahamishwa yafuatayo:-

**-** Ni lini nguzo, nyaya na mita zitapelekwa Loliondo/Wasso ili kusambaza umeme huo?

**-** Nini matokeo ya utafiti wa maji ya Mto Pinyinyi katika kufua umeme, utafiti ambao ulifanywa zaidi ya miaka 10 iliyopita.

**-** Nini msimamo wa Serikali kuhusu uchimbaji na hatimaye ujenzi wa Kiwanda cha *Soda Ash* huko lake

Natron katika Kijiji cha Engaresero na bonde la Engaruka, Wilayani Monduli?

Mheshimiwa Spika, Mgodi wa Naan katika Kijiji cha Enguserogambu ulimilikishwa kwa mchimbaji wa kati *Jumbe and Partners* wa Mjini Arusha licha ya kwamba wagunduzi wa madini hayo (*spesertite*) ni wachimbaji wadogo wa Kijiji cha Enguserosambu-Loliondo. Leseni ya Jumbe *and Partners (PML)* itakwisha muda wake Disemba, 2012.

Mheshimiwa Spika, je, wachimbaji wadogo sasa watamilikishwa machimbo hayo?

**MHE. ENG. HAMAD YUSSUF MASAUNI:** Mheshimiwa Spika, nikiwa kama Mjumbe wa Bodi ya *Puma Energy*, nawapongeza sana kwa uamuzi wenu sahihi wa kuamua kuitumia Kampuni hii ambayo ni miliki ya Watanzania kwa asilimia 50. Nataka nikuhakikishie kuwa *Puma Energy* itatoa ushirikiano na ni fursa ambayo tumeshaiazimia kuitafuta kupitia kwenu. Hii ndiyo faida ya kuwa na Mbunge angalau mmoja kwenye Bodi za Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Spika, tahadhari ni kwamba ili kazi yao nzuri isiharibike wasimamie *TANESCO* ifanye yafuatayo:-

(i) Waimarishe *Transmission au Distribution network;*

(ii) Ongezeni *Access* hasa vijijini;

(iii) Punguzeni *losses* na ongezeni ufanisi;

(iv) *Diversification;* na

(v) *Intergrated water resources management kwenye catchment areas.*

Mheshimiwa Spika, kuhusu gesi nashauri yafuatayo:-

*(a) GU MP* na pia izingatie Zanzibar kwani bado gesi ni suala la Muungano;

(b) Gesi inufaishe watu;

(c) Viwanda (vianzishwe viwanda vizito); na

(d) Gesi iwe mbadala wa mafuta na ipelekwe mpaka vijijini watu watumie.

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri na Naibu Mawaziri kwa hotuba hii nzuri sana na kwa ujasiri waliouonesha kwa makusudi wa kuwaletea maendeleo Watanzania kwani bila ya umeme wa uhakika viwanda vidogo vya wananchi walipa kodi vitaendelea kusua sua.

Mheshimiwa Spika, bila umeme wa uhakika wawekezaji wa viwanda vikubwa hawatawapata na vijana wetu wataendelea kukosa ajira. Gesi itatuokoa kwa kuwa na umeme wa uhakika na Wizara itakaposimamia huu usambazaji wa mabomba ya gesi kuja Dar es Salaam basi iangalie na jinsi Mabomba haya yatakavyokwenda mpaka Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ndio jicho la maendeleo ya nchi yetu kwani bila ya viongozi imara kama hawa walioteuliwa na Mheshimiwa Rais basi Wizara hii haiwezi kwenda Mbele. Iko haja ya kuangaliwa watendaji kwa macho mawili ili wasije wakawakwamisha kwa utendaji wao mbovu tuliouzoea.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. DUSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuunga mkono hoja hii ya bajeti ya Wizara ya Nishati na madini. Aidha, napenda kumpongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri, pamoja na yeye nawapongeza Manaibu, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa kuandaa bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa sababu kubwa maalum, kwanza ni kwa upatikanaji wa umeme Wilayani Nanyumbu (Mangaka na Mtambaswala) ndani ya mwaka huu wa fedha 2012/2013. Naomba Wizara ihakikishe inatimiza ahadi hii bila kukosa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maeneo yaliyoainishwa kwenye barua hiyo naiomba Wizara ivipatie umeme vijijini ambamo umeme huo Mangaka hadi Mtambaswala ili kuchochea maendeleo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, tarehe 21 Julai kulifanyika uzinduzi wa ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam, naipongeza Wizara na Serikali kwa kubuni mradi huu mkubwa. Hata hivyo, inaonekana bado wengi wa wananchi wa Mikoa ya Mtwara na Lindi hawaelewi kwa nini mradi huu utekelezwe, wanaambiwa na Wanasiasa uchwara kuwa wanaporwa uchumi wao. Hivyo, naiomba Wizara kupitia vyombo vya habari magazeti na televisheni itoe elimu kwa wananchi wa maeneo haya ili wajue ni kwa nini mradi huu upo na wao watanufaika vipi, ukweli ni kwamba wananchi wameupokea kwa mtazamo hasi.

Mheshimiwa Spika, wakati wa masika na majira mengineyo, nguzo za umeme zimekuwa zinaanguka mara kwa mara, pengine ni nguzo zaidi ya tano au zaidi, hivyo kusababisha kero kubwa kwa wananchi. Naomba kadhia hii irekebishwe na nguzo zichimbiwe chini ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, kwanza naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Profesa Muhongo, Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri na wenye weledi wa hali ya juu kabisa. Pili, nampongeza kwa imani, uvumilivu na moyo wa kujitolea sana kiutendaji. Huu ni mfano wa kuigwa kwa maana hachoki na amekuwa mstari wa mbele katika kuliletea Taifa letu maendeleo kwa kipindi kifupi tangu kuteuliwa kwake, lakini siachi kuwapongeza Naibu Waziri Mheshimiwa George Simbachawene na Mheshimiwa Augustine Massele kwa uwezo mkubwa aliouonesha

kwa kipindi kifupi tu ambacho wameingia katika Wizara husika.

Mheshimiwa Spika, kama sote tunavyofahamu, Wizara hii ni kioo na roho ya uchumi wa nchi yetu katika nyanja za kiuchumi, majukumu yake ni mazito na yanahitaji umakini mkubwa sana katika utekelezaji. Ni heri tuwaunge mkono na kusaidiana nao katika kurahisisha utendaji wao. Pamoja na hotuba yao kubeba karibu kila kitu na kujibu hoja nyingi, napenda nami nitoe mchango wangu katika hotuba husika japo kwa uchache.

Mheshimiwa Spika, kama hotuba ya Waziri ilivyoonyesha uvumbuzi wa gesi asili nchini umekuwa ni mkubwa sana, hivyo naishauri Serikali iharakishe kuleta Bungeni Sera ya Gesi hatimaye Sheria na Kanuni, hii itasaidia sana kutoa mwongozo na namna bora ya usimamizi wa sekta hii muhimu kwa uchumi wa nchi yetu. Pamoja na yote nasisitiza sana umuhimu wa sheria hizi kuzingatia maslahi ya wananchi wa maeneo husika lakini Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, napendekeza pia sasa Wizara kupitia *TPDC* ihakikishe kuwa gesi inatumika kuinua sekta kama kilimo, viwanda na hata usafiri. Muda mrefu sasa tumekuwa tunaagiza kiasi kikubwa cha mbolea kutoka nje lakini imani yangu kuwa sasa tuwekeze vya kutosha katika Viwanda vya Mbolea katika Mikoa ya Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, Serikali iwekeze vya kutosha katika elimu kwa kuwapa kipaumbele vijana ambao

watakuwa tayari kushiriki katika fani za uchomeaji (*welding*), kuendesha mitambo, umeme na mitaala ya *IT* ili waweze kushiriki vema katika sekta hii adhimu. Kwa kuwa kwa kipindi cha miaka ya sabini na themanini Serikali iliwekeza sana kwa kuandaa wataalam na kuacha kuendelea kwa kipindi cha miaka ya tisini. Naishauri Serikali, wataalam wote wapewe mikataba maalum ili kuweza kuziba pengo kwa kipindi hiki ambacho tunaandaa wataalam wetu wengine. Kutokufanya hivyo ni kupoteza uwekezaji mkubwa na pia tutatoa fursa ya wataalam wote kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Gesi ni pana sana kiasi cha kusema ni mhimili mkubwa sana kwa uchumi wa nchi yetu. Naishauri Serikali itoe elimu ya kutosha kwa wananchi ili wapate kuelewa na kuepuka upotoshaji mkubwa unaofanywa na wasiopenda maendeleo, nashauri waandae hata majarida ambayo yatatoa elimu kwa umma.

Mheshimiwa Spika, Serikali ichukue hatua za haraka kuachana na utaratibu wa kukodi mitambo ya uzalishaji umeme na kununua yake, lakini pia miradi ya uzalishaji wa umeme kwa makaa ya mawe ipewe kipaumbele cha kutosha nchini ili *TANESCO* ijiendeshe kwa faida na kutoa unafuu kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ione umuhimu wa ushirikiano na nchi ya Trinidad and Tobago kwa kuwa ni wa kuenziwa na kuutilia maanani sana. Kwa kipindi kirefu Balozi wao ameomba kutambuliwa na hajapewa ithibati hii mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa naomba nikushukuru kwa kunipa miradi mingi ya umeme kwa vijiji katika Jimbo la Kilwa Kaskazini na kunipokelea maoni yangu kwa kuamini kuwa yatafanyiwa kazi stahiki. Nakutakia kila la heri na namwomba Mungu atulinde sote.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Waziri, Manaibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara na Mashirika na wakala chini ya Wizara kwa kazi yao nzuri ya kuandaa bajeti hii ya Wizara ya Nishati na Madini. Naomba nitoe ushauri wangu kwa Serikali katika mambo sita kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Sheria ya Madini ya mwaka 2010, taarifa ya Jaji Bomani kuhusu sekta ya Madini ilitusaidia kutayarisha Sheria ya Madini ya mwaka 2010, baadhi ya mambo mazuri katika Sheria mpya ya Madini ni pamoja na:-

- Kuongeza viwango vya mrabaha na unaotozwa kwenye *gross* badala ya *netback value*, tunashukuru Serikali imeweza kukamilisha mazungumzo na kuziwezesha Kampuni zote za madini zenye mikataba kuanza kulipa mrabaha kwa matakwa ya Sheria ya Madini ya mwaka 2010.

- Serikali kuwa mwekezaji kupitia *STAMICO* na kuweza kupata Hisa (*free carried interest* na hisa za

kununua) kwenye migodi. Serikali ianzishe mazungumzo na migodi iliyopo na itakayoanzishwa kama Kabanga *Nickel*, Dutwa *Nickel*, *ARMZ Uranium*, Panda *hill Pyrochloral* na mingine ili kukabiliana kuhusu *free carried interests* na hisa za kununua.

- Migodi kuweka hisa zake kwenye Soko la Mitaji Dar es Salaam ili wananchi waweze kununua. Makampuni yote yalazimishwe kuweka hisa zake kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam na wananchi na hasa Watanzania wenye uwezo wahamasishwe kununua hisa hizo ili wawe wawekezaji kwenye sekta hii muhimu.

- Serikali kuzilazimisha kampuni za uchimbaji madini nchini kununua huduma na vifaa vinavyopatikana nchini, ziandaliwe Kanuni na taratibu zitakazohakikisha kampuni hizi zinanunua bidhaa na huduma za ndani. Kampuni zihamasishwe kuanzisha miradi ya wananchi kuwasaidia kuweza kuzalisha bidhaa zenye ubora unaoweza kutumika migodini.

- Kutoa fidia, kuwajengea makazi na kuwahamisha wananchi wanapisha ujenzi wa migodi (*compensation, reallocation and resettlement*), Wizara ya Nishati na Madini kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi zirekebishe Sheria ya Ardhi ili iweze kutekeleza matakwa ya sheria ya madini inayoanzisha suala la fidia lisiwe tatizo tena.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutekeleza matakwa ya Sheria ya Madini ya mwaka 2010, ni vizuri pia Serikali ikakamilisha mapema marekebisho ya

Sheria ya Usonara na Sheria ya Baruti. Naiomba Serikali kutekeleza mambo hayo mapema ili kuhakikisha yanayotokana na sekta ya madini yanaongezeka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuimarisha usimamizi wa sekta ya madini nchini, sekta hii ni sekta muhimu sana ya uchumi nchini na inahitaji kuwa eneo la kipaumbele la Serikali ili kukuza uchumi wa Taifa kwa haraka. Kulingana na Sheria ya Madini ya mwaka 2010, Idara ya Madini ni msimamizi mkuu wa Sekta ya Madini lakini haipewi kipaumbele na Serikali katika kupata watumishi wa kutosha na bajeti ya kutosha. Kwa hiyo, naishauri Serikali ishughulikie mambo mawili yafuatayo:-

- Ifanye Idara ya Madini kuwa Idara inayojitegemea kibajeti kama ilivyo Jeshi la Polisi au Jeshi la Magereza, inahitaji kupewa *Vote* yake ili kwa kutumia mtandao wa Idara ya Madini ulioenea nchi nzima turahisishe usimamizi wa sekta ya madini. Kwa kufanya hivyo, bajeti ya Idara, vitendea kazi, maslahi ya wataalam na uwezo wa Idara kusimamia sekta ya madini vitaboreka; na

- Ianzishe mpango maalum wa kuajiri wataalam mbalimbali wanaohitajika kwenye Idara moja kwa moja kutoka vyuo vikuu kwa kipindi maalum, badala ya kuwatafuta wataalam hao kwenye soko. Mpango huu utajaza pengo la uhaba wa wataalam kwenye Idara ya Madini, kwa sasa nafahamu hali ya uhaba wa wataalam kwenye Idara ya Madini ni mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutunza dhahabu safi kwenye hazina ya Taifa; niliwahi kushauri na nashauri tena kuwa kutokana na bei ya dhahabu kuendelea kupanda kwenye soko la dunia karibu miaka 10 sasa na itaendelea kupanda na kutokana na ukweli kwamba ni madini ya dhahabu yanayowakilisha thamani ya fedha (sarafu) duniani ni wakati muafaka sasa nchi yetu kuanza kutunza dhahabu kwenye hazina ya nchi yetu ili kuweza kurekebisha thamani ya sarafu yetu inapoanguka.

Mheshimiwa Spika, Marekani, mifano ya nchi zinazotunza dhahabu kwa wingi katika hazina za nchi zake ni pamoja na tani 8,000; Ujerumani zaidi ya tani 3,000; Afrika Kusini zaidi ya tani 723 na Uingereza tani 300; Swaziland tani 1,300; *European Central Bank* tani 766. Yapo pia Mashirika ya Kimataifa kama Benki ya Dunia zaidi ya tani 34,000 na *IMF* zaidi ya tani 4,000. Mataifa haya na nchi hizi ni mifano mahsusi ya nchi zinazotumia dhahabu kujiwekea utajiri na kutunza thamani ya sarafu zao.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Wizara ya Nishati na Madini ishauriane na Wizara ya Fedha na Benki kuu kuanzisha mchakato huu wa kutunza dhahabu kwenye Benki Kuu ya Tanzania (sheria ya Benki Kuu inaruhusu kufanya hivyo). Hii itatuimarisha kiuchumi, namna ya kupata dhahabu, hii ni pamoja na kufanya yafuatayo: Kulipwa mrabaha na makampuni ya madini, sehemu ya mrabaha katika dhahabu safi, kuanzisha utaratibu mzuri wa kununua dhahabu hii kutoka kwa wachimbaji wadogo na Shirika la *STAMICO* kuwekeza kwenye

uchimbaji wa dhahabu na kuweka hazina ya dhahabu Benki Kuu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo nchini wanaweza kuwa na mchango mkubwa kwenye uchumi wa Taifa letu wakitayarishwa na kuendelezwa vizuri. Wachimbaji wadogo wa dhahabu waendelezwe, wachimbaji wadogo hawa wanahitaji kusaidiwa kupata mitaji, vitendea kazi na masoko ili shughuli zao za uchimbaji ziwe na tija. Naishauri Serikali ifanye mambo makuu yafuatayo:-

- Iendelee na mchakato wa kuanzisha Mfuko wa wachimbaji wadogo wa kisheria ili uweze kuchangiwa na wadau mbalimbali. Nakumbuka mchakato huo wa kutayarisha Waraka wa Baraza la Mawaziri ulikwishaanza, ukurasa wa 98, kifungu cha 172 kwenye hotuba ya Waziri inaonesha kwamba Wizara imetenga bilioni 2.5 (fedha za ndani) kwa ajili ya wachimbaji wadogo, lakini haioneshi hatua iliyofikiwa kuanzisha Mfuko huu muhimu. Serikali ilipe umuhimu suala hili kwa vile linaweza kuwakomboa wachimbaji wadogo. Mfuko huu uimarishwe uwe wa kisheria na unaweza kuchangiwa na wadau mbalimbali bada ya kutenga fedha tu kutoka Serikalini;

- Ishirikiane na sekta binafsi kuanzisha ununuzi wa dhahabu yote ya wachimbaji wadogo ili kuhakikisha dhahabu hii haitoroshwi nje, tuige nchi ya Ghana ambayo imeanzisha utaratibu wa kununua dhahabu na madini mengi mengine ya wachimbaji wadogo wote. Naomba Serikali ikajifunze Ghana, wao walianzisha mpango unaojulikana kwa jina la *Precious*

*Minerals Marketing Corporation (PMMC)* na umefanikiwa sana kuwaendeleza wachimbaji wadogo hususan kuwapatia wachimbaji wadogo soko la madini na kuongeza pato la Taifa la Ghana; na

-Ihakikishe matumizi ya zebaki katika uchenjuaji wa madini ya dhahabu, kwa kuwasaidia na kuwaelekeza wachimbaji wadogo namna ya kupata na kutumia vifaa vya *tetorts* na ama kutafuta njia mbadala ya kuchenjua dhahabu bila kutumia zebaki kama vile kuyeyusha dhahabu eneo hilo hilo inapochimbwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mgawanyo wa Mrabaha; taarifa ya Jaji Bomani kuhusu sekta ya Madini ilishauri mgawanyo wa mapato yatokanayo na mrabaha wa madini kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa vikiwemo vijiji vinavyozunguka migodi uwe kama ifuatavyo: asilimia 60 ya mrabaha iende kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Madini (*the mineral development fund*), asilimia 20 ya mrabaha iende kwenye Mamlaka ya madini inayopendekezwa kuundwa katika sehemu ya taarifa hii, asilimia 10 iende Wilaya yenye mgodi, asilimia saba iende kwenye Halmashauri nyingine katika Mkoa wenye mgodi na asilimia tatu iende kwenye vijiji vinavyozunguka mgodi.

Mheshimiwa Spika, bado naamini huu ulikuwa ni ushauri mzuri sana ambao ungesaidia sana wananchi wa kwenye maeneo ya madini kupata manufaa. Manung'uniko kutoka kwa wananchi wa maeneo haya kuhusu mgawanyo wa mapato ungemalizika kabisa.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka nikiwa Kamishna wa Madini, Wizara wa Nishati na Madini ilishauri Baraza la Mawaziri mapendekezo haya ya Kamati ya Rais yatekelezwe kwa kuacha fedha kidogo kwenye Halmashauri na Vijiji husika na fedha zingine ziendelee kupelekwa Hazina kama inavyofanyika sasa. Bahati mbaya ushauri huo haukupokelewa, bado naamini suala hili ni la manufaa sana kwetu, naomba Wizara iliangalie upya ili kuishauri Serikali tena kuwaachia asilimia kidogo tu wananchi wa maeneo inakozalishwa dhahabu.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Ukaguzi wa Madini *(TMAA)*; kazi yake kubwa ni kukagua uwekezaji ili makampuni ya madini yaweze kulipa kodi ya mapato stahiki, ukurasa wa 65 kifungu namba 113 cha hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini kinaonesha kuwa mafanikio makubwa ya wakala huu ni kuwezesha Kampuni ya *Resolute* kulipa shilingi bilioni 37.2 na kwamba kazi hii imefanywa kwa ushirikiano na *TRA*. Aidha, ukurasa 106 kifungu Na. 188, unaonesha kuwa kazi kubwa ya *TMAA* ni kufanya kazi ya ukaguzi wa uwekezaji ikishirikiana na *TRA*.

Mheshimiwa Spika, hii inaonesha wazi kuwa tumeunda wakala kufanya kazi zinazofanana na *TRA* na sehemu nyingine inaonesha *TMAA* inafanya kazi zile zile za Idara ya Madini, kwa mfano, tangazo la Wizara kuhusu kusitishwa kwa shughuli za uchimbaji holela wa mchanga katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani kwenye gazeti la Habari leo la tarehe 11 Julai, 2012 ukurasa wa saba (7) linadhihirisha wazi kuwa *TMAA* inafanya kazi za Idara ya Madini.

Mheshimiwa Spika, ukisoma malengo, majukumu na kazi za *TMAA* zilizoainishwa kwenye *framework document* ni zilezile za *TRA*, Idara ya Madini yaani Kamishna wa Madini kwa maana ya Mkaguzi Mkuu wa Migodi na Makamishna Wasaidizi wa Kanda na Wakaguzi wa Migodi wengine na sehemu ya biashara na uchumi, lakini pia ukaguzi wa mazingira unaofanywa na *TMAA* unaingilia kazi halisi za *NEMC* na kitengo cha Mazingira cha Wizara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na sifa zote zinazotolewa juu ya utendaji wa *TMAA,* lakini tunaweza kulisaidia Taifa zaidi tukipunguza matumizi kwa kuhakikisha kazi hizo zinafanywa na Taasisi moja tu, ni vema kujifunza na kuiga mifano ya nchi za Ghana, Canada, Marekani na Austaralia ambapo masuala ya ukaguzi wa uwekezaji yanafanywa na Mamlaka za mapato za nchi hizo na masuala ya ukaguzi wa migodi ukiwemo ukaguzi na ukusanyaji wa mrabaha hufanywa na Idara zinazosimamia sekta ya madini.

Mheshimiwa Spika, hali hii ya kuwa na Taasisi kubwa inayofanya kazi zile zile za Taasisi zingine siyo hekima ni kutumia fedha za Serikali vibaya. Naishauri Wizara ishauriane tena na wadau wengine yaani *TRA*, *NEMC* na Idara ya Madini *GST* na hata Tanzania *National Audit* kuondoa mwingiliano huu. Ujuzi wa wataalam wa *TMAA* tulioujenga ni muhimu sana kwa Taifa lakini unatakiwa kuwekwa mahali pake ili tupate thamani ya kazi yao (*value for money*).

Mheshimiwa Spika, ahsante nashukuru na naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. MBAROUK SALIM ALI:** Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuipongeza safu ya uongozi ya Wizara ya Nishati na Madini inayoongozwa na Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo, kitendo kilichofanywa na uongozi huo wa Wizara kwa kugundua wizi mkubwa wa fedha za Serikali toka kwa Shirika la *TANESCO*, huu ni mfano, ni jinsi gani Serikali inavyopoteza pesa kwa watendaji wasioaminika. Nashauri Makatibu Wakuu wengine pia waige mfano wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, ili nchi yetu itoke katika wimbi kubwa la umaskini.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana na bila utendaji wa ufanisi mkubwa wa Wizara hii, basi umaskini wa Tanzania hauwezi kuondoka. Hivyo basi, pamoja na Serikali kuongeza bajeti ya Wizara hii lakini bado ni kidogo na kuna haja kubwa ya kuongezewa pesa ili waweze kutekeleza miradi mingi ya umeme, kama ripoti ya Kamati ilivyoainishwa sasa tuwe na *slogan* la Nishati Kwanza.

Mheshimiwa Spika, Waziri katika uzinduzi wa bomba la gesi alitamka kuwa kuna gesi nyingi iligundulika ambayo Tanzania inaweza kukusanya zaidi ya trilioni 626.71. Huu ni utajiri mkubwa kwa nchi yetu, wasiwasi mkubwa ni jinsi gani nchi yetu imejipanga katika usimamizi wa rasilimali hii ya gesi na ili tuweze kusimamia vizuri, tunahitaji kuwa na mikakati endelevu ili tuweze kuiendesha nishati hiyo vizuri. Hii ni pamoja na kuwa na wataalam wa kutosha katika ngazi zote (*downs stream and up stream*). Sera na sheria za gesi

ni muhimu ziharakishwe ili ziweze kustawisha usimamizi bora wa sekta hii ndogo ya gesi.

Mheshimiwa Spika, suala la umeme vijijini bado ni tete kwani kasi ya uwekaji wa umeme vijijini bado ni ndogo sana, fedha walizotengewa *REA* ni ndogo sana pamoja na kwamba zimeongezwa. Nashauri *REA* wawezeshwe zaidi ili wakala huu uweze kutekeleza miradi mingi ya umeme vijijini. Mwaka jana tulipandisha kodi ya mafuta ya taa kwa azma kuwa, fedha hiyo ingekwenda katika Mfuko wa *REA*, tatizo kubwa hilo halikufanyika na sasa kuna kadhia kubwa ya mafuta ya taa vijijini na umeme pia hakuna.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Geologia ni sekta muhimu sana, zaidi ya kutambua miamba, lakini Wakala huu pia wana uwezo wa kutambua majanga kama tetemeko la ardhi, pamoja na umuhimu wa Wakala huu, lakini fedha wanazopata ni kidogo na kwa sababu hiyo wanakuwa hawana uwezo wa kufanya kazi zao kwa ufasaha. Nashauri Wakala huu uwezeshwe zaidi na kupewa vifaa vya kisasa na nyenzo nyinginezo ili waweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, niipongeze tena Wizara kwa mabadiliko ya kiutendaji yanayoanza kuonekana na naomba kuchangia hoja, lakini na kuunga mkono bajeti ya Wizara hii. Ahsante.

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru Mungu kwa kuniwezesha siku ya leo kuweza kutoa mchango wangu wa maandishi, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Nishati na

Madini kwa kuleta hotuba yenye matumaini kwa Tanzania, hivyo hivyo kwa Watanzania kwa ujumla wake. Nchi yetu ni siku nyingi mara kwa mara imekuwa ikitumbukia kwenye kiza, kiza ambacho Watanzania walikuwa wakijiuliza nini hasa kinachosababisha tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni aibu nchi yetu kwa majirani zetu lakini hata dunia kwa ujumla. Nchi yetu imekuwa ikisifika duniani kote kwa jinsi Mwenyezi Mungu alivyoineemesha kwa rasilimali nyingi, leo imekuwaje nchi hii mara kwa mara iwe inatumbukia kwenye kiza?

Mheshimiwa Spika, tuangalie majirani zetu Kenya iliwahi kupata mtikisiko wa umeme unaofanana na wa nchi yetu wa kutumbukia katika mgao wa umeme wa nchi yetu wa kutumbukia katika mgao wa umeme, lakini majirani zetu hawa Kenya tatizo hili halikuchukua muda mrefu liliisha wakati majirani zetu hawa hawana rasilimali za kuweza kutushinda. Tatizo la kiza kwa majirani zetu lilisha kabisa hadi leo na wala hawazungumzii tatizo la umeme kwenye nchi yao.

Mheshimiwa Spika, leo Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini baada ya muda mfupi tu kushika Wizara hii ameonesha kwa jinsi alivyo na nia ya kuliondoa giza hili ambalo limekuwa sugu kwa nchi yetu, lakini pia ameonesha jinsi alivyo na uwezo katika sekta hii. Kwa kuwa tatizo hili limekuwa sugu la siku nyingi bila kujua tatizo ni nini na kwa kuwa sasa tatizo limejulikana kwamba kuna watu ambao kwa maslahi yao binafsi ndio ambao wanatusababishia tatizo hili la

nchi muda mwingi kuwa kwenye giza, jambo ambalo linatusababishia hasara kubwa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, vile vile wapo hata Waheshimiwa Wabunge ambao wanahusika au wanashirikiana na wahalifu hawa ambao wanaisababishia nchi yetu hasara kubwa, ni kwa nini wasitajwe hadharani hasa hapa Bungeni ili Watanzania wote waweze kuwafahamu.

Mheshimiwa Spika, wapo baadhi ya Wabunge hapa Bungeni muda wote wanaosimama hujifanya wao ni waadilifu na waaminifu kwa nchi hii, vile vile kwa wananchi. Inasikitisha sana kuona Wabunge hao hao kumbe ndio ambao wanasimama kwenye Bunge hili na hata kwenye vyombo vya habari kuweza kuwatetea Mafisadi hao na Madhalimu hao kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nitamwomba Mheshimiwa Waziri wakati wa kufanya majumuisho atuambie pindi Kamati itakapoundwa kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa jambo hili zito na wakabainika baadhi ya Wabunge kuhusika na kushirikiana na Mafisadi hawa, nini kauli ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha na inastaajabisha kwamba zipo nchi nyingi ambazo zinategemea rasilimali moja tu kwenye nchi hizo, lakini zimepiga hatua na zinazidi kusonga mbele leo itakuwaje kwa nchi yetu tuna rasilimali zote ambazo Mwenyezi Mungu ameziumba na kubwa zaidi tunayo rasimiali ambayo haipatikani dunia nzima yaani *Tanzanite*. Leo vipi nchi

hii baada ya kusonga mbele iwe tunarudi nyuma ama sababu ni hii ya watu kama hawa ambao wanajali maslahi yao kuliko maslahi ya nchi hii?

Mheshimiwa Spika, sasa wakati umefika wa kuweka mambo bayana, Mafisadi wote kuwekwa hadharani na kutajwa kwa majina yao pamoja na Wabunge hao wanaowatetea Mafisadi hao ili nchi isonge mbele.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza tena Mheshimiwa Rais kwa uteuzi alioufanya wa Waheshimiwa Wabunge kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, tangu nimekuwa Mbunge hii ndio hotuba ya kwanza ya Wizara ya Nishati na Madini ambayo imekidhi matakwa ya Bunge kwa uwazi wa utendaji.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mawaziri wote wa Wizara hii na napenda kumtia moyo Katibu Mkuu ili afanye kazi kwa kufuata Sheria, Kanuni na taratibu bila woga wowote kwa kuwa atatatua kero za Watanzania wote. Pamoja na pongezi zangu kwa Wizara naomba nami nikumbukwe kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kasulu Vijijini kupatiwa umeme, hasa katika Kata za Titye na Rungwe mpya ambako kuna maporomoko makubwa ya maji ambayo tunayatumia katika miradi ya umwagiliaji wa kilimo cha mpunga na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru kupata umeme Makao Makuu ya Wilaya ya Kasulu, lakini katika Jimbo la Kasulu Vijijini lenye Kata 19 hakuna Kijiji hata kimoja ambacho kimepatiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, mMiradi mikubwa yote iliyoko Wilaya ya Kasulu hususan miradi ya kilimo iko Jimbo la Kasulu Vijijini, hivyo ni vyema kutupatia umeme wa kutusaidia kufanikisha malengo ya Serikali ya kuondoa umaskini, miradi hiyo ni kama ifuatayo:-

(1) Mradi wa Kilimo kwanza;

(2) Mradi wa umwagiliaji; na

(3) Mradi wa Kilimo cha miwa ili kuzalisha sukari na mazao mengi ya biashara na chakula.

Mheshimiwa Spika, katika Kijiji cha Makere kuna madini ya chokaa ambayo yalitumika kujenga majengo yote ya Serikali katika Mkoa wa Kigoma, tangu wakati wa Mkoloni mpaka leo hii, lakini leo hii wazalishaji au wachimbaji wadogo wanasumbuliwa sana na Idara ya Maliasili na Utalii bila kujali leseni zao. Napenda kujua ni lini Wizara itakuja Kasulu kuwatembelea vijana hao ili kuwapatia ushauri wa kitaalam ili wachimbe chokaa kwa faida na ubora wa bidhaa hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kata zinazohitaji umeme ni karibu zote kama nilivyotaja hapo juu. Je, ni lini *REA* watakuja kutembelea huko? Kwa kuanzia niombe Kata

zifuatazo ziangaliwe: Kata ya Kitagata, Kata ya Kurugongo, Kata ya Titye, Kata ya T/Mpya, Kata ya Rusesa, Kata ya Kasangezi, Kata ya Muzye, Kata ya Heruushingo

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na uzima na leo hii nikaweza kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Nishati na Madini na pia nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumchagua Waziri wa Nishati na Madini Mheshimiwa Sospeter Muhongo, nina imani kubwa kuwa Wizara hii sasa itafanya kazi kwa ufanisi mkubwa, tatizo kubwa lililoikumba Wizara hii ni ubadhirifu na ufisadi ambao watendaji wengi Wizarani na kwenye Taasisi zake hasa *TANESCO*, nashauri Waziri awafanyie utafiti sana watendaji wa *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iangalie upya mikataba mibovu ya kufua umeme na mikataba ya madini. Hii ndio inayotia hasara Serikali kwa kiasi kikubwa. Makampuni yanayochimba madini yachunguzwe sana, hawa wana tabia ya kutorosha madini bila Serikali kujua. Tabia hii inaitia Serikali hasara kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, gharama za umeme zimekuwa ni ghali sana, kiasi cha kuwa wananchi walio wengi wanashindwa kumudu gharama hizi za umeme. Naiomba Serikali iangalie upya gharama za umeme ili

wananchi wa kawaida weweze kumudu gharama hizi ili na wao waweze kufaidika na umeme.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali manufaa ya gesi yainue uchumi wa nchi yetu na pia maisha ya watu yaweze kuboreka kwa neema hii ya gesi Mwenyezi Mungu aliyotupa. Serikali iwe makini katika mikataba ya kuzalisha gesi tusije kuwa kama kwenye mikataba ya madini ambayo mpaka leo hii tunaiona inavyoathirika katika nchi yetu hasa ile ya *Barrick Gold Mine*.

Mheshimiwa Spika, ukiumwa na nyoka ukiona ukuti huachi kushtuka, huu ni msemo wa Kiswahili unaotuonesha athari ya mikataba hii mibovu, ni lazima tuogope isije ikatupata tena.

**MHE. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri ya kuvuna gesi ya Mnazi Bay na kuzalisha umeme, matatizo ya mgao wa umeme katika Mkoa wa Mtwara yamepungua na unapokatika ni masuala ya miundombinu tu siyo kwamba umeme haupo. Naipongeza Serikali kwa kutoa umeme toka Mtwara hadi Newala ambako imetuwezesha kusukuma maji saa zote na hatimaye kupunguza tatizo la upatikanaji wa maji kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka ya nyuma Serikali iliahidi wananchi wa Mtwara kuwa kuna mradi maalum wa kuunganisha umeme majumbani kwa bei nafuu isiyozidi shilingi 70,000/= kwa nyumba. Wanasiasa na hasa Wabunge wa Mkoa wa Mtwara na Lindi

tuliwahamasisha wananchi kuwaandaa kwa shughuli hii, bahati mbaya mradi huu ulikufa baada ya wafadhili kujitoa. Naiomba Wizara ifanye mpango wa kufufua mradi huu ili wananchi wa Mtwara ambao wanazalisha gesi waweze kunufaika.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na urasimu mkubwa kwa *TANESCO* kuunganisha umeme katika nyumba za watu hata pale ambapo umeme uko kwa mfano, Kijiji cha Kikunga, Wilayani Newala kina umeme kwa zaidi ya miaka ishirini iliyopita. Tangu wakati huo watu wengi wamefanya *wiring* lakini bado kuingiziwa umeme. Jirani yake Kijiji hiki kimeungana na Vijiji vya Amani na Pachoto, hakuhitajiki *transformer,* vijiji hivi vimeomba kuunganishiwa umeme, lakini hakuna hafua. Naomba vijiji hivi vishughulikiwe ipasavyo. Nashukuru kwa Vijiji vya Mtangalanga, Makonga na Lengo, tayari vimetengewa fedha na za kupelekewa umeme. Naomba tuharakishe.

Mheshimiwa Spika, mwisho wako wanaochochea watu wa Mtwara wakatae kupeleka gesi Dar es Salaam. Wanasiasa tumewaeleza wananchi kuwa gesi inayobaki Mtwara inatosha kuzalisha umeme wa Mkoa mzima. Ili wananchi waendelee kutuamini ni lazima tuongeze kazi ya kusambaza umeme vijijini ndani ya Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. WARIDE BAKARI JABU:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Nishati na Madini kwa uwasilishaji wake wa bajeti hii. Napongeza Wizara kwa

kupitia *TANESCO* na *ZECO* kwa makubaliano waliyofikia kupitia kero za Muungano, lakini nashauri yale mambo yaliyobakia kama bei ya *distribution power* kwa *ZECO* na mengineyo nayo yatafutiwe ufumbuzi, lakini pia makubaliano yaliyofikiwa ya kupunguza bei ya *unit* kwenye *KVA,* Pemba iwekwe sawasawa na Unguja ili kuwapunguzia mzigo wananchi wa Pemba.

Mheshimiwa Spika, Bomba la gesi kutoka Mtwara mpaka Dar es Salaam, nashauri Wizara ifikirie bomba hilo kufikishwa Zanzibar kwa ajili ya matumizi ya majumbani kwani bei ya gesi ni rahisi kuliko umeme.

Mheshimiwa Spika, Serikali itafute *alternative sources* za umeme kama *geofarm*, mawimbi ya Bahari na mawimbi ya upepo kama ule unaotaka kuwepo Singida ili kuweza kuchangia umeme uliokuwepo.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Bahi haizingatiwi sana katika kupatiwa miradi ya umeme vijijini na hivyo kuwa Wilaya ya mwisho kwa idadi ya kijiji kimoja tu ambacho kazi ya kupeleka umeme inaendelea katika Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, vipo vijiji ambavyo vipo karibu na umeme ulipo ambapo ni kati ya kilometa tatu hadi sita tu lakini havijawekwa katika mpango wa kupatiwa umeme licha ya mimi binafsi na viongozi wote wa Wilaya kufanya juhudi ili vijiji hivyo viingizwe katika mpango wa *REA,* lakini sijapata mafanikio. Naomba

Wizara iipe pia umuhimu Wilaya ya Bahi, vijiji vyake vipatiwe umeme.

Mheshimiwa Spika, hapa chini nakuonesha vijiji na umbali toka chanzo cha umeme kilipo:-

(a) Mpunguzi (Dodoma Mjini) - Chibelela (Bahi) kilomita tatu;

(b) Chigongwe (Dodoma Mjini) - Kigwe ( Bahi) kilomita sita;

(c) Ibugule (Bahi) - Mtitaa (Bahi) kilomita tatu; na

(d) Mpamautwa (Bahi) Kijiji hiki umeme umepita lakini haujashushwa hadi leo, naomba ushushwe.

Mheshimiwa Spika, natarajia majibu ya uhakika ya Wilaya ya Bahi kupata umeme katika vijiji hivyo hapo juu.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuanza mchango wangu kwa kusema naunga mkono hoja, lakini pamoja na kuunga mkono hoja nina machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ifuatilie kwa karibu utekelezaji wa ahadi ambazo zimetolewa na Makampuni ya Madini kwa wananchi wanaoishi kandokando ya migodi. Ahadi hizo ni pamoja na malipo ya fidia kwa vifaa na mali za wananchi ambao walihama maeneo kupisha uchimbaji. Kwa mfano, wananchi wa Vijiji vya Mwime, Mwendakulima na Chapulwa hadi leo wapo baadhi ya wananchi ambao

bado wanadai malipo yao ya fidia, lakini mgodi wa Buzwagi (viongozi) na *Barrick Gold* hawataki kutimiza wajibu wao.

Mheshimiwa Spika, Serikali ifuatilie kwa karibu mahusiano yaliyopo baina ya wawekezaji migodi na wananchi kwa mfano pale Buzwagi hivi ni sahihi mgodi kuwa na maji ambayo yanatumika kumwagilia hata barabara wakati wanakijiji waliopo mita 100 toka kwenye uzio wa mgodi hawana maji na wanafuata maji hadi kilomita tano. Je, haya maisha mazuri baina ya majirani?

Mheshimiwa Spika, naomba sana Waziri na Naibu wafuatilie hali ya mahusiano yaliyopo baina ya migodi na wananchi ili kuondoa tatizo ambalo likiruhusiwa kuendelea litasababisha hata uvunjifu wa amani.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, naomba kwa dhati ya moyo wangu niwapongeze wafuatao: Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri wawili lakini pia Katibu Mkuu wa Wizara hii ya Nishati na Madini kwa jinsi ambavyo wameanza kazi katika Wizara hii ambayo iligubikwa na jinamizi la ubadhirifu wa mali ya umma, ufisadi uliokithiri na rushwa ambayo ilitishia uhai, hususan ndani ya Shirika la Umeme *(TANESCO)*.

Mheshimiwa Spika, madini yamechangia pato la Taifa kwa asilimia 3.8 kwa sasa. Kwa kweli kutokana na hali halisi ya rasilimali ambayo tumejaliwa kuwa nayo ya madini ambayo tumeyachimba na ambayo tunatarajia kuyachimba, mchango wa rasilimali hii

haujaweza kuisaidia nchi hii kuondokana na dimbwi kubwa la umaskini. Ni vyema udhibiti kutokana na utoroshaji wa madini yetu upewe kipaumbele, pia ni vyema kuangalia upya mikataba yote na leseni ambazo wamepewa wawekezaji hasa katika maeneo ya wawekezaji na wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, ni vyema kuona ushauri wa wananchi kwa kupitia Halmashauri zetu kushirikishwa kuanzia hatua za awali ili kuondokana na matatizo na migogoro inayotokea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme, napongeza kwa dhati operesheni inayoendelea sasa hivi nchini hususan katika Jiji la Dar es Salaam kwa wale wote ambao wanajiunganishia umeme kinyemela na kulikosesha Shirika mapato. Hata hivyo, naiomba Wizara iangalie vizuri suala hili kwani kuna uwezekano mkubwa wa wafanyakazi wa *TANESCO* ambao sio waaminifu, wanahusika moja kwa moja na uunganishaji, wizi na ubadhirifu huu ambao kwa sasa hatia na hasara inawaangalia wananchi peke yao. Ni vyema watendaji wote watakobainika kushirikiana na wanachi hao, wachukuliwe hatua za kinidhamu.

Mheshimiwa Spika, deni wanalodaiwa *Pan Africa Energy* ni vyema lifuatiliwe na lilipwe haraka iwezekanavyo na madai yao wameeleza karibu mabilioni ya shilingi, naomba Waziri ashauriane na *CAG* ili hesabu zao wanazosema zikaguliwe na ukweli uweze kujulikana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu gesi asilia, naiomba Wizara yafuatayo:-

- Kuwekeza kwa kuwapatia elimu wazawa kuhusiana na uchimbaji, usafirishaji na hata uuzaji wa gesi;

- *Gas Company* ifufuliwe haraka iwezekanavyo kwani itasaidia kuratibu shughuli zote zinazohusiana na sekta hii;

- Sera ya Gesi pamoja na Sheria zake ziharakishwe na ziwe wazi hasa kwa Halmashauri zote ambazo ziko katika Mikoa ya Kusini ambapo bomba la gesi linapita, lakini pia kwa wadau ambao wanahusika na sekta hii; na

- Ni dhambi kubwa iwapo Wizara itatoa misamaha ya kodi kwa wawekezaji katika sekta hii ya gesi (tusije kurejea makosa ambayo yamefanyika katika madini).

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba Wizara hii imepata Waziri, Manaibu Waziri na Katibu Mkuu ambao ni waadilifu na waamini kwa nchi yao na kwa wananchi wa Tanzania. Ni wazi kwamba matendo maovu yaliyokuwa yakitendeka ndani ya Wizara hii ni ukweli kwamba yalikuwa yakipangwa kwa makusudi. Yaliyojitokeza kwa Wizara ya Nishati na madini ni somo kwa Wizara nyingine zote na kama zitashindwa kupata somo kwa kuiga Wizara hii ni vyema na wao wakawajibika kwa sababu watakuwa bado hawajaweza kupambanua maovu na waovu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania si nchi ya kuwa omba omba, lakini imefikia hatua hiyo kutokana na tabia ya watu waliokuwa hawana uchungu na nchi pia hawaangalii maslahi ya Watanzania walio na kipato cha chini. Leo Wizara hii ndani ya kipindi cha miezi mitatu imekuwa na uwezo wa kukusanya billioni sita kwa mwezi, jambo ambalo miaka yote lilikuwa halipo. Tuna wajibu wa kupata maelezo ya kina kutoka kwa Serikali ni kwa nini Wizara hii chini ya Waziri Muhongo iweze kukusanya bilioni sita kwa mwezi, lakini miaka ya nyuma zisipatikane?

Mheshimiwa Spika, pato la Taifa limeongezeka kwa mwezi kupitia Wizara hii, suala la ukataji wa umeme limechukuliwa ahadi na Waziri kwamba halitokuwepo, tujiulize ni kwa nini nyuma yalikuwa yakijitokeza matatizo hayo. Ni dhahiri kwamba kulikuwa na ubadhilifu mkubwa uliokuwa ukitendeka baina ya viongozi na watendaji wa Wizara waliokuwepo na nikisema viongozi sikusudii viongozi wa Serikali tu, lakini wanakuwa na maslahi mawili; moja, kupata maslahi ya kisiasa kwa ajili ya kuteka mawazo na fikra za Watanzania waione Serikali iliyopo madarakani kuwa ni kandamizi. Pili, kupata maslahi ya kifedha na kujikusanyia fedha isivyo halali huku wakipinga maslahi mengine yaliyo halali.

Mheshimiwa Spika, umeme ni ukombozi wa mwanadamu, umeme ni ajira, umeme ni hazina na umeme ni suluhu ya kuondoa umaskini katika nchi. Hata hivyo, gharama za umeme zimepanda kwa upande wa Zanzibar. Je, kama Mtanzania aliyeko

Zanzibar anapandishiwa bei ya umeme kinyume na Mtanzania aliyeko bara hii si njia moja ya kuuvuruga umoja wetu? Mheshimiwa Waziri anatoa kauli gani kuhusiana na hili?.

Mheshimiwa Spika, nguzo moja ya umeme Zanzibar ni milioni moja na laki mbili, hivyo mwananchi utamfikiaje umeme huo kama gharama ya nguzo iwe ya mwananchi, waya ziwe za mwananchi na vifaa vingine vyote viwe vya mwananchi na mwananchi huyo huyo analipia umeme kila mwezi, ni kwa nini basi hili lisiangaliwe kwa Tanzania nzima mwananchi asiachiwe gharama ya kuunganisha umeme na kulipia gharama za umeme tu.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Waheshimiwa Manaibu wote na watendaji kwa hotuba nzuri yenye mwelekeo wa uhakika wa kuboresha sekta ya nishati na madini. Napenda kumshauri Mheshimiwa Waziri na Manaibu Waziri kufufua mapendekezo yaliyokuwepo mezani, Serikalini kwa miaka 14 (kumi na nne) iliyopita bila kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuanzishwa upya kampuni ya *GASCO;* Kampuni hii iliundwa na kusajiliwa na Mtendaji wake Mkuu kuandaliwa mwaka 1998/1999 ili kusimamia usambazaji na mauzo ya gesi. Mtendaji wake leo ni marehemu ndugu Thomasi Masili. Uvumbuzi wa gesi asilia unaongezeka huko Mtwara, Lindi na Mkuranga, sio busara kuachia usimamizi wa rasilimali hii mikononi mwa Kampuni za Wageni. Sio kosa kuingia ubia lakini chini ya mikataba yenye

dhamira njema, nimeona dhamira ya Wizara juu ya *GASCO*, naomba itekelezwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuanzishwa kwa Kampuni ya *KILAMCO;* kama ilivyokuwa *GASCO* chini ya *TPDC* pia iliundwa na kuandikishwa kampuni ya *KILAMCO*. Lengo lake pia ni matumizi ya Gesi ya Mnazi Bay kwa ajili ya kuzalisha mbolea, ni vema Kampuni hiyo ikaanzishwa ili kuzalisha mbolea na kutumia vizuri hazina kubwa ya gesi asilia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kurejesha Kampuni ya *COPEC*: kutokana na umuhimu wa matumizi ya mafuta Kitaifa siyo busara nchi yetu kuachia jukumu la usambazaji wa mafuta mikononi mwa Kampuni za kigeni, tusihadaike kwamba kampuni hizo zimeandikishwa Tanzania na hivyo ni za Tanzania Kampuni ya Umma-*COPEC* itakuwa kiongozi wa bei dira za mafuta nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme wa dharura *MW* 422; lazima tujiulize swali hili, ilikuwaje *IPTL* kupewa mkataba mrefu wa zaidi ya miaka 20 wakati lengo la awali lilikuwa kupata umeme wa dharura? Gharama za umeme wa dharura kutoka makampuni ya nje ni ghali sana, tuweke dhamira ya kweli kutekeleza miradi ifuatavyo iliyopo ndani ya bajeti ya mwaka 2012/2013 kama ifuatavyo:-

(i) Mchuchuma *600MW*

(ii) Ngaka *400MW*

| | | |
|---|---|---|
| (iii) | Ruhudji | *358MW* |
| (iv) | Rusumo | *75MW* |
| | **JUMLA** | ***1433MW*** |

Mheshimiwa Spika, ukamilisha wa miradi hiyo pamoja na gesi ya Ubungo *105MW* uende sambamba na kuondoa umeme wa dharura ifuatayo:-

| | | |
|---|---|---|
| (i) | *Symbion* | *137MW* |
| *(ii)* | *Aggreko* | *100MW* |
| *(iii)* | *IPTL* | 80 *MW* |
| | **JUMLA** | ***317MW*** |

Mheshimiwa Spika, tusiruhusu kupandikiza kuongeza muda wa mikataba hiyo na tuchambue uhalali uliowezesha *IPTL* kupata mkataba wa muda mrefu. *IPTL* itumie gesi kuendesha mitambo yao. Kwa kuwa mkataba unaipa jukumu *TANESCO* kununua mafuta ya kuendesha mashine zao, basi ijengwe hoja ya kutumia gesi asilia badala ya mafuta mazito *IFO*. Nakumbuka mwanzo kabisa mitambo hiyo iliendeshwa kwa mafuta ya ndege *JET AI*, naomba Wizara ichunguze hilo ili kusaidia kujenga hoja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa mradi wa *Stigler's Gorge* 2100 *MW;* dhamira ya mpango wa mradi huu ilikuwepo zaidi ya miaka 20 iliyopita. Hatukuanza kuutekeleza hata kwa awamu tatu kama

ilivyopendekezwa ndani ya muda huo leo. Tungekuwa tayari tunazo 2100 *MW* za ziada na wala kusingekuwepo na upungufu huu unaolieleza Taifa letu. Tumechelewa lakini tuthubutu na tuanze kwa dhati mwaka 2012/2013. Mapato ya mauzo ya gesi yachangie gharama za utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Miradi ya Umeme MCC.1; Muheza tuna mpango kwa Vijiji 17, kumekuwa na ucheleweshwaji wa miradi hii sasa kwa zaidi ya miaka mitano. Inaanza kufanana na miradi ya Benki ya Dunia ya Maji kwa Vijiji 10. Wizara isimamie ili kuboresha uharaka wa utekelezaji wa miradi hii, utekelezaji kwa uteuzi wa Wakandarasi umeanza Muheza, lakini kasi ni ndogo, yapo malalamiko kwamba Vijiji vilivyoteuliwa awali vimebadilishwa bila kushirikisha jamii.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ifuatie hili ambalo nimetumiwa ujumbe leo asubuhi tarehe 28/7/2012.

Mheshimiwa Spika, Mradi kati ya Wahisani wa Sweden na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza juu ya teknolojia mpya ya umeme; naishukuru sana *REA* na Mkurugenzi wake Daktari Mwakahesya kwa kusaidia kuwezesha mradi huo kuanza. Balozi wa Tanzania nchini Sweeden amefika Muheza mwezi Machi, 2012 kuona kama Halmashauri ya Wilaya ya Muheza itaweza kuchangia utekelezaji wa mradi huo. Napenda kusema kwamba uwezo wa Halmashauri ni mdogo na hivyo kuomba *REA* kuweka nguvu, kusaidia

kwa kuwa mradi huu upo katika majaribio na Tanzania imeteuliwa kuwa sehemu ya majaribio.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja ya Nishati na Madini. Napenda kuchukua fursa hii na kwa dhati kabisa kumpongeza kaka yangu Mheshimiwa Muhongo, Waziri na Manaibu wake wote hasa Mheshimiwa Massele kwa kazi ya uzalendo aliyoifanya kwa niaba ya Wizara kutembelea maeneo ya migodi na kuongea na wananchi ingawa hakuongea na wananchi wote. Mfano, kuna sehemu walikwenda, asiende tu kule Lyamongo na kuacha sehemu ambazo zina kero kubwa kama Kata ya Matongo.

Mheshimiwa Spika, Hivyo Mheshimiwa Waziri tungependa Wananchi hawa pamoja na wadau wa madini kwa maana ya wachimbaji wa madini wadogo wadogo, wa kati na wakubwa ili kusiwepo na malalamiko toka pande yoyote ile kwa maana ya wananchi na wachimbaji.

Mheshimiwa Spika, vile vile nachukua fursa hii adhimu pia kumpongeza Katibu Mkuu wa Wizara Mheshimiwa Eliakim Maswi.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie suala zima la wachimbaji wadogo wadogo. Katika hotuba ya mwaka 2012/2013, Wizara imeainisha kuwa inatenga maeneo ya Itandula, Wilayani Tarime lenye ukubwa wa hekta 37. Lakini Wizara haikutamka wazi kuwa ni leseni

ngapi ndogo ndogo zimetolewa kwa wachimbaji wadogo wadogo na ni wangapi ambao leseni walizopatiwa na wazawa na wengine kutoka nje ya maeneo ya machimbo?

Mheshimiwa Spika, vile vile ningependa kujua kama leseni zimetolewa kwenye maeneo ambayo si ya kwao, je, wamewalipa fidia wamiliki halali wa maeneo hayo? Maana kumekuwepo na malalamiko mengi sana juu ya watu kudai wana leseni za uchimbaji na kutanabaisha maeneo ambayo kuna watu wanamiliki na kufanya shughuli zao za kilimo. Mfano, katika ziara ya Mheshimiwa Massele, kuna kundi la watu walidai wana leseni za kuchimba katika meneo 13, maeneo ya Marera, Mwenyekiti wa kikundi hiki anaitwa David Makoma na hili suala lilipingwa mbele ya Mheshimiwa Massele. Hivyo, napenda kujua hatua iliyochukuliwa ili wananchi hawa wanyonge ambao hawana uwezo wa kuchimba madini basi wapewe fidia mbadala.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua hayo maeneo mengine yaliyotajwa kama Mosabiri, Nyakunguru na Gorongila. Gibaso ni kwa ajili ya wale wanaotaka leseni tu au pia kwa ajili ya ile ahadi ya Serikali ya kuwapa maeneo wananchi wa maeneo ya migodi ambapo baada ya uwekezaji wamekosa ajira na wakaahidi sio tu kuwapa maeneo bali kutoa elimu sambamba na mitaji ili waweze kujiendeleza. Ningependa kupewa majibu katika hayo.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri tumekuwa tukishuhudia mauaji ya vijana wetu ambao ni nguvu kazi ya Taifa letu wakija katika harakati za kujitafutia

fedha ili waweze kujikimu kimaisha kama kusomesha watoto na kutunza familia, sasa wamebaki bila ujira na huku wakifa au kuwa vilema.

Mheshimiwa Spika, vile vile kumekuwepo na malalamiko mengi sana juu ya fidia na mara mwananchi anapokuwa hajaridhika na fidia na hivyo kugoma kupisha kwenye eneo lake hutishiwa na hata kupelekwa jela mahabusu huku nyumba na mazao katika maeneo yao kubomolewa na kuharibiwa. Je, hii ni haki? Mfano ni kwa ndugu Daniel Samwel Nyamahe ambaye alipigwa na kupelekwa rumande ambapo alikaa na alipotoka alikuta *Barick* wamezungushia uzio eneo lake huku wakibomoa nyumba zake takribani tisa pamoja na kuharibu mazao, bila hata kulipwa fidia ambayo wamekubaliana. Hii sio haki kabisa tukumbuke wananchi hawa wanapisha ardhi yenye dhahabu ambapo walitakiwa kulipwa fidia pamoja na *resettlement* ambazo kwa upande wa wananchi wa Nyamongo hawafanyiwi hivyo.

Mheshimiwa Spika, hii ni dhuluma, nina imani na safu ya uongozi wa Wizara na uzalendo wao, hivyo ni dhahiri kuwa wakati umefika wa kuwatendea haki wananchi hawa wanyonge ambao wamekuwa wakidhulumiwa kwa muda mrefu ili tuweze kuwa na mahusiano mazuri na wachimbaji. Pia wachimbaji wanawajibika kufanya au kutoa huduma za kijamii ili kubadili mandhari ya maeneo husika. Maeneo ya madini yanasikitisha sana, inabidi siyo tu kunufaisha eneo la uchimbaji tu bali na Wilaya nzima hasa Makao Makuu ya Wilaya pamoja na Kata jirani ili viweze ku-

*reflect* uwepo wa uchimbaji madini katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, mwisho nizungumzie juu ya fedheha ya ubadhirifu ndani ya *TANESCO* na katika Idara zingine za Mashirika ya Umma, tunaomba hatua mbadala zichukuliwe na hatua mbadala sio tu kuwafungulia kesi bali kuwafilisi mali zote ili kurejesha fedha zote zilizohujumiwa ambazo ni kodi ya wananchi. Huu ugonjwa umekuwa ukitufilisi sana, watu wachache wanajineemesha huku Tanzania tukibaki kuwa maskini.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua ni kwa kipindi cha muda gani au miaka mingapi tuhuma ya kukatwa umeme imekuwa ikifanywa? Vile vile ningependa kujua ni kiasi gani cha fedha kwa ujumla ambacho Taifa limeingia kwa kukatiwa umeme? Hii ni kuhusu fedha walizojipatia hao wahujumu uchumi, achilia mbali zile ambazo wananchi wamepata hasara kwa ukosefu wa nishati hii muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kusisitiza umuhimu wa umeme vijijini kwani asilimia kubwa ya Watanzania wanaishi vijijini (75%) ambapo shughuli kubwa ni kilimo ambapo nishati ya umeme ni kiini cha umwagiliaji, usindikaji wa mazao na kadhalika. Ukiangalia Vijiji vingi vya Mkoa wa Mara na hususan Tarime na Rorya havina umeme, hivyo naomba vipewe vipaumbele.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia kwa upande wa Machimbo ya Madini katika Jimbo la Mbozi Magharibi eneo la Sante, Kata ya Ivuna kuna shughuli ya uchimbaji wa madini unaendelea ambapo wananchi na mimi kama mwakilishi wa wananchi sifahamu. Hivyo basi ili kuweka sawa na kutahadharishwa mgogoro ambao unaweza kutokea, tunaomba tupatiwe maelezo kuhusu uchimbaji madini katika eneo hilo, madini ya aina gani? Leseni wewe umepewa na nani? Shughuli hiyo imewekezwa kwa muda gani? Pia wananchi watafaidikaje na mradi huo wa machimbo ya madini hayo?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Miradi ya Umeme, kwa kuwa katika Jimbo la Mbozi Magharibi ambalo kwa sasa ndiyo Wilaya mpya ya Momba hatujawahi kabisa kuwa na umeme kabisa katika Kata zote 14 tangu tupate uhuru. Hivyo basi tunaiomba Serikali ihakikishe kuwa kwa mwaka huu wa fedha angalau baadhi ya maeneo tupate umeme hali ambayo itatuwezesha kusukuma maendeleo katika Wilaya yetu ya Momba.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Serikali kwa kupunguza gharama za bei ya uzalishaji wa umeme. Kwa kweli katika jambo hili Serikali yetu imechangia moja kwa moja kusaidia Mtanzania. Hivyo, napenda kuishauri Serikali ielekeze nguvu zake zaidi katika kuongeza upatikanaji wa vifaa vya

uzalishaji wa umeme kwani ni dhahiri kutokana na punguzo hilo, wananchi wengi wataitikia wito wa kujiunganishia wenyewe.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nataka kuishauri Serikali juu ya kuongeza uangalifu katika suala la kuwafuatilia watendaji wa *TANESCO*, inatokana kama mtandao mkubwa wa uharibifu wa watendaji kwa nia ya kujinufaisha binafsi. Ubinafsi katika shirika hili umepelekea *TANESCO* kubeba jukumu la madeni makubwa, hii ina athari kubwa kwa uchumi wa Taifa hili na ina athari kubwa kwa maendeleo ya wananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naishauri Serikali iongeze nguvu zaidi katika kusambaza huduma hii muhimu vijijini. Hivi sasa idadi ya Watanzania wanaoishi vijijini tunasaidia pia kasi ya uharibifu wa mazingira yetu ambayo kwa sasa asilimia 95% ya Watanzania vijijini wanatumia nishati ya kuni katika kuendeleza maisha yao. Hii ni hatari sana na sababu kubwa ya janga hili ni kutokana na nishati ya umeme kutopatikana katika vijiji vyetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwapongeza Waziri, Naibu Mawaziri na Wataalam wa Wizara, kwa hotuba nzuri na iliyowasilishwa vizuri. Nampongeza pia Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upizani na Kamati, kwa maoni yao yenye lengo la kuimarisha Sekta ya Madini na Nishati.

Mheshimiwa Spika, pia niipongeze Wizara kwa hatua ilizochukua kuhakikisha kuwa nchi haiingizwi kwenye giza lisilokuwa na sababu za msingi. Waziri na wasaidizi wake wote waendelee kuchukua hatua ili hatimaye Taifa letu liondokane na mgogoro wa nishati ambao umelikumba Taifa kwa muda mrefu. Mambo yafuatayo ambayo yamekuwa yakiwaumiza wananchi wazalendo yafanyiwe kazi mara moja:-

(i) Miradi isiyotekelezeka. Miradi ya namna hii huonesha kuwa Wizara ni ya kisanii, si sifa nzuri hata kidogo;

(ii) Mikataba mibovu ya nishati (gesi na mafuta). Tuangalie mahali pengine wanafanyaje;

(iii) Umeme usiokuwa na uhakika; na

(iv) Tuhuma za ufisadi uliokithiri ngazi za juu Wizarani.

Mheshimiwa Spika, Mambo hayo yafanyiwe kazi kwa makini ili Taifa lisonge mbele.

Mheshimiwa Spika, niongelee pia nishati jadidifu kwa sababu ya mabadiliko ya tabianchi, nchi nyingi duniani zimejielekeza kwenye nishati jadidifu. Mbali na kwamba tunahitaji nishati ya kutosha kwa matumizi binafsi, viwandani na sehemu nyingine inabidi Wizara ianze kuandaa sera makini ya nishati jadidifu hasa kuhusu joto ardhi, jua, upepo, biogesi, makaa ya mawe safi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, sasa nitajielekeza kwenye Jimbo langu la Bukombe, nashukuru kwamba sasa Serikali imeamua kupeleka umeme Bukombe, wananchi wa Bukombe wanachopenda ni kwa Serikali sasa kufuata ratiba kikamilifu ili mradi utekelezwe kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba, vijiji vyote ambako nguzo na nyaya za umeme vitapita, vipatiwe umeme na vijiji vingine ambavyo havijapata basi navyo vifikiriwe ili mwaka ufuatao 2013/2014 viwekwe kwenye utaratibu wa umeme wa *REA*.

Mheshimiwa Spika, niongelee pia miradi mingine ya umeme ambayo Bukombe iliahidiwa mwaka jana 2011/2012. Katika hotuba ya bajeti ya mwaka jana (2011/2012), ukurasa wa 115 na ukurasa wa 117 miradi ifuatayo ilibainishwa:-

(1) Mradi wa taa za mwanga bora vijijini *(community-based power trading*) mradi huu ulipaswa kutekelezwa Chato, Biharamulo, Kahama na Bukombe.

(2) Mradi wa Tanzania *Affordable Rural Electrification Plan*. Huu ulipaswa kutekelezwa Bukombe na Kibondo.

Je, miradi hii imefika wapi kiutekelezaji au ilikuwa ni miradi hewa? Naomba majibu.

Mheshimiwa Spika, pia nitaongelea tatizo moja la ukorofi wa baadhi ya wawekezaji kutofuata sheria/mikataba katika sekta hii, wawekezaji hawa

wamekuwa wagumu kutimiza wajibu wa kijamii wa Mashirika na hata kulipa kodi. Nampongeza Waziri kwa kuliona hili na kuanza kuchukua hatua wakati wa kuwabembeleza umekwisha.

Mheshimiwa Spika, licha ya kupitia mikataba, Sera na sheria na kuziba mianya yote, Wizara inapaswa kusimamia kwa ukaribu utekelezaji wa mikataba husika kwani ukorofi wa kibeberu wa hawa wawekezaji unahitaji uangalizi na ufuatiliaji wa karibu.

Mheshimiwa Spika, mifano ya ukorofi ni mingi na Wizara inaifahamu:-

(a) Ukweli kwamba *Barrick Gold* haijatekeleza vipengele vya Sheria mpya ya Madini ya 2010. Wawekezaji wote waitwe na waambiwe kuwa fungate imekwisha.

(b) Kumekuwa na kelele nyingi za malalamiko kuhusiana na wawekezaji wa Mgodi wa Nyamongo. Ilifikia hatua Mheshimiwa Nyangwine alisema atashika mapanga na sasa wawekezaji wameanza kutekeleza kidogo kidogo, lakini bado waongeze kasi kwani wana Tarime wamechoka kuibiwa na kunyonywa na mwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Wizara iendelee kuwa na msimamo imara, isiendelee kuwabembeleza wawekezaji.

Mheshimiwa Spika madini, Sera ya Madini ya Mwaka 1997 na Sheria ya Madini ya 2010, kwa kiasi

kikubwa viliwapendelea wawekezaji kwa kuwaandalia mazingira mazuri ili wawekeze bila matatizo. Wachimbaji wadogo wadogo hawakutengewa mazingira mazuri na hapakuwa na mipango thabiti yoyote ya mafunzo, mikopo au mpango wowote wa kupewa zana. Siku hizi kuna makundi ya watu yaliyounda Ushirika wa Uchimbaji Madini, mathalani huko Bukombe, ambayo yamekosa maeneo ya kuchimba dhahabu kwa sababu maeneo mengi yana leseni. Hali hii inawakatisha tamaa wananchi wenye nia ya kushiriki katika kuvuna rasilimali ya dhahabu. Ninashauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyopendekeza mwaka jana, wachimbaji wadogo watengewe maeneo pembezoni mwa migodi mikubwa kuondoa tatizo la migogoro baina ya wachimbaji wakubwa na wachimbaji wadogo. Kadhalika, hatua za makusudi zichukuliwe kufuta liseni za maeneo ambayo hayajaendelezwa (rai iliyotolewa kwenye Hotuba ukurasa wa 91 liwe ni agizo). Kwa mfano, ukiangalia ramani ya madini ya Wilaya ya Bukombe, karibu Wilaya nzima imejaa leseni lakini maeneo yaliyoendelezwa ni machache sana. Wizara isahihishe jambo hili ili tuondoe malalamiko kuwa watu fulani walijipendelea kupata leseni huku wananchi wenyeji wakibaki hawana kitu.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Mafunzo kwa wachimbaji wadogo kilichopendekezwa cha Rwamugasa Kiharakishwe kuanzishwa, kitawasaidia sana wachimbaji wadogo kwa sababu wengi hawana maarifa ya kutosha kuhusu uchimbaji na hatari zake.

Mheshimiwa Spika, suala la kuwezeshwa kifedha ni muhimu. Kama ilivyoelezwa katika Hotuba, utaratibu wa kutoa mkopo uandaliwe kwa makini ili wachimbaji wadogo wanufaike.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kauli yake (ukurasa 106 – 107), inayosisitiza kuwa migodi yote inaanza kulipa kodi bila visingizio. Wizara ifuatilie kwa karibu utekelezwaji wa agizo hili. Kadhalika, ifanye utafiti katika nchi nyingine mathalani Botswana, Guinea, Ghana na Zimbabwe ili kuangalia wao wanaendeshaje usimamizi wa Sekta ya Madini na viwango vya kodi, kama kodi yetu kwa migodi bado ni ndogo basi kuna haja ya kuirejea na kuirekebisha.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine linahusu mazingira; Wizara ifuatilie kwa makini suala hili. Mara nyingi wawekezaji lengo lao ni faida, lazima wafuatiliwe kuhusu athari za kimazingira za shughuli zao. Je, Wizara ina mipnago yoyote ya kufuatilia athati za kimazingira za shughuli za wachimbaji wadogo wadogo? Nauliza hili kwa sababu yaelekea hakuna mpango wowote ule.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, Sekta ya Madini kwa muda mrefu imekumbwa na tuhuma za ufisadi. Wizara ijitahidi kulishughulikia tatizo hili. Je, suala la Jairo limefikia wapi mbona Serikali ipo kimya kuhusu Maazimio ya Bunge kuhusu jambo hili?

**MHE. MBAROUK SALIM ALI:** Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuipongeza safu ya Uongozi ya

Wizara ya Nishati na Madini inayoongozwa na Mh.Professor Sospeter Muhongo. Mh.Spika kitendo kilichofanywa na uongozi huo wa Wizara kwa kugundua wizi mkubwa wa fedha za serikali toka kwa shirika la *TANESCO*. Huu ni mfano ni jinsi gani serikali inavyopoteza pesa kwa watendaji wasioaminika. Nashauri Makatibu wakuu wengine pia waige mfano mzuri wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini; ili Nchi yetu itoke katika wimbi kubwa la umaskini.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana na bila utendaji na ufanisi mkubwa wa Wizara hii basi umaskini wa Tanzania hauwezi kuondoka. Mh.Spika, hivyo basi pamoja na serikali kuongeza bajeti ya Wizara hii lakini bado ni kidogo na kuna haja kubwa ya kuongezewa pesa ili waweze kutekeleza miradi mingi ya umeme. kama ripoti ya Kamati ilivyoainisha sasa tuwe na *Slogan* la Nishati KWANZA.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri katika uzinduzi wa bomba la gesi alitamka kuwa kuna gesi nyingi iligundulika ambayo Tanzania inaweza kukusanya zaidi ya trilion 626.71. Mh.Spika huu ni utajiri mkubwa kwa Nchi yetu. Wasiwasi mkubwa Mh.Spika ni jinsi gani Nchi yetu imejipanga katika usimamizi rasilimali hii ya gesi. Na ili tuweze kusimamia vizuri tunahitaji kuwa na mikakati endelevu ili tuweze kuiendesha Nishati hiyo vizuri, hii Mh.Spika ni pamoja na kuwa na wataalamu wa kutosha katika ngazi zote (*downstream and upstream*). Mh.Spika pia sera na sheria za gesi ni muhimu ziharakishwe ili ziweze kustawisha usimamizi bora wa Sekta hii ndogo ya gesi.

Mheshimiwa Spika, Suala la umeme vijijini bado ni tete kwani kasi ya uwekaji wa umeme vijijini bado ni ndogo sana. Mh.Spika fedha walizotengewa *REA* ni ndogo sana pamoja na kwamba zimeongezwa; nashauri *REA* wawezeshwe zaidi ili wakala huu uweze kutekeleza miradi mingi ya umeme vijijini. Mwaka jana tulipandisha kodi ya mafuta ya taa kwa azma kuwa fedha hiyo ingalienda katika mfumo wa REA. Tatizo kubwa, hilo halikufanyika, na sasa kuna kadhia kubwa ya mafuta ya taa vijijini na umeme pia hakuna.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Geologia ni Sekta muhimu sana. Zaidi ya kutambua miamba lakini wakala huu pia wana uwezo wa kutambua majanga kama tetemeko la ardhi. Mh.Spika pamoja na umuhimu wa wakala huu lakini fedha wanazopata ni kidogo; na kwa sababu hiyo wanakuwa hawana uwezo wa kufanya kazi zao kwa ufasaha.

Mheshimiwa Spika, nashauri wakala huu uwezeshwe zaidi na kupewa vifaa vya kisasa na nyenzo nyinginezo ili waweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, niipongeze tena Wizara kwa mabadiliko ya kiutendaji yanayoweza kuonekana na naomba kuchangia hoja hii na kuiunga mkono bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Ahsante.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja ya Wizara ya Nishati na Madini kuhusiana na Makadirio na Matumizi

ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Aidha, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara hii Ndugu Eliakim Chacha Maswi kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii. Naamini sasa tutaona utendaji wa *TPDC* na taasisi nyingine zilizopo chini ya Wizara hii ukiimarika.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa umeme wa uhakika mjini una uhusiano wa moja kwa moja na jitihada zetu kama Taifa katika kupambana na umaskini. Nishati ya umeme ni nyenzo muhimu kwa sekta za uzalishaji mali, ukuzaji wa ajira, kuongeza kipato kwa wananchi wanaojiajiri katika sekta rasmi na zisizo rasmi, upatikanaji wa huduma bora na afya, upatikanaji wa huduma ya uhakika ya maji safi na salama, elimu mashuleni na vyuoni na upashanaji habari kupitia simu, *internet*, redio na televisheni.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa saba wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri tunaelezwa kuwa ni asilimia 18.4 tu ya Watanzania ndio ambao tumeweza kuwaunganishia umeme. Aidha, kati ya hao ni asilimia 6.6 tu ya Watanzania waishio vijijini ndio wameunganishiwa umeme. Hii inamaanisha kwamba asilimia 68.4 ya Watanzania waishio vijijini hawajaunganishwa kwenye umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa maana nyingine nikisema kwamba sera zetu zinafifisha uibuaji na utumiaji fursa za kiuchumi zilizopo katika maeneo ya vijijini, tumezuia fursa ya wananchi vijijini kuongezea thamani mazao

yao na tumedumaza maendeleo ya viwanda katika maeneo yaliyokosa umeme. Kwa hali hii hatupaswi kushangaa tunapoona wimbi kubwa la watu kukimbilia mijini kutafuta ajira. Wimbi hili la watu wanaokimbilia mijini, hususan vijana tunalitengeneza sisi wenyewe kutokana na kutoweka mazingira wezeshi kiuzalishaji na huduma muhimu vijijini.

Mheshimiwa Spika, Taifa haliwezi kusema kuwa linapiga hatua za kimaendeleo endapo zaidi ya asilimia 50 ya watu wake wanatengwa kutumia fursa zilizopo kuwaendeleza. Kama kweli tunayo dhamira ya dhati ya kuondoa umaskini vijijini, hatuna budi kuwekeza katika kupeleka umeme vijijini, kwa sababu kupeleka umeme vijijini tutaibua fursa nyingi za kiuchumi na uzalishaji wa ajira.

Mheshimiwa Spika, kule Mkinga hususan katika Kata za Kigongoi na Bosha tunazalisha Karafuu, Iliki, Pilipili Manga, Mdalasini na sasa tumeanza kufufua zao la kahawa ambalo lilikuwa limetelekezwa. Kwa muda mrefu wananchi wameshindwa kufaidika na ukulima wa mazao haya kutokana na kuuza mazao kwa bei ya chini. Kwa sasa amejitokeza mwekezaji ambaye yuko tayari kuweka Kiwanda cha kuayongezea thamani mazao haya ikiwemo kuzalisha mafuta ya Makonyo. Hata hivyo, fursa hii kupotea kutokana na kukosekana umeme katika Kata ya Kigongoi inayojumuisha Vijiji vya Vuga, Hemsambia, Mgambao Shashui, Kidundui, Kwekuyu na Bombo Mbuyuni.

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 1987 wakati Jimbo la Uchaguzi la Mkinga likiwa sehemu ya Wilaya

ya Muheza na hatimaye kupatiwa hadhi ya kuwa Wilaya kamili, Serikali imekuwa ikiwaahidi wananchi wa Mkinga kuwapatia umeme katika vijiji mbalimbali. Aidha, kuanzia bajeti ya mwaka 2007/2008 na kuendelea Serikali imekuwa ikivionesha Vijiji vya Mkinga kuwa katika mpango wa kuwapatia umeme kupitia *REA* kama ifuatavyo:-

(a) Daluni – kazi ya kupeleka umeme Kijiji cha Daluni inahusisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 11, umbali wa kilomita 10, uwekaji wa transfoma ya *KVA* 50 na njia ndogo ya msongo wa volti 230/400 zenye urefu wa kilomita mbili; na

(b) Gombero – kazi ya kupeleka umeme Kijiji cha Gombero inahusisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 33 umbali wa kilomita 19, uwekaji wa transforma mbili na ujenzi wa njia ndogo za umeme za msongo wa volti 230/400 za urefu wa kilomita mbili.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, licha ya kuwemo katika bajeti kwa miaka yote hii, ukamilishaji wa ahadi ya Serikali kuvipatia vijiji hivi umeme haujafanyika na sasa imejengeka hofu miongoni mwa wananchi kuwa vijiji hivi huenda vikaachwa katika kupatiwa umeme. Namwomba Waziri atuambie, kwa mwaka huu utekelezaji wa miradi hii utafanyika au ni hadidthi ile ile ya miaka nenda rudi ya kuwemo katika bajeti na orodha ya miradi itakayotekelezwa na *REA* lakini hakuna utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa nyakati tofauti (Mkutano wa Tisa, Kikao cha Kumi na Nne, 2007 na

Mkutano wa Kumi na Nne, Kikao cha Sita, 2009) Serikali imekuwa ikitoa ahadi katika Bunge lako kuwa tayari kazi za awali za kuufanyia tathmini mradi huu zimekamilika, ikiwa ni pamoja na kubaini gharama, tayari *TANESCO* imekwishawasilisha *REA* maombi ya Jumla ya Shilingi Bilioni 3.76 kwa ajili ya kufikisha umeme Daluni na Gombero na kwamba wakati wa kupeleka umeme kwenye vijiji hivyo itahakikisha kuwa vijiji vilivyo jirani na maeneo hayo (Vuga, Hemsambia, Bwiti, Magati, Mapatano, Bantu, Machimboni, Jirihini, Vunde Manyinyi na Dima) navyo vinapatiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya kazi kubwa ya kuanzisha skimu ya umwagiliaji katika Kata ya Mwakijembe, skimu ambayo itakuwa ukombozi na kichocheo kikubwa cha ukuaji wa uchumi na pato la watu wa Mkinga. Je, Serikali haioni busara ya kuijumuisha Kata hii katika kuipatia umeme kutokea Duga ambapo si mbali sana. Aidha, kwa busara hiyo hiyo naiomba Serikali ifikirie uwezekano wa kupeleka umeme kwenye Kata ya Bosha, Kata ambayo inazo fursa nyingi za uwekezaji katika kilimo. Kwa sasa tayari yupo mwekezaji ambaye ameonesha nia ya kuwekeza katika kilimo cha maua katika shamba la Kwamtili. Vile vile naiomba Wizara kupitia *REA* ifikirie uwezekano wa kuzipatia umeme wa *Solar* Shule za Wilaya ya Mkinga zilizopo nje ya mfumo wa umeme wa Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kukosekana upatikanaji wa nishati ya umeme ya uhakika kwa maendeleo ya Taifa ni kiashiria kimojawapo cha umaskini. Takriban asilimia 75 ya Watanzania wanaishi vijijini na wanategemea kilimo kuendesha maisha yao ya kila siku. Aidha, ili

kukidhi mahitaji yao ya nishati, ukataji miti kwa ajili ya kupata kuni na uchomaji wa mkaa kimekuwa ndio chanzo kikuu cha nishati vijijijni. Matumizi haya ya kuni na mkaa yanachangia sana katika kuongezeka kwa kasi ya uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, wakati takwimu zikionesha Tanzania kuwa na ekari 33 milioni za misitu, uharibifu wa misitu unakadiriwa kusababisha upotevu wa hekta 500,000 za misitu kwa mwaka; kati ya hizo hekta 300,000 sawa na kilometa za mraba 3,320 za misitu hupotea kutokana na uchomaji wa mkaa kila mwaka. Takwimu za Benki ya Dunia zinaonesha kuwa kwa mwaka takribani tani 1,000,000 za mkaa hutumika nchini; huku Dar es Salaam ikiwa ndio kinara wa matumizi hayo kwa asilimia 50.

Mheshimiwa Spika, vile vile tafiti zinabainisha kuwa kwa kasi hii ya ukataji miti kwa ajili ya kuni na uchomaji mkaa, nchi yetu katika kipindi kisichozidi miaka kumi ijayo itashuhudia misitu yetu ikiwa imekwisha. Kama Taifa lazima tufanye jitihada kuhakikisha kuwa tunainusuru misitu yetu kwa kuwapatia wananchi vyanzo mbadala vya nishati. Lazima tuhakikishe tunakuwa na mipango itakayotuwezesha kuitumia vyema hazina yetu ya gesi kuzalisha umeme utakaopatikana kwa bei ambayo hata mtu wa kijijini ataweza kuimudu. Ni vyema vile vile tuongeze kasi ya kufikisha Gesi majumbani mwa watu wengi ili waweze kuitumia.

Mheshimiwa Spika, fedha tunazotenga kwa ajili ya *REA* hazitoshi na mbaya zaidi hata hizo kidogo

zinazotengwa hazitolewi zote, lazima bajeti ya nishati ijielekeze katika kuhakikisha kuwa *REA* inapata fedha za kutosheleza mahitaji ili iweze kufikisha huduma ya umeme kwa haraka vijijini ambako asilimia 75 ya Watanzania inaishi. Tukifanya hivyo tutaweza kuzuia uharibifu wa mazingira unaosababishwa na ukataji miti ovyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja nikiamini kwamba, Serikali itazifanyia kazi changamoto nilizoainisha na ushauri nilioutoa.

**MHE. ABDULLA JUMA SAADALLA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie gesi Zanzibar. Nchi yetu imepewa na Mungu baraka ya kuwa ndio mkombozi wa Mtanzania, napendekeza sambamba na usambazaji wa uwekaji wa bomba la gesi Tanzania bara, utafiti, upembuzi na ufadhili vifanywe kwa kuona ni kwa namna gani bomba hili litafika Zanzibar kwa faida ya wananchi wanaoishi Zanzibar. Jambo hili litazamwe wazi wazi ndani ya Sera mpya ya gesi itakayoundwa. Napendekeza kuwa katika uwekezaji wa gesi, lazima wananchi wamilikishwe hisa za uwekezaji tangu mwanzo wa uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, sasa nichangie kuhusu umeme wa upepo, hili ni jambo la msingi na tunatarajia litasaidia sana katika kuongeza umeme ndani ya gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, nafahamu kuwa hatua zimeshaanza kuchukuliwa ila wananchi wapewe fidia zao, hati miliki za ardhi na Kijiji lazima zitolewe na Wizara ya Ardhi, mbali na fidia *Resettlement ya Displaced Villagers* ifanywe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Compliance Monitoring Unit*, Mheshimiwa Spika, naungana na Wabunge wengine kuwa *process* ya kumkabidhi mwekezaji ardhi ya kuchimba madini basi lazima kuwe kuna chombo cha kufuatilia *Compliance* ya Sheria za uwekezaji ikiwemo *MoU* baina ya wananchi, Serikali na mwekezaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu urani na wachimbaji wadogo wadogo; tunafahamu kuwa Serikali imeshaandaa utaratibu mzuri wa kuchimba urani, sawa na sera ya uchimbaji pamoja na marejeo na kanuni zilizofadhiliwa na *Mantra*. Hili halina tatizo lakini tuwe makini na mwekezaji huyu, lazima tujikite katika uwekezaji rasilimali watu ili wasome sheria, ufundi, uchimbaji, usambazaji, usafirishaji na utupaji wa urani. Pia Sera ya Madini inaruhusu wachimbaji wadogo wadogo (*small scale miners*) wachimbe kuchangia mgodi mkubwa wa Karibu.

Mheshimiwa Spika, naomba Sera isiruhusu *small scale miners* kuwepo kuhusiana na *Uranium*. Nafahamu watu wataona kuwa huu ni utajiri wa bure, lakini madhara yake ni makubwa na ikiwezekana hata ulinzi wa maeneo ya machimbo, p*rocessing*, usafirishaji na kadhalika. Muhimu kuepukana na *Briefcase Bomb*.

Mheshimiwa Spika, nawapa hongera sana kwa asilimia mia moja.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa bomba la mafuta kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza (*pipeline*). Utafiti wa mradi ulianzia mwaka 1983, *Technical feasibility* 1988 na *economic feasibility* 1989 na mradi ulipata idhini ya utekelezaji kutoka Ikulu tarehe 17 Julai, 1989. Ilipofika mwaka 1997 mradi huu ulipata Baraka za Mheshimiwa Rais (Benjamin Mkapa), faida za mradi huu zinajulikana kwa uchumi wa Kanda ya Ziwa na kwa niaba ya watu wa Kanda, naomba kupata kauli ya Serikali kwamba utekelezaji wa mradi huu utaanza lini?

**MHE. UMMY A. MWALIMU:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja. Pili, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri ya kusimamia sekta hii muhimu kwa maendeleo ya Watanzania. Ni imani yangu na ya watu wengi kuwa mtasimamia ipasavyo Wizara hii muhimu ili iweze kuchangia ipasavyo maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, nauomba uongozi wa Wizara, Waziri, Naibu Mawaziri na Katibu Mkuu kuendelea kuhakikisha kuwa daima maslahi ya nchi ndio yanakuwa msingi mkuu wa maamuzi yote yatakayofanywa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, nishati na maendeleo ya wanawake; ningependa Wizara ihakikishe inatekeleza kwa vitendo Sera ya Taifa ya Nishati (*revised* 2003)

katika masuala ya nishati na usawa wa jinsia hasa kuhakikisha nishati ya kisasa inapatikana kwa matumizi ya nyumbani hasa vijijini ili kuwapunguzia mzigo wanawake na wasichana.

Mheshimiwa Spika, wanawake ndio watafutaji wakubwa wa kuni kwa ajili ya kupikia, pia ndio wanaohakikisha kunakuwepo nishati kwa ajili ya *lighting*. Karibu asilimia 85 ya nishati inayotumika majumbani inatokana na kuni au mkaa. Hali hii itaendelea hadi lini? Wanawake wengi pia vijijini wanapoteza maisha wakati wa kujifungua kutokana na kukosekana kwa huduma za nishati ya kisasa (umeme katika vituo vya afya).

Mheshimiwa Spika, wakati umefika sasa kwa Wizara kuhakikisha upatikanaji wa huduma za nishati ya kisasa unapewa jicho la jinsia. Nipatiwe maelezo ni mipango au mikakati gani ipo au imewekwa ya kuhakikisha usawa na jinsia na upatikanaji wa huduma za nishati ya kisasa kwa Watanzania hasa wanawake walio vijijini. Rejea Sera ya Taifa ya Nishati, Rev. 2003 *Policy statements No*. 60, 61, 62 na 63.

**MHE. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bajeti ndogo ya *REA*; ni vyema iongezwe ili usambazaji wa umeme vijijini uweze kwenda kwa kasi. Hususan kusambaza katika shule zote za sekondari na vituo vya kutolea huduma ya afya Wilayani, Serengeti.

Mheshimiwa Spika, wale wote watakaopatikana na kuhujumu uwepo wa umeme wachukuliwe hatua kali za kisheria. Ni vyema kwa makusudi kabisa wote watakaobainika na kuhujumu umeme iwe mfano, wachukuliwe hatua kulingana na Sheria ya Wahujumu Uchumi na takwimu zilizotolewa ni kiasi gani kimepotea kutokana na kukatika au mgao wa umeme.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo wasaidiwe, wachimbaji waliojitolea katika Wilaya ya Serengeti kama *Park* Nyigoti, Majimoto, Ringwani (Kalambo) na Borenga hawajawezeshwa na wengine wanajiita watafiti, lakini hakuna uwazi, hao wanachimba na ku-*process* madini au wanatafiti kweli na kama kweli wanatafiti hivi hakuna ukomo wa kutafiti?

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, Serikali iwainue wachimbaji wadogo wadogo kwa kuwapa mafunzo juu ya masuala yote yahusuyo uchimbaji pamoja na mafunzo juu ya utunzaji mazingira, lakini pia wapewe mikopo ya vifaa vya kuchimbia. Najua kuna juhudi zimeanza kufanyika za kuwainua wachimbaji wadogo wadogo lakini bado kuna malalamiko mengi, wao ndio huwa wa kwanza kugundua yalipo madini, lakini mara nyingi huondolewa kwa mabavu na maeneo yao wanapewa wachimbaji wakubwa. Hata wanapohamishiwa maeneo mengine, si rahisi waweze kushindana na wachimbaji wakubwa bila kuwezeshwa.

Mheshimiwa Spika, leseni za wachimbaji wadogo wadogo zinachelewa sana kupatikana,

wanazungushwa sana. Bei ya leseni nazo zimepanda sana. Serikali iangalie na ione umuhimu wa kupunguza bei kwani sasa hivi wachimbaji wana malalamiko makubwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu gesi asilia, Sheria ya Gesi na Sera ya Gesi pamoja na bomba la gesi. Nchi yetu imejaliwa gesi nyingi sana, nashauri Sera na Sheria ya Gesi iletwe mara moja Bungeni. Sheria itasaidia kudhibiti ufisadi na udhaifu katika sekta hii, pia kuepuka migogoro inayoweza kuhatarisha usalama wa nchi. Ujenzi wa bomba la gesi ni hatua muhimu na kubwa, lakini ni vema Serikali ilete au iweke wazi mkataba huo ili wananchi waelewe hali halisi na tuhakikishe maslahi ya Taifa yanalindwa na hii itasaidia kuondoa au kuepusha migogoro inayoweza kuhatarisha usalama wa nchi.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa bomba la gesi ni hatua muhimu na kubwa, lakini ni vema Serikali ilete au iweke wazi mkataba huo ili wananchi waelewe hali halisi na tuhakikishe maslahi ya Taifa yanalindwa na hii itasaidia kuondoa au kuepuka matatizo ya awali yaliyoko kwenye mikataba ya madini iliyopo sasa. Vile vile lazima wananchi wa Lindi na Mtwara wawe *beneficiaries* wa kwanza wa mradi husika na Serikali itueleze rasmi jinsi mikoa hiyo itakavyofaidika.

Mheshimiwa Spika, bei ya mafuta ya taa si suluhisho la uchakachuaji wa mafuta; maisha ya wananchi maskini wa vijijini na wa mijini wanaathirika na bei ya mafuta ya taa, hali hii imeongeza ugumu wa maisha ukizingatia mfumuko wa bei unazidi kila

kukicha. Serikali itueleze kwa nini *EWURA* wanaingia gharama ya kununua vinasaba vingine vinavyowekwa na *EWURA* wakati inaelezwa kwamba uchakachuaji unaendelea wakati *solution* ilikuwa kupandisha bei ya mafuta ya taa? Kama imegundulika *solution* hiyo imefeli, basi bei ya mafuta ipunguzwe ili wananchi wapone na adha ya mfumuko wa bei unaosababishwa na bei za mafuta kupanda.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji katika Sekta ya Madini, naishauri Serikali kuweka hadharani ripoti ya taarifa zote zilizowahi kutolewa kuhusiana na uwekezaji katika uchimbaji wa madini nchini kuanzia mwaka 1995 hadi 2010 na kama Serikali imefaidika na nini kutokana na uwekezaji huo ili kama kuna upungufu mkubwa tunao uwezo wa kuendelea au kubadili sheria.

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Spika, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini, naunga mkono hoja kwa asilimia 99 na asilimia moja chukueni maneno ya Mheshimiwa Mussa Zungu Azzan aliyochangia mfanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, viongozi hawa wa Nishati na Madini wameteuliwa, wamedhalilishwa vya kutosha wana makovu ya vidonda ndugu walivyopata toka kwa ndugu zao Wabunge. Mungu alisema: “Angalieni nawatuma katikati ya mbwa mwitu, nanyi iweni wenye busara na wapole kama hua.” Nawapongeza kwa kuvumilia adha mnayoipata.

Mheshimiwa Spika, macho yangu hayajaamini kama kweli katika Bunge hili kuna watu wenye kejeli,

kiburi na jeuri na wenye majivuno, lakini naamini Mwenyezi Mungu atawalipa sawasawa na mapenzi yake.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Sospeter Muhongo, Waziri na kundi lake, Naibu Mawaziri Mheshimiwa George Simbachawene na Mheshimiwa Stephen John Masele wote wa Nishati na Madini pamoja na Commando Eliakim Maswi, Katibu Mkuu wa Nishati na Madini kwa kudhalilishwa hivyo, Mungu mwenyewe atakitwaa kitambaa na kuyafuta machozi kutokana na majaribu mnayopata kutokana na uaminifu wenu. Si hivyo tu, bado mtakumbana na uchafu, ufisadi, uchawi, uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda na watu wenye hila na midomo ya upotoshi, iweni makini mchague ya kunena, ombeni hekima kama Mfalme Suleiman.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa zawadi hii nzuri ambayo ameiteua iwatumikie Watanzania, Naamini sasa Serikali imepata viongozi wenye uwezo katika Wizara hii, wenye fikra sahihi na matendo thabiti katika kuliendesha gurudumu la Taifa ili kuleta maendeleo katika jamii.

Mheshimiwa Spika, nawaombeni sana viongozi hawa wa Nishati na Madini kuwa macho na vituo vingi vinavyoota kama uyoga na wakati wengine wanafunga vituo vyao au kuendesha kwa shida na si hivyo tu naombeni muwe macho kwenye bomba la mafuta (mita).

Mheshimiwa Spika, kuhusu REA; mtakapokuwa mnataka kuanza zoezi hilo anzieni Rukwa jamani, Laela na Kasanga na katika mpango ujao msisahau Kilando, Wampembe, Kate, Muze, na Ilemba. Maeneo hayo yamechangamka na watu wanaokaa maeneo hayo wanao uwezo wa kulipia *bill* za umeme. Pamoja na yote hayo msisahau Kaseya na mpakani kuna Ofisi za uhamiaji, Polisi, *TRA*, Forodha, Mifugo na Afya ili kuwavuta watu waweze kujenga majengo ya kibiashara paweze kuonekana kama Tunduma vile.

Mheshimiwa Spika, mgema ukimsifia tembo hulitia maji na kwa nini nawapongeza? Ni mwanzo mzuri mlioanza nao. Simamieni kwa makini ushushaji wa meli za mafuta kwa muda muafaka na kuhakikisha mnajipanga kudai madeni ya *TANESCO* na kulipa madeni ya bilioni 319 ili kuonesha ufanisi wenu kuwa ni wa hali ya juu, pia hakikisheni mnajenga Ofisi za kununua madini ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na taarifa ya kupotea umeme kila siku milioni 4.1 kwa ajili ya uchakavu wa miundombinu: Je, Wizara inatuambiaje?

**-** Meli za mafuta zimekuwa zinakaa bandarini siku 45 kwa sababu gani? Kuzuia matatizo haya ya kiini macho mnajipangaje?

**-** Kwa nini tunadaiwa billion 319 wakati pesa ilikuwa inakusanywa?

**-** Kwa nini *TANESCO* imepewa hati safi ya ukaguzi wa mahesabu na *CAG* wakati kuna madudu haya? Huyu naye aingizwe kwenye golikiki.

**-** Watu hao binafsi ambao walikuwa hawalipi bilioni 240 na Taasisi hizo ni zipi ambazo hazilipi zichunguzwe kuna nini?

Mheshimiwa Spika, Mwalimu Nyerere, baba wa Taifa alisema uhuru na kazi, fanyeni kazi kwa upendo, furaha na amani, uvumilivu, utu, wema, fadhila, uaminifu na muwe wapole kiasi mtakuwa juu ya sheria wala hazitawahukumu.

Mheshimiwa Spika, anayesema kwa nini mafuta yalipanda bei Tanzania, hata Nigeria inayochimba mafuta yenyewe yalipanda toka Naira 65 hadi kufikia Naira 200 kufuatana na anguko la uchumi katika soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, mwisho nasema, pendaneni ninyi kwa ninyi kwanza. Mheshimiwa Rais atambue watu wa Musoma wana asili ya utawala bora hata kama ni elfu 20 awaweke wainue Taifa letu, asisahau watu wa Kigoma kama nao ni waaminifu, japokuwa kila mwenye kupata cheo huitwa mtu wa Mrundi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Spika, suala la umeme Same Magharibi, katika Jimbo langu kuna vijiji vingi ambavyo vimepitiwa na umeme (*high*

*tension*), lakini hakuna transfoma na *low tension* line (*LT)*. Vijiji ambavyo naviombea *LT line* ni hivi hapa: Vudee Msanga, Bangalala, Mabilioni, Ishindo, Njoro na Gonjanza. Aidha, Vijiji ambavyo havina umeme kabisa ni Saweni, Gavao, Rindini, Hezamu na Ndolwa. Naomba kupata majibu ni lini nitaletewa umeme katika maeneo niliyoyataja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba kumshukuru Mungu, kwa kunipatia zawadi ya uhai ili nami pia niweze kuchangia katika Hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, kipekee, nawapongeza Viongozi wote wa Wizara hii muhimu kwa nchi yetu kwa kuanzia na Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mtera pamoja na kuwa na chanzo muhimu cha maji ya Bwawa la Mtera ambalo hutumika kuzalisha umeme kwa maendeleo ya nchi yetu, jambo la kutia huzuni ni kwamba, katika vijiji 76 ni vijiji viwili tu ndivyo vina umeme ambao umeletwa na Wamisionari wa Kanisa la Kiangrikana, bila wao tungekuwa 0 kwa 0. Hata hivyo, naishukuru Serikali kwa kunipatia umeme kwenye vijiji vitatu vya Mlowa Barabarani, Makangwa na Iringa Mvumi. Kwa awamu hii, kwa kuwa nguzo zimewekwa marundo kwa marundo, naomba kazi hiyo ifanyike kwa kasi sana, tusiache nguzo ziliwe na mchwa. Ombi langu kwako Mheshimiwa Waziri ni kuwa awamu ya pili vikumbukwe Vijiji vya Fufu, Manzase na Mloda.

Mheshimiwa Spika, kwa Tarafa ya Mvumi, tusisahau Kata ya Muungano katika Vijiji vya Muungano na Ilolo, ambako umeme umepita karibu sana. Naomba pia tupatiwe umeme katika Kijiji cha Ndembwe kwenda Kata ya Handali kwa ajili ya Sekondari ya Kata, Tarafa ya Mpwayungu kutoka Mpunguzi.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mjini kupitia Kata ya Mwitikila, Jimbo la Bahi mpaka Naguloo hadi Mpwayungu, umeme ukiwaka utakuwa ukombozi mkubwa kwa Wananchi wa Jimbo la Mtera.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *Shanta Mining* imekuwepo katika maeneo ya Kinyamberu, Samberu na Mhimbi katika Kata ya Mang'onyi ya Jimbo la Singida Mashariki tangu mwaka 2005. Kwa kipindi chote hicho, Kampuni hiyo imetwaa maeneo ya wananchi kwa nguvu bila ya kupata ridhaa ya maandishi ya wenye ardhi na bila ya kuwalipa wananchi hao fidia ya haki timilifu na ya wakati mwafaka.

Mheshimiwa Spika, yote hii ni kinyume cha Sheria ya Madini, 2010, Sheria ya Ardhi za Vijiji, 1999 na Kanuni za Ardhi za Vijiji za Mwaka 2001.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006, Mkuu wa Mkoa wa Singida aliunda Tume ya Uchunguzi wa Madai ya

Wananchi iliyoongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Singida wakati huo Ndugu Florence Horombe. Tume hiyo ilitoa ripoti iliyothibitisha kwamba, *Shanta Mining* ilikuwa imeingilia maeneo ya wananchi bila ya kufuata taratibu za kisheria na bila ya kuwalipa fidia. Hadi sasa mapendekezo ya Tume ya Horombe kuhusu malipo ya fidia kwa wananchi hayajatekelezwa, licha ya *Shanta Mining* kuyakalia maeneo yao kwa miaka saba sasa. Namwomba Waziri atoe Kauli ya Serikali ni lini wananchi wa maeneo tajwa ya Kata ya Mang'onyi watalipwa fidia yao halali na malimbikizo ya riba ya miaka yote ambayo *Shanta Mining* imekalia maeneo yao isivyo halali.

Mheshimiwa Spika, tarehe 20 Januari, 2012, Waziri wa Nishati na Madini wakati huo Mheshimiwa William Ngeleja, alitoa leseni ya uchimbaji ML 455/2012 kwa *Shanta Mining*. Leseni hiyo ni ya muda wa miaka kumi na inaeleza kwa maeneo ya leseni hiyo ni Misughaa na Mponda Kaskazini. Maeneo yote mawili yapo katika Kata ya Misughaa ya Jimbo la Singida Mashariki. Hata hivyo, kwa miaka yote ambayo *Shanta Mining* imeendesha shughuli za utafiti, haijawahi kufanya kazi hizo katika Kata ya Misughaa bali miaka yote wamekuwa Kata ya Mang'onyi na vijiji vyake ambavyo siyo maeneo ya leseni ML 455/2012. Naomba Wizara ichukue hatua za dharura kuhakikisha *Shanta Mining* inaenda kwenye eneo la leseni yake.

Mheshimiwa Spika, Mashapo ya Mang'onyi yanakadiriwa kuwa na wakia 120,000 za dhahabu zilizothibitika. Hiki ni kiasi kidogo ukilinganisha na mashapo ya migodi mingine ya dhahabu hapa nchini.

Hii ndiyo sababu maisha ya leseni hii kuwa miaka kumi badala ya muda wa kawaida wa miaka ishirini na tano. Kwa sababu hizi, ni busara maeneo haya ya dhahabu yaachiwe kwa wachimabji wadogo ili wananchi wa vijijini nao wapate ajira yenye kipato kikubwa kama uchimbaji wa dhahabu na shughuli za kiuchumi zinazohusiana na wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, moja ya maeneo ambayo yamesababisha makubwa ya kigeni kutolipa kodi stahili katika Sekta ya Madini, Mafuta na Gesi Asilia ni gharama za uendeshaji *(general and administration costs*). Katika Mikataba yote kati ya Serikali na Makampuni ya Sekta hizi, gharama za uendeshaji huwa zinatolewa katika mahesabu ya mapato kwa ajili ya kugagatua kiwango cha kodi kinachotakiwa kulipwa na makampuni haya.

Mheshimiwa Spika, Mashirika kama Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania *(TPDC)*, hayana uwezo wa kiutendaji kuelewa na/au kudhibiti gharama za uendeshaji za makampuni ya uwekezaji. Matokeo yake ni kwamba, gharama hizi zinakuwa kubwa na makampuni yanakuwa hayalipi kodi stahiki kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ichukue hatua za muda wa kati na za muda mrefu za kuelimisha idadi kubwa ya Watanzania katika fani za kitaalam za mafuta na gesi asilia ili tuwe na kada ya wataalam watakaotuwezesha kufahamu mbinu za makampuni zinazoyasaidia kutolipa kodi.

**MHE. MWANAMRISHO TARATIBU ABAMA:** Mheshimiwa Spika, katika kuichangia hoja hii ya Wizara ya Nishati na Madini, nitazungumzia kuhusu wachimbaji wadogo. Wachimbaji wadogo wanateseka sana. Je, Serikali inawapangia nini wachimbaji wadogo ambao maeneo yao yamechukuliwa na wachimbaji wakubwa?

Mheshimiwa Spika, nimeona katika bajeti yako wachimbaji wadogo wamepangiwa mikopo shilingi bilioni 2.5 pesa za ndani na dola za marekani milioni nne na shilingi bilioni 6.4 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, kawaida mdogo hufunikwa na mkubwa kwa maslahi ya mtu au watu. Mikopo hii ni lazima kuhakikisha ina wafikia walengwa, kwani kuna wachimbaji wengine huwa hawataki kuchimba ila hutaka kuhodhi maeneo halafu wanayauza kwa wachimbaji wakubwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara Nishati na Madini chini ya Waziri na Naibu Mawaziri, wazidi kuwa makini kuliokoa Taifa hili la Watanzania.

Mheshimiwa Spika, pili, uwepo utaratibu ambao utakuwa unawatambua na kuepuka wachimbaji wadogo kugombana na wachimbaji wakubwa ili kuepuka kuchangia maeneo.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji waongezewe thamani kwenye madini yao, kwa kujengewa viwanda vya kuongezewa thamani madini yao, kupatiwa

mashine za kukatia madini na Serikali ishughulikie bei za mashine hizo, wachimbaji wadogo watafutiwe masoko ya kuuza thamani zao. Serikali iwatafutie kipimo cha madini na kama kipo basi wauziwe kwa bei nafuu ili wakimudu.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi, kuwapongeza Waziri wa Nishati na Madini - Mheshimiwa Prof. Muhongo, Naibu Waziri wa Nishati na Madini anayeshughulikia nishati - Nheshimiwa George Simbachawene, Naibu Waziri wa Nishati na Madini - Mheshimiwa Stephen Masele, Katibu Mkuu mtani wangu Eliakimu Maswi na Watendaji wote walioshiriki kuandaa Bajeti hii nzuri, yenye mwelekeo wa kurudisha heshima ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kuwa, Wizara kupitia Waziri na Naibu Mawaziri, wakishirikiana na Katibu Mkuu Maswi, wamefanya kazi nzuri kwa kufuatilia Taasisi zake na kugundua Taasisi ya *TANESCO* imefanya ubadhirifu mkubwa wa kufuja fedha kwa kutoa *tender* kwenye makampuni ambayo yalikuwa yanauza mafuta kwa bei ya juu sana, yaani lita Shilingi za Kitanzania 1,800 wakati ilikuwepo kampuni iliyokuwa inataka kuuza kwa bei ya shilingi 1,500.

Mheshimiwa Spika, hivi kweli Mtendaji wa kuliokoa Taifa na uzalendo wa juu; ninaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu muwaunge mkono Watendaji wenye uzalendo kama Ndugu Eliakim Maswi. Kutafuta

taarifa mbalimbali kwa maslahi ya nchi siyo vibaya bali tusitumiwe na mtu au kikundi cha watu kwa maslahi binafsi. Tabia hii tutakuwa hatuwatendei haki Watanzania wanaotegemea sana uwakilishi wetu, vile vile tutakuwa tunawavunja moyo Watendaji na Mawaziri wetu. Ninapenda kumtia moyo Ndugu Maswi, akaze buti kazi yake ni ya mfano wa kuigwa.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Serikali kwa kutenga shilingi bilioni 140 kwa ajili ya kupeleka umeme vijijini. Pamoja na pongezi hizi, napenda kuendelea kuiomba Serikali ili ujenzi wa umeme vijijini uende haraka ni vyema fedha zilizotokana na kuongeza kodi ya mafuta ya taa ambazo zimetokana na kudhibiti uchakachuaji ya shilingi billion 300 zipelekwe *REA* pamoja na fedha zilizokuwa zinapatikana kwa ajili ya vinasaba sasa vinasaba vitoke kwani uchakachuaji haupo tena baada ya kupandisha bei ya mafuta ya taa nazo ni shilingi bilion kumi kwa mwaka ziende *REA.*

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kasi ya kupeleka umeme vijijini itaonekana haraka sana. Ninasubiri majibu mazuri kutoka kwa Mheshimiwa Profesa Muhongo, Waziri mwenye dhamana na Naibu Mawaziri wote wawili, wakati wakijibu hoja za Wabunge. Umeme ukifika kwa Watanzania wote utasaidia akina mama kuondokana na kupikia mkaa na kuni hadi wanakuwa na macho mekundu na wanauwawa kwa kudhaniwa wachawi.

Mheshimiwa Spika, napenda kurudia rai yangu kuwa kuna umuhimu wa pekee kwamba, Serikali ifanye bidii kutengeneza Sera na Sheria kabla ya kuanza

shughuli za gesi ili kuondokana na mikataba mibovu, jambo litakaloleta tija ya uzalishaji kupitia gesi asilia.

Mheshimiwa Spika, endapo gesi itasimamiwa ipasavyo, Taifa litapata shilingi trilioni 600; hii itatosha kutekeleza Miradi yote kwani Bajeti ya Serikali sasa ni shilingi trilioni 15 tu. Itaondoa umaskini na wananchi wote watanufaika kuanzia Mkoa wa Mtwara na Mikoa yote nchini.

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kuishauri Serikali kuanzisha Mfuko wa Mapato ya Gesi na utumike kutekeleza Miradi ya Maendeleo nchi nzima. Hii itaturahisishia kujua gesi imechangia kwa kiwango gani kuwaletea Watanzania maendeleo.

Mheshimiwa Spika, vile vile mipango ianze sasa ya kujenga viwanda vinavyotumia gesi; mfano, Kiwanda cha Mbolea, Kiwanda cha Kemikali na kadhalika ili uzalishaji na matumizi vianze mara moja miaka mitano mpaka minane ijayo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa kuendesha semina ya madini Singida na maeneo mengine nchini. Ninapenda kukiri kuwa, semina hiyo imesaidia sana kuwapa uelewa wachimbaji wadogo, watendaji wa vijiji na wananchi wanaozungukwa na migodi. Ninaiomba Serikali iongeze fedha za kuendesha semina na kuwawezesha fedha za kununua vitendea kazi. Tukiwakopesha wachimbaji, itasaidia wachimbaji kufaidi matunda waliyopewa na Mungu.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali ihakikishe mikataba yote ya madini inawekwa wazi na iwe yenye kuwanufaisha Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ninasisitiza kuwa *service levy* itokanayo na migodi iwe asilimia 0.3 kama sheria inavyosema, hatuna sababu ya kuyumba.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba Serikali maeneo yote yaliyoahidiwa kupelekewa umeme Mkoani Singida, itekelezwe kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyekiti wangu wa Kisekta, kwa kushiriki katika kutusaidia kuishauri Kamati masuala ya kitaalam, nasi kuyashauri mashirika ili kuimarisha ufanisi.

Mheshimiwa Spika, napenda kumalizia kwa kuunga mkono hoja.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, nami napenda kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza, napenda kuwapongeza Waziri, Mheshimiwa Muhongo na Naibu Waziri; Mheshimiwa Masele na Mheshimiwa Simbachawene, kwa kuteuliwa katika Wizara hii. Ni matumaini yetu kuwa upele umepata mkunaji.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwaambia kuwa, Watanzania watakuwa na imani nanyi kwa jinsi mlivyoanza kazi, tunawaombea Mwenyezi Mungu awape afya na nguvu zaidi ili mtuondoe tulipo.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri aniambie jambo moja wakati wa majumuiisho; Geita katika Kata ya Mtakuja, eneo la Nyakabale, kuna ardhi ambayo *GGM* waliihitaji na uthamini ukafanyika kwa ushirika kati ya Watendaji na Wawakilishi wa *GGM,* lakini cha ajabu wakati wa malipo ya fidia, mtu mwenye migomba 200 alilipwa migomba 50, miti ya mbao 300 kalipwa 70 na mambo mengi ambayo wamelipwa kwa kupunjwa. Hiyo ni miaka minane iliyopita, lakini wakazi hao wamefuatilia mpaka wamekaa chini. Katika Bunge la Saba niliuliza swali lakini jibu nilipewa kuwa *GGM* kwa sasa hawahitaji eneo hilo tena.

Mheshimiwa Spika, Wizara haijaenda hata siku moja kuwaambia hawahitaji eneo hilo. Pia Naibu Waziri aliyepita nilimwomba tuongozane aende akawaambie wananchi kuwa pesa waliyopewa wale lakini ardhi bado ni mali yao, alikubali lakini hatukuenda nae huko.

Mheshimiwa Spika, hebu tazama leo ni miaka ninane shughuli za maendeleo hazifanyiki. Naomba niulize kama baada ya Bunge hili tutaongozana na Waziri au Naibu Waziri ili tukawafariji watu hawa? Naomba kauli kutoka Wizarani ili wananchi hawa waweze kufanya shughuli zao za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, napenda nimwulize Waziri; miaka minane wananchi hawa hawafanyi shughuli za maendeleo; ni nani atawalipa gharama ambazo hawakufanya kilimo, hawakuendeleza makazi na hata kuziba maeneo nyumba zao zimebomoka?

Mheshimiwa Spika, kauli ya Waziri kwa wananchi hao. Naomba matamko yenu sana tena sana ili Wakazi wa Nyakabale wawe na amani.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. MAHMOUD HASSAN MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, sina shaka na utendaji wa Waziri na Naibu Mawaziri waliopo kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na imani kubwa niliyokuwa nayo kwa Waziri na Manaibu wake, bado kuna matatizo makubwa sana katika Wizara katika maeneo ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, nikianza na umeme ni tatizo kubwa sana na la kushangaza sana katika Tarafa ya Kibengu, iliyopo Wilaya ya Mufindi katika Jimbo la Mufindi Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, Bwawa la Kihansi lipo Tarafa ya Kibengu, yenye Kata tatu; Kata ya Mapanda, Kibengu na Ihalimbo zenye vijiji 17. Vyanzo vikuu vya maji vipo katika vijiji hivi na bwawa hili linatoa megawatt 184 kweneye Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, wananchi katika Tarafa hii, waliombwa zaidi ya miaka 15 iliyopita na Serikali kupitia *TANESCO*, kuacha kulima kwenye vyanzo vya maji na wananchi katika Jimbo langu walikubali na waliahidiwa kupewa umeme kama mbadala. Cha kusikitisha, leo ni zaidi ya miaka 15.

Mheshimiwa Spika, hitaji la Tarafa ya Kibengu ni *megawatt* mbili; hili linatusikitisha sana, tumemwona Naibu Waziri, tumekutana na Uongozi wa *TANESCO* nikiwa na Madiwani wangu kutoka katika Tarafa hii ya Kibengu, lakini cha kusikitisha tunapewa ahadi nzuri zisizotekelezeka.

Mheshimiwa Spika, nimeshawasiliana na Naibu Waziri, Mheshimiwa George Simbachawene, kwenye hili nataka nitoe angalizo Serikali inatakiwa itoe jibu ili wananchi wajue hatima yao.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, naomba nichukue fursa hii, kuishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kutekeleza ahadi katika Kata ya Ifwagi sasa umeme unawaka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi zangu, naomba sana Serikali hasa *TANESCO,* itekeleze ahadi yake ya kupeleka umeme katika vijiji vya Mfikilwa na Ikongosi. Pia wapeleke umeme kwenye Taasisi za Shule ya Sekondari ya Ifwegi na kwenye Gereza la Isupilo.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ambayo Serikali inatakiwa kutusaidia ni katika Vijiji vya Ludilo na Ilasa. Kuna Mradi wa *Mwinga Hydro Electricity* kwa ajili ya vijiji 13 katika Wilaya ya Mufindi. Kwa masikitiko makubwa sana, vijiji hivi ambapo umeme unapita vimeachwa. Tumeongea mara nyingi na Uongozi wa *TANESCO* na Wizara, lakini mpaka leo hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, napenda kusikia kauli ya Serikali kuhusu suala la umeme katika vijiji hivi.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni la Kata ya Rungemba, ambalo lilitakiwa kuwa tayari umeme unawaka na wananchi katika maeneo haya wameshalipwa fidia zaidi ya mwaka, lakini kwa masikitiko makubwa, kazi ya kuweka umeme katika eneo hili bado haijaanza mpaka leo. Naomba kusikia tamko la Serikali lini wataanza kazi ya kupeleka umeme katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, nataka nirudie tena, nina imani kubwa sana na uwezo wa Waziri, Mheshimiwa Prof. Sospeter Muhongo na Naibu Mawaziri wake; Mheshimiwa George Simbachawene na Mheshimiwa Stephen Masele, kwa gia kubwa waliyoanza nayo katika uchapakazi katika eneo hili la Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa George Simbachawene, kwa utendaji wake na pia nampongeza sana Mheshimiwa Stephen Masele, kwa ujasiri na uadilifu wake katika kusimamia haki katika maeneo ya Madini aliyoyatembelea katika Nyanda za Ziwa na Melelani.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba majibu kwenye hoja zangu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja na kumpongeza Waziri na Timu yake yote Wizarani, kwa matayarisho na uwasilishaji mzuri wa Bajeti.

Mheshimiwa Spika, nitajikita katika masuala mawili katika mchango wangu; Sekta ya Gesi na Umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa juhudi za kutafuta gesi na mafuta. Ugunduzi wa gesi Mtwara na Lindi ni habari njema kwa Taifa letu; hivyo, ni muhimu Serikali ikawekeza sana katika Sekta hii ambayo ndiyo itakuwa mojawapo wa ufumbuzi wa Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sana Serikali haraka iweke Sera Mahususi ya Gesi na Sheria ili zibainishe namna gani Serikali inaweza kusimamia kwa makini rasilimali hii muhimu ya gesi.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali ielekeze au iongeze jitihada zake kufikisha umeme vijijini ili kuchochea maendeleo hasa katika Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa mwenendo huu wa kutenga bajeti kidogo, itachukua muda kufikisha au kukamilisha mpango wake wa kufikisha umeme vijijini. Hivyo basi, Serikali haina budi kuongeza bajeti ya umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa uamuzi wake wa kupunguza gharama za kuunganisha umeme kwa karibu asilimia hamsini.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja na kukumbushia umalizaji wa Mradi wa Umeme Vijijini katika Wilaya ya Ulanga.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu, ambaye ameniwezesha kuwa na uhai na afya hasa katika Mwezi huu Mtukufu, awajalie wale wote ambao wameshikamana nayo heri kubwa ndani yake; amina.

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la madini. Pamoja na kuwa madini ni neema ya nchi yetu, lakini inaonekana kutosaidia ipasavyo wananchi hasa sehemu ambayo inachimbwa madini hayo.

Mheshimiwa Spika, mahusiano mabaya kati ya wawekezaji na wananchi, yanasababishwa na Sera na Mipango mibaya ya madini, hivyo, hupelekea wananchi kukosa fursa muhimu na huduma muhimu katika vijiji vyao. Utakuta mahusiano mabaya yanasabaisha maafa makubwa sehemu mbalimbali ambazo zinatoka madini. Wananchi kukosa imani na Viongozi wao na Serikali yao, Vijana wanakosa ajira na kubaki yatima katika nchi yao, vijana wanapojaribu kuokota baki ya mawe ambayo yameshapembuliwa dhahabu, wanauwawa kwa risasi pasipo huruma.

Mheshimiwa Spika, mahusiano mabaya husababisha uduni wa maisha ambamo wanazalisha madini, wananchi wanakosa elimu bora, matibabu bora, maji safi na salama, umeme na barabara safi, wanakosa huduma muhimu zote lakini Dhahabu, Almasi *Tanzanite*, Rubi na nyinginezo vinaondoka.

Mheshimwa Spika, Wananchi wanabaki na athari ya umaskini na uchafuzi wa mazingira katika vijiji; hii ni hatari na athari kubwa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, matatizo yanayowakumba wachimbaji wadogo ni sana. Miongoni mwa matatizo hayo ni urasimu mkubwa wa kutafuta leseni. Hili ni tatizo kwa wachimbaji wadogo na kupelekea kutumia gharama kubwa katika ufuatiliaji. Eneo moja kutolewa leseni mbili, bajeti hawafikii wachimbaji wadogo, zana duni katika uchimbaji, kukosa umeme maeneo ya uchimbaji, vitisho vinavyotolewa na baadhi ya viongozi, elimu na soko bora kwa thamani ya mali zao.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iangalie kwa umakini sana na kuboresha wachimbaji wadogo wadogo. Kwa mujibu wa Waziri wa Nishati na Madini wakati wa uzinduzi wa bomba la mafuta toka Mtwara hadi Dar es Salaam, Tanzania ina utajiri wa gesi yenye thamani ya shilingi trilioni 626.71, sawa na bajeti ya miaka 40 ijayo. Wasiwasi uliopo kwa watu walio wengi sasa hivi ni namna tutakavyotumia vizuri utajiri huu kuinua uchumi wa nchi. Mambo ya kuzingatia ili tunufaike ni lazima Serikali iweke wazi mikataba endelevu, uwezo wa kuvuna rasilimali hii hasa wataalam wa ndani na mengine yafananayo na hayo.

Mheshimiwa Spika, utajiri wa gesi usiwe laana kwa nchi yetu. Nchi nyingi zenye rasilimali kama gesi, madini na mafuta, zimeingia kwenye lindi la migogoro. Kama Taifa, tuwe makini sana ili kwa umoja wetu, Mwenyezi Mungu atuepushie mbali utajiri wa gesi usiwe laana bali ulete baraka. Nchi kama Nigeria walipogundua mafuta, kwa vile hawakujiandaa namna ya kufaidika na baraka hii, walijikuta wakiingia katika migogoro ya wenyewe kwa wenyewe ikiambatana na fujo na maandamano ya watu wa makundi mbalimbali ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba Serikali iwe makini tusifike huko.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. HIGHNESS S. KIWIA:** Mheshimiwa Spika, Mradi wa Umeme kupitia *MCC* ambao kimsingi kwa taarifa za awali kwa upande wa Kata zangu za Sangabuye (Kayenze) na Buswelu ulipaswa uwe umekamilika katika maeneo hayo, lakini mpaka sasa utekelezaji wake haujaanza. Kwa mujibu wa mkataba wa mkandarasi, kwa maeneo aliyokuwa amepangiwa, alipaswa kazi hiyo awe ameanza kufikia mwezi wa tisa mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, naomba nipewe ufafanuzi na sababu zilizopelekea Mradi huo wa Umeme kupitia *MCC* kutokuanza na kukamilika hadi sasa?

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Sina haja ya kurudia kutoa

pongezi, kwani walizopewa zinatosha sana, ninachotaka kusema nami naungana na wote waliotoa pongezi kwani wanastahili.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu wake na Watendaji wote, kwa kuwapatia umeme wa uhakika wananchi wangu wa Mtwara Vijijini na kutuhakikishia kupata *service levy* ya asilimia 0.3.

Mheshimiwa Spika, napenda kuihakikishia Wizara ya Nishati na Madini ushirikiano katika kutekeleza Mradi wa Bomba la Gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara kuhakikisha kuwa inasimamia maslahi ya Wananchi wa Mtwara Vijijini na Mtwara kwa ujumla. Wahakikishieni Wananchi wa Mtwara umeme wa uhakika, kazi kwenye Sekta ya Gesi na kuhamasisha wawekezaji kujenga viwanda Mtwara na pia watumie huduma kutoka Mtwara.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. GREGORY G. TEU:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Naibu Mawaziri na Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Spika, yahusu kuendeleza usambazaji umeme katika Makao Makuu ya Wilaya na Vijiji hususan katika Jimbo la Mpwapwa – Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naupongeza sana Wakala wa Nishati Vijijini *(REA),* kwa kazi nzuri wanayofanya kule

Jimboni Mpwapwa, ingawa bado kuna maeneo kadhaa ambayo kwa bahati mbaya, hayakuainishwa wakati maandalizi. Maeneo haya yamerukwa na kuachwa katikati, umeme utakapowaka maeneo haya yatakuwa yameachwa bila umeme.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Wakala wa Nishati Vijiji *(REA)* wanaoendelea na kazi hivi sasa Jimboni Mpwapwa, wasiondoke katika Jimbo la Mpwapwa bila kukamilisha usambazaji umeme katika maeneo yaliyoachwa siyo makusudi bali maelekezo hafifu ya awali. Kuondoka na kurudi tena kwa awamu nyingine, itakuwa gharama kubwa sana ukizingatia mitambo mikubwa inayotumika.

Mheshimiwa Spika, maeneo yanayohusika na kasoro hii ni haya yafuatayo:-

(a) Kata ya Matomondo (Jimbo la Mpwapwa), vijiji husika ni Chisalu, Tambi, Mlembule, Mwenzele, Mbori na Makuputa;

(b) Kata ya Lupeta (Jimbo la Mpwapwa), vijiji husika ni Bumila na Chang'ombe;

(c) Kata ya Chunyu/Nghambi (Jimbo la Mpwapwa), vijiji husika ni Kazania na Kiyegeya; na

(d) Kata ya Maze (Jimbo la Mpwapwa), vijiji vinavyohusika ni Isinghu, Kwamshango na Chiseyu.

Mheshimiwa Spika, inawezekana Wizara inao utaratibu wake ambao sipingani nao. Ninachoshauri ni

kwamba, *REA* wakiondoka katika eneo ambako wapo hivi sasa, kurudi tena baadaye (Awamu ya Pili), gharama zitakuwa kubwa ni kheri wamalizie kabisa kisha waondoke.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana *REA* kwa kazi nzuri wanayoifanya.

**MHE. ZAHRA ALI HAMAD:** Mheshimiwa Spika, Sera ni Dira, bila ya Dira mwelekeo wa safari unakuwa mgumu kufika. Wizara inachelewa kukamilisha Sera ya Gesi, naomba ikamilike ili kuonesha njia ili yale makosa makubwa ambayo tulifanya nyuma kama ya madini tusiyarudie tena, yanatia aibu na si aibu tu bali kudidimiza uchumi wa nchi yetu, ambapo asilimia kubwa ya wananchi wetu ni maskini, wasiotimiza milo angalau miwili kwa siku. Naomba Sera itekelezwe haraka sana ili lengo letu liweze kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, naungana na Waheshimiwa Wabunge wote ambao walichangia kuwa kwa vile mashine za kutengenezea vito ni za gharama sana, basi ni vizuri uchimbaji huo wakaachiwa wenyewe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na kumtakia Waziri na Manaibu wake heri na fanaka.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, ambaye kwa muda mfupi ameweza kuielewa Wizara yake vizuri na kuhimili changamoto zake.

Mheshimiwa Spika, naenda moja kwa moja kwenye hoja ya umeme vijijini. Kwa kweli *REA* wanajitahidi, nimevutiwa kuona kuwa robo ya Vijiji vya Wilaya ya Kalina vimetajwa lakini Waziri umeacha vijiji vifuatavyo: Kijiji cha ulindwanoni ambacho ndipo yapo Makao Makuu ya Wilaya ya Kaliua. Kwenye Kijiji hiki cha Ulindwanoni ndiko ambako na nyumba atakayoishi Mkuu wa Wilaya wa Kaliua ilipo. Naomba sana kijiji hiki nacho kijumuishwe.

Kijiji cha Usinge kutokana na wingi wa watu pale, takriban karibu watu 20,000 na pia kutokana na watu kujishughulisha sana na ujasiriamali wenye kuhitaji nishati ya umeme, mpaka wamefikia kubuni mbinu zao wenyewe za kuwa na nishati hii ya umeme, lakini wakati mwingine kwa mbinu ambazo siyo salama. Tulishapata ajali ya moto ambao uliunguza soko zima na maduka yaliyokuwa yamezunguka soko hilo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hii ndiyo maana Tume ya Wataalam ilipokuja kufanya *feasibility study* walipendekeza kijiji hiki kipewe jenereta. Naomba sana kijiji hiki kipewe jenereta hii. Vile vile namwomba Mheshimiwa Waziri akitembelee Kijiji hiki cha Usinge kama ambavyo Waziri aliyekutangulia alivyokuwa amewaahidi wananchi hawa.

Mheshimiwa Spika, katika *feasibility study* hiyo hiyo vijiji vifuatavyo viliwekwa katika utaratibu wa kupatiwa umeme:-

(a) Kata ya Ugunga: Vijiji vya Ugunga, Tuombemungu, Limbula, Limbula Siasa na Mkuyuni;

(b) Kata ya Igagala: Vijiji vya Imalampaka, Kamsekwa, Mtakuja, Kazanaupate, Wachawaseme na Kombe; na

(c) Kata ya Kazaroro: Vijiji vya Imalamihayo, Kazaroho, Igwisi, Usangi, Lukalanga, Usimba, Nsimbo na Kasungu.

Mheshimiwa Spika, naomba sana vijiji hivi vizingatiwe katika utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, mwisho, pale Kijijini Kasungu, Kata ya Kaliua, palitokea *explosion* kubwa sana wakati kampuni moja ya Wazungu walipokuwa wanachimba kisima ikabidi wakimbie baadaye wakaliziba shimo hilo. Tunahisi panaweza kuwa na gesi, naomba Waziri aje afanye utafiti wa kina mahala hapa maana huenda nasi tunaweza kuwa na neema hiyo ya gesi.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kumpongeza tena Mheshimiwa Waziri na kumtakia utendaji kazi mwema.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Waziri, Mheshimiwa Prof. Muhongo na Manaibu wake wote wawili, kwa kazi nzuri sana ya kuokoa mabilioni ya fedha yaliyotaka kuliwa na wajanja wachache; hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Umeme wa Rumakali – 222 MW, umo kwenye mpango wa kati wa kuzalisha umeme 2017, lakini nimeangalia Kitabu cha Hotuba ya Waziri sijaona hata setensi moja inayoelezea kuhusu Mradi huu. Wananchi waliokuwa wanasikiliza Hotuba wanahoji kwamba, Mradi huu umechakachuliwa tayari? Naomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, umeme vijijini; nimewakilisha maombi Wizarani na kwa Waziri (Naibu), kuhusu vijiji vilivyopitiwa na nguzo za umeme toka Mbeya kuja Makete. Vijiji hivi ni Kitulu, Ujuni, Nkenja, Isapulano na Luvulunge. Vijiji hivi vitaendelea kulinda nguzo mpaka lini? Naomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, ninaleta maombi Wizarani na *REA* kuhusu upelekaji umeme Kata ya Ipelele na Iniho (Makete). Wataalamu walikwenda kupima, napenda kujua upelekaji wa umeme utaanza lini?

Mheshimia Spika, Miradi ya Umeme wa Maji: Tumepeleka maombi ya Mradi wa Maporomoko Madogo Madogo katika Vijiji vya Ipelela na Iniho. Wataalam wamekwisha kwenda kupima eneo hili, ningependa kujua nini hatima ya Mradi huu wa Umeme? Naomba ufafanuzi.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mshimiwa Spika, napenda kusisitiza juu ya kuwanyonga wahujumu wa uchumi nchini. Kwa kuanza na hao ambao wamekuwa wakisababisha mgao wa umeme ndani ya *TANESCO* kwa makusudi na kisha tuingie Bungeni kuwakamata na kuwanyonga Wabunge wote wanaohusika kuunga mkono upuuzi unaofanywa na Watendaji wachache Serikalini.

Mheshimiwa Spika, kamwe *TANESCO* na Taifa havitaweza kuendelea kwa kuwalinda watu wote wanaowatetea watu kama akina Mhandisi Mhando, ambao wanataka kununua mafuta kwa bei ya juu. Hawa si wenzetu hata kidogo.

Iwapo mnaogopa kunyonga, tutunge Sheria nami mnipatie cheo cha kuwa Mnyongaji Mkuu tena kwa risasi hadharani baada ya mtu kupatikana na hatia ya uhujumu uchumi. Hakuna sababu ya kupoteza muda kila siku kulumbana Bungeni na nje ya Bunge kumbe kuna watu wachache wana maslahi yao wanayoyajua; hili halikubaliki.

Mheshimiwa Spika, naomba majibu wakati wa majumuisho ni lini utaletwa Muswada Bungeni wa kunyonga wahujumu uchumi?

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, asubuhi nilipotoa mchango wangu wa maandishi nilisahau kuwa Serikali iliahidi kupeleka umeme katika Tarafa ya Simbay (Makao Makuu), kupitia Wareta,

Dirma na Simbay kutoka Nangwa. Pamoja na kwamba, Mradi umeanza kutekelezwa, lakini umechukua muda mrafu; ni takriban miaka miwili, naomba kasi ya utekelezaji iendelee. Vilevile kulikuwa na Mradi wa Kupeleka Umeme Masakta, Masagaroda na Getesam, lakini ulisimama kutokana na ujenzi wa Barabara ya Minjingu – Singida. Ujenzi wa barabara umekamilika; hivyo, naomba umeme sasa upelekwe *REA*, waliniahidi kuweka umeme wa *solar* katika Shule zetu za Sekondari za Kata.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Hanang nitashukuru kama shule zetu zitanufaika na umeme ulioahidiwa.

**MHE. SYLVESTER M. KASULUMBAYI:** Mheshimiwa Spika, Jimbo la Maswa Mashariki na Wilaya ya Maswa kwa ujumla wake, umejaliwa kuwa na utafiti wa rasilimali za mifugo, pamba, alizeti, mbaazi, mpunga na ardhi nzuri inayokabiliwa na ukame na ina utitiri mwingi wa madini ya aina ya dhahabu, almasi, chuma, shaba, *nikel* na mengine mengi kama yanavyoonekana katika QDS 49/2, QDS 49/1, QDS 49/3, QDS 49/4, QDS 50/1, QDS 50/3 na QDS 35/3.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali kwa kupitia Wizara ya Nishati na Madini, wakati wa kuhitimisha ione haja ya kuiwekea mgawo wa umeme Wilaya hii katika Vijiji vyake vya Ipililo, Bushashi, Ngulinguli, Mwabayanda, Isageng‘he, Mbalagane, Mwakidiga, Mwadila, Mandang‘ombe na Gula.

Mheshimiwa Spika, vijiji hivyo vikigawiwa umeme, Maswa itaanza kuvitumia vipaumbele vyake vya

kuimarishia uchumi kwa kuzitumia rasilimali nilizozitaja. Umeme utasukuma uanzishwaji wa usindikaji wa ngozi ambazo zinapatikana kwa mamilioni ya tani, viwanda vidogo vya alizeti, uanzishaji wa kiwanda cha nyama, ng'ombe wanapatikana wa wingi uanzishaji wa kiwanda cha nguo, pamba huzalishwa kwa mamilioni ya tani katika Wilaya ya Maswa.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Maswa iliyopatiwa utajiri wa madini ya aina nyingi, wananchi kwa kutaka kuyavuna madini hayo, wameamua kujiunga katika Umoja wa Wachimbaji Madini Wadogo Wadogo wa Wilaya ya Maswa ambao umeshasajiriwa *BRELA.*

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo hawa wameviomba vibali vijiji vinavyohusika ili waanze kuchimba madini hayo na hivyo ninaiomba Wizara ya nishati na Madini iwatengee maeneo ya kuchimba madini hayo kufuatia maabara ya madini iliyoko Dodoma kuthibitisha kuwa sampuli zilizotumwa na wachimbaji zilithibitisha kuwepo kwa Dhahabu, Almasi, Shaba, Chuma, *Nikel* na mengine mengi.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji hawa wadogo ninaomba wapatiwe leseni ili waingie katika ajira isiyo rasmi na hivyo waweze kuujenga uchumi wa Maswa na kuchangia kuongeza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Manaibu wake; Mheshimiwa Simbachawene na Mheshimiwa Masele, wakishirikiana

na Kamanda Maswi kama Katibu Mkuu. Nawapongeza sana, nakumbuka miaka ya 1995 kama sijakosea huyu Katibu Mkuu alikuwa Mwanachama wetu wa NCCR-MAGEUZI; hongera sana.

Mheshimiwa Spika, walifanyika uamuzi wa kizalendo, kuthibitisha kuwa huenda kwa muda mrefu tumekuwa tukinunua mafuta kwa bei isiyo stahili; hivyo, napendekeza uchunguzi ufanyike tuweze kujua tangu mwaka 2006 tumenunua mafuta kwa bei isiyo stahili kwa kiasi gani na hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya wahusika. Kama tumeweza kushusha bei ya mafuta kutoka shilingi 1800 mpaka 1400 ni ushidi kwamba, kuna hasara kubwa tumepata.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu kujua na kushiriki karibu katika tafiti za gesi. Zipo zinatumia dola milioni moja kwa siku, gharama hizi ni kubwa sana na zitakuja kutuathiri baadaye wakati wa uzalishaji (*over expenditure concept).*

Mheshimiwa Spika, mfumo wa kupata au kununua umeme kutoka makampuni ya kukodi ni hasara kubwa. Nimefanya uchunguzi kwa kampuni chache tu za *AGREKKO, SONGAS, IPTL, SYMBION,* toka 2002 hadi 2012 tumepoteza zaidi ya shilingi trilioni moja. Hizi ni gharama ambazo tumezilipa pasipo kununua umeme. Hii mikataba haifai; hivyo, nashauri uangaliwe utaratibu wa kuondokana nazo.

Mheshimiwa Spika, napongeza kwa maendeleo ya ujenzi wa bomba la gesi, lakini tukumbuke kuwa ili kupunguza gharama ni muhimu tupate mitambo yetu

mipya, baada ya kupata gesi tuweze kufua umeme kwa kutumia mitambo yetu wenyewe.

Mheshimiwa Spika, napongeza majibu ya Naibu Waziri, Mheshimiwa Simbachawene, kwa uamuzi wa Wizara kuiingiza Wilaya Mpya ya Uvinza kwenye Mpango wa *REA*, kuhakikisha tunatumia ziada ya umeme unaopatikana Kigoma Mjini, kuhakikisha Wilaya Mpya ya Uvunza inapata umeme ndani ya mwaka huu wa fedha. Mradi wa Malagarasi utaleta Mapinduzi ya Kilimo na Viwanda na hivyo huduma na biashara na nchi za Burundi, Congo DRC na Zambia.

Mheshimiwa Spika, hoja ya Mwadui; mchakato mzima wa uchimbaji, usafirishaji wa uuzaji wa almasi bado unahodhiwa sana mwekezaji; hivyo, Serikali haina uhakika wa mapato na thamani ya almasi. Kwa maelezo zaidi, rejea Ripoti ya Uchunguzi iliyofanywa na Kamati ya *PAC* na kuwasilishwa hapa Bungeni Agosti 6, 2004 bila kujadiliwa kutokana na nguvu za kifisadi zilizokielemea Kiti na Bunge wakati huo.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naipongeza Wizara na Mawaziri wote katika Sekta hii ya Nishati na Madini, kwa Hotuba nzuri sana, yenye matumaini makubwa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa ushauri kama ifuatavyo:-

Tunaomba *REA* wapewe fedha zaidi ili kusambaza umeme vijijini kwenye Jimbo langu la Manyovu, ndiko kuliko na Wilaya Mpya ya Buhigwe ambayo matumaini

ya kupewa umeme yameoneshwa ndani ya Hotuba hii. Tunaomba tupewe kipaumbele cha umeme kwa wananchi wote wa vijiji vyote.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Manyovu, kuna Hospitali ya Heri Mission, yenye umeme. Rai yangu ni kwamba, *REA* waangalie namna ya kusaidia ili umeme huo uweze kusaidia taasisi za karibu na wananchi walio karibu na chanzo hicho. Ninawaomba *REA* wafike na kutoa ushauri na kutuarifu juu ya hatua ya kufanya.

Mheshimiwa Spika, ninaomba vijiji vitakavyopata umeme Kigoma, Jimbo la Manyovu, Wilaya Mpya ya Buhigwe, isisahaulike. Nilitaka kujua katika vijiji 25 ni vingapi ndani ya Jimbo la Manyovu.

Mheshimiwa Spika, tunaomba ukaguzi wa mita za luku uendelee kuchunguzwa ili zisimwonee mteja au *TANESCO.*

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kuokoa shilingi bilioni sita za ununuzi wa mafuta. Nasi kama Wabunge, tunawapongeza Wizara kwa hatua hiyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nawatakia mafanikio mema na ninaunga mkono hoja.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Nishati na Madini, kwa Hotuba nzuri aliyowasilisha Bungeni leo. Nawapongeza Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu wa Wizara na Watumishi wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini ni Wizara muhimu sana katika maendeleo ya nchi yetu. Kwa kuwa na Nishati hata uchumi unakua kwa kasi, kwani nishati ya umeme ni kichocheo kikubwa cha kukua kwa uchumi. Nichukue fursa hii kuishukuru Wizara na Serikali kwa ujumla, kwa Mradi wa *MCC,* unaofanya kazi ya kupeleka umeme katika Mikoa sita ya Tanzania, Geita ikiwa ni mojawapo. Kwa sasa nguzo zinasimikwa kwa kasi sana hasa katika Jimbo la Busanda kule Bukoli, Nyarugusu, Rwamgasa, Katoro, Bukondo, Chigunga na Nyachiluluma. Ninaomba nipate taarifa ya utekelezaji hasa kujua ni lini umeme huu utawaka. Sambamba na hili, naiomba Serikali ihakikishe umeme huu unapelekwa katika Sekta muhimu katika jamii mfano katika Shule za Sekondari, Vituo vya Afya na Zahanati.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba, ukurasa wa 51 imezungumzia kuwa uchimbaji mdogo ni mojawapo ya vyanzo muhimu vya ajira, lakini sijaona Wilaya ya Geita kutengewa maeneo kwa ajili ya uchimbaji mdogo. Ninaomba wakati wa majumuisho, nipate maelezo juu ya wananchi wangu wa Nyarugusu, Nyaruyeye na Buziba kwamba wametengewa maeneo wapi?

Mheshimiwa Spika, maeneo niliyoyataja wananchi wake wamekuwa na kilio cha muda mrefu sana juu ya kutotengewa maeneo ya uchimbaji. Sera Mpya ya Madini ya 2010 imebainisha wazi kabisa kwamba, Serikali itatenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Sasa basi naiomba Serikali iwaangalie

wananchi hawa, iwatengee maeneo ya uchimbaji hasa katika maeneo niliyoyataja.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kuhusu mikopo na mitaji. Ukurasa wa 52 wa Hotuba umezungumzia kwamba, Serikali ilitenga shilingi bilioni 119 mwaka 2011/12 na kwamba, fedha hizi zimetumika kwa ajili ya ukopeshajii na ukodishaji wa vifaa kwa wachimbaji wadogo maeneo ya Rwamgasa, Wilayani Geita. Naomba kujua hao wananchi waliopewa hizo fedha ni akina nani na wamepata fedha kiasi gani? Hili litanisaidia kuwapa ufafanuzi wananchi hasa wachimbaji wadogo wa Geita.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa mawazo yangu katika hoja hii kama ifuatavyo:-

Napenda kumpongeza sana Waziri na Manaibu wake, kwa kuteuliwa kwao kushika Wizara hii. Kama Mheshimiwa Rais alivyo na imani nanyi, ndivyo nami nilivyo na imani na ninyi. Mungu awasimamie mfanye kazi vizuri kwa niaba ya Watanzania na faida kwa nchi. Pia naomba Katibu Mkuu akaze boot, Mungu atamsaidia pamoja na Watendaji wote.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nipongeze utaratibu wa kupeleka umeme vijijini. Nawaomba tu msipunguze kasi kwani ndiko kundi kubwa la vijana lilipo ambalo halina ajira, kwa kupeleka umeme vijijini vijana wengi

watajiajiri; hivyo, nami naomba niombee baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Ndago, inasikitisha kwamba, umeme umeishia Ndago Madukani tu, lakini ukienda mbele kuna Shule ya Sekondari ya Kata (Ndago Sekondari), ambayo inahitajii umeme lakini pia ndiko anakoishi (nyumbani) kwa Mbunge huyu anayeandika mchango huu. Kwa miaka mingi nimekuwa nikiomba angalau ufike pale shuleni, ombi hilo halijazaa matunda mpaka leo. Hivyo, naomba sana tupeleke umeme Kijiji cha Kibaya, Ndago Sekondari.

Mheshimiwa Spika, maomba umeme upelekwe Urughu – Kata na Mtekente - Kata katika Wilaya ya Iramba.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba, Bajeti hii itapelekea kupata umeme katika Wilaya Mpya ya Mkalama. Niombe tu isichukue muda mrefu pamoja na Ikungi kwani kwenda kwa haraka kutapelekea maendeleo ya haraka katika Wilaya hizi mpya.

Mheshimiwa Spika, kutokana na tatizo la maji katika Mji wa Singida, Mkoa ulipata Mradi wa Maji katika Kata ya Mwankoko, ambao ungemaliza tatizo la maji. Tatizo kubwa ilikuwa ni umeme ambao *TANESCO* wanatakiwa wapeleke ili kuwasha mitambo ya kupampu maji hatimaye kusambaza kwa Wakazi wa Mji wa Singida.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Waziri, ambaye mara

baada ya kumpa ki-*note* cha kumweleza tatizo hili, alinijibu kwa barua rasmi ya tarehe 10 Julai, 2012, yenye kumbukumbu Na. CBD,248/324/02/94. Kweli hapa namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, naomba wahusika tafadhali msimwangushe kama alivyoahidi kutekeleza Mradi huu katika mwaka huu wa fedha wa 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, suala la ugawaji wa viwanja vya madini naona bado lina utata hasa katika kutoa leseni. Hivi ni kwa nini Serikali isiweke utaratibu, mara wanapotoa leseni waende kwa wananchi husika kupitia Serikali husika ili wamtambulishe mwekezaji wa eneo husika kutoa masharti mapema kuliko ilivyo sasa, kwani mwekezaji anapoomba leseni, Serikali bila kujali kama eneo lile lina wachimbaji wadogo wadogo ama hakuna, wao wanatoa tu leseni. Kweli wachimbaji wadogo wanaweza wakawa hawajavamia eneo husika, lakini ni vyema kutoa taarifa mapema na kama wameshavamia pia wapewe utaratibu mapema.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Serikali ikapime madini yanayochimbwa katika Tarafa ya Ndago, Luzelukulu na Mbelekese, kisha iniletee majibu hapa Bungeni. Pia nitapenda kujua ni mwekezaji gani amepewa leseni na ni ya kuchimba ama ya utafiti na kijiji husika au kata wananufaikaje.

Mheshimiwa Spika, napongeza sana Maonesho ya Vito yaliyofanyika Arusha Mount, Meru Hotel. Yalifana sana na wanunuzi walikuwa wengi na watu wetu waliuza na wengine walirudisha fedha bila kupata vito, hivyo inaonesha ni jinsi gani soko lilikuwa zuri.

Mheshimiwa Spika, nashauri Maonesho yote yaboreshwe na iwe kila mwaka, lakini tuwaandae watu wetu vizuri ili angalau kuwa na soko la uhakika na tutoe elimu ya kutosha waache kupunjwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kama itakuwa vyema, endapo madini yetu ya asili ambayo duniani kote hayapo ni hapa tu, yaani *Tanzanite,* tuyatengenezee utaratibu ama Sheria kwamba yawe ni Nyara ya Taifa, yaani kama ilivyo pembe za ndovu na kadhalika kuwa na utaratibu ili kuwadhibiti watu wanaopora na kuyapunguza thamani madini yetu.

Mheshimiwa Spika, namwamini Mheshimiwa Waziri, akae na Watendaji wake aone jambo hili, kama litafaa chukua huo ushauri najua utapata ushindani, lakini baadaye vizazi vijavyo vitakushukuru.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nashukuru kwa mwaliko wa Wizara nilioupata kwenda kushiriki Maonesho ya Vito vya Thamani Arusha. Nilijifunza mengi na nimewasaidia sana wajasiriamali wangu (vijana) wa madini kupata *contact* na soko moja kwa moja. Ahsanteni sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Spika, nakupongeza kwa kuniruhusu kuchangia kwa maandishi. Kwanza, namshukuru Mola wangu kwa kunipa uzima na kuweza kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, kwa Hotuba yake inayowapa matumaini Watanzania. Nawapongeza pia kwa kupunguza bei ya umeme kwa wananchi ambao wanataka kuingiza umeme.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna vyanzo vingi vya kuleta umeme hapa Tanzania kama vile makaa ya mawe na gesi asilia. Kwa hiyo, naomba Serikali vile vijiji vilivyo na vyanzo hizo basi lazima vionekane haraka kwa kupatiwa umeme.

Mheshimwa Spika, hivi sasa Mtwara kuna gesi ya kutosha kwa umeme na tayari kazi imeshaanza chini ya Wachina; kwa hiyo, sehemu ile vijiji vyake vipate umeme.

Mheshimiwa Spika, Ngaka kuna makaa ya mawe ambayo yameshaanza kuchimbwa na kupelekwa nje ya nchi; kwa hiyo, nashauri Vijiji na Wilaya yake wafaidike na umeme wa mkaa wa mawe ili wafaidike na umeme kwa mali inayotoka sehemu yao.

Mheshimiwa Spika, nazidi kuunga mkono hoja na pia nazidi kukushukuru wewe.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, mimi nachukua fursa hii kuchangia Hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kero za wananchi waliozungukwa na migodi; wananchi waliozungukwa na migodi wamekuwa wakiishi katika mazingira magumu licha ya kuwa na rasilimali nyingi zilizowazunguka. Pamoja na hayo, kumekuwa na ahadi hewa nyingi wanazopewa na wawekezaji kama vile kuwajengea shule, kuwachimbia visima, kujenga zahanati na kadhalika, lakini yote hayo yamekuwa hayafanyiki, zaidi ya kuwachia mashimo na mahandaki yenye kuhatarisha maisha yao na ardhi hiyo haifai tena kwa kilimo. Yote hayo kumekuwa na kesi nyingi za unyanyasaji wa wananchi hao pindi wanaposogea maeneo ya migodi ikiwemo kupigwa, kujeruhiwa, kuuwawa, kupigwa risasi za moto na kesi hizo zimekuwa hazijulikani hatima yake.

Je, kwa nini Serikali hawafuatilii ahadi za wawekezaji kwa wananchi ili ziende sambasamba na utekelezaji wao?

Je, mpaka sasa ni kesi ngapi zimeshatolewa hukumu kuhusu unyanyasaji wa wananchi katika migodi?

Mheshimiwa Spika, ni hatua gani zilizochukuliwa kwa wawekezaji waliotoa ahadi kwa wananchi zisizotekelezeka?

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara hii haioni sasa hivi ni wakati mwafaka wa kuweka mikataba yao wazi ili kila mwananchi ajue, kwa sababu ni rasilimali ya Taifa na mikataba hiyo iandikwe kwa Lugha ya

Taifa ili mwananchi aelewe ili kuondoa migogoro baina ya wananchi na Serikali?

Mheshimiwa Spika Serikali ina mpango gani wa kuwafidia wananchi ambao ardhi yao imeharibikwa na wawekezaji ambayo haifai kwa kilimo wala kwa shughuli zozote za maendeleo?

Mheshimiwa Spika, Serikali hii imekuwa ikiwapuuza, kuwadharau na kuwanyanyasa wachimbaji wadogo wadogo na kuwakumbatia wewekezaji wakubwa kutoka nje, ambao wamekuwa wakikwepa kulipa kodi hata Serikalini. Nchi nyingine huwawezesha wachimbaji wadogo wadogo, aidha kwa kundi kubwa au vikundi vidogo vidogo kuwa wawekezaji wazawa kwenye maeneo yao. Wachimbaji hawa wadogo wadogo hawana elimu na wala Serikali haijatenga bajeti ya kutosha ya kuwasaidia wachimbaji. Kutokana na Serikali kutotaka kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo wadogo kwa makusudi, inasababisha wachimbaji wadogo wadogo kuharibu mazingira.

Je, lini Serikali itaona kuna umuhimu wa kutoa elimu ya kutosha kwa wachimbaji wadogo wadogo ili waweze kujiajiri wenyewe na kupunguza tatizo la ajira kwa Serikali?

Je, lini Serikali itaona kuna umuhimu wa kuwawezesha wachimbaji wadogo wadogo kuwa wawekezaji wazawa na kuwatafutia masoko ya uhakika?

Mheshimiwa Spika, tatizo la uchakachuaji wa mafuta, limekuwa likiongezeka siku hadi siku. Inaonekana uvumbuzi wake ni mgumu kupatikana, pengine kuna mahusiano mazuri baina ya wachimbaji na watu husika. Muda mrefu kumekuwa hakuna hatua zozote zinazochukuliwa dhidi ya wachakachuaji hao, lakini ikiwa itatumika sheria ya kuweka mipira yenye kuonesha nishati hiyo katika vituo vya mafuta tofauti na sasa hivi mipira hiyo ni meusi, hata mtu kufanya ubadhirifu ni rahisi kwa wenye vituo. Kumekuwa na vituo vya mafuta vinavyojengwa holela kwenye makazi ya watu na kuwasababishia usumbufu wananchi hao na kuhatarisha maisha yao.

(a) Je, Serikali na Wizara ina utaratibu gani wa kukagua visima vyote vya mafuta na kuhakiki vilivyo bora ili kuepusha uchakachuaji wa mafuta?

(b) Je, mpaka hivi sasa ni vituo vingapi vilivyopata adhabu kutokana na kuchakachua mafuta au pampu?

(c) Je ni mara ngapi kwa mwaka vituo vya kuuzia mafuta vinakaguliwa?

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na usumbufu mkubwa wanaoupata wananchi katika maombi ya kufungiwa mita mpya au kubadilisha mita. Tatizo lingine ambalo linawakera wananchi ni kununua umeme katika njia ya mtandao wa simu za mkononi na kutoupata umeme huo kwa muda unaotakiwa au kukosa kabisa na kupoteza pesa zao.

(a) Je, Wizara ina mikakati gani ya kuhakikisha kuwa usumbufu wanaoupata wateja wa kufungiwa mita umekwisha?

(b) Wizara na Serikali wana mikakati gani kukomesha wizi huo kwa wananchi wanaonunua umeme bila kupata umeme na bila ya kurudishiwa pesa zao?

**MHE. SALEH A. PAMBA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nampongeza sana Waziri, Mheshimiwa Muhongo, Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Masele na Mheshimiwa Simbachawene, kwa uteuzi wao. Tuna matumaini makubwa kwao.

Mheshimwa Spika, nawapongeza tena kwa Hotuba nzuri sana, yenye kuleta matumaini mapya kwa Sekta hii ya Nishati na Madini. Ninayo maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutupatia gesi ya kutosha. Gesi iliyopo hapa nchini inatosha kwa zaidi ya miaka 100. Kinachotakiwa ni kuwa na Sheria nzuri na usimamizi wa Sekta ya Nishati. Gesi isaidie pia maendeleo ya maeneo ambayo gesi inatoka. Makampuni ya gesi yasaidie maendeleo ya maeneo hayo, hatutaki *scenario* ya *Delta* kama ya Nigeria hapa.

Mheshimiwa Spika, gesi hii isiishie Dar es Salaam pekee, ifike katika Mikoa mingine kama Tanga, Morogoro ili kukuza uchumi.

Mheshimiwa Spika, ninataka kujua hatua iliyofikiwa katika kupeleka umeme katika Kata ya Mkaramo. Kwa kuwa kila kitu kimekamilika; michoro, upembuzi yakinifu na gharama ni shilingi 742,000,000; je, kazi hiyo itaanza lini?

Mheshimiwa Spika, namwomba Profesa na Timu yake waendelee na uzi huo huo, tupo pamoja nao.

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ardhi ni suala mtambuka, tunafahamu kwamba, kwenye ardhi kuna kila kitu chini ya ardhi na juu ya ardhi. Mungu katupenda, nasi tumshukuru kutupa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nianze na suala zima la ardhi na vilivyopo juu kwamba, ardhi ni rasilimali watu, wanyama, mimea, mito, maziwa madogo na bahari kuu zote zapendeza na misitu. Ardhi ni rasilimali kwetu, yahitaji kutunzwa kwa hali na mali. Ndani yake mna ardhi, chini kuna mali pia. hebu tuone harakati za ugunduzi wa madini mara zote wachimbaji wadogo ambao ni wazawa wa eneo husika kinachosikitisha ni baada ya kugunduliwa wale wachimbaji wadogo wanaondolewa na Serikali na kupewa wawekezaji; hivi ni nani katuroga? Mifano ni mingi, mikataba mibovu iangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, Madini ya *Tanzanite* kule Arusha yaligunduliwa na wazawa, lakini kwa sasa machimbo yote yako chini ya Makaburu, hata madini ya *Tanzanite* kwa sasa katika Soko la Kimataifa

yanauzwa kwa Nembo ya Makaburu. Kwa sasa madini yanapatikana maeneo mengi, ikiwemo *Rubby.* Dhahabu imegundulika Kondoa, Dodoma na aina nyingi zaanza kuonekana huko. Nafikiri baada ya muda mfupi, wananchi hawa wataondolewa katika maeneo haya na kuletwa wawekezaji, harufu ipo.

Mheshimiwa Spika, niongelee mapato yatokanayo na madini. Kwa mujibu wa Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini ya 2012/13, bei ya dhahabu na madini mengine imepaa kwa kiasi kikubwa katika Soko la Kimataifa. Siamini sisi kama Taifa tumeweza kwendana na kasi ya mabadiliko ya bei hii. Tumezidi kuruhusu makampuni yafaidi rasilimali zetu bila mpangilio, tunachofaidi zaidi ya mrabaha ni mapato yatokanayo na kodi ya makampuni *(Corporate Tax)*. Serikali ieleze faida tunayoipata kutokana na madini hasa baada ya kupanda kwa bei.

Mheshimiwa Spika, kwa nini wachimbaji hawana hati miliki au hawawezeshwi kupata hati miliki ya maeneo ya uchimbaji? Kasumba hii ya kuendelea kuwasujudu wawekezaji hasa wa nje, kuwawezesha kupata hati miliki huku tukiwaacha watu wetu itaisha lini? Tuna vijana wetu wengi wasomi na ndiyo wanaovumbua madini hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inaingia hasara kubwa sana ya kulipia gharama za kusimamia kesi ambazo tulipoteza au tulishindwa.

Mheshimiwa Spika, umeme ni kero kubwa kwenye maeneo yetu. Kama tatizo ni maji mbona Tanzania ina

maeneo mengi ya kuwekeza maji tukapata umeme. Kama tatizo ni maji umeme asilia si upo kwa nini wananchi wasipatiwe mafunzo ya jumla wakapata umeme?

Mheshimiwa Spika, watu wetu wengi ni maskini hawawezi kulipia gharama za umeme kwani utakuta mtu ana nyumba ya vyumba vinne na kadhalika, analipia bili kubwa kuliko mwenye mashine ya kuranda mbao au mashine ya kusaga nafaka. Unajiuliza mwanzo alikuwa analipia bili ndogo ghafla inapanda mara mbili ya hapo; hivi kwa mtindo huo tutapata wateja wengi?

Mheshimiwa Spika, mita za umeme zinazolipiwa *TANESCO* kwa bei kubwa mno hufanya mtu wa kawaida kujenga nyumba na kushindwa kuweka mita; alipie nguzo, achangie; hivi kwa kipato gani hicho? Sasa umefika wakati Serikali iangalie masuala haya na kutoa elimu kwa umma ni kiwango gani watu wachangie?

Mheshimiwa Spika, mafuta ya umeme yanahujumiwa na wafanyakazi wenyewe wa *TANESCO* na kuwauzia wafanyabiashara na kusadikiwa wapo wanayoyatumia kwa kukaangia chipsi, samaki na matumizi mengine. Je, mafuta haya hayana madhara kwa binadamu?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kwa maandishi kuhusu Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, naanza na mgao wa umeme; hili limekuwa tatizo kubwa sasa na kwa muda mrefu hakuna taarifa yoyote inayotolewa hasa katika Jiji la Arusha. Wiki mbili zilizopita kulikuwa na kukatika sana kwa umeme ila kinachosikitisha zaidi ni kujulikana kwa taarifa hizi za baadhi ya watu Serikalini, kukata umeme kwa makusudi kabisa, kwa kipindi cha muda fulani ili tu kununua mafuta kwa ajili ya ku-*run equipments.* Hapo hapo kuna *deal* ya ufisadi, hivyo kunufaika na manunuzi hayo kupitia makampuni ya mafuta yaliyoshindikana au kupewa *tender* hiyo kwa ajili ya maslahi ya baadhi ya watu binafsi, ambao sitaki kuwataja hapa kwani Kanuni zetu za Bunge haziruhusu kutaja majina ya watu moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, athari za kukatika umeme au mgao linavyoweza kuiathiri jamii na nitatoa mifano au kuzungumzia zaidi hospitalini.

Mheshimiwa Spika, pengine nikiongea kwa mifano halisi tunayokutana nayo katika maisha, nadharia inaweza kusaidia kuona uhalisia na kusababisha watu waseme basi imetosha na hasa hao ambao wamekuwa wakileta mgao feki. Katika hili tukifikiria umeme kwa njia mbadala zaidi ya mwanga, tutapata sababu nyingine ya kuendelea kuhamasisha mapambano kwa maisha bora. Mfano, hospitalini na katika mazingira ya *theatre* kuna *emergency* au *operation* iliyokuwa inaendelea kisha unaambiwa

mgao umeanza na umeme utarudi baada ya 12 na wagonjwa wote uliokaa nao hali mbaya kila mmoja analia maumivu makali na *imagine* nchi ambayo wafadhili wamenunua Pls za kutosha kisha kwa sababu uhifadhi ni mbovu jamani.

Mheshimiwa Spika, angalia suala zima la uhifadhi wa damu, inaelekea kuna maeneo ambayo kuna jenereta kama sehemu za mjini lakini mahali kama Kibakwe, Longido, Katesh na kadhalika na Wilaya za pembezoni hili litawezekana vipi?

Mheshimiwa Spika, tatizo la kuhifadhi maiti linawapa wakati mgumu sana wahudumu wa *mortuary* zetu.

Mheshimiwa Spika, wagonjwa waliopo nchi nzima, mtu anajua kafika hospitali, anategemea kupona baada ya kuwekewa mashine ya *oxygen* kwa ajili ya kumwongezea hewa, *but* ghafla umeme unakatika na anaambiwa hautarudi baada ya 12 hrs.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili linasababisha vifo ambayo hata Mwenyezi Mungu hakuviita bado. Kwa hali hii maisha bora yatatokea wapi jamani? Tutapunguza lini vifo visivyo vya lazima kwa wananchi wetu, halafu unasikia ni mkakati wa baadhi ya watu ili wafaidike na fedha.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze mchango wangu na suala la madini.

Mheshimiwa Spika, sasa ni miaka mingi sana nchi yetu inafanya kazi hii ya uchimbaji wa madini, lakini kinachosikitisha na kushangaza ni kuwa, kwa muda wote huo Serikali na Wananchi kwa ujumla tumekuwa hatufaidiki na rasilimali hii ambayo Mungu ametujalia nayo.

Mheshimiwa Spika, siyo siri na ni ukweli kwamba, hata wale wananchi ambao wanaishi katika maeneo yanayotoa madini, hawafaidiki na maisha yao yanaendelea kuwa duni.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tumegeuka kivuli cha mvumo, kivuli kinafaidisha walio mbali. Tumekuwa tukishuhudia wageni ambao tunawaita wawekezaji, wanafaidika kwa kuchukua madini yetu na kwenda kufaidisha nchi zao na familia zao huku wakiiacha Tanzania na watu wake tukiwa duni. Kama hiyo haitoshi, baadhi ya wawekezaji wanatoa rushwa kwa baadhi ya wenye mamlaka na wanawafungulia akaunti nje ya nchi na kuwawekea mamilioni ya dola ili wapate nafasi ya kuendelea kuihujumu nchi.

Mheshimiwa Spika, kama tulipoteza kwenye madini sasa itoshe. Naomba niseme kwamba, gesi hii tulionayo kama hatutakuwa makini, hili ni bomu ambalo tunatembea nalo na tusipokuwa makini tukalichezea litaturipukia.

Mheshimiwa Spika, Nigeria walipopata mafuta kwa kuwa hawakuwa wamejiandaa, waliingia katika vita vya wenyewe kwa wenyewe kutokana na Serikali kukosa kuzingatia kwamba, mafuta yalikuwa ni mali ya

watu wote na hivyo wachache tu ndiyo waliokuwa wanafaidika.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuomba kwamba, kwa kuwa Watanzania wote kuanzia Rais, Mawaziri, Wabunge na hata Wananchi; Wakulima na Wafugaji walioko Mijini na Vijijini, wote wameweka matumaini yao katika gesi hii iliyopo nchini. Naiomba Serikali iwazingatie zaidi wale wananchi ambao wapo katika maeneo ambayo gesi imepatikana na tuache kutoa nafasi ya wachache kujinufaisha wao na familia zao ili kuiondoa nchi yetu na matatizo yanayoweza kutokea kama yalivyowapata wenzetu wa Nigeria.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Zanzibar nako imeonekana kuwepo kwa mafuta na gesi, naomba Waziri utakapofanya majumuisho uwaeleze Wazanzibari msimamo wa Serikali ya Muungano ili waanze kazi ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi kwa maslahi yao na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naomba kauli ya Serikali juu ya jambo hili ili kazi hii iweze kuanza kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo ya Waziri wa Nishati na Madini, imebainika kuwa kuna upotevu wa fedha unaofanywa na Watendaji wa *TANESCO,* kwani iliarifiwa kwamba, *TANESCO* inakusanya jumla ya

shilingi bilioni 60 mpaka 70 kwa mwezi na jumla ya shilingi bilioni 10 mpaka 15 ikiwa ni matumizi ya mwezi. Je, fedha nyingine zilizobakia zinakwenda wapi?

Kutokana na sababu hizo, tunaomba Wizara itoe ufafanuzi halisi wa fedha zinazobakia baada ya matumizi hayo. Pia ninaishauri Wizara ikaze buti katika suala la mapato na matumizi ya *TANESCO*

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ihakikishe kwamba katika nchi yetu hii hakutakuwa na mgao wa umeme na siku ikitokea kukatokea mgao wa umeme basi Uongozi wa Wizara uwajibike bila ya kushurutishwa.

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. Pili, nampongeza Waziri na Naibu Mawaziri, kwa mwanzo mwema, ujasiri na utendaji kazi wa hali ya juu na ushupavu walionao. Mnatakiwa mjichunge na kujilinda na watu ambao walikuwa na maslahi binafsi na sasa inaonekana kufikia tamati.

Mheshimiwa Spika, nawashauri mpitie upya Mikataba ya Madini na ile itakayoonekana ina harufu ya ufisadi na haina maslahi na nchi ni bora ifutwe mara moja au ipitiwe upya.

Mheshimiwa Spika, nahitimisha kwa kutaka kauli ya Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa gesi ni kati ya masuala ya Muungano je, ni lini Sera ya kutandika bomba hilo kuelekea Zanzibar itaanza?

**MHE. ABDALLA HAJI ALI:** Mheshimiwa Spika, Mwenyezi Mungu ni mkubwa, muweza wa mambo yote na ni mwenye Rehema kwa waja wake.

Mheshimiwa Spika, aidha, nakupongeza wewe binafsi kwa Uongozi wako mahiri na imara katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu ningependa kutoa nasaha zangu kwa Waziri wa Nishati na Madini, Manaibu wake na Watendaji wote.

Mheshimiwa Spika, takriban Wabunge wote na wananchi mbalimbali wamekuwa wakimpongeza Rais kwa kusadifu vyema katika uteuzi wa Waziri wa Nishati na Madini. Hivyo, namwomba Waziri aitunze heshima hii ambayo Rais kampatia Waziri.

Mheshimiwa Spika, Waziri na Makamu wake wawili wamejitwika jukumu zito na sote tunakiri kwamba, kazi yao ni nzito na ngumu sana, lakini kwa umahiri na uadilifu wa Waziri, Wananchi wamejenga matumaini na wana imani nao na dalili njema zimeanza kujitokeza mapema. Wananchi wanafurahia kauli za Waziri hata pale aliposema kwamba, hakuna sababu ya mgao wa umeme uwezo tunao.

Mheshimiwa Spika, pia wananchi wanafurahia sana kwa kupunguziwa gharama za kuunganisha umeme vijiji na mijini; tunaipongeza Wizara na Watendaji wote juu ya hili.

Mheshimiwa Spika, Hotuba ya Waziri imekuwa nzuri na bora sana, kwani ni Hotuba pekee ambayo

imeliunganisha Bunge lako na Wabunge wote, bila kujali itikadi za vyama vyao, wamekuwa wamoja katika kumwunga mkono Waziri na Wasaidizi wake juu ya jambo hili. Hii imedhihirisha ile dhana ya kulitaka Bunge liwe la kisasa na liwe Bunge moja ili kukidhi haja na matakwa ya wale ambao wametuchagua ili kuwawakilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Waswahili wanasema: "Mti mwema hupozwa na matunda yake." Maana ni kwamba, mti ukizaa matunda mema hupopolewa kana kwamba kuzaa umefanya makosa. Hivyo, Waziri na Manaibu wake ni watu makini na ni watu safi. Je, Watendaji wa chini wakoje?

Mheshimiwa Spika, ili kuitunza heshima hii ya Rais kwa kuwateuwa nyinyi na kumfanya Rais uteuzi wake uwe wa mafanikio na ninyi pia mwendelee kung'ara kama mlivyoanza, basi ni wakati sasa wa kuisafisha Wizara yenu na kuwaondoa wale wote ambao hawawajibiki kwa maslahi ya umma bali wanajinufaisha wenyewe na kuididimiza nchi.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri na Manaibu wake, wasimamie haki na Mungu atawapa nguvu juu ya jambo hili, msitishwe, msirubuniwe, msihongeke, msiyumbishwe na wala msiogope. Nawaomba huo ufisadi unaotajwa mpambane nao na mhakikishe hata mkifika kusulubiwa basi na waliosababisha muwe mmekwisha wasulubu.

Mheshimiwa Spika, kama Rais alivyowaamini na sisi tujenge imani kubwa juu yao na nawasihi sana

watende kazi zenu kwa umakini mkubwa ili wasije kumwangusha Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mungu awape nguvu na uvumilivu Mheshimiwa Waziri na Timu yake katika kazi zao.

**MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nampa pongezi nyingi Waziri, Naibu Mwaziri na Katibu Mkuu wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanayofanya. Pia nawapongeza sana kwa kugundua njama za kuliweka Taifa hili katika giza kwa azma ya kupata utajiri wa haraka.

Mheshimiwa Spika, tumamshukuru Mungu kwa kutujalia kugundua gesi nyingi katika nchi yetu. Tunaloliomba Wazanzibari ni kuwa mipango itayarishwe ili gesi hiyo baadaye ifike Zanzibar, kama ulivyofika umeme. Hatua hii itasaidia sana kupunguza matumizi ya makaa na kuni na hivyo kuhifadhi mazingira ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya bei ya mafuta ya taa kupandishwa, uchakachuaji wa mafuta umepungua kwa kiwango kikubwa. Serikali pia imeweza kuokoa zaidi ya shilingi bilioni 40.00 kwa mwezi. Tatizo kubwa lililobaki ni mafuta yanayokwenda nje ya nchi, wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu hutumia nafasi hii kwa kuyabakisha mafuta hayo hapa nchini, yaani mafuta hayavuki mipaka yetu kwenda nchi za jirani yalikokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, naiomba *EWURA* na *TRA* wajipange na kujitayarisha ili kulidhibiti suala hili, kwani fedha nyingi sana zinapotea kwa njia ya kushusha shehena za mafuta nchini. Njia za kufanya ni kuweka petroli kuhakikisha magari ya mafuta yanashusha shehena zao nje ya nchi.

**MHE. ZARINA S. MADIBA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri na Watendaji wote wakiongozwa na Katibu Mkuu. Nina imani kubwa sana na Timu hiyo ya Wizara na ninaamini itaweza kuikomboa nchi yetu kiuchumi kwani umeme ni nyenzo kubwa sana katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni ngumu sana kwani imegubikwa na ufisadi wa muda mrefu sana hadi wamefanya ni haki yao kula rushwa. Ninawaomba msiwe na wasiwasi kabisa, tupeni taarifa ya ukweli hata ikibidi kvunja kanuni kwa maslahi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali sasa inafaa kuangalia hizi Sheria au Kanuni kama hii ya Manunuzi. Kanuni na Sheria hii imekuwa ikitumiwa vibaya kukandamiza ufanisi wa sehemu mbalimbali na kulinda ufisadi. Sisi kwenye viwanda vya nchini tumekuwa tukilalamikia Sheria hii. Tunaomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha sasa aone umuhimu wa kuiangalia Kanuni au Sheria hii ya manunuzi ili zile Kanuni zinazolinda ufisadi zirekebishwe na zile zinazoshindilia viwanda vyetu pia zibadilishwe.

Mheshimiwa Spika, mafuta ya taa ni njia moja kuu ya chanzo cha nishati vijijini. Mafuta ya taa yamekuwa yakitumika pia kwenye vitotozi (*incubator*) vijijini, ambazo zinawasaidia akina mama kufuga kisasa. Kutokana na bei ya mafuta ya taa kupanda, akina mama hawa wamelazimika kuviachia vitotozi hivyo na kupata hasara. Wanawake hao waliweza kutotoa vifaranga 100 kila mwezi na kupata vifaranga zaidi ya 1,000 kwa mwezi, ukilinganisha na vifaranga 352 kwa mwaka. Ninaomba bei ya mafuta ya taa iangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja ya kusaidia wachimbaji wadogo wadogo. Naomba nielewe *interest* ya ndugu zangu kuwa washiriki. Ninaona jinsi wanavyohangaika kwa kutumia nyenzo duni. Vijana hao wakisaidiwa wanaweza kuchangia Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ameyasema mengi mazuri kwenye Hotuba yake, ni kitanzi watu wana *expectation* kubwa sana na ninyi. Niwaombee kheri, amani na msiogope tupo pamoja nanyi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, nachangia hoja katika eneo la kodi za migodi ya madini kwa Halmashauri za Wilaya ambazo zina migodi. Sheria ya Fedha ya Halmashauri za Wilaya ya Mwaka 1982 inataja vyanzo vya fedha kwa Halmashauri na moja ya vyanzo hivyo ni asilimia 0.3 ya mapato ya migodi. Wakati huo huo Mgodi una

mkataba na Serikali ambao una kipengele ambacho kinazuia mgodi kulipa asilimia 0.3 ya mapato yake na badala yake unataka ulipe dola laki mbili tu kwa mwaka. Dola laki mbili kwa mwaka ni pesa kidogo sana, ukilinganisha na mapato ambayo migodi inapata na asilimia 0.3 ya mapato ni kiwango ambacho Migodi inaweza kulipa bila kuathiri mapato au faida.

Mheshimiwa Spika, rai yangu ni kwamba, Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982 ilitungwa na Bunge na hivyo inapaswa iwe kubwa na itawale ile ya Mkataba wa Mgodi na Serikali. Kipengele cha Mkataba wa Mgodi na Serikali kinachozuia migodi kulipa asilimia 0.3 ya mapato yake yote ya mwaka na badala yake kulipa dola laki mbili tu kwa mwaka kiondolewe kabisa na migodi yote ianze kulipa asilimia 0.3 ya mapato yake kwa mwaka kama ushuru wa huduma.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kusoma vizuri Hotuba na kwa kuchapa kazi vizuri. Ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ya kwanza ni umeme. Tunataka umeme Lindi, Newala, Kilwa, Liwale na Ruangwa kwani gesi ipo, tatizo ni nini?

Mheshimiwa Spika, TPDC wapewe pesa za kutosha ili waweze kusambaza umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, tunaomba wachimbaji wadogo wasaidiwe katika Mkoa wa Lindi nako kuna Madini ya kutosha. Wilaya zote katika Mkoa wa Lindi kuna madini kama ifuatavyo: Wilaya ya Ruangwa kuna *Green Garnet*, *Green Tomaline*, Safaya, Dhahabu na Unga wa Rangirangi; Wilaya ya Nachingwea kuna Dhahabu na Safaya; Wilaya ya Lindi kuna *Gypsum* na Chumvi; Wilaya ya Kilwa kuna *Gypsum, Gas* na Chumvi; na Wilaya ya Liwale kuna Dhahabu, Safaya na Madini ya Vito.

Mheshimiwa Spika, tunaomba wasaidiwe mikopo ili waweze kuchimba madini watu wapate ajira.

**MHE. OMARI R. NUNDU:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuipongeza Wizara kwa Hotuba nzuri na pia kwa matayarisho mazuri ya Hotuba na kazi za Wizara. Kwanza, nampongeza kwa kutuhakikishia kuwa mgao wa umeme hautakuwepo tena; hii ni faraja kubwa. Pia ninaipongeza Wizara kwa kupunguza tozo la kuunganisha umeme, kitu ambacho kitachochea uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono kuongeza bajeti ya usambazi wa umeme vijijini. Hapa ninaomba Wizara ivipatie umeme mapema vijiji vyote ambavyo miundombinu ya umeme tayari ipo, vijiji ambavyo vimepitiwa na nyaya za umeme. Katika Vijiji vya Kibafuta, Chongohani, Mkembe, Machui, Kisimatui, Pande A na Pande B.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Tanga umebainika kuwa na Madini ya Vito vya Thamani vya aina nyingi

bali Vito hivyo vinauzwa nje na nyakati nyingine kupitia nchi jirani kwa sababu Tanga hakuna Kituo cha Kuboresha Vito hivyo.  Ninaiomba Serikali ilifanyie kazi suala la kuanzisha Kituo hicho.

Mheshimiwa Spika, imedhihirika kuwa Mmea wa Mkonge una matumizi mengi pamoja na uzalishaji wa umeme; ni wazi kuwa jitihada za dhati zikifanywa basi vijiji vingi vilivyoko kwenye Mashamba ya Mkonge na Miwa vitafaidika hivyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nimpongeze Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Profesa Muhongo (Mb), Manaibu Waziri wake; Mheshimiwa Simbachawene (Mb) na Mheshimiwa Maselle (Mb).  Pia pongezi zangu zimfikie Ndugu Maswi, Katibu Mkuu, kwa ujasiri wake na Timu yake yote.  Nawapongeza Watumishi wote wa Wizara na Idara zake walio waaminifu.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niulizie ule mpango wa kupeleka mashine za kuzalisha umeme katika Wilaya ya Mafia umefikia wapi na pia mchakato mzima wa usambazaji umeme vjijini nao upo katika mchakato gani au umefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, naomba sana Wizara inisaidie kutoa taarifa kuhusu michakato hiyo miwili niliyoisema.

**MHE. SAMIA SULUHU HASSAN:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeonesha mwelekeo mzuri katika Sekta ya Nishati. Naomba jitihada za kuondoa ufisadi kwenye Sekta hii ziendelee hatua kwa hatua. Nashauri nguvu pia ielekezwe upande wa madini kwani nako pia kuna ufisadi wa kutisha.

Mheshimiwa Spika, Viongozi wa Wizara wajiepushe na vishawishi vya matamanio kwa Wabunge Wanawake wenye sifa dhaifu na baadaye kuwashushia heshima na haiba yenu.

**MHE. ALLY KEISSY MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ichunguze mafuta yote yanayopelekwa kwenye mitambo yote ya *TANESCO* nchi nzima na hasa iliyopo Dar es salaam. Yanapelekwa mafuta hewa kabisa, idadi ya mafuta siyo halali, ni wizi ilhali shahili. Pia zabuni za nyaya za umeme kupewa mtu binafsi kwa upendeleo wakati kuna kiwanda ambacho Serikali ina hisa wala huwa hawajulishwi kabisa hiyo ni rushwa ya wazi kabisa na dalili ya kuuwa viwanda vyetu.

Mheshimiwa Spika, naomba umeme unaotoka Kigoma Mpanda – Sumbawanga – Iringa upitie kwenye Vijiji vya Kasu, Lyazumbi, Paramawe, Mwai, Mtenga, Mashete na Londokazi. Vijiji hivyo vyote vipo njiani katika Barabara ya Mpanda – Sumbawanga. Pia naomba ahadi ya Naibu Waziri aliyekuwepo

Mheshimiwa Adam Malima katika ziara yake ya Namanyere Nkasi, alituahidi kutuongezea nguzo kwa kilomita tano.

Mheshimiwa Spika, naomba pia umeme kwenda Bandari ya Kipili na Kirando utekelezwe haraka sana. Kwa sasa vinasaba haitakiwi kwa kuwa mafuta ya taa na dizeli bei sawa ila hiyo shilingi sita kwa lita itolewa mara moja.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri wote wawili, kwa kazi nzuri waliyoanza nayo ambayo inaleta matumaini.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali itekeleze mipango hii yote mizuri tuliyosomewa katika Hotuba ya Waziri. Naishauri Serikali idhibiti uchimbaji wa *Tanzanite* ambayo ni madini yanayopatikana Mererani Mkoa wa Manyara. Madini haya hayawanufaishi Watanzania wengi, yamekuwa yakisafirishwa zaidi Kenya. Naiomba Serikali idhibiti uuzwaji huu holela ili Watanzania wengi waweze kufaidika.

Mheshimiwa Spika, tatizo la umeme limekuwa likisumbua sana, hali inayopelekea hali ya maisha kuwa ngumu, kusimama kwa uzalishaji viwandani, vijana kukosa ajira maana wengine wamejiajiri kwenye shughuli mbalimbali zinazotumia umeme kwa mfano saloon na nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, tumeona wenzetu Thailand wanakabiliana na tatizo la umeme kwa kutumia miwa,

takataka. Naishauri Serikali iangalie ni jinsi gani tutakabiliana na tatizo hili hasa pale kina cha maji kinapopungua.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kazi kubwa inayofanya katika kushughulikia tatizo la umeme. Pia isimamie vyema ujenzi wa Bomba la Gesi kutoka Kilwa hadi Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kusimamia vyema Mradi wa Umeme katika Jimbo langu la Kisarawe. Nawashukuru sana Watendaji wa Wizara na *TANESCO.* Namshukuru Ndugu Mramba wa *TANESCO* na Watendaji wenzake, kwa kuona umuhimu wa kusimamia Mradi wa Umeme Kisarawe hadi Msanga.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu wote wawili, Katibu Mkuu na Timu nzima, kwa lengo na dhamira ya dhati ya kufanya *re-formation* Wizarani. Nawashukuru kwa kupunguza gharama za kuunganisha umeme hasa vijijini. Nikipata fursa ya kuzungumza nitagusia, lakini pia ningependa kujua *destination* na *beneficiaries* wa *Sub-station* ya *KIA.*

Mheshimiwa Spika, la pili, ningeomba Miradi yote ya Umeme *(On Going Projects)*, iliyokuwa Arumeru iendelee kama ilivyopangwa kwenye ramani, mingi imesimama kwa sasa. *Finally,* ninaunga mkono jitihada

zote chanya zenye lengo la kuipatia *REA* fedha zaidi kwa ajili ya kutekeleza Miradi yote hususan ya *Phase II* ili na vijiji vyangu vya Arumeru vipate kufikiwa na umeme. Tungependa kufahamu Wizara inategemea kukamilisha lini Miradi ya *REA Phase II?*

Mheshimiwa Spika, nawatakia kila la kheri katika mkakati wa kufanya *re-formation* Wizarani na siyo *transformation*.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa hatua za mwisho za kukamilisha Mradi wa Umeme wa Mwandoya. Kwa kuwa Wizara inatekeleza Mradi wa Kupeleka Umeme Makao Makuu ya Wilaya ya Itilima; na kwa kuwa kutoka Itilima kwenda Mwandoya (Makao Makuu Jimbo la Kisesa) ni kilometa 40 tu: Je, Serikali wakati inatekeleza Mradi wa Itilima itaunganisha na Mwandoya ili pia kuunganisha na Makao Makuu ya Mkoa wa Simiyu?

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri kwa agizo la kutaka Kampuni zote zilizochimba madini kwa miaka mitano na kuendelea, zianze kulipa kodi ya mapato bila kuleta visingizio. Nampongeza kwa ujasiri huo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ameagiza wafunge migodi na waondoke, lakini hajasema ni lini agizo hili litaanza kutekelezwa na hatua atakazochukua kwa wale watakaokaidi. Naomba afafanue.

Mheshimiwa Spika, kuendeleza uchimbaji mdogo wa madini katika aya ya 171, maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uchimbaji mdogo yenye jumla ya hekta 105,163 na kwamba Serikali itatoa bilioni 8.9 kuendeleza wachimbaji wadogo. Kwa nini Serikali haijatenga maeneo ya wachimbaji wadogo katika mgodi wa Mwadui katika Vijiji vya Maganzo na kadhalika?

**MHE. SALUM KHALFAN BARWANY:** Mheshimiwa Spika, idadi ya Watanzania wanaotumia nishati ya umeme ni kiasi kidogo sana, kwani taarifa inayoelezwa hapa ni asilimia 17 tu ya Watanzania wote na zaidi ya asilimia 83 nchini hawapati umeme. Hii ni dhahiri kabisa tupo nyuma kama Taifa katika matumizi ya umeme.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Mikoa ya Mtwara na Lindi kuiokoa nchi hii kwa kuwa na nishati ya umeme, bado hatuoni katika Gridi ya Taifa na Waziri hajasema lolote katika hili.

Hatuna Wataalamu wa kutosha katika taaluma ya Gesi nchini; ni vyema tukawa na Chuo cha Wataalamu wa Gesi ambao watadhibiti rasilimali. Sera ya Sheria ya Gesi ni muhimu kuletwa kwa haraka, haikuwa vizuri kuanza Mikataba kabla ya Sera na Sheria hiyo. Nataka Serikali ifanye haraka kuleta Sera hiyo katika Bunge la Tisa, Novemba, 2012.

Mheshimiwa Spika, gharama ya kuunganisha umeme kupunguzwa ni vyema katika Mikoa ya Kusini. Wizara ingeifikiria zaidi Mikoa hiyo kupatiwa ahueni ili

wajisikie wao hasa wameisaidia Nchi badala ya Tshs. 177 kama ilivyokubalika katika Km. 4 katika maeneo ya Mtwara, eneo liongezwe.

Mheshimiwa Spika, Mataifa mengi Duniani yameingia kwenye vurugu baada ya kupatikana madini katika Mataifa haya. Tukiruhusu Mataifa ya Nje kumiliki rasilimali hii, Mikataba inatufunga hata tukihitaji kufanya marekebisho tunashindwa.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu tumiliki hisa kwa asilimia kubwa na ikiwezekana asilimia zote zimilikiwe na Serikali.

Mheshimiwa Spika, suala la Gesi ya Mikoa ya Lindi na Mtwara hatutarajii tu kupata umeme wa kuwasha la hasha, hatutarajii tu kupewa ahadi ya kujengewa shule, zahanati na barabara hapana. Tunahitaji *industrialised area,* eneo la kiuchumi na uchumi endelevu. *Automaticaly,* hayo tunayoahidiwa yatakuja yenyewe baada ya uchumi wetu kuimarika, uchumi unaojitegemea.

Mheshimiwa Spika, tunajiuliza kwa nini Kituo cha Gesi kijengwe Bagamoyo badala ya kujengwa Mtwara au Lindi? Miji hii kwa nini isiwe Miji ya Gesi kwa maana ya Miji ya Viwanda?

Mheshimiwa Spika, tuna sifa na vigezo vyote vya kuwa Miji ya viwanda; kwa nini Dar es Salaam? Tuna *Natural Habours* ambazo zingeweza kusafirisha gesi yetu katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kugundulika kwa gesi Mikoa ya Kusini, Lindi ikiwa ni mojawapo inatarajiwa kutoa mwanga na matumaini ya miaka mingi ijayo. Nasema hivi kwa kuzingatia kwamba Mikoa hii imekuwa nyuma na imetengwa kwa muda mrefu sana kimaendeleo. Gesi hii sasa iwe ni Mwanga Kusini, ilete baraka Kusini, ilete dira mpya Kusini na zaidi ya yote ibadili taswira nzima ya Mikoa hii ya Kusini. Ni vema Serikali ikaweka mkakati wa kuanzisha Ukanda wa kiuchumi imara katika Mikoa hii ili iweze kuleta manufaa ya kweli badala ya kuishia kutoa maji, madawati na mengine yafananayo. Naungana na watu wengi wanaotahadharisha kuwa gesi hii ilete baraka na si laana, tujipange.

Mheshimiwa Spika, tangu wiki hii ianze, kumekuwepo na ushabiki, shutuma na nyingine zinazofanana miongoni mwa Wabunge kuhusiana na tuhuma ndani ya Wizara hii. Kitendo hiki kinaleta udhalilishaji mkubwa kwa Bunge mbele ya jamii. Naishauri Wizara iyafanyie kazi mawazo yote yaliyotolewa hasa yale yanayohusu Wizara ili kuepuka aina yoyote ya ubadhirifu. Hiki ni kiashiria tosha kwamba wapo watumishi ndani ya Wizara waliokubuhu kwa rushwa kiasi kwamba wanapata ujasiri wa kuligawa Bunge kwa kuwashawishi baadhi.

Mheshimiwa Spika, wakati Bunge linajitahidi kujisafisha, Wizara nayo ijipange kujiimarisha. Waziri, Manaibu Waziri wote na Katibu Mkuu watumie sifa, baraka na moyo waliopewa na Wabunge kuliletea Taifa manufaa. Waangalieni wasije wakalewa sifa wakapoteza mwelekeo.

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Timu ya Watendaji wote, kwa kutuletea Bungeni Hotuba yenye kurudisha matumaini mapya kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atueleze ahadi yake ya kuwa mgao wa umeme Tanzania basi! Je, amejipanga kiasi gani kwani Wizara yake imezungukwa na Ufisadi?

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini iliwaahidi Wakazi wa Wilaya ya Rufiji wanaoishi katika maeneo ya karibu na mpaka wa Nyamisati kuwa umeme wataupata kupitia *REA.* Je, ni lini Wananchi hawa watapatiwa nishati hii muhimu ili nao waweze kujikwamua kiuchumi?

Mheshimiwa Spika, Wananchi wangu wanaoishi maeneo ya Ikwiriri wanalalamika kuwa Meneja wa *TANESCO* katika Tarafa ya Ikwiriri na Watendaji wake wana tabia ya kuwaongezea gharama za ankara ya umeme tofauti na matumizi wanayotumia.

Mheshimiwa Spika, je, utaratibu huu ni sahihi? Namwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie Wanarufiji wanyonge.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. RASHID ALI OMAR:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nachukua fursa hii kumshukuru kwa dhati Mwenyezi Mungu, kwa kunijaalia mimi na Wabunge wenzangu kuwepo katika Bunge lako hili tukiwa wazima wa afya na kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu ambayo ni muhimu sana kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu wa maandishi, naomba kwa heshima ya Bunge lako, nianze kwa kukushukuru wewe binafsi, kwa kuendesha vikao kwa umahiri na umakini, kwa hekima na busara; Mungu akusaidie zaidi.

Mheshimiwa Spika, pili, shukrani zimwendee Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano, kwa uteuzi wake wa Uongozi wa Juu wa Wizara hii ya Nishati na Madini, kwa kumteua Waziri, Naibu Mawaziri na Katibu Mkuu mpya. Wote wanaonesha kila dalili za uchapaji kazi unaohitajika; kwa mfano, kwa muda mfupi waliweza kugundua na kuokoa shilingi bilioni sita ambazo zilikuwa zipotee kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa za Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini wakati wa uzinduzi wa bomba la mafuta toka Mtwara hadi Dar es salaam, inaonesha Tanzania inao utajiri wa gesi yenye thamani ya Shilingi trilioni 626.71 za Tanzania. Hii tunaweza kuikadiria kwamba ni kiasi cha bajeti yetu isiyopungua miaka 35 - 40 ijayo. Hofu na wasiwasi wangu ni namna gani tutakavyousimamia na kuutumia utajiri huu ili kuinua uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ili tunufaike na utajiri huu ni lazima utajiri huu usiwe wa laana. Nchi kama Nigeria walipogundua mafuta kule kwao kwa vile hawakujiandaa vyema juu ya namna gani ya kufaidika na neema hii, walijikuta wakiingia katika migogoro ya wenyewe kwa wenyewe, ikiambatana na maandamano ya watu wa makundi mbalimbali ya kijamii, yaliyoleta uvunjifu wa amani na kusababisha vifo vya watu.

Mheshimiwa Spika, naomba niishauri Serikali na Wizara hii tuwe na tahadhari juu ya mgao wa neema kwa wale wadau walio katika maeneo yatakayozalisha madini hayo.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa madini yanayotarajiwa kuvunwa kwa wingi ni *Uranium*. Lazima Serikali na Wizara iangalie madhara kiafya ya binadamu na madini haya.

Mheshimiwa Spika, naomba niishukuru Serikali, ni dhahiri kwamba Mheshimiwa Rais Kikwete ametuteulia Waziri na Watendaji Wakuu wenzake wa Wizara mahiri. Sisi Wabunge wa Bunge lako tutashikamana na Mheshimiwa Profesa Muhongo na wenzake (Watendaji) wa Wizara, kuchambua na kuchunguza uzembe, ubadhirifu na ufisadi katika Wizara hii muhimu inayosimamia maisha ya watu wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, naomba niishauri Serikali kuwa, sisi Wabunge tuko pamoja nanyi, lakini atakaebainika kuhujumu uchumi wetu, achukuliwe hatua kali.

Mheshimiwa Spika, kama Serikali itakusudia tunaweza kuondoa hujuma na kulipeleka Taifa letu pazuri. Ahsante.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Waziri, ukurasa wa 9 kifungu cha 15, imeelezwa kuwa kuna maendeleo katika Sekta ya Madini kuhusiana na migodi hulipa mrabaha wa asilimia nne. Bahati mbaya mgodi uliotajwa kulipa mrahaba huo wa asilimia nne ni *Geita Gold Mine* pekee. Ninataka kuelewa kwa nini Mgodi wa North Mara wa Barrick na Bulyankuru na migodi mingine haikuorodheshwa katika walipaji wa mrabaha huo mpya?

Mheshimiwa Spika, *STAMICO* imeingia makubaliano ya ubia na *Tanzania American International Development Corporation (2000) Limited* katika suala la madini kwa asilimia 45 kwa 55. Pia *STAMICO* wemeingia Mkataba wa Makubaliano ya Ubia na *Obtala Resources Limited* kwa hisa ya asilimia 50 kwa 50. Kitendo hicho ni kizuri na kitawafanya Watanzania waweze kushiriki kwenye suala la madini.

Mheshimiwa Spika, tatizo lililopo la Serikali yetu ni juu ya kuchangia asilimia zetu zinazotuhusu, wakati wote huwa hatuchangii ipasavyo, matokeo yake yale mazuri yanayotegemewa huwa hayapatikani.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ielewe kuwa nchi yetu inakabiliwa na tatizo kubwa la kugeuka jangwa kulingana na ukataji mkubwa wa miti kwa ajili ya nishati

ya kupikia, aidha kwa kupikia kuni au mkaa, kwa sababu wananchi wanahitaji kuni kwa kupikia chakula na kwa vile hakuna nishati mbadala ya kupikia ni lazima wategemee misitu kwa kupikia.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeajiandaa vipi katika kupata nishati mbadala ili nchi yetu iepukane na kuingia kwenye jangwa?

Mheshimiwa Spika, uzoefu uliopo katika nchi yetu ni kuingia katika mikataba isiyo na tija kwa wananchi. Hilo limedhihirika katika Mikataba ya Migodi ya Uchimbaji wa Dhahabu. Hivi imeshapatikana na *Urani* ipo tayari pengine mwaka 2013 itachimbwa. Kwa hofu ya mikataba ya nyuma; je, Serikali ipo katika nafasi gani katika Mkataba wa Uchimbaji wa *Urani* na gesi?

Je maslahi ya nchi yamezingatiwa au maslahi ya wawekezaji tu ndiyo yaliyozingatiwa?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa Neema na Rehema zake nyingi anazaonineemesha; ni wajibu kutamka *Alhamdulillah*.

Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa mchango wangu, nachukua fursa hii kumpongeza Raisi wetu mpendwa, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa upeo alionao wa kuweza kumwona na kumteua Profesa Sospeter Muhongo, kuiongoza Wizara hii. Pia nampongeza kwa dhati Profesa Muhongo, kwa uwezo,

bidii, juhudi, maarifa na zaidi uzalendo wake kwa nchi yetu. Nawapongeza pia Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Masele na Mheshimiwa Simbachawene na Katibu Mkuu, Bwana Eliakim C. Maswi. Napenda kuwaambia kazeni buti na Wabunge tupo pamoja nanyi.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ina jukumu na dhima kubwa kwa ustawi wa uchumi wa nchi yetu na wananchi mmoja mmoja kwa ujumla. Nishati ya umeme ni nyenzo muhimu sana kwa maisha ya kila siku na maendeleo yao na ya nchi. Serikali kupitia Wizara hii na hasa kwa timu hii mpya, iwe makini sana ili nchi ipate umeme wa uhakika kuondoa aibu ya mgao. Nchi kama Tanzania, iliyojaaliwa vyanzo vingi vya umeme kuliko nchi zote Barani Afrika isipokuwa Congo tu (DRC), ni aibu sana kukosa umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, tatizo lililothibitika la ukosefu wa umeme nchini ni hujuma za kifisadi za makusudi zilizokuwa zikifanywa na Wizara na Taasisi zake! Hotuba ya Wizara hii imetoa matumaini, lakini Serikali kupitia Wizara hii isimamie Sera zilizopitishwa na ikatae vishawishi vya kifisadi kwa maslahi ya nchi hii. Wizara isimamie upunguaji wa gharama za umeme ambazo ni kubwa sana kwa sasa, kiasi ambacho watu wa kipato cha chini ambao ni asilimia 75 ya Watanzania wanashindwa kuzimudu.

Mheshimiwa Spika, wakati umefika sasa Serikali kuileta Bungeni Mikataba yote ya Uzalishaji Umeme ili kubaini mikataba yote mibovu na ama tuirekebishe au tuifute kabisa. Wakati wa kuwaachia wawekezaji

kuzalisha umeme ambao haununuliki kwa Mikataba ya Kifisadi sasa umepita.

Mheshimiwa Spika, ni wakati mwafaka pia kuileta Bungeni Mikataba ya Madini ili tuiangalie na tuisaidie Serikali kuishauri namna ya kuirekebisha. Mapato ya nchi kutokana na madini hayaridhishi! Hatua zichukuliwe, bado hatujachelewa sana. Bunge ni Mhimili muhimu sana kati ya Mihimili mitatu ya Dola. Serikali sasa iwe karibu na Bunge ili kuliendeleza Taifa Letu. Wakati wa Serikali kufanya maamuzi yasiyo na tija utaliangamiza Taifa hili, ambalo mimi binafsi najivunia.

Mheshimiwa Spika, Serikali itoe maamuzi kwa Madini ya Vito kama *Tanzanite, Saphire, Ruby* na kadhalika yachongwe nchini. Hii itasaidia kuongeza ajira kwa vijana wetu, lakini pia kongeza thamani ya madini yenyewe na hivyo kuongeza mapato. Ni aibu kwa madini ya *Tanzanite,* yenye jina la nchi yetu, kuchongwa Nairobi Kenya na hivyo kutoa taswira kama madini hayo ni ya asili ya Kenya. Namwomba Mheshimiwa Waziri alishughulikie jambo hili ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. ESTER AMOS BULAYA:** Mheshimiwa Spika, Serikali ihakikishe Kampuni ya *Tanzanite One,* kabla haijaingia Mkataba mpya kuzingatia yafuatayo:-

- Ihakikishe inakamilisha ahadi zake za kupeleka maendeleo kwenye jamii inayozunguka mgodi huo, kuna malalamiko hawajatimiza ahadi hizo.

- *Tanzanite* hawajalipa mrabaha wa dola milioni mbili; nini hatima ya fedha hizo?

- Kampuni ya *GGM* nayo imekwepa kulipa (*Service Levy*) tangu mwaka 1999 wakati Sheria inawataka kulipa asilimia 0.3 ya mapato katika Halmashauri.

- Mmejipanga vipi kuhakikisha mnawadhibiti Mafisadi waliojipanga kuhujumu Miradi ya Gesi ili waendelee kuuza mafuta mazito?

- Watu wenye leseni ambao wamekumbatia maeneo lakini hawayafanyii kazi wanyang'anywe. Tunajua wapo vigogo wenye maeneo lakini hawayaendelezi huku wachimbaji wadogo wanahangaika.

- Serikali mmejipanga vipi kuwasaidia vijana, wananufaika na madini yao kwa kuwawezesha kwa makundi kupata vifaa vya kuchimbia ili na wao wawe wabia.

- Mungu awabariki wote, mwendelee kuwa wazalendo, tutawaunga mkono. Ulinzi wenu ni muhimu sana.

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Ludewa, ninayo furaha na heshima kubwa kutokana na utendaji mzuri wa Waziri na Manaibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini. Waziri wa Nishati na Madini na Katibu

Mkuu, fanyeni kazi, simameni imara. Sisi Wabunge makini tupo nyuma yenu, tutawapigania na tunaunga mkono jitihada zenu.

Mheshimiwa Spika, bajeti hii ya Nishati na Madini ni bajeti yangu ya kwanza kuiunga mkono, ni bajeti inayotoa nuru mpya ya matumaini kwa Watanzania. Kwa mara ya kwanza, ninaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ili kuhakikisha tunakuwa na umeme wa kutosha unaotokana na maji, Mashamba ya *Mbarali Farms* na *Kapunga Farms* na mashamba mengine makubwa yote yafungwe mara moja katika Bonde la Usangu ili *Mtera Dam* lijae na kutoa umeme mwingi. Ni ujinga kulima *upstream,* wakati *hydroelectric scheme* ipo *down stream.*

Mheshimiwa Spika, wakulima wa mpunga wapelekwe Bonde la Rufiji - *Down Stream, the Great Ruaha and below Stigler's Gorge* isiyo Kilombero, *if we plan to harness the gorge too for power.*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. TEREZYA L. HUVISA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nawapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri kwa kazi nzuri wanayoifanya hasa nawapongeza kwa kuamua kupunguza bei za kuunganisha umeme kwa wananchi hasa wa vijijini. Kitendo hicho kitasaidia sana kusambaza nishati ya umeme vijijini ili kuinua hali ya uchumi nchini, maana viwanda vidogo vidogo vitaweza kuanzishwa vijijini. Vile vile uwepo wa umeme

kwa wananchi kutatoa fursa ya kupata nishati mbadala kwa mahitaji ya nyumbani na viwandani.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo ikiimarika Sheria ya Mazingira itakuwa imetekelezeka kwa sababu kuni na mkaa havitatumika kwa ajili ya nishati ya kupikia. Naomba miradi yote hasa ya uchimbaji madini izingatie Sheria ya Kuhifadhi Mazingira. Ni vizuri watoaji leseni ya uchimbaji washirikiane vizuri na Baraza la Hifadhi ya Mazingira ili kutekeleza vizuri Sheria ya Uchimbaji pamoja na ya Mazingira.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kuchangia hoja katika Wizara ya Nishati na Madini. Kwanza, nampongeza sana Waziri na Serikali kwa kuliweza tatizo la kutokuwepo au kuzimika kwa umeme mara kwa mara. Natambua changamoto zinazoikabili Wizara lakini inaonesha sasa kuwa Wizara na Serikali wana kusudio la dhati katika kudhibiti na kushughulikia matatizo ya Wizara husika.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ya kwanza ni kuhusu kutokuwa na wataalam wazalendo watakaoweza kuzifanya kazi za kitaalam katika machimbo au migodi yetu pamoja na uhaba wa wataalam uliopo namwomba Waziri aje na mikakati ya kuwapeleka vijana kujifunza utaalam ili kuweza kufanya kazi katika machimbo yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuongelea gharama za mwanzo kwa wateja wapya wanaohitaji umeme, gharama ziko juu sana na kuweka umeme umbali wa kuhitaji nguzo moja tu unahitajika kulipa si chini ya shilingi 1,400,000 na baada ya gharama hizo bado unahitaji kuendelea kulipia umeme. Nashauri Serikali kuchukulia suala la umeme kama la kibiashara na kwa hiyo wao wafanye gharama zote ili wananchi wabakie na gharama za kununua umeme tu. Kuwatoza wananchi gharama hizo ni kuwaonea na kuwabebesha mzigo usiokuwa wa kwao.

Mheshimiwa Spika, nichangie pia kuhusu usumbufu wanaopata wateja wapya wa *TANESCO* wanapohitaji kupatiwa umeme. Pamoja na gharama na kuwa na uwezo wa kulipa gharama hizo wanapata usumbufu mkubwa sana na kukaa hadi miaka mitatu wakiwa wanafuatilia umeme, naomba Waziri alete mkakati wa kuwapatia haraka umeme wateja wapya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Spika, madini mbalimbali yanayochimbwa nchini bado hayaleti faida kwa wakazi waliomo katika maeneo yanayochimbwa madini hayo, imekuwa ni vigumu kuamini wengi walio karibu na maeneo ya uchimbaji hali zao za maisha ni mbaya tofauti na matarajio.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mkakati gani wa ziada wa kulazimisha Makampuni ya Madini kupeleka huduma za msingi na za lazima kwa maeneo ya karibu ya vijiji vilivyozungukwa na madini?

Mheshimiwa Spika, wananchi waliozungukwa na Mgodi wa Buhemba kule Mara na *Tanzanite* kule Arusha hawajapata manufaa yoyote. Kiwango cha gesi kilichogundulika Lindi na Mtwara iwe ni chachu ya kuboresha maisha na kupunguza umaskini katika Mikoa ya Kusini, isiwe wananchi wa Lindi na Mtwara, wawe ni waangalizi wa bomba la gesi linalotoka Mtwara - Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kuwapelekea umeme vijijini iongezewe kasi ili angalau ifikie asilimia 65, kwani kasi ya maendeleo itafikiwa ikiwa Serikali itaongeza kasi ya kupeleka umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iondoe malipo ya bei ya nguzo za umeme kwa wateja, si vizuri hata kidogo, Serikali kutoza bei ya nguzo za umeme wakati nguzo hizo ni uzalishaji unaotokea hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Spika, huko Meatu kuna shule inaitwa Shule ya Sekondari Kimali, naiomba Wizara ifikishe umeme katika shule hii ambayo iko Kilomita nne tu kutoka ilipo *Grid* ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, badala ya punguzo la bei ya kuunganisha umeme kuanza Januari, 2013, sasa ianze Agosti, 2012 ili kuwawezesha watu wengi zaidi kuunganisha umeme kabla ya *Christmas* na mwaka mpya.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza Waziri, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara hii. Nashauri yafuatayo:-

Kwanza, eneo likigundulika lina madini basi wenye eneo husika washirikishwe kwenye mkataba na mwekezaji, mathalani hisa asilimia 51 kwa 49. Hii itasaidia kuwapa wazawa wetu uwezo mkubwa wa kimapato na hatimaye kuongeza mapato ya Serikali na hivyo kukuza uchumi wa Taifa.

Pili, maeneo yote yanayovunwa madini, husababisha uharibifu wa mazingira, suala la *EIA* lipewe kipaumbele na fidia kwa uharibifu wa mazingira, lengo la saba la Milenia lizingatiwe.

Tatu, kwa kuwa suala la Shirika la *TANESCO* linaonesha wazi kwamba, kuna udhaifu mkubwa wa kiutendaji ndani ya shirika hili, basi ni vema menejimenti ikafumuliwa na kuundwa upya. Pia Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la *TANESCO* ivunjwe mara moja. Aidha, wote walioshiriki katika kulihujumu Shirika hili mkondo wa Sheria uchukue nafasi yake, uchunguzi uanzie tangu mwaka Juni, 2006.

Nne, suala la gesi asilia lifanyiwe kazi haraka iwezekanavyo kwa kutunga sera na sheria itakaotoa miongozo na usimamizi wa rasilimali hii kwa maendeleo endelevu kwa Taifa letu.

**MHE. GREGORY G. TEU:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri waliyoanza kuifanya baada ya kuwapo mabadiliko, wakati mwingine mabadiliko huleta neema.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika eneo la madini yanayopatikana kama Wilaya ya Mpwapwa. Maeneo yanakopatikana madini mbalimbali ni haya yafuatayo: Winza (Kibakwe), Izomvu, Mwenzele, Mlembule (Mpwapwa) na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa kuna kasi kubwa sana ya wachimbaji wakubwa wakiwemo wageni kuendelea na uchimbaji wa madini katika maeneo niliyotaja hapo juu bila ya utaratibu wa kisheria, hivyo kuwasaidia wananchi na wachimbaji wadogo waliopo katika maeneo husika. Hali hii inawafanya wananchi wanaoishi katika maeneo hayo kushawishika kuuza maeneo ambayo wana uhakika kuwa maeneo hayo yana madini.

Mheshimiwa Spika, hali hii inaifanya Serikali kupoteza mapato, hususan Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa licha ya kuwa na madini kiasi cha kutosha lakini inakosa mapato. Vile vile wachimbaji wadogo wanazidiwa na wachimbaji wakubwa (binafsi) wanaokuja na kunyemelea maeneo na wengine kuhodhi maeneo makubwa kwa kuyanunua au na kumiliki. Je, Wizara inachukua hatua gani kwa kuyatambua, maeneo yote yenye madini na kuyalinda yasivamiwe na wachache katika Wilaya hii ya Mpwapwa? Je, Wizara itasaidiaje kuifanya

Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa kuweza kujipatia mapato na ajira kwa vijana? Je, Wizara inadhibiti vipi uharibifu huu unaoendelea pamoja na kuharibu mazingira.

**MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Manaibu Waziri na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri wanayofanya. baada ya pongezi, naomba kuchangia katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa mtazamo wa haraka haraka umeme wa kuzalishwa kwa gesi ni rahisi kuliko matumizi ya mafuta. Mtazamo huu kwa hakika siyo sahihi sana, kwani unaendekeza tabia sahihi sana, kwani unadekeza tabia ya kutotafuta suluhisho rahisi na la kudumu. Gesi siyo *renewable* na hivyo iko siku itakwisha.

Pili, gesi hii ingeelekezwa kwenye matumizi mengine ambayo yangechochea kukua kwa uchumi na kupunguza kasi ya mahitaji ya pesa za kigeni na mazingira, kama nishati mbadala.

Mheshimiwa Spika, nachelea iko siku wajukuu wetu watatuuliza, iweje tuliamua kuchoma nishati moja ili kupata nishati nyingine? Nashauri tuwekeze zaidi kwenye joto ardhi kupata umeme, *Solar Source, Wind* na njia nyingine ambazo ni *renewable*. Hatujaweka umuhimu wa kutosha kwenye makaa ya mawe. Suala la kuchoma gesi kufufua umeme liwe la mpito *(transitional short term measure)* na ipewe muda wa ukomo wa ufuaji umeme kwa kuchoma gesi.

Mheshimiwa Spika, naomba mradi wa umeme wa *MCC* unaoendelea kujengwa huko Sengerema uharakishwe, maana awali ilitarajiwa kuwa umeme utakuwa umewashwa ifikapo mwezi Mei, 2012. Hadi sasa hakuna *transformer* hata moja, imefungwa na wananchi wanaendelea kuhoji, lini umeme utawashwa?

Mheshimiwa Spika, katika mradi wa *REA* pia ambao uko katika hatua za awali za utekelezaji, naomba Kisiwa cha Kome kipewe kipaumbele cha juu ili kuleta imani kwa wananchi wa Visiwani (vipatavyo 38 Jimboni Buchosa) kwamba Serikali yao ya Chama cha Mapinduzi inawajali na mipango ipo ya kuwapatia miundombinu kwa ajili ya maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, iko teknolojia ya kufua umeme kwa upepo katika maeneo yaliyojitenga kama vile Visiwa, mashamba makubwa au vituo vya kitafiti mbali na maeneo ya makazi. Teknolojia hii bado ni siri huko Marekani, na endapo Wizara itahitaji habari zaidi juu ya jambo hili, basi nitaitafuta kwenye taarifa zaidi aweze kupata maarifa hayo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ANNAMARYSTELLA. J. MALLAC:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia Wizara hii muhimu kwa maandishi. Nianze kwa kumtanguliza Mwenyezi Mungu aliye na asili ya mema yote.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina Mikoa na Wilaya ambazo zina madini yanayoendesha maisha ya watu ikiwa kama ni sehemu ya ajira kwao, na ni wazi wachimbaji wadogo wadogo hufaidika sana kunyoosha maisha yao kama wanapata msaada kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, misaada tunayoiongelea ni kama kutengewa maeneo ya wachimbaji wadogo wadogo, kuhakikisha usalama, kuwekewa huduma za afya katika maeneo ya machimbo yao na kutafutiwa soko.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Katavi na Rukwa pia tuna neema ya kuzungukwa na madini mbalimbali kama dhahabu, shaba na grina. Pia kuna wachimbaji wadogo wadogo ambao wanakidhi maisha yao kwa uchimbaji wao mdogo. Lakini vijana bado wanahangaika maeneo ya kuchimba, kwani Serikali haijawatengea maeneo vijana bali wanajichanganya katika maeneo ambayo yamemilikiwa na wachimbaji wenye pesa zao, ndipo wanakwenda wanachimba mabaki au masalio walimochimba.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kupitia Wizara na Waziri mwenye dhamana ahakikishe Wizara imetenga maeneo rasmi kwa vijana wachimbaji wadogo wadogo ili waepukane na usumbufu wanaopata wa kukandamizwa na watu au wachimbaji wakubwa wenye pesa ili vijana wajikwamue katika umasikini na kupata maisha yenye unafuu kupitia madini, tofauti na sasa maeneo mengi yameshikwa na Waarabu, Wachina na kadhalika.

Serikali pamoja na kukaribisha wawekezaji, inapashwa kuwapa kipaumbele wazawa na hasa vijana.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikisema akina mama wapewe kipaumbele, na daima akina mama wamekuwa wakijitoa katika sekta mbalimbali kuhakikisha wanajishughulisha ili kukabiliana na changamoto na ushindani wa ajira. Kuna mtandao wa akina mama wanaohamasisha matumizi ya nishati mbadala ya makaa ya mawe badala ya kuni. Wizara ya Nishati na Madini imeshafanya utafiti wa suala hili la akina mama hawa na wakathibitisha kwa maandishi kuwa suala hili la kutumia nishati hii mbadala ni nzuri na endelevu na yenye faidia kwa Taifa letu. Akina mama hawa waliiomba Wizara Fedha, tena kwa mkopo, ili waanzishe zoezi hilo Mkoa wa Rukwa na Wizara iliwajibu kuwapatia pesa hizo toka bajeti ya mwaka 2011/2012, lakini mpaka hivi leo akina mama hawa wamekuwa wakipigwa porojo tu. Sasa hapa tunajenga au tunabomoa?

Naiomba Wizara kupitia Waziri wa Wizara hii kuchukua hatua ya kuwasaidia akina mama hawa waliloonesha nia na njia ya kupambana na umasikini na kuliingizia pato Taifa kupitia Nishati hii ili watimize nia na azma yao, kwani suala lao lina faida na tija kwa Taifa letu, maana hata maeneo ambayo ni ya kwao, Serikali imekuwa ikiwazungusha kwa kuwawekea vikwazo ambavyo havina sababu za msingi.

Mheshimiwa Spika, tuweke vipaumbele kwenye mambo yenye faida kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, umeme bado ni tatizo kubwa, sehemu nyingine, mfano, Mkoa wa Katavi bado tunatumia majenereta ambayo ni ya muda mrefu sana kiasi kwamba wakazi wanapata umeme kwa mgao na kwa wafanyabiashara inayotegemea umeme ni shida.

Mheshimiwa Spika, Serikali sasa ijitahidi kuhakikisha wachimbaji wadogo wadogo wanatengewa maeneo ya uchimbaji na wanapata maji safi na salama, barabara, wanatafutiwa soko na mikopo.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Rais kwa kuteua *team* nzuri ya Mawaziri kuongoza Wizara hii muhimu sana. Nakupongeza Mheshimiwa Waziri Prof. Sospeter Muhongo, tuna imani naye, lakini pia Mheshimiwa Rais amempatia vijana mahiri kumsaidia Mheshimiwa George Simbachawene na Mheshimiwa Stephen Masele. Wizara hii ni *strategic* sana katika uchumi wetu. Umeme hautakiwi kukatika katika viwanda vyetu ambavyo tunataka viwe msingi wa nchi yenye uchumi wa kati *(medium income country)* ifikapo mwaka 2025. kwa mujibu kwa dira yetu ya maendeleo, vinahitaji umeme wa uhakika ili kufanya kazi zake vizuri.

Baba wa Taifa aliwaambia Watanzania kwamba, madini ndiyo tegemeo kubwa la Watanzania na akasema wakati huo kwamba, tusingeanza kuyachimba mpaka wakati ambao tungekuwa na wataalam wetu *(geologists)* ili waweze kuzungumza lugha moja na wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wanaamini kwamba kauli hiyo ya Baba wa Taifa ni sahihi na hivyo wanategemea kwamba Serikali itakuwa makini sana katika kusimamia Sekta hii ya Madini.

Mheshimiwa Spika, Serikali inabidi iwasimamie vizuri wawekezaji ili Watanzania wafaidike na madini ambayo ni zawadi ya Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Ngara imebarikiwa kuwa na madini mengi hasa dhahabu ambayo hayajachimbwa. Wajerumani waliacha maandishi yanayosema, Ngara ni Wilaya tajiri kuliko zote kwa *deposits* za madini.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Wilaya ina mgodi wa *Kabanga Nickel.* Mgodi huu ni wa pili kwa ukubwa duniani baada ya ule wa Canada (*interms of deposit)*. Naiomba Wizara iwe karibu na wawekezaji katika mradi huu wa kujiandaa kuwapatia umeme wa megawati 30 zinazohitajika mgodi utakapoanza kufanya kazi. Pia Serikali iwe makini wakati wa mchakato wa kuwahamisha wananchi na kuwa-*resettle* ili kupisha mgodi. Wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu mwaka 2010, Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alipokuwa Wilayani Ngara alitoa ahadi ya kuupatia Mji mdogo wa Rulenge umeme wa *generator* pamoja na vijiji vinavyouzunguka Mji wa Ngara.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara isaidie kuhakikisha Mji wa Rulenge unapata umeme huo kwa

kutumia Shirika la kueneza umeme vijijini *REA. REA* wamepiga hatua nzuri kwa kuwekeana Mkataba na Halmashauri ya Ngara kuhusu umeme wa Rulenge.

Mheshimiwa Spika, naiomba pia Wizara isimamie umeme wa *ORIO,* Kampuni ya *Holland*. Kampuni ya *ORIO* ilishawekeana Mkataba na *TANESCO* ili kuweka *generator* mbili kwenye Kituo cha *TANESCO* cha Ngara ili kusambaza umeme katika Miji midogo ya Mugoma na Benaco na vijiji vya Kabaheshi, Nyamahwa na Kashinga mpaka sasa *generetor* hizi hazijafungwa.

Mheshimiwa Spika, maporomoko ya Rusumo Wilayani Ngara kwenye mpaka wa Tanzania na Rwanda yana uwezo wa kutoa umemd wa Megawati 90 na ni mradi wa nchi tatu; Rwanda, Burundi na Tanzania, na kila nchi itapata Megawati 30. Naiomba Wizara ihakikishe mradi huu haukwami na unaendelea haraka. Umeme wa Rusumo utaziwezesha Wilaya za Ngara, Biharamulo na Kibondo kupata umeme wa *grid*. Mgodi wa *Kabanga Nickel* pia utafaidika na umeme huu.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kwa kuleta hotuba nzuri ya Wizara hii na kazi nzuri anayoifanya. Nina imani naye na ninamhakikishia *support* yangu ya hali na mali. Nampongeza kwa kauli nzuri aliyoitoa Mtwara kuhusu *TANESCO* kulipia madeni yake na kukataza mawazo ya Makampuni ya gesi kuweka rehani visima vyetu vya gesi kutokana na madeni ya *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Manaibu Waziri wa Wizara ya Nishati na Madini – Mheshimiwa George Simbachawene na Mheshimiwa Stephen Masele kwa kuonyesha umahiri mkubwa katika kutekeleza majukumu yao kwa umakini sana pamoja na kwamba wamekaa muda mchache katika nafasi zao. Pongezi zangu pia ni kwa Katibu Mkuu - Ndugu Eliakimu Maswi kwa msimamo wake madhubuti wa kulinda na kutetea fedha za umma. Tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumtia nguvu na ujasiri.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Waziri wa Nishati na Madini - Mheshimiwa Prof. Muhongo kwa jinsi alivyonipa msaada wa haraka wakati nilipompelekea suala la umeme Vijiji vya Jimbo la Karagwe. Nimefurahishwa na kasi yake. Pia namshukuru Mkurugenzi Mtendaji *(REA)* - Ndugu Mwakahesya na Ndugu Msofe kwa kunikaribisha na kunisikiliza ofisini kwao siku ya Jumamosi. Hakika ni wasikivu na wameonyesha wanajali.

Mheshimiwa Spika, umeme Jimbo (Wilaya) ya Karagwe, Vijiji ninavyoviombea umeme viko makundi mawili. Mradi unaoendelea umekwepa vijiji vifuatavyo: Omurusimbi, Rukale, Misha, Ruhita, Rubale, Kibogoizi, Rugu, Kasheshe, Bujala, Nyakasimbi, Kahanga, Kijiji cha Ihembe Na. 2, na Vitongoji; Rwanda/Kashambi.

Mheshimiwa Spika, vijiji tajwa hapo juu vimerukwa katika mradi wa umeme vijijini unaoendelea wa Bisheshe, Nyaishozi na Ihembe. Naomba *REA* wapeleke umeme katika vijiji hivi ikiwemo na Vitongoji vya Karehe na Kamuli katika Kijiji cha Nyakahanga ambako ndiko

umeme huu unakotokea, lakini wamesahauliwa. Pia Shule za Sekondari, Zahanati, Makanisa, Mfano, Parokia ya Nyaishozi zimesahauliwa.

Mheshimiwa Spika, umeme huu umepita barabarani na kuingia ndani mita 100 tu. Vijiji vyangu vingi viko nje ya barabara kuanzia kilomita moja na nusu hadi tano kwa kila kijiji. Naomba mradi uingie ndani waliko wanavijiji wanyonge, kwani baada ya mradi kukabidhiwa *TANESCO,* wananchi walio wengi hawataweza kulipia umeme huo.

Mheshimiwa Spika, kuna ahadi za Mheshimiwa Rais alizozitoa mwaka 2005 na 2010 kuvipelekea umeme vijiji vya Jimbo la Karagwe. Vijiji hivyo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Vijiji vyote vya Tarafa ya Nyabiyonza, Kijiji cha Chamuchuzi, Kijumbura, Kaiho, Kanywamagana, Kanogo, Chabuhora, Kandegesho, Nyakakika, Kayungu, Nyabweziga, Kakulaijo, Kibondo, Nyabiyonza, Nyakaiga, Bukangara, Ahakishaka, Kafunjo, Kamagambo, Rwenkorongo, Kiruruma, Biyungu, Nyakagoyagoye, Nyamieli na Nyakaswa.

Mheshimiwa Spika, hivi vijiji vyote vimepakana, hivyo ni rahisi kuvifika. Ni ahadi ya muda mrefu. Naomba bajeti hii ya mwaka 2012/2013 umeme uwashwe.

Mheshimiwa Spika, vijiji vingine ni Ihanda, Rukole, Chonyonyo, Omuchime Rulavo, Chanika, Runyaga, Ruhanya, Kinyinya, Katwe, Katembe, Kituntu,

Rwambaizi, Nyakahita, Kanoni, Kigarama Juu, Kigarama Chini, Bwera, Igurwa, Kibona na Kagutu.

Mheshimiwa Spika, hivi vijiji ambavyo viko maeneo yanayopakana, hivyo ni rahisi vyote kufikika.

Mheshimiwa Spika, vijiji vilivyopo Mji mdogo wa Kayanga ni Kijiji cha Nyakahanga, Bujuruga, Kayanga Vijijini na miti. Hivi viko ndani ya mamlaka ya Mji mdogo wa Kayanga, lakini havina umeme.

Mheshimiwa Spika, Vijiji vya pembezoni vinavyohitaji kuangaliwa kwa jicho la huruma pia ni Kijiji cha Omukakajinja, Rugela na Nyarugando (vijiji vyote hivi viko Kata moja ya Rugela). Naomba vipewe umeme.

Mheshimiwa Spika, pia vipo vijiji vya pembezoni vya Kata ya pembezoni ya Kihanga navyo ni Kijiji cha Kishoju, Mulamba, Kihanga, Katanda, Kibwera na Mushabaiguru.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Karagwe ni Jimbo linalopakana na Uganda na Rwanda. Limeathirika na wakimbizi, vita vya Uganda, gonjwa la Ukimwi, Meli ya MV. Bukoba kuzama na hivyo kuathiri shughuli za uchumi. Hivyo basi, wananchi hawa wanahitaji huruma ya Serikali kuwainua kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, niendelee kwa kupongeza kazi nzuri inayofanywa na Katibu Mkuu pamoja na Waziri na Manaibu wote. Hatua inayoendelea hivi sasa ya kuhakikisha Wizara inakuwa safi, naiunga mkono kwa asilimia mia moja. Ushauri wangu ni kwamba, zoezi la kuhakikisha Watendaji wabadhirifu wanaondoka, liendelee kwa nguvu hiyo hiyo na lisirudi nyuma hata kidogo, kwani Wizara hii imekuwa na uozo kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, hatua hii inahitaji ujasiri, hivyo nawaombea kwa Mungu ujasiri alionao uendelee hivyo hivyo, katu asiogope kwa kuwa naamini Mwenyezi Mungu amewaweka hapa ili watukomboe Watanzania.

Mheshimiwa Waziri, tunamshukuru Mungu kwa uwepo wenu na daima tutakuwa wote kwa hali zote.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, Naibu wake na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuhakikisha tatizo la umeme limeondoka. Tumekuwa na tatizo la umeme kwa muda mrefu sana kiasi cha kukata tama, lakini sasa inaelekea kuwa historia. Hongereni sana, endeleeni hivyo.

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwa Serikali kwa kusaidia tatizo la umeme kuzidi ghafla au kupungua ghafla jambo ambalo lilikuwa linawatia hasara sana wananchi wa Mkoa wa Dar es Saalam. Serikali imefunga *transformer* mpya katika Mkoa wetu, hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na wingi wa pongezi, sasa niishauri Serikali yangu sikivu ya Chama cha Mapinduzi kwamba, Serikali inapata gharama kubwa ya kuwaunganishia wananchi umeme toka eneo hadi eneo, katikati kuna nyumba nyingi ambazo hazina umeme kabisa, hii ni hasara kwa *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, nini kifanyike? *TANESCO* ni Shirika ambalo linatakiwa aliendeshwe kibiashara zaidi na liajiri wabunifu ambao watalifanya Shirika letu letu liendeshwe kibiashara na kifaida zaidi. Ni wajibu wa *TANESCO* kushawishi wananchi walio eneo la katikakati ya mtu anayepelekewa umeme wakubali kufungiwa umeme hata kwa kulipa gharama kwa awamu mbili au tatu, lakini Shirika litakuwa limevuna. Tuache ubinafsi, tuangalie uzalendo. *TANESCO* badala ya kukusanya kwa nyumba moja, itakusanya nyumba nyingi na Shirika litapata angalau fedha za kujiendesha badala ya sasa kusubiri ruzuku ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukiishauri *TANESCO* ibadilike hata kiutendaji, siku moja kuchukua vijana waka-*promote* umeme na kufanya ukaguzi wa nyumba hadi nyumba kuhakiki matumizi ya umeme na wale ambao hawana umeme washawishike kutumia umeme. Hakika tutapata ongezeko la kipato, kwani

*promotion* na *advertsment* ni *party* ya biashara na ni lazima kutengewa fungu katika shughuli yoyote ya biashara.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali katika suala la mafuta ya mitambo kwamba, pamoja na juhudi za Serikali kujenga bomba la gesi kwa kusaidia wananchi kupata umeme wa gharama nafuu, lakini katika kipindi hiki cha mpito, Serikali isifanye makosa kwa kununua mafuta ya gharama za juu.

Mheshimiwa Spika, napongeza juhudi za Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake na Katibu Mkuu kwa kuokoa Shilingi bilioni tatu kwa kila wiki mbili na Shilingi bilioni sita kwa mwezi. Fedha hizi ni nyingi sana na zitatusaidia kufanyia shughuli mbalimbali za maendeleo. Hongereni sana na nawaunga mkono kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, ni vyema sasa wanasheria wa Serikali ndani ya Wizara waangalie *Procurement Act* na yale maeneo yanayofuka ufisadi yaletwe Bungeni turekebishe haraka, sheria hii isiwe kikwazo cha maendeleo.

Mheshimiwa Spika, bei ya mafuta mazito ni ndogo sana, wakati nje ya Tanzania (Ghuba) Falme za Kiarabu iko chini sana. Wizara kama imefanikiwa kuona ufisadi wa kununua mafuta kwa bei kubwa, suala la Puma na *TANESCO* iwe changamoto kwetu, Serikali iagize mafuta kwa gharama zake toka nje na tuje tutumie katika mitambo yetu wenyewe. Tufanye majadiliano na kampuni yetu ya Puma ambayo

asilimia 50 ni yetu, kutafuta njia ya majadiliano pasipo kuwaletea hasara.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia, bajeti ya Wizara ipitishwe.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri wa Nishati na Madini na Wizara hii kwa kuchapa kazi vizuri pamoja na uadilifu anaouonyesha katika kulitumikia Taifa letu. Pia napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Manaibu Mawaziri wote wawili wa Wizara hii kwa uchapaji kazi wao, bila kumsahau Katibu Mkuu wa Wizara. Kwa hakika nguvu za Waziri, Manaibu Mawaziri pamoja na Watendaji wengine wa Wizara hii wakiunganisha pamoja, nina imani kuwa wanaweza kufanya lolote la maana katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, binafsi siungi mkono hoja hii kwa kuwa kuna mambo mengi sana ambayo yanahitaji fikra zaidi kuyatatua kuliko nguvu. Pia kwa historia mbaya sana ya Wizara hii kuhusu eneo la Nyamongo (ambalo ni *North Mara*) lililoko Wilayani Tarime, bado hakuna ufumbuzi wowote uliokwishapatikana.

Mheshimiwa Spika, hoja zangu hazitakuwa tofauti na za mwaka 2011, kwani hadi sasa utekelezaji wa yale niliyoyaongelea kwenye bajeti ya mwaka 2011 bado unasuasua ingawa umenza taratibu. Hivyo namwomba Waziri anijibu maswali yafuatayo:-

Suala la umeme wa *REA* ni hakika na ukweli ulio wazi kuwa umeme huu wa *REA* ukifika katika vijiji vyote vya Tanzania, nchi ya Tanzania itapiga hatua mbele zaidi kwa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ni lini ahadi ya Waziri Mkuu wa Tanzania - Mheshimiwa Mizengo Peter Kayanza Pinda ya kukipatia umeme Kituo cha *Kurya cultural Centre* kilichoko Kijiji cha Msanga, Kata ya Goronga, Tarafa ya Ingwe, Wilaya ya Tarime itatekelezwa?

Mheshimiwa Spika, mradi wa *REA* katika vijiji vya Nyamwigura, Rozana, Kemakorere, Nyarero, Nyamwaga, Keisangura, Tagare, Muriba, Kumwika, Kobori, Itivyo, Mangucha, Kegonga, utakamilika? Huu mradi ni maarufu kama mradi wa umeme wa Itivyo Wilayani Tarime.

Mheshimiwa Spika, kwanini gharama za kuingiza umeme katika nyumba ambazo ziko karibu na mradi huu zisipunguzwe ili kuwawezesha wananchi masikini kujiwekea umeme katika nyumba hizo? Je, mradi wa *REA* katika vijiji vya *Security Road* Wilayani Tarime toka Rorya Susuni Kubiterere, Remagwe, Nyabisaga, Borega, Ganyange, Kimusi hadi Nyantira utaanza na kukamilika lini? Je, mradi wa *REA* katika Vijiji vya Nyakunguru, Kibasuka Nyarwana Weigita, Kembwi, Manga hadi Komaswa utaanza lini na utakamilika lini?

Mheshimiwa Spika, napenda kuleta ombi maalum kwamba, kwa kuwa Wilaya ya Tarime ina rasilimali za kutosha kwa wananchi wake kuweka umeme katika nyumba zao, naiomba Wizara ihakikishe kuwa mradi

wa *REA* unaanza mara moja katika Vijiji vya Kata zote za Tarime zikiwemo za Nyandoto, Gorong'a, Itiryo, Nyanungu, Kiore, Kibasuka, Bumera, Kitare, Magoto na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali kupitia Wizara hii inasema nini juu ya umeme unaokatikakatika kutokana na mgawo wa kutengenezwa na Watendaji walioko Wizarani? Je, Serikali kupitia Waziri wa Wizara amewachukulia hatua gani?

Mheshimiwa Spika, vitendo vya rushwa vimeshamiri sana kwenye Shirika la *TANESCO*. Je, Serikali inalifahamu hilo? Kama inalifahamu, imejipanga vipi ili kuondoa aibu hii? Kuna tetesi kuwa kuna baadhi ya Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wanapokea rushwa toka kwa Watendaji wa *TANESCO*. Je, Serikali inalifahamu hilo? Imechukua hatua zipi? Halikadhalika, kuna tetesi kuwa baadhi ya Wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini wanajihusisha na biashara isiyo halali na *TANESCO*. Je, Waziri anasemaje kuhusu hilo?

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kuwa, nchi yetu ya Tanzania imebarikiwa kupata maliasili ya madini ya kila aina, mfano almasi, dhahabu, *uranium, tanzanite* na mengine mengi ambayo hayana hata majina. Je, sekta ya madini inalinufaishaje Taifa hili?

Mheshimiwa Spika, iuna tetesi kuwa makuadi wa madini (madalali) ndio wanaonufaika na Sekta hii ya Madini kuliko nchi. Waziri anasema nini juu ya hilo? Waziri amejipanga vipi kurekebisha mikataba mibovu

ambayo viongozi wenye uroho walisaini kwa pupa na sasa inaliangamiza Taifa na hivyo kuifanya Tanzania kuwa kichwa cha mwendawazimu au shamba la bibi na babu katika Sekta hii ya Madini? Je, mrahaba mpya ambao nasikia ni 4% ni halali kwa Taifa hili? Kama siyo halali, ni nini kifanyike? Kwa nini tusigawane 50% kila pande baada ya kutoa gharama ya uzalishaji? Ni nani anayedhibiti na kuangalia uzalishaji wa kiasi gani cha dhahabu katika migodi yetu?

Mheshimiwa Spika, gesi ni bahati ya pekee ambayo Mwenyezi Mungu muumba wa Mbingu na Nchi ametujalia. Nasikia ina thamani ya Shilingi trilioni 600. Huu ni utajiri ambao kwa kweli nchi yetu imejaliwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imejipanga vipi kuvuna hiyo gesi? Serikali imejipanga vipi ili kuhakikisha kuwa asilimia 60 ya gesi hiyo yote inalinufaisha Taifa? Serikali inatoa mafunzo gani kwa wananchi ili kuwaandaa kwa matumizi ya gesi katika majumba yao? Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwaandaa Watanzania ili waweze kununua magari yanayotumia gesi na siyo *petrol* wala *diesel*?

Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara wengi wa mafuta hasa *petrol* huchanganya nishati hiyo na maji, mafuta ya taa na kadhalika. Hali hii inapelekea uharibifu mkubwa wa magari. Kwa mfano, kampuni ya *Big Bon* inaongoza kwa kufanya mchezo huu. Je, Waziri kupitia Wizara yake analijua hilo? Je, amechukua hatua gani hadi sasa? Je, haoni kuwa *EWURA* imeshindwa jukumu na wajibu wake, hivyo ivunjwe ili kianzishwa chombo kingine badala yake?

Mheshimiwa Spika, mgodi wa dhahabu North Mara, maarufu kama mgodi wa Nyamongo Wilayani Tarime, ni mgodi ambao umegubikwa na changamoto nyingi sana. Je, Wizara inasaidiaje kutoa fidia halali kwa wanaohamishwa ili kupitisha uwekezaji katika eneo la Nyamongo? Kwa nini fidia hizo zimechelewa kulipwa hadi sasa? Kwa nini mwekezaji hajatekeleza ahadi zilizopo kwenye mikataba, za kutoa huduma za kijamii kama vile maji, umeme, shule, barabara na afya? Wizara inasaidiaje kufanikisha suala hili?

Mheshimiwa Spika, sakata la maji ya Mto Tigiti (maji yenye sumu) lilitikisa Bunge hili kwa muda sasa. Kwa nini hadi sasa wale wote walioathirika katika maji ya Mto huu hawajalipwa fidia? Je, *NEMC* iliishauri Serikali kuhusu suala hili? Je, Kamati za Kudumu za Bunge za Nishati na Madini na ile ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, ilitoa ushauri gani kwa Serikali kuhusu sakata hili?

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara hii imefikia hatua gani ya kuwaelekeza wachimbaji wadogo wadogo? Fedha zilizotengwa na mgodi kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo takribani US $5,000,000 iliwekwa katika akaunti gani? Kama ziko Wizarani, kwa nini hazitumiki? Kama hazijatolewa na mwekezaji, Serikali inasema nini? Je, ujenzi wa ukuta *(fence)* katika eneo la mgodi, utarudisha mahusiano mema kati ya mwekezaji na wananchi wanaozunguka mgodi huo? Kwa vipi? Je, hilo ndilo suluhusho la kudumu?

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ahadi kemkem toka kwa mwekezaji kuwa mpango kabambe wa kujenga barabara ya *Nyamwaga Road* itokayo Tarime Mjini – Kemakorere – Nyamwaga - Nyamongo hadi Mto Mara yenye umbali wa takribani kilomita 53 kwa kiwango cha lami. Je, kupitia Wizara hii, Serikali inatoa ushauri gani juu ya utekelezaji wa ahadi hizi? Ni lini mgodi utaanza kulipa Halmashauri *loyalty* ya US$ 1,000,000 badala ya US$ 200,000 ambayo inalipwa kwa sasa? Je, kodi ya huduma, yaani *services levy,* inalipwa ipasavyo katika Halmashauri ya Wilaya ya Tarime?

Mheshimiwa Spika, uharibifu wa mazingira katika mgodi wa dhahabu wa *North Mara,* yaani Nyamongo, ni kero kwa wananchi wa eneo husika. Je, Serikali kupitia Wizara hii, inatoa ushauri gani juu ya milipuko ya baruti maji ya sumu na kadhalika, ambayo huwakumba mara kwa mara watu wa eneo husika?

Mheshimiwa Spika, Vijiji vyote vya Kata za Nyangoto na Kemambo vilivyoko Nyamongo vinanufaika na asilimia moja ya mgodi isipokuwa kijiji kimoja cha Mrito. Kwa nini kijiji hiki hakijaingizwa kwenye mradi wa vijiji vinavyonufaika na mgodi?

Mheshimiwa Spika, tatizo la ajira katika mgodi wa *North Mara* linatatuliwaje? Ni lini mgodi utapima Mji wa Nyamongo na Mji wa Nyamwaga kama ahadi nyingi zinavyoelekeza? Je, mgodi una mpango wowote wa kujenga nyumba za kisasa katika Miji hii miwili? Ni lini mgodi utajenga Chuo cha Ufundi *(VETA)* katika eneo la Nyamongo ili kukamilisha ahadi ya mgodi? Je,

mauaji yasiyo na kikomo huko Nyamongo yatakoma lini?

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Tarime wanakaa juu ya dhahabu, wanatembea juu ya dhahabu na hata wanalala juu ya dhahabu, lakini wanakabiliwa na umasikini uliokithiri? Je, Serikali inasema nini juu ya hilo?

Mheshimiwa Spika, kwanini wananchi wengi wa Tarime hawashirikishwi katika suala la biashara na huduma nyingine kwenye mgodi?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Waziri wa Nishati na Madini pamoja na Naibu Mawaziri wote wawili. Wameanza vizuri na mipango yote waliyoiainisha inatutia matumaini makubwa juu ya uongozi wao. Aidha, napongeza sana timu yenu ya utendaji ikiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara kwa utendaji mahiri na umakini sana. Napenda pia nipongeze hotuba nzuri ya bajeti ya Wizara, na ninaiunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kwa vile Wizara ilikwishatoa ahadi ya kutelemsha umeme kwenye maeneo yanayopitiwa na nguzo za umeme na yale ya karibu na maeneo yaliyo na umeme, naomba kwa mara nyingine kupata kauli ya Serikali juu ya ahadi hiyo kwa vijiji vya Msange kilometa nne toka Chamwino Ikulu, Chinangali – Mwegamile kwenye njia kuu ya umeme toka Dodoma kwenda Kongwa na Mpwapwa.

Kitongoji cha Mpera kilometa mbili ndani ya Kijiji cha Chamwino Ikulu. Maeneo haya yalikwishatathiminiwa na *TANESCO* na uongozi wa Wizara uliowatangulia kupitia kwa Waziri na Naibu Waziri. Walikwishakutana na wananchi wa maeneo hayo na kuwapa ahadi ya kupatiwa umeme. Naiomba kauli ya Serikali kwa mara nyingine juu ya ahadi hiyo kwa wananchi wa vijiji hivyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru sana Serikali kwa kupanga kunipatia umeme kupitia mradi wa *MCC* kwenye Kata za Manchali, Majeleko na Chilonwa zilizoko kwenye Jimbo langu la Chilonwa. Pamoja na shukurani hizo, naomba Serikali iwajulishe wananchi na Taasisi mbalimbali ambazo ziko karibu na maeneo ambayo umeme huo utapitia iwapo watasambaza umeme huo pia. Maeneo yanayohusika ni Shule ya Sekondari Manchali, Shule ya Msingi Chalinze, Shule ya Sekondari Chilonwa. Kwa vile maeneo haya yapo kwenye njia ya umeme huu wa mradi wa *MCC,* naomba kuleta ombi kwa Serikali kuangalia uwezekano wa kuzifikishia umeme Taasisi hizi ili ziweze kutoa huduma kwa wananchi wanaohusika na Taasisi hizi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa narudia kuwapongeza Waziri pamoja na Naibu Mawaziri na kuwaunga mkono. Naomba kupewa majibu ya hoja zangu hizo mbili.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. ABDULAZIZ M. ABOOD:** Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya maeneo ambayo yamekuwa

yakilalamikiwa na wananchi wengi wa Jimbo la Morogoro Mjini kwa muda mrefu sasa. Kuna Shirika halijawatoa huduma hii muhimu ya nishati ya umeme katika jamii na hivyo kukwamisha shughuli mbalimbali za kiuchumi na hata kulikosesha Shirika lenyewe mapato makubwa.

Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo hayajapatiwa huduma hii ni Kihonda *(VETA)*, Mtaa Kilongo Kata ya Mkundi, Kayenzi Mtaa wa Sina Kata ya Mafisa, *Kola 'A' Missionary*, Mtaa wa *Area 'K'* Kata ya K/Changani, Mtaa wa Mji Mwema, Kata ya Tungi na Kata ya Mindu, Bingwa na Towelo Kata ya Mlimani. Sehemu hizi zina wananchi wengi sana waishio katika maeneo mengi bila ya kuwa na umeme. Kwa mfano, Mtaa wa Kilingo Kata ya Mkundi pekee ina wakazi karibu 900 wanahitaji huduma ya umeme. Kihonda Veta wakazi karibu 700 nao wanahitaji huduma hii.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, ukitizama tathimini hii, ni wakazi wengi sana ambao hawajapelekewa umeme katika Jimbo la Morogoro Mjini ukizingatia Manispaa ya Morogoro inataka iwe Jiji. Kuna baadhi ya maeneo, kwa mfano, Mafisa kuliwekwa nguzo, lakini cha kushangaza nguzo hizo ziliondolewa bila taarifa yoyote, na wananchi wa maeneo hayo ndio waathirika zaidi.

Mheshimiwa Spika, pia kukua kwa Taasisi nyingi zinazojihusisha na jamii ambazo zinakosa huduma hizo, na baadhi ya Taasisi hizo ni Vituo vya Kulelea Watoto Yatima, Shule za Msingi na Sekondari, Vituo vya Afya, na wajasiriamali ambao wengi ni wanawake. Aidha,

kutopatikana kwa nishati hii, kunawadidimiza wananchi kiuchumi.

**MHE. SYLVESTER M. KASULUMBAYI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kukupongeza kwa kuteuliwa kwako kuwa Mbunge na kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nishati na Madini, Wizara iliyo nyeti sana katika ustawi wa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nikuhabarishe kuwa, Jimbo la Maswa Mashariki pamoja na kuanzishwa rasmi mwaka 2010, limo ndani ya Wilaya Kongwe iliyoanzishwa na Wakoloni hapo mwaka 1927, miaka 85 iliyopita.

Mheshimiwa Spika, Jimbo hili ni miongoni mwa Majimbo yanayonyemelewa kwa kasi ya kumezwa na jangwa kufuatia na ukame uliopo unaosababisha uotaji wa miti kadri inavyopandwa kuwa hafifu sana, hali inayopelekea wanawake kukata minyaa ili kupata kuni na kukusanya vinyesi vya ng'ombe ambavyo huvitumia kama kuni mbadala ya kuwawezesha kupikia vyakula hali ambayo kazi ya kupika vyakula vyao huandamana na wingi wa moshi unaowasababishia macho yao kuwa mekundu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri katika kuanza kuwapunguzia adha hii inayowakabili wananchi wa Jimbo la Maswa Mashariki ili nao waanze kutumia nishati itakayozuia ukataji wa miti na uokotaji wa vinyesi vya ng'ombe ili miti na vinyesi vya ng'ombe kuvibakizia kazi ya kurutubisha ardhi na kuimarisha utunzaji wa mazingira ya Jimbo la Maswa Mashariki.

Mheshimiwa Spika, hivyo, kutokana na umuhimu huo, nakuomba vijiji vifuatavyo uone haja ya kuvigawia umeme. Vijiji hivyo ni Kijiji cha Ipililo cha Kata ya Ipililo - Maswa (Simiyu), kijiji cha Ngulinguli cha Kata ya Ngulinguli – Maswa (Simiyu), Kijiji cha Mwabayanda cha Kata ya Mwigwa – Maswa (Simiyu), Kijiji cha Isageng'he cha Kata ya Sukuma – Maswa (Simiyu), Kijiji cha Mbalagane cha Kata ya Lalago – Maswa (Simiyu), Kijiji cha Mandang'ombe cha Kata ya Lalago - Maswa (Simiyu), Kijiji cha Mwadila cha Kata ya Sukuma – Maswa (Simiyu), Kijiji cha Gula cha Kata ya Lalago – Maswa (Simiyu), Kijiji cha Mwakidiga cha Kata ya Lalago - Maswa (Simiyu).

Mheshimiwa Spika, ninayo matumaini makubwa kuwa ombi hili Mheshimiwa Waziri atalifanyia kazi ili wakazi hao nao waweze kuanza kutumia nishati ya umeme katika kuwarahisisha kuujenga uchumi wa nchi yetu na kuachana na matumzi ya kuni na vinyesi vya ng'ombe ili miti na vinyesi vya ng'ombe viendelee kuirutubisha ardhi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kukuwasilishia ombi hili muhimu kwa Mheshimiwa Waziri. Naomba wakati atakapokuwa anahitimisha hotuba yake ya bajeti, anijulishe kilichojiri dhidi ya ombi hili.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa maoni yangu kuhusu hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Sospeter Muhongo kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, umeme ni wa muhimu sana katika kuendeleza maisha ya Watanzania, kuendeleza uwekezaji na kadhalika. Hata hivyo ni wananchi wachache sana wamenufaika na umeme. Hotuba ya Nishati na Madini, ukurasa wa saba, ni aibu kwamba miaka 50 baada ya uhuru Watanzania waishio Vijijini, ni 6.6% tu ndio wameunganishiwa umeme ikiwa ni 18.4% ya Watanzania wote waliounganishiwa umeme kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni imebainika kwamba kuna mpango wa kuviwekea rehani baadhi ya visima vya gesi katika Kisiwa cha Songo Songo kwa madai ya mwekezaji kutafuta fedha katika Taasisi za Kimataifa nje ya nchi. Ningependa kuhoji, ni nini kauli ya Serikali kuhusu hilo?

Mheshimiwa Spika, ahadi ya kupatikana kwa kiasi cha Megawati 3000 za umeme ilitolewa na Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete katika hotuba yake kwa Taifa ya kuukaribisha mwaka 2012, pale aliposema kwamba, ujenzi wa bomba la gesi toka Songo Songo na pia toka Mtwara hadi Dar es Salaam, utaligeuza tatizo la umeme kuwa historia. Je, bomba hilo litakuwa na uwezo wa kusafirisha gesi yenye futi za ujazo ngapi na ni lini ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais itaanza kutekelezwa?

Mheshimiwa Spika, mitambo iliyopo Dar es Salaam inayoendeshwa kwa kutumia gesi ya Songosongo kama vile *Songas, Symbion,* mitambo ya Ubungo ya *TANESCO*, Jacobson ya *TANESCO* - Tegeta kwa ujumla wake inazalisha Megawati 522. Lakini gesi iliyopo ya

Megawati 400 haiwezi kukidhi Megawati hizo zote kwa mara moja. Hii ina maana kwamba mashine zote zingepata gesi zingeweza kutembea na ku-*produce* umeme kwa wakati mmoja na hivyo kupunguza utegemezi wa umeme wa maji ambao katika hali halisi, kwa hivi sasa una upungufu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna uwezo mkubwa wa mitambo ya gesi kuliko gesi iliyopo. Serikali iharakishe mradi wa bomba la gesi kutoka Mtwara na Songo Songo ili mitambo yote ya kuendesha gesi ifanye kazi kwa wakati mmoja na hivyo kuepusha Taifa na baa la mgao wa umeme.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba *TANESCO* hawakusanyi mapato ipasavyo na inavyostahili. Uzalishaji wa umeme haulingani na mapato yanayokusanywa. Changamoto zifuatavyo zinazorotesha utendaji na mafanikio ya *TANESCO*, wizi wa umeme kwa kutumia vishoka wa umeme. Upotevu wa umeme kutokana na miundombinu mibovu, wadaiwa wakubwa hawalipi kwa wakati na wengine hawalipi kabisa.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* ingeweza kufanya yafuatayo ili kuboresha mapato yake. Eneo la *Distribution* wange-*out source* kuwapa Kampuni nyingine, wao wadai tu malipo. Nchi nyingine wanafanya hivyo, mfano, *Latin America* na nchi nyingine za Ulaya. Umeme mwingi unaopotea kwenye *hightension* kwa sababu ya miundombinu mibovu na pia wizi (vishoka) wasakwe na kuadhibiwa, miundombinu iboreshwe kwa kuweka *transmission lines*

zenye uwezo mkubwa kutoka KV 220 na kuongezwa hadi KV 400 au KV 600.

Mheshimiwa Spika, kutokana na *connection* kuwa nyingi, uwezo wa *transfoma* zilizopo umepungua, kwa mfano, Dar es Salaam, zibadilishwe mapema iwezekanavyo ili kuondoa usumbufu uliopo kwa watumiaji wa umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na uwasilishaji wake makini na kwa ufasaha. Nawapongeza pia Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Viongozi na Watumishi wa Wizara kwa uandaaji wa hotuba yenye mwelekeo na matumaini.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii pia kuipongeza Wizara kwa usimamizi mzuri wa sera za Nishati na Madini. Mradi wa umeme vijijini ni mkombozi wa Watanzania wengi ambao wanaishi vijijini, na kichocheo kikubwa cha maendeleo ya nchi yetu. Wizara na hasa Waziri aendelee kusimamia kwa umakini utekelezaji wa Mradi wa Umeme Vijijini ili tupate mafanikio.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Bagamoyo, tuna changamoto kubwa ya upatikanaji wa Nishati ya Umeme kwa wananchi vijijini. Kuna vijiji kadhaa ambavyo vinapitiwa na nguzo na nyaya za umeme, lakini vyenyewe havipati umeme. Mwaka 2008 Wizara

ilipitisha umeme mkabala na barabara ya Dar es Salaam mpaka Kitopeni (Bagamoyo). Katika barabara hiyo, kuna vijiji kadhaa vikiwemo Mapinga, Kerege, Zinga, Kiromo na Kitopeni. Tatizo ni kuwa wanaofaidika ni wale tu ambao wapo jirani sana (labda mita 100 - 300) na nguzo zilizopo. Nje ya hapo, gharama ya kuvuta ni kubwa sana, wananchi wanashindwa. Maombi yetu katika laini hiyo ya Dar es Salaam – Bagamoyo. Wizara iongeze mtandao wa laini ya umeme ili wananchi wengi zaidi waweze kuvuta umeme kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, pia kuna vijiji kadhaa katika maeneo mengine ambayo ama vinapitiwa na umeme, au viko karibu sana na umeme, lakini havipati huduma hiyo ya umeme. Hivi ni pamoja na vijiji katika Kata ya Yombo (Yombo, Matimbwa, Chasimba na Kongo). Kata ya Kiromo ni Kijiji cha Buma ambacho kina idadi ya wananchi wengi wanaotaka huduma hiyo. Katika Kata ya Zinga Vijiji vya Pande na Kondo vimesubiri huduma hiyo kwa miaka mingi na umeme upo karibu yao sana.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anipe majibu, ni lini vijiji hivi katika Wilaya ambayo inapakana na Dar es Salaam vitapata huduma ya umeme?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE.EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nashukru kwa fursa hii ya kuchangia hoja ya Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ni kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kuwapongeza Viongozi Waandamizi wote wa Wizara hii, yaani, Mheshimiwa Prof. Muhongo, Naibu Mawaziri na Katibu Mkuu ambao wote ni wapya, kwa kuaminiwa na kuteuliwa kushika dhamana za uongozi walizonazo. Binafsi, nawafahamu vizuri utendaji wenu, na kwa kweli tayari mmeanza kuonyesha cheche zenu, labda kwa asiye na macho tu au mwenye lake jambo ndiye haoni. Aidha, nawapongeza kwa bajeti nzuri yenye kupeleka umeme Chela Ngaya, Bulige, Busangi na Ntobo kama nilivyoomba, nitaachaje kuiunga mkono? Hivyo naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na matumaini hayo makubwa, naomba Waziri na timu yake niwaongezee hadidu za rejea kwa kazi yao ya mwaka 2012/2013 ambazo ni kero kwa Wanamsalala.

Mheshimiwa Spika, Halmashariuri ya Wilaya ya Kahama, ina madai ya jumla ya Dola 7,406,993 ambazo ni ushuru wa huduma *(service levy)* ambayo haijalipwa na migodi toka migodi ya Bulyanhulu (2000) na Buzwagi (2009) ianze uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, mikataba ya uwekezaji ya migodi hii ilivunja sheria ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 inayoziruhusu Halmashauri kutoza ushuru huo kwa asilimia 0.3 ya pato ghafi la mwekezaji, badala yake mikataba hiyo iliweka ukomo wa Dola 200,000 kama

mbadala wa *service levy* ambayo ni ndogo kuliko *service levy* yenyewe.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Bomani ambayo mimi nilikuwa Mjumbe pamoja na akina Maswi, iliona upungufu huo na kushauri Serikali irekebishe Sheria ya Madini ya mwaka 2010, ikazingatia ushauri huo. Lakini hadi leo majadiliano, utekelezaji haujafanyika. Suala la kuongeza *royalty* toka 3% hadi 4% ambalo nalo limo kwenye sheria mpya na linatokana na *observation and recommendation* ya Tume ya Bomani limeanza kutekelezwa. Hili la *service levy* nalo ni budi litekelezwe mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, kama Serikali ilivyounda Kamati ndogo ya Bunge kufuatilia chenji ya rada Uingereza, wananchi wa Msalala wameunda Kamati ndogo ninayoingoza nije kudai chenji yetu pia. Naomba Wabunge wenzangu mtusaidie chenji yetu tulipwe. Naomba Mheshimiwa Waziri mtusaidi tulipwe.

Mheshimiwa Spika, naipongeza *REA* kwa kuendelea kutekeleza mradi wa umeme Mpera, Ntungulu na Mwakata Jimboni kwangu. Nashukuru pia kwa kukubali maombi yetu ya kupeleka umeme Vijiji vya Nyambula, Nyamigege, Busangi, Chela, Ngaya, Bulige na Ntobo. Naomba utekelezaji uanze wiki ijayo. Hata hivyo, naomba kuikumbusha Serikali kuhusu mradi wa umeme wa Bukombe ambao unanufaisha vijiji vyangu vya Segese, Shilela, Nyikoboko, Lunguya na Ikinda. Ahadi hii jamani imechelewa mno kutekelezwa, kwani ni ya mwaka 2008. Naomba nisikie na wananchi

wasikie mradi huu sasa, na kwa hakika kabisa, utaanza lini kutekelezwa?

Mheshimiwa Spika, pamoja na Kahama kuwa na maeneo mengi ya madini, hakuna eneo hata moja lililotengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Kila wanapogundua wanafukuzwa. Tunaomba wachimbaji wadogo walioko Masabi, Nyangalata, Nyamakwenge na Mwazimba wasiendelee kuondolewa, waachiwe maeneo hayo. Tunaomba maeneo mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, kuna madai ya wananchi wa Kakola walioharibiwa mali zao mwaka 1996 wakati wa kuanzisha mgodi wa Bulyanhulu. Bado wananchi hao wapatao 200 wanadai. Wamehangaika Mahakamani hadi wameishiwa hata fedha za kuendesha kesi. Walishaomba tangu mwaka 2009 kwamba Serikali ione uwezekano wa kumaliza suala hili kwa maelewano. Tunaomba sana ombi lao hilo lizingatiwe na ikiwezekana tatizo hilo liishe mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kushukuru. Kama nilivyosema awali, naunga mkono hoja ili Profesa Muhongo na timu yake walimalize hili.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii muhimu. Kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa namna ambayo katika kipindi kifupi amefufua upya matumaini ya Taifa letu kujikomboa kutokana na mgawo wa makusudi uliokuwa ukikumbwa na kusimamiwa na watumishi wasio na huruma walioajiriwa katika Serikali na Shirika la

Usambazaji wa umeme nchini Tanzania *(TANESCO).* Ni faraja iliyoje kumpata kiongozi ambaye ameweza kubaini uozo uliokuwa umegubika Sekta ya Umeme Nchini? Tunamwombea heri Mheshimiwa Waziri na Wasaidizi wake, changamoto zinazolikabili Taifa hili ni za hali ya juu katika Sekta ya Umeme, licha ya kuwepo kwa raslimali za kutosha zinazohusiana na uzalishaji wa umeme, kwa mfano, maji, gesi, jua, upepo, joto ardhi, urani na makaa ya mawe.

Mheshimiwa Spika, naishauri kwa moyo wa dhati Serikali na Wizara yenye dhamana kwenye Sekta ya Nishati na Madini, nchi sasa inakabiliwa na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi, kutokana na uharibifu wa mazingira, na ukataji miti kwa lengo la kuchoma mkaa unaouzwa Mjini kwa matumizi mbalimbali ya nyumbani. Ni muhimu Wizara ije na mkakati kabambe wa kuzalisha umeme kutokana na makaa ya mawe ambayo yanapatikana kwa wingi Kusini mwa Tanzania huko Kiwira, Mchuchuma na kadhalika. Uzalishaji wa umeme utakapoongezeka, ni vyema ukaenda sambamba na ujenzi wa njia za kusambaza umeme na kuupeleka vijijini.

Umeme ukipatikana, uuzwe kwa bei nafuu ili kuepusha nchi yetu kugeuka jangwa. Aidha, kwa kuwa nchi yetu imejaliwa kuwa na rasilimali ya gesi asilia katika Mikoa ya Lindi na Mtwara, ni muhimu sasa Serikali ikaandaa mkakati kabambe wa kusambaza gesi hiyo kwa kuanzia Majiji ya nchi hii ambayo ni Dar es Salaam, Tanga, Mwanza, Mbeya na Arusha. Baada ya Majiji yetu kupatiwa huduma ya gesi, ifuate Majiji Makuu ya Mikoa na Wilaya.

Mheshimiwa Spika, mkakati huu utanusuru kwa kiasi kikubwa misitu na miti inayochomwa kwa lengo la kupata mkaa unaotumiwa kwa kiwango kikubwa mjini. Chanzo kingine cha umeme ni kuanza mkakati wa kujenga vinu vya kuzalisha umeme *(nuclear readers),* lengo ni kunusuru mazingira ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba ahadi ya Serikali na Wizara itoe msukumo wa kipekee katika kuyapatia umeme maeneo yote ya Wilaya mpya ya Mbongwe ili kusukuma maendeleo kwa kasi zaidi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wilaya ya Mbongwe imejaaliwa kuwa na wingi wa madini ya dhahabu katika maeneo ya Ihenda, Nyakafuru, Lugunga, Bukandwe na Nyakasahuma, lakini tatizo lililopo ni kwamba wachimbaji wadogo wadogo hawajawezeshwa kupata nyenzo na miundo msingi katika kuwasaidia wachimbaji hawa kuongeza tija katika shughuli zao. Naiomba Serikali iongeze jitihada za kuyaainisha maeneo yanayofaa kwa shughuli zao za uchimbaji ikiwemo kuwapatia leseni zitakazowawezesha kuyamiliki kihalali maeneo wanayofanyia kazi. Hii ni kwa mujibu wa taratibu za kisheria.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini kwa uamuzi wake wa kuipatia Wilaya yetu ya Mbongwe huduma ya umeme kupitia mradi wa *electricity V* na Wakala wa Umeme Vijijini *(REA)*.

Mheshimiwa Spika, naomba mchakato uharakishwe. Naunga mkono hoja.

**MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Sababu za kuunga mkono hoja ni kutokana na Serikali kulikabili tatizo la umeme angalau kwa mwaka huu hatujawa na mgao mkali.

Mheshimiwa Spika, napongeza Wizara ya Nishati na Madini, Waziri, Manaibu Mawaziri na Katibu Mkuu, kwa kazi kubwa wanayoifanya katika Wizara ya Nishati na Madini ya kuinusuru Wizara hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu, nitatoa masikitiko kwa umeme wa Zanzibar (miundombinu siyo mizuri) sijui ni nani, lakini naomba iangaliwe.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi za Serikali za ujenzi wa bomba la gesi, lakini gharama za mafuta ni kubwa sana. Naipongeza Serikali kwa kuokoa Shilingi bilioni sita kwa mwezi, na naomba waangalie maeneo mengine kuona jinsi ya kunusuru hali kama hiyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeokoa fedha nyingi sana, wamefanya uzalendo mkubwa sana na tunawaunga mkono asilimia mia kwa mia.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Nishati na Madini - Mheshimiwa Profesa Muhongo na Katibu Mkuu wake

Ndugu E. Maswi kwa kuteuliwa kushika nyadhifa hizi za Uwaziri na Ukatibu wa Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, Shirika la *TANESCO*, limekuwa lenyewe, hakuna mshindani, na hivyo utendaji wake siyo wa kufurahisha. Yapo mambo mengi yanafanywa na Watendaji ya kuwahujumu Watanzania. Watanzania nao pia wanahujumu Shirika.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mchache, viongozi hawa wameonyesha mafanikio, wameonyesha kufunga mirija ya wizi na matumizi mabaya na ufisadi wa Watendaji wa *TANESCO*. Ninashauri waendelee na wachukue hatua kwa wafujaji wa fedha ya umma. Kununua mafuta Purma, kuli-*save* Shilingi bilioni tatu ambazo miaka mingine zilikuwa zinawekwa mifukoni. Wahusika wachukuliwe hatua za kisheria walipe fedha wanazofuja.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu imeonyesha *TANESCO* kumbe inaweza kulipa madeni kwa kukusanya zaidi ya bilioni 50 kwa mwezi naishauri Serikali iangalie uwezekano wa kuwapa Watanzania umeme wa uhakikia na endelevu kukatika kwa umeme mara kwa mara kumetesa watanzania kiuchumi na kijamii. Biashara nyingi zimedorora na maeneo mengine ujambazi kutokea kwa sababu ya giza. Nashauri bei ya umeme pia iangaliwe ipungue kidogo.

Mheshimiwa Spika, yako maeneo mengi nchini ambayo yana maporomoko madogo ambayo vijiji au *private sector* wanaweza kuzalisha umeme wa *Megawatt* chache za kutosha Kijiji, Zahanati, Shule na kadhalika zilizopo, na umeme unaozidi wakawauzia

Serikali. Naishauri Serikali ifanye utafiti wa maeneo kama haya ili umeme utakaopatikana utumike u-*save* mzigo mkubwa wa umeme wa *grid,* badala yake, umeme wa *grid* uelekezwe zaidi katika Miji mikubwa.

Mheshimiwa Spika, viwanda vya sukari vinaweza pia kupata umeme kutokana na *residue* zinayotokana na miwa. Kiwanda cha *TPC* Moshi kinatengeneza umeme wa Megawati 15. Wanatumia Megawati 10, Megawati mbili wanawapa Kijiji na Megawati tatu wanauzia *TANESCO*. Naishauri Serikali, viwanda vyote vyenye *residue* za aina hiyo waelekezwe watengeneze umeme kuipunguzia mzigo Serikali.

Mheshimiwa Spika, Bwawa la Nyumba ya Mungu linalosaidia Kituo cha Umeme cha Hale Tanga, sasa hivi hali yake imezidi kuwa mbaya. Kwa sababu Serikali inahitaji kuzalisha umeme, nashauri Serikali ichukue hatua za ziada kuliweka sawa ili umeme wa kutosha uendelee kupatikana.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wakubwa wa dhahabu na madini mengine, kuna wakati wanatafiti maeneo na wanaona kuwa eneo hilo halina madini ya kutosha kufungua mgodi. Nashauri maeneo kama haya Serikali itoe leseni za Makampuni hayo na iwagawie wachimbaji wadogo kwa mpangilio maalum.

Mheshimiwa Spika, Kenya inajulikana kama *exporter* mkubwa wa *Tanzanite* katika nchi za Afrika Mashariki, lakini mchimbaji na mwenye *Tanzanite* ni Tanzania. Nashauri Serikali, *Tanzanite* inayochimbwa

ikatwe hapa hapa Tanzania na kuwepo Umoja wa Wachimbaji ambao watathibiti uuzaji holela wa madini hayo.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo hatarishi ambayo Serikali inatoa *prospective licence* na wakati mwingine liseni za uchimbaji, mfano ni Msitu wa Shengena Wilayani Same. Eneo hilo ni hifadhi ya Taifa na ni eneo ambalo ni hatarishi kwa maporomoko ya ardhi *(land slides).* Maporomoko kama hayo mwaka 2009 yaliua watu 24, wachimbaji, wanabeba udongo na malori kupeleka Kenya ati una *bauxite*. Wakati wanachimba mlimani, chini ya mlima kuna kaya zaidi ya 3000. Je, Serikali haioni kuwa kuna haja kufanya utafiti wa maeneo kabla ya kutoa leseni za wachimbaji hawa katika misitu ya Shengena?

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali kwenye kuzalisha umeme ishirikishe pia wahandisi wazawa wa umeme. *Experience* yao pia inaweza kusaidia hasa katika vyanzo vipya vya kuzalisha umeme. Wakishirikishwa, inawezekana pia wakasaidia kutoa taarifa zozote za hujuma zinazopangwa na Watendaji wa *TANESCO*. Tunaishukuru Serikali kufanya utafiti na kugundua gesi huko Mtwara. Tunaishukuru kufunga Mkataba na Kampuni ya China kujenga bomba la kusafirisha gesi mpaka Dar es Salaam na Tanga.

Naishauri Serikali kwamba bomba hili lijengwe mpaka Arusha kwa sababu mapato mengi ya pato la Taifa yanatokana na utalii ambao unatoka Arusha na Kilimanjaro. Kama wakazi wale wakipata gesi wataacha kukata miti, mazingira yataboreka na utaliii

utashamiri na pato la Taifa. Pili, nashauri Serikali isimamie ujenzi wa bomba hili na bomba limilikiwe na Serikali na isiruhusiwe kampuni binafsi kumiliki labda kwa Mkataba unaofaa na siyo wa kinyonyaji.

Mheshimiwa Spika, nashauri gesi iingizwe Dar es Salaam, iwe na bei nafuu ili kupunguza matumizi ya mkaa (mazingira).

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kwimba ina vijiji vingi havina Nishati ya umeme na hata kama nishati hiyo wangepelekewa, kwa sababu nyumba zao ni za tembe na zimeezekwa kwa nyasi.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ianzishe mradi wa kuhamasisha wananchi hao kuboresha nyumba zao kwa kushirikiana jambo ambalo limefanikiwa Rwanda, kwa kuzingatia hali halisi ya vijiji. Napendekeza Wizara katika kitengo chake cha huduma za jamii, watoe mashine za kufyatulia matofali na mabati ili kuwawezesha wananchi kuwa na nyumba ambazo zitafaa kuweka nishati ya umeme na hata ile ya *Solar*.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itoe maelezo jinsi gani bajeti hii ya Wizara inazingatia kuboresha maendeleo ya wanawake kuanzia Wizarani na jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya nchi yoyote siku hizi yanapimwa kwa kuangalia jinsi gani wanamwezesha mwanamke. Hili linazingatiwa sana na wenzetu wa nchi zilizoendelea kama Marekani. Bajeti za Wizara zote huzingatia matumizi kwa uwiano wa kijinsia.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze jinsi Wizara yake inavyotekeleza majukumu yake kwa kutambua nafasi ya mwanamke katika jamii.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa jitihada zake za kupunguza mgao wa umeme.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni mwaka 2001 aliahidi kuwasaidia wananchi wa Tarafa ya Mlola kupelekewa umeme.

Mheshimiwa Spika, naishukuru *REA* na Wizara kwa ujumla kuonyesha dalili na nia thabiti ya kupeleka umeme Tarafa ya Mlola kwa kutuma wataalam kwenda kupima *(survey)* ya kupeleka umeme vijiji vya Kata za Kwekanga, Malimbwi Kilole Ngwelo na Mlola. Katika Tarafa ya Mlola. Baada ya mashauriano na uongozi wa *REA,* tulikubaliana umeme sasa utokee kwenye msongo wa KV 33 kuanzia eneo la Malindi kupitia eneo la Vijiji vya Mziragembei, Mghangai kuelekea Malimbwi na Tawi litoke hapa Mshangai kuelekea Kwakanga, Karenda, Kilole hadi Mbwei na Mhezi ipatiwe tawi dogo na kutoka Mbwei umeme upelekwe Kijiji cha Ungo hadi Mlola.

Mheshimiwa Spika, naomba umeme kwenda Kata ya Ngwelo upitie kijiji cha Makole kutokea Kwekanga. Kwa kufuata Mpango huo, vijiji vyote vya Kata nilizotaja zitapata umeme wa uhakika wa msongo wa KV 33 badala ya mpango wa awali kwamba umeme utakaopelekwa Tarafa ya Mlola hususan Kwekanga ungetumia njia ya msongo wa KV 11 kutoka eneo la Kwemakame.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata umeme Kata ya Kwekanga, Ngwelo, Malimbwi, Kilole na Mlola, naomba Serikali iangalie uwezekano wa kupeleka umeme Kata ya Makanya ambayo kipekee ndiyo haitaguswa na mpango wa sasa wa kupeleka umeme Tarafa ya Mlola.

Mheshimiwa Spika, kuchelewa kuunganishiwa umeme wananchi wa Kijiji cha Gare eneo la Kizara ambao waliomba umeme na kulipia mwaka 2002, hadi leo hii mwaka 2012 hawajapata umeme. Nimewasilisha viambatanisho kwa Waziri wa Nishati na Madini - Mheshimiwa Profesa Muhongo. Naomba wananchi hao wapate haki yao ya kupatiwa umeme.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na tatizo la muda mrefu la umeme kwa ukosefu wa maji hasa kwenye bwawa la Mtera, kwamba maji yanapungua. Nilikuwa naulizia, Mto Pangani ni lini uliwahi kupungua maji? Kwanini Serikali isielekeze nguvu kubwa kwenye Mto Pangani ambao huwa haukauki maji?

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Korogwe vijjini, kuna maeneo mawili ya nguvu ya umeme, lakini cha kushangaza, kwenye Jimbo hilo ambalo vyanzo ni viwili, vijiji havina umeme kabisa.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *REA* inasambaz umeme vijijini. Je, ni kwanini hawajawahi kusambaza umeme hata kwenda kupima Korogwe Vijijini, badala yake inahusika Mjini tu?

Mheshimiwa Spika, kuna vijiji ambavyo vimepitiwa na umeme lakini vijiji havina umeme. Kwa mfano, Kata ya Mnyuzi na Kijiji cha Kwamzindawa, Mkwakwani, Gereza la Lusanga Kata ya Kwagunda, Mngaza, Kata ya Kerenge Kubaoni, Lusanga, Kwemazandu, Matalawanda Kata ya Magoma Mbuyuni Kikwajuni, Sekioga Kata ya Dindira, Kwefingo, Mgwashi Kata ya Vugiri Bagamoyo, Makweli, Mlalo Kata ya Mkalamo, Masimbau. Naomba Serikali iangalie kwa undani sehemu hizi ukizingatia nguvu ya umeme inatoka hapa.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo wadogo wapewa maeneo maalum na hati ili wapate mikopo Kalalani na Kigwasi kule kwenye Jimbo la Korogwe vijijini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja ya Wizara hii ya Nishati na Madini kwa asilimia mia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuunga mkono hoja, naomba sasa kuchangia kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imetenga fedha za kupeleka umeme kwenye Wilaya Mpya ya Chema katika mwaka huu wa fedha, naomba umeme huo utokee katika Kijiji cha Mondo ambapo kuna umeme wa *grid* ya Taifa ili upite katika vijiji vya Waida, Sori, Pongai, Cheku, Kelema na Paranga ambayo licha ya kuwa na idadi kubwa ya watu, pia ni kilomita chache kutoka Chema kuliko kuchukua umeme kutoka Kondoa Mjini ambako ni mbali zaidi ya mara tatu na hakuna kijiji chochote kilichopo kati ya Kondoa na Chemba kwa kufuata barabara kuu.

Mheshimiwa Spika, umeme umefika katika Kijiji cha Dalai ila kilometa nne tu kabla ya kufika katika Kijiji cha Tandala ambacho kina watu zaidi ya 15,000 ambao wanahitaji umeme huo kwa udi na uvumba. Naiomba Serikali kupitia *TANESCO* kufikisha umeme katika kijiji hiki ambacho hakihitaji hata nguzo zaidi ya 20.

Mheshimiwa Spika, vijijini vya Mapanga na Churuku vina umeme ambavyo vipo kilomita chache kutoka Vijiji vya Kerikima Jangalo Itotwa na Mlongia ambavyo vina idadi kubwa ya wakazi wasiopungua 40,000 ambao wanahitaji umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima kubwa, naiomba Serikali kupeleka umeme katika vijiji hivi ili wananchi wapate umeme na Serikali iongeze mapato yake.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena, nampongeza Mheshimiwa Waziri Prof. Muhongo, Naibu Mawaziri Boniface Simbachawene na Naibu Waziri Mheshimiwa Stephen Masele kwa kuteuliwa kwao, na naamini watakuwa kichocheo cha kuboresha nishati ya umeme na madini.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Madini ya *North Mara Gold Mine (Barrick Minning Company)* kudhulumu Wilaya ya Serengeti. Kwa vile kuna *beacons* za eneo la umiliki la Madini la Kampuni hii ya Barrick, lipo katika Wilaya ya Serengeti Kata ya Kisaka Vijiji vya Borenga na Nyiboko, kwa nini hakuna mgao katika Wilaya ya Serengeti na pia mchango wao katika vijiji hivyo?

Mheshimiwa Spika, kwa vile kuna vyanzo vingi na mbadala wa umeme kama gesi na maporomoko kama Majimoto, Rorya (Panyakoo) na Tarime (Nyakunguru) kwa *reserve* kubwa sana ya gesi pia katika Mto Mara eneo la Balagonja kwa maporomoko ya maji makubwa ni kwa nini usianzishwe mradi mkubwa wa kufua umeme ili kupunguza kero ya upungufu wa umeme (17%) ili kufikia 2015, tufikie 30%.

Mheshimiwa Spika, kwa vile bahati nzuri umeme huu wa *grid* umefika Tarime (Nyamongo) ni kwa nini bidii ya makusudi haifanyiki ili kusambaza umeme huo kwenda Wilaya ya Serengeti?

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini umeme wa kuaminika hauletwi toka Uganda (Jinga) ili kuendelea kuongeza vyanzo vya kupata umeme na pia kupanua uhusiano wa Afrika Mashariki?

Mheshimiwa Spika, je, Wizara ina mpango gani wa kupunguza gharama ya umeme ili kutoa fursa ya kupunguza uharibifu wa mazingira, kwa sababu umeme kuwa ghali inachangia sana kuharibu misitu na mazingira?

Mheshimiwa Spika, mrahaba ni kidogo sana (4%) Serikali itazame upya ili kupandisha pato kutokana na madini kutoka 14%.

Mheshimiwa Spika, nashauri sheria ya madini ipitiwe kwa vile bado kuna kero nyingi.

Mheshimiwa Spika, madini ya urani hayajafahamika vizuri kwa wananchi kwa vile wananchi wengi hawajui kwa kina juu ya hatari na athari za madini haya. Je, Serikali ina mpango gani ili kuelimisha wananchi na kuwalinda?

Mheshimiwa Spika, kuongeza nguvu *(voltage increase)* na kuweka *transformer* maeneo yaliyopewa umeme mwaka 2004; sehemu nyingine ni *single phase:* Je, *REA* (Wizara) ina mpango gani kuweka umeme wa *three phase* na kuweka *transformers*?

**MHE.MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati

kwa kazi kubwa anayoifanya ya kupambana na ubadhirifu na ufujaji wa mali ya umma hasa katika Shirika la *TANESCO*. Namwomba Mheshimiwa Waziri pamoja na Manaibu zake waongeze jitihada za kupambana na wale ambao hawaitakii mema nchi hii.

Mheshimiwa Spika, suala la umeme vijijini, ni muhimu sana Wizara ikaweka kipaumbele kikubwa kupeleka umeme vijijini, kwani tukitaka maendeleo ya haraka katika nchi hii, lazima umeme vijijini uwafikie wananchi walio wengi katika nchi ambao wengi wao wanaishi huko. Tukiimarisha kupeleka umeme huko, wananchi wengi watakuwa na fursa ya kuweza kusindika mazao wanayoyazalisha katika maeneo yao wanaoishi.

Mheshimiwa Spika, umeme wa *grid* ya Taifa katika Mikoa ya Pembezoni, Mikoa ya Rukwa, Katavi na Kigoma haina umeme wa *grid* ya Taifa. Tunaiomba Serikali kupitia Wizara, ilete umeme wa *grid* ya Taifa ili uweze kuinua uchumi katika Mikoa hiyo, kwani umeme wa uhakika ukiwepo tutakuwa na uhakika wa kupata wawekezaji ambao watawekeza katika Nyanja ya Kilimo, Madini, Uvuvi na kadhalika. Maeneo yetu yana vivutio, tatizo kubwa ni kukosekana kwa umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, mradi wa makaa ya mawe ni muhimu sana ukaimarishwa kwa kuweka mikakati ya kusimamia mradi huu ufanye kazi ili uweze kutoa Megawati za kutosha kwa ajili ya kupeleka umeme katika maeneo ya nchi hii na kupata ziada ya kuuza nje ya nchi na kulipatia pato la Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara inihakikishie uwezekano wa kupata umeme katika maeneo ya Ziwa Tanganyika maeneo ya Karema na Ikola. Eneo hili ni muhimu sana ukizingatia shughuli za eneo hili ni uvuvi ambao kama wakipata umeme upo uwezekano mkubwa wa kukuza uchumi katika eneo hili na tulishapata wawekezaji katika *sector* ya uvuvi ambao wanataka kufanya shughuli za uvuvi na kujenga viwanda vya kuchakata samaki katika eneo hilo. Tatizo kubwa ni ukosefu wa umeme.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara iweze kutoa umeme katika Kata Kata ya Kabungu na Mpanda ndogo kwani ziko karibu sana na maeneo ya Mjini ambako umeme upo, kwani tukisogeza umeme katika kata hizo, kuna uwezekano mkubwa wa kusaidia Shule za Sekondari zilizopo katika Kata hizo na kuwasaidia jamii zifanye shughuli za kiuchumi vizuri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kuchangia bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa njia ya maandishi. Awali ya yote, naunga mkono bajeti hii ipite na kama kuna mabadiliko, basi yawe yale ya kuongeza fedha na siyo kupunguza.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, katika Wizara hii ni hoja ya kujipanga upya. Wizara na asasi zote zilizoko chini yake yawabidi kutambua kuwa kwa kiasi kikubwa Maendeleo na Ustawi wa Taifa hili

unategemea uendeshaji na udhibiti wa sekta hii. Kwa lugha ambayo labda haitapendeza kwa masikio ya watu wengine, tuko katika hali duni na kasi ya maendeleo hairidhishi Watanzania kwa sababu ya kushindwa ku-*manage* sekta hii ya Nishati na Madini. Naunga mkono bajeti hii kwa matumaini kuwa masikio ya Serikali kupitia Wizara hii yatasikia na kuweza kutekeleza yale yanayoshauriwa na yanayowastahili wananchi wa Taifa hili. Nina imani na Viongozi na Watendaji wa Wizara hii mpaka hapo sasa tuanze.

Mheshimiwa Spika, nafasi ya umeme katika kuchangamsha uchumi wa Taifa na mchango wa *REA*, utendaji wa *REA* katika uhai wake wa miaka mitano unaonekana na kuvuma nchi nzima. Miradi 119 imejengwa yenye gharama ya Shilingi bilioni 257.67,84 ikiwa imekamilika na miradi 35 ikiwa inaendelea hoja yangu ni kuwa, kama Shilingi bilioni 260 zimelifanya Taifa lizizime na kuona matumaini katika *REA,* basi kwa mwaka mmoja wa bajeti kiasi kikubwa kitengwe ili hatua iliyotuchukua miaka mitano tuivuke kwa miezi sita tu. Hiyo ndiyo busara ya mwana mikakati Charles Handy. Mwanachura huwa asubiri dimbwi lipate joto jua likitoka, bali huchupa toka dimbwi moja kwenda dimbwi lingine mpaka afikie dimbwi lenye joto analotaka. Watanzania vijiji tunawaombea umeme, siyo vibatari, na ndiyo maana tukaongeza kodi mafuta ya taa. Tengeni Shilingi bilioni 600 tuingie kwenye dimbwi lenye maji yenye joto tulitakalo umeme vijiji vyote. Inawezekana.

Mheshimiwa Spika, uongozi wa Wizara unapashwa kuelekeza macho kwa mtoto huyu mzuri anayeanza kutambaa. Wapeni Mamlaka majukumu na njia za uwajibikaji Watendaji wa asasi hii. Kueni karibu na *REA,* fuatilia utendaji wao na pimeni malengo yao kwa vipindi vifupi. Moja, hii itasaidia kuwapa msukumo wa ndani katika kutekeleza malengo; pili, itawaepusha na watu wenye nia mbaya ambao bila kutafuna maneno watakuwa wananyemelea fedha nyingi zinazotengwa na Serikali ili wazitafune. Tatu, ukaribu utatuwezesha kujua mapema kama *train* yetu imetokea kwenye reli na hivyo kurudi kabla hata wasafiri wengine hawajajua. *REA* na *value for money*!

Mheshimiwa Spika, Shirika la Umeme *TANESCO* ni muhimu, mbali ya kuzalisha na kusambaza umeme, hiki ni Chuo. Watanzania wanaoingia katika Taasisi hii wana fursa sawa ya kujiendeleza na kupanda ngazi bila kujali nasaba zao. Hoja yangu hapa ni kuwa *TANESCO* iimarishwe kwa mfumo ilionao kwa kutumia *SBUs* katika kuleta ufanisi, lakini isimegwe vipande. Ni ukweli uliowazi ikimegwa vipande, walio wengi watakimbilia *generator,* lakini zaidi Watendaji wazawa watabaki katika madaraja ya chini bila kujali wana ujuzi na utendaji uliotukuka kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* ina tatizo la ukusanyaji wa madeni yake. Moja, iwapo sheria zinazoendesha asasi hii zina upungufu, basi ziletwe Bungeni tuwape meno makali. Pili, kwa mtazamo wangu watendaji wake wenye elimu na ujuzi wa ufundi wanapashwa kupigwa msasa wa sheria na biashara. Hoja yangu hapa ni kuwa mkusanya madeni awe na

elimu ya ufund,i uzoefu wa ufundi, na msasa wa biashara. Epukeni kuajiri watu wasioweza kutofautisha *volt* na *watt* kuja kufanya kazi ya biashara na kukusanya madeni. *TANESCO* ni asasi ya kiufundi, hivyo Idara zote zizungumze lugha ya ufundi. Tatu, ni kutumia mtindo wa *total marketing* katika kukusanya madeni.

Mheshimiwa Spika, mtindo huu umetumika sana katika nchi za Mashariki ya mbali ambazo Watanzania tunapenda kuzisifia na kuzitolea mfano. Chini ya mfumo huu, kila mfanyakazi ni mlinzi na mkusanyaji wa tozo za Shirika. Mfano, kwa Jiji la Dar es Salaam, Shirika linapaswa kuhakikisha kila Mtaa au la, basi Mitaa minne mpaka mitano anaishi mfanyakazi katika mtaa au Kata. Kazi ya mtu huyu ni kusikiliza, kuchunguza na kutoa taarifa kwa jambo lolote lenye manufaa kwa Shirika. Inapobidi, chini ya utaratibu maalum, wafanyakazi hawa wanaweza kupewa jukumu la kukagua malipo ya Ankara. Ni kheri katika Shilingi bilioni 200 zilizoko mikononi mwa wateja zikalipwa mara moja na motisha wa asilimia tano kwa Watendaji wanaosimamia na kufuatilia.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* inaendana na mitambo ya kukodi. Tunapojenga bomba la gasi asili ni vema basi tuelekezwe ni vipi tutaanza kuondoa mitambo ya kukodi na kununua ya kwetu. Hoja hapa ni ratiba ya kuondoa kuwekea *order* na kuleta ya kwetu tukizingatia kuwa utengenezaji wa mitambo uchukue miaka miwili mpaka mitatu. Visingizio zaidi siku za mbeleni visitumike kuwatupia watanzania mitambo chakavu ambayo wenye nayo wamekuwa wakitutoza

*capacity change* kwa viwango vya juu sana. Tujipange kwa ajili ya kesho.

Mheshimiwa Spika, mwisho, katika Sekta ya Umeme nizungumzie umeme utokanao na vyanzo vya maji. Wakati umefika sasa Serikali kwa kutumia Wizara, Idara na Vitengo vyake vyote vinavyohusika na Mito na Maji kuhusika kwa nguvu zote katika kutunza hazina hii. Vyanzo vya maji, mito, misitu, hifadhi ya maji na mabwawa, lazima yaangaliwe kitaalam na yalindwe. Mabwawa yaliyojengwa kwa gharama kubwa ni vema tuyatunze ili yazalishe umeme kwa ufanisi, matumizi ya maeneo oevu na mito bila kuangalia matumizi na manufaa mapana ya maji, lazima yakemewe na Serikali kwa nguvu sana.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie sekta ya mafuta jamii ya *petrol* au *downstream activities.* Mafuta ni jukumu la Wizara ya Nishati. Nakiri kuwa, nimemweleza Mheshimiwa Waziri kwa mifano na amekubali kuwa upungufu katika sheria unaifanya sekta hii, ujumbe na/au ikae bila uangalizi makini. Hii ni sekta nyeti inayohitaji uangalizi wa karibu wa Serikali. Siyo sahihi kuamini kuwa sekta binafsi katika ushindani wa sasa, sheria na siasa zisizotabirika itaweza kuendeleza sekta kwa kushamirisha shughuli pande zote za nchi.

Mheshimiwa Spika, narejea msimamo wangu wa kutaka kuwepo kampuni ya kitaifa (*National Oil Company),* iliyojengeka na kukua taratibu kuanzia chini *(organic growth)* akihusisha mizizi na matawi ya wananchi. Hapa namaanisha Serikali za Mitaa, Halmashauri za Wilaya, Asasi za Serikali, Mashirika ya

Umma na Makampuni binafsi ambayo mikakati yao ya utendaji ni kujinasibisha na Serikali. Sikubaliani na mipango na mikakati ya kampuni *COPEC*. Hiki siyo tunachohitaji, tunataka kujenga mtandao toka chini. Kampuni ya Taifa inayoendesha kwa namna fulani kituo kinachomilikiwa sehemu na Halmashauri ya Kilwa au Chama cha Ushirika cha *KCU* na Bukoba. Katika hali tuliyonayo, sioni kampuni binafsi inayokopa kwa riba ya soko na masharti ya kurudisha mkopo baada ya miaka mitano ikajenge Kituo cha Mafuta Kisiwani Goziba au nyumbani Rutoto.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine, kutokuwa na kampuni ya kitaifa katika dunia hii iliyojaa mitikisiko ya kiuchumi, ni hatari kwa uchumi na usalama wa nchi. Katika hali ya mtikisiko, busara kwa kampeni binafsi ni kukimbia soko. Anayetaka mifano kwa hili, ana lake jambo.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie mfumo wa ununuzi wa mafuta kwa wingi, *Bulle Procurement System.* Mfumo huu ukianzishwa kwa azimio la Bunge letu Tukufu na unaendeshwa na *regulations* zilizopitishwa na Waziri mwenye dhamana. Niliunga mkono azimio na kupinga *regulations* na mpaka sasa bado nazipinga. Muhimu hapa ni kuwa, yote yale niliyoyapinga yameanza kutokea labda jambo moja au mawili. Mafuta yana vitu vitatu muhimu; *quality, availability* na *affordabilitiy*. Hatukuwa na tatizo la upatikanaji wa mafuta kabla ya mfumo huu na sasa hali ni ile ile ukiacha kidogo mafuta ya taa.

Mheshimiwa Spika, tatizo la bei liko pale pale na mfumo haujaleta nafuu. Hii ni kutokana na kutokuwepo miundombinu sahihi, lakini pia kanuni za uendeshaji kuwa na mapungufu upande wa uhakika wa kiasi kilichoanzishwa kuna maboresho hasa kwa wale wazembe wa kufanya kazi wanaopendelea kila kitu waletewe Mezani. Tumeshuhudia tofauti katika kiasi kwa kulinganisha takwimu, bandari ya kupakia, kushusha na matankini. Umeibuka ugonjwa wa upotevu wa mafuta katika mtandao wa mabomba Kurasini, tatizo ambalo nilikuwa mmoja wa waganguzi wake waliolidhibiti kwa mafanikio makubwa. Napenda niwapongeze watendaji waliokuja kunitaka ushauri japo kwa uficho.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa ni ubora wa mafuta yanayoingizwa nchini. Taarifa ya Mkemia Mkuu na *EWURA* zimethibitisha kuwa *petrol* iliyoingizwa nchini kati ya Januari na Machi ilikuwa na *ethanol* kupita kiasi karibu asilimia 10 zaidi. Vyombo vyetu vimeonyesha upungufu *TBS* na *EWURA* mpaka baada ya kilio kikubwa. Lakini baya zaidi, *regulations* za Waziri mwenye dhamana zimekuwa kimya. Taifa na Watanzania wamepata hasara ambayo siyo Wizara au *EWURA* anayekuwa tayari kusema ni kiasi gani. Naishauri Serikali ilazimishe mamlaka husika kutamka kiasi cha hasara na walaji waombwe msamaha tujipange upya.

Mheshimiwa Spika, mbali na mapungufu katika *regulations,* ni mtindo wa utendaji Serikalini ambapo Idara, Mamlaka na Mashirika kila kimoja kinajipanga kama himaya inayojitosheleza na isiyohitaji ushirika toka

nje. Vyombo vinavyotawala au kuendesha Sekta ni *TPA, TBS, EWURA, PIC* na Wizara yenyewe. Hawa wote kila asasi inasimama kama kiumbe kisicho na uhai, mfano, jiwe au chuma. Mfano, wa *ethanol* unatosha kuelezea mapungufu ninayoyasema, lakini kurejea kwa mlundikano wa meli nje ni mfano mwingine. Iweje gati la Kurasini lipangiwe kupokea meli tisa kwa mwezi ili hali meli moja inatumia siku tatu mpaka nne kushusha mzigo. Wakati huo huo kuna meli ya mafuta mazito *(HFO)*, mafuta ya kula *(VD)* na wakati mwingine *LPG*.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu hapa ni kuwa, asasi ziongozwe na utumishi kwa umma yaani kuwapa Watanzania kile wanachotaka. Wasiongozwe na sheria zilizounda mamlaka hizo, bali sheria hizo wazitumie kutekeleza majukumu. Nashauri Sekta ya Mafuta ibaki na idhibitiwe na Wizara ya Nishati na asasi nyingine wawe wawezeshaji.

Mheshimiwa Spika, nimepitia nyaraka za mawasiliano za *PIC,* kuna hatari inalikabili Taifa, kuna kauli zisizo rafiki, kauli za kutishiana na kusababishiana hasara za mamilioni ya Dola za Kimarekani, kauli za kupelekana Mahakamani. Hoja yangu hapa ni: Je, iwapo *PIC* atapelekwa Mahakamani na kuamriwa alipe mfano Dola milioni 20. Fedha hizi atazitoa wapi au zilipwe kupitia kanuni ya bei ya mafuta? Iweje Muungano wa Makampuni binafsi utendaji wao uwabebeshe mzigo Watanzania mbumbumbu? Una mapungufu katika hili *(regulations)* na katika Tanzania yenye mmomonyoko wa maadili na Ulimwengu wa wasaka faida, sintoshangaa kusikia *PIC* inashitakiwa, inashindwa kesi na walaji wanabebeshwa mzigo.

Dhamira ya Serikali ni nzuri, uamuzi wa Bunge ni sahihi, ila utekelezaji ulipuuza ushauri wa Kamati ya Nishati, Wabunge, na wale waliosema kwa nia njema.

Mheshimiwa Spika, nichangie sekta ya gesi ya asili. Awali ya yote tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa hatua tuliyofikia. Gesi nyingi imevumbuliwa, imekubalika bomba la Mtwara lijengwe, lijengwe na makandarasi wengi kuhakikisha shughuli (kupunguza muda wa ujenzi) lakini zaidi limilikiwe na Serikali. Natoa pongezi kwa hilo, kwani ilikuwa vita kali, mapambano ya upinzani wa waziwazi. Nayasema haya kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge, Serikali na wananchi kwa ujumla kwamba ulikuwepo upinzani wa hatari, hivyo tumeshinda pambano. Kwa kutambua hili, kutawafanya wale waliopewa dhamana watekeleze majukumu yao wakijua kuwa kunaweza kuwepo nguvu pinzani zinazoweza kufurahia kukwamua kwa mradi huu muhimu.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie haja ya maandalizi ya kudhibiti matumaini ya Watanzania juu ya neema hii. Pia nidokezee juu ya haja ya kutumia mapato ya gesi asilia kushamirisha shughuli za wananchi bila kuwaacha wakiwa tegemezi wa kupata kila kitu bure. Ni kutokana na maeneo haya Kamati ya Nishati ikapendekeza kuundwa kwa *ERA (Energy Regulatory Authority),* tuwe na timu ya watu sasa watakaoshinda na kulala wakiwaza juu ya nishati, neema ya gesi waioanishe na nishati zote, wabainishe neema na athari za nishati na vyanzo vyake na wajiandae leo kuidhibiti Sekta ya Nishati miaka 100 ijayo. Hoja hapa ni kuwa, nachelea shughuli za

kushitukiza au dharura ambao sasa unataka kuwa utamaduni wetu.

Mheshimiwa Spika, nihitimishe mchango wangu mdogo kwa kuzungumzia Sekta ya Madini. Naishauri Serikali ifuatilie kwa karibu na kutoa taarifa juu ya machimbo ya Kyerwa na Karagwe. Machimbo ya Tin-Kyerwa yalitekelezwa kwa misingi ya kiuchumi wakati huo. Sasa ziko habari kuwa watu toka nchi jirani wanasomba kifusi toka Kyerwa na kupeleka kwao. Ipo taarifa kuwa moja ya nchi jirani inao mtambo wa kusafisha madini hayo na sehemu kubwa ya malighafi inatoka kwetu.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ni kuwa Serikali ibebe jukumu la kubainisha manufaa ya rasilimali hii na kama kuna manufaa, tujenge kiwanda cha kusafisha katika Wilaya mpya ya Kyerwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, nimefarijika na hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa 82 kuhusu ufuaji na usambazaji wa umeme Mpanda. Unafadhiliwa na Uholanzi kiasi cha Megawati 2.5. Napenda kushauri, ni wakati muafaka sasa wakati huu wa maandalizi ya mradi huu ukaenda sambamba na kufikisha umeme huo Kakese Mbugani na maeneo ya jirani na ili idadi inayokusudiwa ifikiwe, ni lazima kujenga njia za kusafirisha umeme katika maeneo yote na viungo vya Mji wa Mpanda, kuanzia Ilembo, Kasimba, Nsemlwa, Kawajense, Shanwe na Misunkumilo.

Mheshimiwa Spika, nina matumaini makubwa mapendekezo haya yatazingatiwa.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako na kwa Mawaziri wenye dhamana juu ya Wizara hii. Awali ya yote, napenda kumshukuru sana Mungu kwa kunipa uhai na kuniwezesha kupata fursa ya kutoa mchango wangu mdogo sana katika Wizara hii hasa upande wa Nishati.

Mheshimiwa Spika, napenda sana kuitumia kauli hii; "kama unashindwa kuvumbua usishindwe kuiga."

Mheshimiwa Spika, wote tunajua nyumba ni mali na dhamana isiyohamishika na nyumba ndiyo inayofungiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, wenzetu Kenya walikuwa wanao mpango mzuri sana wa kuwakopesha wananchi wake huduma ya ufungaji wa umeme uliokuwa ukijulikana kwa jina la *Stima loan*.

Mheshimiwa Spika, mpango huu ulitoa mafanikio makubwa sana kwa kuwapa wananchi wengi nishati hii na malipo ya mkopo wa kufungiwa umeme ulilipwa katika bili za mwezi kwa watumiaji na mikopo hiyo imelipwa vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, nimeona niliseme hili makusudi kwa kuwa watu wetu wengi Mijini na Vijijini ambapo huduma ya umeme imefika, wanapata shida kubwa

sana kwa kuwa fedha yote wameitumia katika ujenzi wa nyumba zao.

Mheshimiwa Spika, kama Wizara kupitia Shirika lake la Umeme *(TANESCO)* likizingatia haya na kushirikiana na wataalamu wake walipo, basi wananchi wetu watapata nishati hii na itatusaidia sana kutunza mazingira yetu hasa kati matumizi ya kuni na mkaa.

Mheshimiwa Spika, bado matumizi ya mita za Luku yanahitajika sana hasa katika Miji ya Musoma na kwingineko.

Mheshimiwa Spika, katika Mji wangu wa Musoma, kuna shida kubwa sana la *Meter* za kusomea matumizi ya umeme na pendekezo la wakazi wengi wa Mji wetu ni kufungiwa mita za Luku ili kuepukana na foleni kubwa inayokuwepo kwa sasa katika ulipaji wa bili za mwezi ambao umeonesha usumbufu mkubwa na hasa bili za makadirio tofauti na *Unit* halisi inayotumika kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuunganishwa kwa gridi ya Taifa, Mji wa Musoma ulikuwa na *generator* ya kufua umeme ambayo tulikuwa tunatumia na nina uhakika Mheshimiwa Waziri anajua vizuri ma-*jenerator* haya yaliyokuwa yapo maeneo ya Nyakato Musoma Mjini. Tungependa wakati wa majumuisho, basi Mheshimiwa Waziri atusaidie kujua ma-*generator* hayo yako wapi kwa sasa na yanafanya nini?

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, napenda tu kuwatia moyo Waziri na Manaibu wake, pia Katibu Mkuu wa Wizara, kama mipango yao itatekelezeka kwa kasi na kiasi kikubwa, basi kuna badiliko kubwa sana kwa maisha na uchumi wa nchi, pia mwananchi mmoja mmoja na hiyo ndiyo dira ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nawatakia mafanikio mema katika utekelezaji wa bajeti hii.

**MHE. KASSIM K. MAJALIWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kuishukuru Wizara na Shirika la *TANESCO* kwa kukubali kuendelea na kazi ya kuboresha huduma ya umeme Wilaya ya Ruangwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mpango wa Wizara na Serikali ni kutoa huduma ya umeme hadi vijijini, Ruangwa bado inapata huduma isiyo ya uhakika ya umeme kwa sababu mbalimbali ikiwemo njia mbovu ya mzunguko kutoka Mtwara, Tandahimba, Newala, Masasi, Nachingwea hadi Ruangwa.

Mheshimiwa Spika, nimefanya mawasiliano na Katibu Mkuu kuomba ujenzi wa njia mpya fupi na ya uhakika kwa kuunganisha Nyanganga hadi Nkowe (Ruangwa), njia inayotoa umeme wa uhakika ili Ruangwa, pia Wilaya ya Nachingwea ipate umeme wa uhakika utokao Lindi.

Mheshimiwa Spika, njia hiyo mpya itawezesha vijiji vikubwa saba kupata huduma ya umeme (Nanganga ya Ruangwa, Malolo, Michenga, Chimbila A, Chimbila B, Nandagala, Namahema). Hatua ya awali iliyofikiwa naomba iongezwe uwezo ili *TANESCO* na Lindi ianze kazi ya ujenzi wa njia hiyo. Naomba pia kupatiwa umeme katika vijiji vikubwa vilivyo kwenye njia ya Mbekenyera, Namichiga hadi Mandawa ambako wataalam wa *TANESCO* walishafika kwa hatua ya awali.

Mheshimiwa Spika, kwa mpango huu nawashauri kuwa mpango wa kufikisha umeme Wilaya ya Liwale mfanye maunganisho Wilayani Ruangwa kwa sababu za kupunguza gharama.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, umeme ni nyenzo muhimu katika maendeleo ya jamii yoyote ile hususan vijijini. Ni jambo la kusikitisha kuona baada ya miaka 50 ya Uhuru ni asilimia 14.5 tu ndio wanatumia umeme. Kwa kweli hatua hii hairidhishi, naamini Serikali itafanya juhudi kubwa ili kufikia mwaka 2015 angalau 30% ya Watanzania wapate umeme. Usambazaji wa umeme hapa nchini umekuwa ukichukua muda mrefu kutokana na sababu nyingi ikiwemo gharama kubwa za kuweka umeme, ughali wa nguzo, lakini kubwa zaidi ni ubinafsi uliopo ambapo wananchi husubiria wengine waweke nguzo ili wapate urahisi. Ni rai yangu basi mtu anapoweka nguzo, wale watakaoweka umeme baadaye kwa kupitia nguzo ile wamlipe yule wa awali. Hata hivyo, bado tunaitaka

Serikali ipunguze bei ya nguzo kutoka Sh. 900,000/= hadi Sh. 500,000/= ili wananchi waweze kuweka umeme au nguzo ziwe bure na mwananchi alipie tu *service line.*

Mheshimiwa Spika, Watanzania wote wamefurahishwa sana na upatikanaji wa *gas* asilia kule Lindi na Mtwara. Habari hii njema siyo tu itakuza pato la Taifa, lakini pia itapunguza kwa kiasi kikubwa ukataji hovyo wa mti kwa ajili ya mkaa. Ni rai yangu kuwa Serikali itapunguza sana bei ya gesi hii ili wananchi wengi waweze kutumia gesi hii asili.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imebarikiwa kupata madini ya aina nyingi pamoja na vito vya thamani kubwa ikiwemo *Tanzanite*, Almasi na nyingine nyingi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na madini na vito hivyo vyote, bado vinaliingizia pato la Taifa kwa chini ya 4%. Tunajiuliza, nini sababu ya pato hili dogo? Tatizo ni nini? Nini sasa kifanyike ili Taifa liweze kupata pato zaidi? Kumekuwa na malalamiko mengi kuhusu mchanga na udongo ulio na madini kupelekwa nje ya nchi kwa ajili ya kufanyiwa tafiti. Je, ni lini Serikali itakuwa na vifaa vya kisasa kuchunguza madini na vito hapa hapa nchini ili kuwaondoa wananchi wasiwasi wa kuchakachuliwa au kuibwa kwa rasilimali zake?

**MHE. AMOS G. MAKALLA:** Mheshimiwa Spika, nianze kuwapongeza na kuwashukuru Waziri na Manaibu wake wawili kwa kupokea maombi yangu ya kupeleka umeme katika vijiji vya Kidudwe, Kunke, Lusanga, Ng’ambo, Kipala, Makumu, Mbuyeni, Melela,

Kibati na Poma. Naishukuru Serikali kwa kupokea maombi yangu niliyoyatoa Bungeni katika bajeti ya mwaka 2011/2012 na aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini - Mheshimiwa William Ngeleja, alinijibu amepokea maombi yangu na Serikali itatekeleza.

Mheshimiwa Spika, nashukuru uongozi mpya chini ya Waziri wa Nishati na Madini Prof. Sospeter Muhongo kwa kunijibu na sasa nafurahi Vijiji na Kata hizo zipo katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2012/2013. Naomba tu utekelezaji sasa wa upelekaji umeme maeneo hayo ili kuchochea ukuaji wa uchumi na huduma za jamii.

Mheshimiwa Spika, naomba pia Wizara itembelee machimbo ya dhahabu Matale kuwasaidia wachimbaji wadogo wametumia zana duni, wasaidiwe pia mitaji kwa ajili ya kununua zana za kisasa. Aidha, Serikal itabakiza eneo la madini Melela, Kata ya Melela ili kutoa ushauri na maelekezo kwa wananchi wakazi, na athari ya hifadhi ya madini na mipaka yake ili maeneo yasiyo na madini wananchi wapewe kwa ajili ya kilimo na fidia kwa walioathirika na utafiti wa madini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza sana Serikali kwa nia yake ya dhati na jitihada ilizozifanya kuhakikisha wananchi wanapata umeme. Binafsi na kipekee nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake kwa jitihada na

uwezo mkubwa waliioonesha wa kumudu majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi hii nikumbushie tu ahadi ya umeme katika Vijiji vya Maluga, Ng'anguli, Makunda, Kitusha, Kitukutu, Kizaga, Simbalungwala, Mkulu, Motomoto, Zinziligi, Kibaya, Songambele, Kibigiri, Kizonzo, Mseko, Malendi, Mgongo, New Kiomboi, Meli na Kisiri.

Mheshimiwa Spika, pia naomba ombi maalum kwa Waziri na Serikali kukiangalia Kijiji cha Kaseria kupata umeme kwa kupitia mpango ulioanza kupeleka umeme Sepuka, kwani vijiji hivyo vinapakana. Hiyo itakuwa imesaidia sana hata kufikisha umeme hadi Kata ya Mbelekese.

Mheshimiwa Spika, aidha, niombe Serikali kuwasilisha mswada wa maswala ya gesi ili nchi iingie kwenye biashara ya gesi ikiwa na sheria ya gesi. Hii ni jambo muhimu sana kwa nchi yetu kwa wakati huu.

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba Serikali iangalie upya Sheria ya Uchimbaji ili kusaidia wachimbaji wadogo wadogo kupewa leseni ili kuondoa migogoro migodini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia na kutoa ushauri wangu katika hoja hii ya Nishati na Madini. Kwanza kabisa, napenda kukumbusha ahadi nyingi ambazo zimeahidiwa kuhusu

kupeleka umeme Jimboni Nyang'hwale, imekuwa kama hadithi tu! Ahadi hizo tangu mwaka 1998 hadi 2012 hakuna utekelezaji hadi leo, pamoja na walioahidi ni viongozi wa ngazi za juu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1998 Mzee Malecela aliahidi, mwaka 1999 Naibu Waziri – Mheshimiwa Malima aliahidi, mwaka 2005 Mzee Malecela aliahidi, mwaka 2009 Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete aliahidi, tarehe 6 Julai, 2012 Naibu Waziri – Mheshimiwa Stephen Julius Masele aliahidi mbele ya wananchi katika Mkutano wa hadhara pale Kharumwa ambapo ni Makao Makuu ya Wilaya mpya ya Nyang'hwale. Pia Waziri alishuhudia nguzo ambazo zimetupwa njiani kama maonyesho zaidi ya miezi minane. Ni lini sasa umeme utawaka Jimboni Nyang'hwale?

Mheshimiwa Spika, pili naomba kuchangia pia kuhusu uchimbaji wa dhahabu unaofanywa na *Blang'uru Gold Mine*, uchimbaji huo ambao unafanyika katika eneo la Jimbo la Nyang'hware katika vijiji vya Iyenze, Mwasabuka, Nyamikonze na *STAMICO*. Ni ukweli usio na shaka kabisa kwamba kuna madhara makubwa ambayo yamejitokeza hivi karibuni baada ya milipuko ya miamba inayofanywa na mgodi huo hivi karibuni, baadhi ya nyumba na majengo ya Shule ya Msingi ya Iyenze zimepasuka vibaya na ardhi pia imepasuka na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini tarehe 6 Julai, 2012 katika ziara yake amethibitisha kwa kuona kwa macho yake.

Pia tarehe 6 Julai, 2012 Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini ameweka jiwe la msingi la shule

mpya kabisa lenye madarasa manne na ofisi mbili na nyumba moja yenye familia mbili za walimu hapo kijiji cha Mwasabuka. Kijiji cha Iyenze jiwe la msingi jengo la Zahanati Iyenze, majengo yote yamefikia kufungwa lenta, tarehe 24/07/2012 saa 12.00 asubuhi mlipuko mkubwa ulitokea na majengo yote yamepata nyufa nyingi sana na ardhi kupasuka. Je, hasara hiyo na hatari hiyo Serikali na mgodi huo unachukua hatua gani kufidia hasara hiyo na kuepusha madhara makubwa ambayo yanaweza kuangamiza wananchi wa maeneo hayo? Naomba kauli ya Serikali kwa hili.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Waziri na Manaibu Waziri kwanza kwa kuteuliwa kuongoza Wizara nyeti kwa uchumi wa nchi yetu. Lakini pili, kwa kushirikiana na Katibu Mkuu - Ndugu Maswi kuandaa bajeti ya Wizara yao na kuiwasilisha vyema hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru Wizara pia kwa kusimamia vizuri mradi wetu wa umeme wa *generator* Wilaya ya Namtumbo na sasa upo katika hatua inayoridhisha, ila tu nakumbusha tena mradi ule ulikuwa uwe wa Megawati moja, lakini *generator* inayoletwa ni ya Megawati 0.4. Mimi nina wasiwasi kwa kuwa Wilaya ya Namtumbo ndiyo inayozalisha mahindi, alizeti, ufuta na mpunga kwa wingi na wananchi wake wamehamasika kununua na kujenga viwanda vya kusindika mazao yao ili waweze kuongeza thamani yake na kuuza kwa bei itakayoweza kukuza uchumi wao. Hivyo, kwa umeme wa Megawati 0.4 utakuja kusumbua kwakuwa utakuwa mdogo kusumbua kwa kuwa utakuwa

mdogo. Ndiyo katika mawasiliano mbalimbali niliyofanya ya mdomo nimekuwa nikijibiwa na mradi ule ni wa muda, unakuja mradi wa kuunganishwa katika umeme wa *grid* ya Taifa lakini mradi ule wa sasa wa *generator* ulikuwa wa Megawati moja, hata katika hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini ya bajeti zilizopita alizungumzia, akasema Serikali imetenga fedha za kuweka umeme wa *generator* katika Wilaya za Namtumbo, Sumbawanga, Ngorongoro na alielezea Megawati zitakazopatikana Namtumbo, Megawati moja.

Tunaomba Serikali katika bajeti ijayo mtutengee Megawati 0.6 *generator* ili tuwe na umeme wa uhakika utakaoongeza pato la uzalishaji wa wananchi wa Namtumbo wakati tunasubiri kuunganishwa katika umeme wa *grid*.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Viongozi Wakuu wa Wizara kwa kuokoa hela za Taifa katika manunuzi ya mafuta ya kuendeshea vinu vya kuzalisha umeme kwa mafuta. Nawaunga mkono kwa hatua nzuri mliyochukua.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imegundulika kuwa na madini mengi na yatakayoweza kuubadilisha uchumi wa nchi yetu kwa haraka. Hivyo, ushauri wangu kwa Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini na Wizara zinazohusika moja kwa moja na kuendeleza rasilimali watu ambao watakuja kusaidia kusimamia miradi hiyo sisi wenyewe Watanzania. Naomba kufahamu, Wizara imejiandaaje kuona fursa hii tuliyonayo, tuna wataalam wangapi vijana

watakaokuja kusimamia uzalishaji wa gesi na mtandao wake unaotarajiwa kuwa mkubwa na kuwa unafanya kazi kubwa? Naamini siyo tu kwa kuzalisha umeme katika vituo vya kuzalisha, bali pia utasambaza katika vituo vya gesi kwa ajili ya magari na pia kwa matumizi ya nyumbani. Je, mpaka sasa tunao wataalam wangapi? Je, tuna mpango gani wa kuwapeleka vijana wetu nje kwenye nchi zenye vyuo vyenye uzoefu wa kufundisha wataalam wa gesi kwa kusimamia uzalishaji na usambazaji wake ili wapate elimu hiyo kwa haraka waje kutusaidia ili tusiwe watazamaji tu wa utaalam huo?

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ishirikiane kwa karibu na sekta husika na uzalishaji wake kukamilika mchakato wa uanzishaji wa uzalishaji wa urani tulionao nchini ili tuweze kuongeza pato la Taifa. Lakini pia ni ushauri wangu kwamba ni vyema kupata pia wataalam wetu wenyewe wa kusimamia uzalishaji wake na usafirishaji na uhifadhi wake. Ni jambo la muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara itazame, tunao wataalam wangapi katika eneo hilo na *potential technical man and women* ambao tunaweza kuwaendeleza na kuja kufanya kazi hizo?

Mheshimiwa Spika, naomba sekta husika zishirikiane kwa haraka kuona jinsi ya kutekeleza kwa pamoja kupata wataalam wengi zaidi watakaokuja kukabiliana na fursa tuliyopata ya madini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini ni Wizara nyeti sana kwa uchumi wa nchi yetu. Umeme ni chanzo kikuu cha nishati kwa ajili ya kuendesha mitambo mbalimbali kwa ajili ya viwanda na kutoa huduma mbalimbali kwenye taasisi za umma. Aidha, nishati ya umeme imetoa ajira kwa Watanzania wengi.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kupongeza juhudi za Waziri wa Nishati na Madini pamoja na Wasaidizi wake, lakini bado juhudi kubwa zaidi zinahitajika katika kupelekea umeme vijijini ambako ndiko Watanzania wengi waliko. Umeme ukipelekwa vijijini utapunguza wimbi la vijana kukimbilia Mijini kwa sababu watakuwa na uwezo wa kubuni ajira mbalimbali ambazo pia zitakuza uchumi wa Taifa kwa kufanya rasilimali watu kutumika vizuri.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mbarali ni miongoni mwa Wilaya zenye vijiji vingi ambavyo havina umeme. Nimekuwa nikiomba mara nyingi ili Mbarali nayo iingizwe kwenye mpango wa *REA* bila mafanikio. Nataka kujua ni lini mpango huu utaingizwa Wilaya ya Mbarali ili vijiji vya Ilongo, Igalako, Sonyanga, Uturo, Ukwavila, Utengule ambavyo vimepitiwa na umeme unaopita kwenda Mbeya Mjini na wao wapate nishati hiyo muhimu. Kama hiyo haitoshi, zipo Kata za Madibira, Mheshimiwa Rais alipotembelea alitoa ahadi ya kupeleka umeme kutokana na shughuli kubwa ya kilimo cha umwagiliaji na kuwa na mitambo ambayo haifanyi kazi kwa kukosa umeme. Aidha, zipo Kata za Ruiwa, Utengule, Luhanga, Igava, Ipwani, Mawindi na

Mwatenga hazina umeme pamoja na kuwa na huduma mbalimbali za jamii.

Mheshimiwa Spika, naleta ombi maalum kwamba, Gereza la Mbarali halina umeme, askari wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu nyakati za usiku. Umeme haupo mbali sana na mahali unapoweza kuunganishwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio mengi katika Wizara hii, naomba juhudi kubwa zielekezwe kwenye umeme wa gesi, nishati ya jua na makaa ya mawe. Kwani umeme wa kutegemea maji umeathiriwa sana na hali ya hewa. Mfano, kumekuwa na malalamiko sana kuwa kilimo cha umwagiliaji hasa Mbarali kinaathiri maji kwenda bwawa la umeme la Mtela, lakini ukweli unabaki pale pale kuwa ni uhaba wa mvua kutokana na mabadiliko ya tabianchi. Kwani hata wakulima wa Mbarali baadhi ya maeneo mazao yao yamekuwa yakikauka kwa kukosa maji. Isitoshe jinsi maji yanavyotumika, ipo mikondo mbalimbali inayorudisha maji Mto Ruaha. Kipindi cha mvua nyingi maji huwa mengi na kipindi cha Mvua chache maji huwa machache.

Mheshimiwa Spika, aidha, changamoto huwa hazikosekani. Upo ufisadi ambao umekuwa ukiitafuna Wizara hiyo kutokana na kuwa na baadhi ya viongozi (watendaji kutokuwa na uadilifu) pambana nao, tupo pamoja hatukubali mpaka wote wenye tabia hiyo wamalizike. Katika ufisadi huo, lipo tatizo la gharama za uunganishaji umeme na bei ya nguzo za umeme ambazo zinaandaliwa hapa hapa nchini, lakini bei ni

kubwa mno, heri ukanunue nje ya nchi. Nalo hili liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, mikataba ya madini iliyowekwa kifisadi ndiyo inayofanya Taifa kuingia hasara. Ingelifaa kutazamwa upya ikiwa ni pamoja na kuona mikataba ya nchi nyingine inayowekwa kwa manufaa ya Taifa.

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika, napongeza juhudi kubwa na maarifa vinavyofanywa na uongozi wa juu wa Wizara ukiongozwa na Waziri mwenyewe, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Makamishina na kadhalika. Kasi mliyoanza nayo Waheshimiwa Mawaziri, Katibu Mkuu, mwendelee nayo. Nina imani Watanzania walio wengi na Waheshimiwa Wabunge wanaunga mkono. Kanyaga moto twende.

Mheshimiwa Spika, mimi ni muumini mkubwa wa gesi. Naamini gesi ndiyo itakayomkomboa Mtanzania ndani ya muda mfupi. Sekta hii itachangia kwa kiasi kikubwa, kwa haraka na kwa uhakika katika maeneo yafuatayo kuwa na umeme wa uhakika usikokatikakatika, wa bei nafuu, itatuingizia fedha za kigeni, kwani tutauza nje gesi na hivyo kuimarisha Shilingi ya Tanzania, itachangia kuongeza ajira, itahamashisha uanzishwaji wa viwanda *(vya plastic)* na hasa mbolea, itachochea utumiaji wa mbolea ya bei ya chini kwa wingi ambayo itachangia kuongeza tija katika Sekta ya Kilimo na hivyo kuchangia kupunguza umasikini, fedha (mapato) zitakazopatikana kutokana na gesi zitaweza kuwekezwa katika maeneo na sekta

mbalimbali nchini kama vile afya, elimu, maji, kilimo, viwanda na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iwe makini sana katika kuchukua hatua ili kuhakiksha kuwa hatufanyi makosa kama ilivyotokea kwenye sekta yetu ya madini. Ni lazima tuhakikishe sera yetu ya madini inakuwa nzuri, sheria nzuri na kanuni safi. Tusipofanya hivyo, vizazi vijavyo vitatulaumu sana na Mungu atatulaani.

Mheshimiwa Spika, nawatakia kila la kheri. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. JOSEPHINE GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri Mheshimiwa Prof. Sospeter M. Muhongo kwa hotuba yake nzuri. Nawapongeza Manaibu Waziri, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Stephen J. Masele pamoja na Katibu Mkuu wa Watendaji wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, umeme uliopo Kasulu na Kibondo ni mwingi sana kuliko matumizi. Hivyo, naomba wananchi wote ambao wameshalipia ili kuweza kusambaziwa nyaya kusudi wapatiwe umeme. Meneja wa *TANESCO* Kasulu hatendi haki hata kidogo kwa sababu aliwalipisha wananchi pesa Sh. 200,000/= badala ya Sh. 69,000/= na kuwapatia risiti za Sh. 69,000/= kwa kudai kuwa Sh. 200,000/= ni kwa ajili ya kulipia nguzo. Baadhi ya wananchi wakatii na kutoa pesa hizo. Cha kusikitisha, pamoja na kulipia gharama hizo, hawapatiwi umeme.

Mheshimiwa Spika, naomba wananchi hao waliokwishalipia wapewe umeme badala ya visingizio vilivyopo sasa, kuwa hakuna nguzo wala nyaya. Je, kama hakuna nguzo wala nyaya, kwanini Meneja aliwatapeli wananchi kwa kuchukua pesa zao?

Mheshimiwa Spika, naomba wachimbaji wadogo wadogo wawezeshwe ili waweze kupatiwa mitaji, vifaa vya uchimbaji, na soko. Vijana wengi hawana ajira, hivyo wakiwezeshwa kupewa fursa wataweza kujiajiri wao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba meneja wa *TANESCO* Kasulu ahamishwe.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, naomba kuunga mkono kwa asilimia mia moja.

**MHE. DKT. SEIF S. RASHID:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza niwasilishe pongezi nyingi za dhati kwa Serikali katika juhudi zake za kuongeza kiwango cha uzalishaji wa nishati na kuondoa uwezekano wa mgao wa umeme nchini.

Mheshimiwa Spika, niliomba Serikali kutoa kipaumbele kwa uzalishaji wa umeme wenye unafuu kwa mtumiaji ili wengi wetu tuweze kuitumia nishati hii kwa unafuu zaidi na kupanua wigo wa matumizi ya nishati hii.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha ombi rasmi na kukumbusha ombi langu nililowasilisha mwaka 2011 ili

umeme uliofika Wilaya ya Rufiji uwanufaishe watu wengi zaidi badala ya wengi wao hivi sasa kuwa ni watazamaji tu.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali kwanza kuvipatia umeme vijiji ambavyo vimepitiwa na umeme. Ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wetu kuvipatia umeme vijiji hivyo ikiwa ni pamoja na Kiwanga, Chimbi A, B, C, Utunge, Kitundu na Kindwitwi. Naomba kwenye vijiji ambavyo vimeshapata umeme, lakini umeme huo haujasambazwa na imewaacha watu wengi wakiwa watazamji na hivyo kusababisha malalamiko tena hata katika sekondari zetu pale Muhoro na Utete hawajapatiwa umeme. Naiomba Serikali kuwapatia umeme watu wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, niliomba umeme ambao upo tayari katika Mji wa Ikwiriri usambazwe angalau kwa awamu kuelekea Mloka na hivyo kutoa fursa kwa vijiji zaidi ya 14 kunufaika na mradi huo, ambao mwaka 2011 nilijibiwa hapa Bungeni kwa mradi huo unahitaji fedha nyingi kwa sababu ya umbali wake. Kwa vile vijiji zaidi ya 14 vipo ndani ya hizo kilometa 100, wastani wa umbali wa kilometa tano kutoka kijiji kimoja hadi kingine. Mradi huu utaongeza uwezekano wa kuwekeza viwanda vya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo na kukuza utalii wa pori la *Selous* na kuchochea maendeleo ya dhati katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kusambaza umeme kutokea Kijiji cha Nyamwage kuelekea Mbwara ambako pia kuna Sekondari na Kijiji cha jirani

yake cha Nambonji ambapo Kituo cha Afya kinajengwa hapo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupta fursa ya kuchangia kwa maandishi na kwa muhtasari, naiomba Serikali katika mambo haya matatu, kuwashushia umeme vijiji ambavyo umeme umepita kwao katika Wilaya ya Rufiji Kiwanga, Chumbi, Utunhe, Kitondo, Kindwitwi, katika vijiji ambavyo vimepatiwa umeme usambazwe katika vijiji hivyo ili watu wengi wanufaike na umeme huo, kusambaza umeme kutokea Ikwiriri kupitia vijiji 15 hadi kijiji cha Mloka kwa awamu na kutokea Nyamurage hadi Nambunjo kupitia Mbwara.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na naunga mkono hoja.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Prof. Sospeter Muhongo na Waziri wa Nishati na Madini kwa hotuba yake nzuri na yenye uchambuzi wa kina kuhusu maendeleo ya Nishati na Madini katika nchi yetu. Napongeza sana jitihada ambazo Waziri na Naibu Mawaziri wake wameonyesha katika kipindi cha muda mfupi waliokaa katika Wizara hii. Nawapongeza pia Manaibu Mawaziri wote wawili, Mheshimiwa George Simbachawene na Stephen Masele kwa kazi ya hali ya juu ambayo wanaifanya katika Wizara na hivyo kuinua kiwango cha ufanisi. Pongezi sana.

Mheshimiwa Spika, nampongeza kwa namna ya kipekee Katibu Mkuu wa Wizara hii, Ndugu Eliachim Maswi kwa jitihada zake za hali ya juu ambazo zimeleta ufanisi mkubwa na wa hali ya kutoa matumaini kwa Watanzania. Aidha, nampongeza Dkt. Mwakiyesia - Mkurugenzi wa *REA* kwa utumishi wake wa kutukuka katika *REA*. Baada ya pongezi hizi, naomba kutamka kwamba ninaunga hoja hii mkono.

Mheshimiwa Spika, naomba kukumbushia barua yangu nilivyomwandikia Mheshimiwa Waziri kuhusu miradi ya kusambaza umeme Wilayani Siha ambayo imechukua muda mrefu bila kukamilika. Miradi hii ni ile ya *West Kilimanjaro* katika Kata ya Ngare-Nairobi na Ndumeti Kata ya Livishi, Kijiji cha Nshere-hehe na Mowo Njamu katika eneo la Kyaboo na Kijiji cha Mese, Kata ya Nasai eneo la Omarinyi lililopo Kijiji cha Kowoko Kaskazini na eneo la Kikwe lililopo Kijiji cha Koboko Kusini na vijiji vya Kishisha na Mae bado vina nguzo zimelala chini na wananchi wamekuwa wanasubiri kwa miaka mingi bila mafanikio.

Mheshimiwa Spika, naomba sana, miradi hii ikamilishwe, kwani gharama kubwa imekwishatumika kuianzisha kwa kupika maeneo husika na kusimamisha nguzo katika baadhi ya maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nakumbushia eneo la Lawate kuelekea Kijiji cha Ngumbaru ambapo ndipo stesheni ya kusambaza umeme ilipo katika kuhitimisha rai yangu. Naomba kushauri *REA* iongezewe kiasi cha fedha kinachopelekwa katika wakala hii, kwani kama

nilivyoeleza, wameonyesha jitihada za hali ya juu katika usambazaji wa umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. EDWARD N. LOWASSA:** Mheshimiwa Spika, napongeza hotuba nzuri uamuzi wa kushusha gharama za kuunganishwa umeme ni mzuri sana. Napongeza.

Mheshimiwa Spika, harakisheni suala la sera na Sheria ya Gesi yake kusema kwa uhakika sera hiyo na sheria hiyo italetwa lini Bungeni? Bila sera na Sheria ya Gesi itakuwa hatuwatendei haki Watanzania.

Mheshimiwa Spika, katika kuandaa sera, uangaliwe uwezekano wa kuunganisha uchumi na fedha zitakazotokana na gesi kusaidia ajira kwa vijana kwa kuwekeza katika kilimo na maeneo yatakayotoa ajira kwa vijana. Tuangalie sana ili upatikanaji wa gesi usiwe *a curse,* bali *a blessing.*

Mheshimiwa Spika, mwisho, kamilisheni usambazaji wa umeme Mto wa Mbu.

**MHE. RITA L. MLAKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara kwa hotuba nzuri sana ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia eneo la madini. Nimesikitishwa kuona nchi yetu inachimba madini ya thamani ya Dola za Marekani bilioni 2.2 na sisi kama nchi tunapewa Dola milioni 62 tu. Nashauri Serikali tupitishe sheria ya kutuwezesha kununua hisa

katika migodi hiyo ili angalau nchi yetu iweze kunufaika na madini hayo.

Pia ningeshauri *STAMICO* iwe na sheria nyingi zaidi katika migodi ya Buhemba na Backreef, wabia wawe na *minority shares.*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. LUCY P. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kulieleza Bunge lako Tukufu, utafiti umefanyika kuhusu uchimbaji wa madini ya urani kwamba hautaathiri mazingira: Je, utafiti umefanyika kuona ni kwa kiasi gani afya za wanadamu na wanyama wataathirika kwa uchimbaji wa madini hayo? Je, kuna uharaka gani wa kuchimba madini haya wakati haya yaliyopo bado hatujaweza kwa kiasi kikubwa kuhakikisha wananchi wanafaidika nayo?

Mheshimiwa Spika, umeme wetu umekuwa ukitegemea maji, lakini kwa sasa hivi pamekuwepo na ukame sana kupelekea ukosefu wa mvua, hivyo kuathiri mitambo inayotumia maji kama Mtua na kadhalika na mwaka huu mvua hazikunyesha za kutosha, hivyo kuna kila dalili lazima kutakuwepo na mgao mkubwa wa umeme siku za karibuni. Je, kwa mpango wa muda mfupi, sababu siyo jambo la kushtukiza, *TANESCO* imejipanga vipi kuhakikisha watu wanapata umeme? Palikuwepo na ma-*genetor* karibia

kila Mkoa: Je, ni ma-*generator* mangapi yanafanya kazi katika kila Mkoa, ili yasaidie katika tatizo la umeme?

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa tumekuwa tukitumia umeme wa dharura kwa kutumia mitambo ya kukodi ambayo ina gharama kubwa na Serikali inapata hasara kubwa ya kulipa *capacity charges* na hii inapelekea bei kubwa sana kwa mtumiaji (mwananchi) kwa kulipa bei kubwa. Ni lini tutamaliza hii *system* ya kutumia umeme wa dharura? Je, miaka yote hii, itachukuwa muda gani kujifunza? Mchakato wa kutumia umeme wa makaa ya mawe na gesi asilia umefikia wapi? Kwa sababu kwa sasa huu umekuwa ni wimbo katika kila hotuba ya bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya gesi kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, naipongeza Serikali kwa hili kwa sababu kwa kiasi kikubwa tutaokoa mazingira yetu. Lakini naomba kutoa tahadhari kwamba Serikali itoe elimu kwa watumiaji kuhusu kulipuka na pia pawepo na maandalizi ya kutosha. Kwa mfano, kila nyumba lazima iwe na *fire extinguisher* na Serikali lazima iwe na magari ya kutosha ya zimamoto pindi panapotokea moto, yaweze kwenda sehemu tofauti.

Mheshimiwa Spika, pamoja na EWURA kusimamia na kuthibiti mafuta ya *petrol* yasiyo na ubora hayauzwi katika vituo vyetu, licha ya Serikali kuagiza mafuta kwa pamoja *(bull procurement system) bado* bei ni ghali licha ya kupandisha bei ya mafuta ya taa, bado mafuta yanachakachuliwa. Je, Serikali inaweza kutoa

maelezo licha ya *EWURA* kufanya ukaguzi na licha ya mafuta ya taa kupanda bei, bado uchakachuaji upo? Sababu ni nini? Kulikuwa hakuna haja ya kupandisha mafuta ya taa bei na kuwatesa wananchi wenye kipato cha chini na kushindwa kununua mafuta na badala yake wanaendelea kukata miti kwa ajili ya matumizi ya kuni za kupikia na mkaa na kupelekea kuharibu mazingira.

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULLA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kupata nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu wa maandishi katika hotuba hii iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Manaibu Waziri wake lakini pia naomba kuwapongeza watendaji wote wa Wizara hii ya Nishati na Madini kwa kuandaa vizuri kabisa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa, naomba nimpongeze sana kaka yangu mpendwa Katibu Mkuu wa Wizara hii, Ndugu Maswi kwa kazi nzuri kabisa anazozifanya pale Wizarani.

Mheshimiwa Spika, Katibu Mkuu ni mfano wa kuigwa kabisa na Watanzania wote. Uzalendo wake, usafi wake na uchapakazi wake, vinafaa kabisa kusifiwa. Anafanya kazi nzuri sana. Mimi naomba sana Waheshimiwa Wabunge wote tumpongeze kwa hilo na siyo kumkatisha tamaa kama wanavyofanya watu wengine.

Mheshimiwa Spika, mimi namtaka Mheshimiwa Maswi pamoja na Waziri na Manaibu Waziri wasonge mbele, kazi ni nzuri, endeleeni kufukuza watu wasiokuwa na uzalendo na nchi yetu, hata mkifukuza wote, tutaajiri watumishi wengine wapya. Vijana wengi wapo, hawana kazi, wamemaliza Chuo Kikuu, watafanya kazi. Napongeza sana kazi yenu ni nzuri sana, songeni mbele.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu nauelekeza zaidi kwa wachimbaji wadogo wa madini.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iwawezeshe kupata mikopo ili waweze kupata vifaa vya kisasa vya uchimbaji ukilinganisha na vya sasa wanavyotumia. Aidha, pia Serikali iwape mafunzo na semina wachimbaji wadogo hawa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, naunga mkono hoja.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi bajeti hii ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri yenye matumaini, lakini pamoja na hayo, kuna mambo ambayo yanakera katika jamii yetu kutokana na mambo ambayo Wizara hii inayafanya.

Mheshimiwa Spika, mwananchi wa kawaida aliyeko huko kijijini, ambaye hata hati ya kimila hana, anakuwa kama mkimbizi kwenye eneo lake, mfano, yanapogundulika kuwa eneo hilo lina madini bila kumshirikisha mwenye eneo, kibali cha utafiti kinatoka moja kwa moja Wizarani. Hata mwenye eneo hana taarifa yoyote au leseni ya uchimbaji anapewa mwekezaji bila mwenye eneo kushirikishwa. Utaratibu huu ni mbovu na ni unyanyasaji mkubwa kwa wenye maeneo hayo.Uutakuta utafiti wenyewe unafanyika zaidi ya miaka 10, wanatafiti nini?

Mheshimiwa Spika, Serikali haiwatendei haki wananchi wetu na tunasababisha umasikini mkubwa kwa wananchi kulipwa gharama ambayo haifanani na mali inayotolewa katika eneo lake na inasababisha hata wananchi wakakosa sehemu ya kulima.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, kwa umuhimu mkubwa, Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu, naomba anijibu ule utafiti unaofanywa na Kampuni ya *Barrick* katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Jimbo la Solwa Kata ya Mwakitolyo utakwisha lini? Kwani mwaka 2011 watu hawa walisema wamekamilisha utafiti na baada ya muda mfupi wanaanza kazi rasmi, lakini toka mwaka 2011 mpaka leo hii hakuna kinachoendelea zaidi ya utafiti. Bado haitoshi, kuna Kampuni nyingine ya Kichina nayo ipo Halmashauri ya Shinyanga. Wizara mnasema wanafanya utafiti, ule siyo utafiti ni uchimbaji, kitu ambacho kinafanya wananchi hawa washindwe hata kulima.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, lakini naomba majibu ya huo utafiti unaoendelea Mwakitolyo zaidi ya miaka kumi sasa.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuunga mkono hoja ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara kwa kupitia *EWURA* wawe waangalifu sana katika kupunguza bei ya mafuta, kwani mpaka sasa ukweli wananchi bado hawaridhiki na bei za mafuta pamoja na kuanzisha mfumo wa ununuzi wa *Bulk* ambao tulitegemea kupata nafuu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria mama, sielewi kwa nini Makampuni yanalipa US $ 250,000 tu kwa Halmashauri zinazohusika badala ya kulipa *source levy* ya 0.03% kwa mujibu wa sheria. Naomba Waziri atakapojumuisha, atoe maelezo ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, katika suala la bei ya kuunganisha umeme, nampa hongera sana Mheshimiwa Waziri, kwani nina imani kubwa hata hapo baadaye mambo yakiwa mazuri, basi wananchi wa Tabora watapata nafuu sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Katibu Mkuu kununua mafuta bila ya kufuata Sheria ya Manunuzi, mimi nataka kumpongeza na kumhakikishia kwamba, Wabunge wenye uchungu na nchi yao watamuunga mkono hatua aliyochukua ya kuokoa Shilingi bilioni tatu. Anastahili tunzo *(honourable)* na Mungu amjalie.

Mheshimiwa Spika, tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri awe mwangalifu sana katika Mikataba ya Gesi ili Serikali iweze kufaidika na miradi hii.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba Mheshimiwa Waziri aangalie Jimbo langu la Tabora Mjini ambalo lina Kata 25; kati ya hizo, kuna Kata 11 za Mjini na Kata 14 ni za Vijijini. Kwa hiyo Kata hizi naomba na zenyewe zipatiwe umeme katika mpango wa Wakala wa *REA*. Nina imani na ofisi ya Waziri itatusaidia sana wakazi wa Tabora.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Wizara ya Nishati na Madini mia kwa mia. Ahsante.

**MHE. BRIG GEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2012/2013 kwa asilimia mia moja. Hotuba ya Waziri ni nzuri. Pamoja na changamoto nyingi zilizopo mbele yake, ninaamini kuwa matarajio yote yanatekelezeka. Hata hivyo, katika Jimbo la Mlalo umeme ulikwishafika katika Tarafa moja ya Mlalo. Umeme huo pia ulikuwa ufikishwe kwenye Tarafa ya Mtae na Umba ili kukamilisha mradi huo. Kushindwa kutekelezwa kwa mradi huo, imekuwa ni chanzo kikubwa cha malalamiko ya wananchi wa Jimbo hilo. Inashauriwa Mamlaka ya Umeme Vijijini *(REA)* ilishughulikie tatizo hili haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, ninawasilisha.

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE**. Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo, Waziri wa Nishati na Madini pamoja na Mheshimiwa George Simbachawene na Mheshimiwa Stephen Masele, Naibu Mawaziri kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara hii na kwa kazi nzuri waliyokwishaifanya tokea wakabidhiwe kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Bwana Eliakim Maswi, Katibu Mkuu na Makamishna na Wakurugenzi wa Idara mbalimbali Wizarani, Wenyeviti wa Bodi na Watendaji Wakuu wa taasisi zilizo chini ya Wizara pamoja na watumishi wote, kwa jitihada wanazofanya kutekeleza sera na sheria za sekta za nishati na madini ili kuongeza mchango wa sekta hizo kwenye uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu Sera ya Nishati. Upungufu wa umeme nchini umeathiri uchumi na maendeleo ya jamii kwa ujumla kwa sababu ya viwanda na shughuli nyingine zenye kuhitaji umeme kutofanya kazi kwa kiwango kilichopangwa. Nchi yetu imejaliwa kuwa na rasilimali ya madini ya urani ambayo ni chanzo muhimu katika uzalishaji wa nishati ya umeme. Kwa kutambua rasilimali hiyo tuliyo nayo, ni vizuri tukapanga kushirikiana na nchi zenye uzoefu katika ujenzi na usimamizi wa vinu vya kuzalisha umeme wa nuklia ili kuzalisha umeme wa kutosha nchi nzima na sehemu yote ya Afrika kusini mwa jangwa la Sahara.

Mheshimiwa Spika, pili, utekelezaji wa mipango ya umeme vijijini, mwaka juzi Wizara iliwajulisha wananchi wa Wilaya ya Arumeru Magharibi kuwa imetenga kiasi cha shilingi 7.5 bilioni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya umeme kwenye kata tano kati ya 21 za Wilaya hiyo. Tulifarijika sana baadhi ya miradi ilipoanza kutekelezwa ilitupa matumaini kuwa sasa mipango ya wananchi kuanzisha viwanda vidogo ili kutoa fursa za ajira, kuongeza thamani ya mazao yao pamoja na kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maji na mengineyo. Hata hivyo, inasikitisha kuona kuwa mkandarasi ambaye ni *TANESCO* wamekuwa wakitoa sababu mbalimbali za kuchelewa utekelezaji wa miradi hii. Naomba Wizara itujulishe kuwa ina mpango gani wa kutekeleza miradi hiyo na ni lini inatarajiwa kukamilika?

Mheshimiwa Spika, tatu, tarehe 26 April 2012, Naibu Waziri wa Nishati na Madini akifanya ziara kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Arusha (*Arusha District Council*) ambapo katika mikutano ya hadhara kwenye Kata mbalimbali aliahidi kuwa Serikali itaingiza kwenye Mpango wa kupatiwa umeme vijiji visivyokuwa na umeme kwenye Halmashauri hiyo. Aidha, alimwagiza Meneja wa Mkoa wa *TANESCO* kuwa wafanye upembuzi na kuwasilisha taarifa Wizarani ili shughuli hiyo ianze bila kuchelewa. Namwomba Mheshimiwa Waziri awajulishe wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha juu ya hatua iliyofikiwa katika kuwezesha vijiji vilivyo kwenye Wilaya hiyo kupata umeme. Kwa taarifa kwa Mheshimiwa Waziri kuwa Wilaya ya Arumeru inakabiliwa na tatizo la

muda mrefu la maji, moja ya sababu zinazokwaza uendeshaji wa vyanzo vya maji ni ukosefu wa umeme. Kwa niaba ya wananchi wa Wilaya yangu, naomba sana tusaidiwe kuondokana na adha hii.

Mheshimiwa Spika, nne, leseni za madini. Uzoefu umeonesha kuwa leseni za uchimbaji madini mbalimbali ikiwemo mchanga, *morum* na vito mbalimbali zimekuwa zikitolewa na Makamishna Wasaidizi wa Kanda bila kushirikisha wadau muhimu wakiwemo wamiliki wa ardhi yenye madini hayo. Iko mifano mingi kwenye Wilaya yangu ambapo uchimbaji umesababisha migogoro. Nashauri kuwa Wizara itoe mwongozo kwa Makamishna Wasaidizi wa Kanda ili kuhakikisha kuwa wananchi wanaomiliki ardhi yenye madini wanafaidika na rasilimali hizo kwa kuwa wabia au kulipwa fidia inayostahiki ikiwa wataridhia utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha na narudia kusema naunga mkono hoja kwa dhati.

**MHE. DKT. DAVID M. MALLOLE**. Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kidogo katika nishati inayotokana na umeme wa jua *(solar power*). Zipo aina nyingi za nishati kama vile umeme wa maji, gesi, mafuta na kadhalika. Aina zote za nishati ni ngumu sana kuziweka. Umeme wa maji unahitaji ujazo wa maji mengi kwenye mabwawa, gesi inahitaji gharama kubwa ya kutandika mabomba ya gharama kubwa yatakayokwenda maili nyingi, umeme wa mafuta pia ni gharama kubwa, umeme wa jua hauna gharama kubwa sana. Ni rahisi

sana kutumia umeme wa jua kwa ajili ya mwanga, pasi za umeme, *fridge, television* na majiko ya kupikia.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutumia kampuni za ndani na nje, watangaze tenda za kusambaza umeme wa jua nchi nzima, kwenye majumba, hospitali, shule na taasisi nyingine nyingi ili kuokoa mazingira ya ukataji misitu ovyo. Kampuni za umeme wa jua pia zisambaze majiko ya umeme wa jua kwa mwendo wa kasi sana nchi nzima. Kadiri muda unavyoendelea, Serikali pia itafikisha vyanzo vingine vya nishati nchi nzima, mfano nishati ya umeme wa maji, gesi, makaa ya mawe, mafuta na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kama tutaendelea kufikiria njia kubwa za nishati mathalani nishati ya umeme wa maji, gesi na mkaa, tutachelewea sana na nchi nzima itaathirika vibaya kwa kufyeka miti na kupanua jangwa la Sahara Afrika ya Mashariki na Kusini mwa Afrika kwa hasara yetu wenyewe na vizazi vijavyo. Tusambaze haraka nishati ya umeme wa jua, nishati nyingine zitafuata baadaye.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Spika, nachukuwa nafasi hii kuchangia kwa maandishi kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuteuliwa kwake kuwa Mbunge na Waziri wa Nishati na jinsi ambavyo ameanza kuonyesha uzalendo katika utendaji kazi

wake, akisaidiana na Ndugu Eliakim Maswi ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara, nawatakia kila la kheri, wazidi kuwa wabunifu kufichua uovu ambao umekuwa ukifanywa na viongozi na watumishi wasio na uzalendo na nchi yetu. Pia nawapongeza Manaibu Mawaziri wa Wizara hii ambao ni kiungo kikubwa katika kumsaidia Mheshimiwa Waziri na kuleta ufanisi mzuri wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya jitihada kubwa kufanya utafiti katika nchi yetu na kuweza kufanikisha kupata gesi katika Mkoa wa Mtwara huko *Mnazibay*. Jitihada hizi ni kubwa sana na ni mafanikio ambayo Watanzania hasa wananchi wa Mkoa wa Mtwara wana matumaini makubwa sana kwamba tatizo kubwa la umeme ambalo tulikuwa nalo sasa ufumbuzi umepatikana.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya uzinduzi wa ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi toka Mtwara na Dar es salaam. Hii ni hatua kubwa ya maendeleo. Rai ya Wanamtwara ni kwamba tupewe kipaumbele katika kusambaza umeme vijijini ili kuwaondolea wananchi adha kubwa ambayo inawakabili kwa miaka mingi sana. Hakutakuwa na faida kama gesi inatoka Mtwara kisha wananchi wanaendelea kuwa gizani. Gesi asili ni maendeleo, tunaomba Serikali ifanye jitihada za kuwekeza na kutafuta wawekezaji ambao watajenga viwanda Mkoani humo ili kuharakisha na kuchochea maendeleo na kutoa ajira kwa wananchi wa Mkoa wa Mtwara na Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mtwara, ni Mkoa ambao ulisimama kimaendeleo kwa miaka mingi,

upatikanaji wa gesi hii nina imani kubwa itaharakisha maendeleo katika sekta mbalimbali. Hivyo, naiomba Serikali na Wizara kwa ujumla katika zoezi la kusambaza umeme vijijini, iangalie maeneo ya taasisi kama vile zahanati, shule za msingi na shule za sekondari, misikiti na makanisa na maeneo yenye huduma za jamii kusaidia kupeleka nguzo bure ili kuwapunguzia gharama wananchi na kuwawezesha kuweka umeme katika taasisi hizo ili waweze kutoa huduma stahiki. Kwa mfano, shule zitawawezesha vijana wetu kusoma na kuzitumia maabara katika shule za sekondari lakini hata umeme katika zahanati, wananchi watapata huduma bora na chanjo na akina mama wajawazito kujifungua bila kulazimika kutoa mchango wa mafuta wakati wa kujifunga na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* ni shirika ambalo linategemewa sana na wananchi mijini na vijijini kupata huduma za umeme lakini wananchi wamekuwa wakikosa imani na huduma wanazotoa kwani wamekuwa wakitoa bili kubwa kwa wateja wao kuliko matumizi yanayotumika lakini pia wananchi wamekuwa wakipeleka maombi ya kuwekewa umeme vijijini kwa miaka mingi lakini hawapati huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, nina maombi yafuatayo kwa Serikali:-

(a) Wananchi ambao watawekewa umeme vijijini hasa Jimbo langu la Masasi wawekewe Luku kuepusha kupewa bili tofauti na matumzi yao;

(b) Vijiji ambavyo vilishapeleka maombi *TANESCO* wapewa kipaumbele katika kuwekewa umeme kama vijiji vya Nangose Temeke, Chikunja vilivyopo Wilaya ya Masasi; na

(c) Upelekaji wa nguzo za umeme katika taasisi vijijini, Serikali isaidie kwani hali ya wananchi vijijini ni duni.

Mheshimiwa Spika, natumaini maombi yangu yatapatiwa majibu yenye tija, kwa wananchi umeme ni uchumi, umeme ni maendeleo.

**MHE. RASHIDI ALI ABDALLAH**: Mheshimiwa Spika, kwanza sina budi kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha leo hii kuchangia kwa maandishi. Pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya Taifa lolote ulimwenguni yanahitaji kuwepo kwa umeme wa uhakika. Sasa ni vyema kabisa kujikita kwa nguvu zote za kitaifa kupambana na mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kupata umeme wa uhakika. Nchi nyingi sana zilizo makini wanaweka sera ya umeme *(power)* kuwa ni jambo la kwanza la Kitaifa. Nasema hivi kwa sababu bila ya kuwa na umeme wa uhakika, Serikali haiwezi kuleta mapinduzi ya viwanda na kwa maana hiyohiyo hatuwezi kuleta mapinduzi ya kilimo na hivyo uchumi wote wa Taifa utakuwa ni mdogo. Kwa maana hiyo, naiomba Wizara hii kuliona

hili na kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, pili, uchimbaji wa madini na mikataba. Madini ni utajiri mkubwa katika Taifa letu. Jambo la msingi ni kuanza kujikita na kujipanga upya kupitia Sheria za Leseni za Uchimbaji pia kupitia mikataba ya wachimbaji ili mikataba hiyo iwe kwa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, ndani ya Wizara hii, uko ufisadi mkubwa sana. Mheshimiwa Waziri ni vyema sana kupitia kila sekta ili kuhakikisha ufisadi uliopo ndani ya Wizara hii unakomeshwa kabisa.

Mheshimiwa Spika, tatu, gharama za umeme. Bado gharama za umeme kwa watumiaji ni kubwa mno, hailingani na pato la wastani la Watanzania. Sioni sababu ya maana kwa nini nchi zilizoizunguka Tanzania umeme ni rahisi ukilinganisha na Tanzania. Pia mafuta ni rahisi katika Mataifa hayo kuliko Tanzania. Hii inatokana na viongozi katika Wizara hii kukosa uzalendo na hivyo kuangalia ubinafsi zaidi. Kwa hiyo, naiomba Wizara hii kupitia Waziri kupunguza gharama za umeme mara moja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri na Manaibu wake, Katibu Mkuu na timu ya Wizara iliyokubali na kudhamiria kuleta mageuzi ya nishati katika nchi yetu na pia kuifanya Tanzania inufaike na utajiri wake

mkubwa wa madini, naomba msilegeze uzi. Hata hivyo, naomba sana mliangalie suala la kupeleka umeme vijijini kwa uzito mkubwa. Hii ni kutokana na ukweli kuwa taasisi za elimu zilizopo vijijini kama vile shule za sekondari zinatoa elimu yenye upungufu kwa vitendo kutokana na kutokuwepo umeme kwa matumizi ya maabara.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya bajeti ya mwaka uliopita 2011/2012, Serikali iliahidi kukamilisha utekelezaji wa miradi ya umeme Jimboni Busega (zamani Wilaya ya Magu) lakini hadi sasa miradi hiyo inaendelea kwa kasi ndogo sana. Miradi hiyo ni:-

(i) Nassa – Nyamikoma – Kalemela unaotekelezwa na kampuni ya Symbion;

(ii) Lamadi - Bariadi kupitia vijiji vya Mkula na Lutubiga. Kuna hospitali kubwa Mkula, watekelezaji ni kampuni ya NAMIS ikasimamiwa na *TANESCO* Bunda;

(iii) Nyashimo - Ngasamo kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika; na

(iv) Mwanangi – Badugu - Busani kwa ufadhili wa *ADB* ukisimamiwa na *TANESCO* Magu/Mwanza. Transforma tu ndiyo ilikuwa ikihitajika. Wananchi wana matumaini sana kwa miradi hii, naomba ahadi isiishie kuwa hewa.

Mheshimiwa Spika, Mji Mdogo wa Lamadi, licha ya kuwa na umeme katika maeneo ya biashara kandokando ya barabara, kuna maeneo makubwa ya

makazi hayana umeme, hii ni pamoja na kijiji jirani cha Lukungu ambapo wananchi kwa ushirikiano na wadau wa maendeleo tumejenga kituo kikubwa cha watoto wenye mahitaji maalum ambacho hakina umeme. Tunaomba kupitia mipango ya Wizara ifanye haraka kuvipatia umeme vijiji hivi ambavyo ndivyo kitovu cha uchumi katika Wilaya mpya ya Busega.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Busega, tunazo taarifa ya kuwepo hazina kubwa ya chokaa katika Kata za Shigala na Kabita, kampuni binafsi zimeanza kuchangamkia kukamata maeneo kwa kununua ardhi kwa bei ndogo kwa wananchi. Tunaomba mwongozo haraka wa namna ya vijiji kuingia mikataba na makampuni haya ya wachimbaji. Hali kama hii imejitokeza kwa kampuni ya Kichina katika kijiji cha Ngongoko, Kata ya Malili. Tusipelekee wananchi wetu kwenye umaskini.

Mheshimiwa Spika, Serikali inazo taasisi nzuri sana za madini *GST*, *STAMICO* na Chuo cha Madini, naomba taasisi hizi ziimarishwe ili ziweze kulinufaisha Taifa. Ziongezewe rasilimali fedha, watumishi na vifaa ili waweze kufanya vizuri hasa katika kipindi hiki ambapo sekta ya madini inakua na kasi. Chuo cha Madini ambacho binafsi nimekitembelea, kinahitaji kuboreshwa haraka ili kiweze kuongeza udahili kwa kukiongezea mabweni, bwalo na madarasa. Pia kipewe uwezo wa kuajiri Wakufunzi na kuwasomesha zaidi waliopo. Napongeza mpango wa kuanzisha mtaala wa mafuta na gesi katika chuo hicho. Naomba pia kiwe na mafunzo ya muda mfupi ili kuwafundisha

wachimbaji wadogowadogo nchini ili waboreshe mbinu za uchimbaji.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Busega na Bariadi Magharibi, kumegunduliwa pia hazina kubwa ya madini ya *nickel* katika milima ya Ngasomo na Dutwa. Hadi sasa hofu imeanza kutanda katika vijiji vinavyozunguka maeneo haya jinsi gani wananchi watafidiwa kwa kuondolewa katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali isije ikaingia kwenye mtego wa wawekezaji na kuwalipa fidia kiduchu wananchi na kuwaachia umaskini. Ikiwezekana wananchi wapewe ubia katika migodi hii. Hivi sasa tayari hata zile kazi ndogondogo zimeshapewa watu wa mbali na maeneo ya Ngasomo au Jimbo la Busega. Hii ni kinyume cha Sheria ya Uwekezaji wa Madini. Naomba hali hii irekebishwe mara moja na isiruhusiwe kutokea pale uwekezaji kamili utakapotokea. Naomba sana eneo la Ngasomo na Jimbo la Busega liepushwe kuwa Nyamongo nyingine. Pale Ngasomo pia kuna wachimbaji wadogowadogo wa dhahabu. Wachimbaji hao hawagusi eneo muhimu la *nickel* lakini tayari wameanza kuhofishwa na mwekezaji.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana Waziri na Naibu wake kwa msimamo wa kulinda wachimbaji wadogowadogo kama alivyoongea nao kwenye kikao cha Dodoma na pale nilipowaleta kuongea na wataalam wa Wizara kwenye ofisi ya madini.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Wizara isimamie vizuri uwekezaji wa *nickel* pale Ngasomo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Spika, napenda kupata majibu kwa nini Afisa Madini wa Mkoa wa Kigoma anashindwa kukusanya na kuzibana kampuni zinazochimba madini katika Kata ya Ilagala Mkoani Kigoma katika Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma na Kapala Msenga? Kwa kuwa ni zaidi ya miaka thelathini madini hayo hayalipiwi *service levy* wala mrahaba, nataka kauli ya Waziri.

Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itauunganisha Mkoa wa Kigoma na gridi ya Taifa ili vile viwanda endelevu na ambavyo ni *powerful* viweze kuanzishwa Mkoani humo.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS**: Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wao wote kwa hotuba nzuri inayotekelezeka na inayotia matumaini.

Mheshimiwa Spika, kwa shukrani za pekee, naishukuru Wizara ya Nishati ya Tanzania Bara kwa kuisaidia Zanzibar kupata umeme wa uhakika kwa kupitia Baharini kwa manufaa ya Wazanzibar wote.

Mheshimiwa Spika, jambo zuru lazima lipongezwe na kumsaidia mwenzio lazima ushukuriwe. Hivyo katika ukurasa 88 - 89 imetoa picha nzuri ya punguzo la

kuunganisha umeme mjini na vijijini kwa punguzo kubwa. Huo ndio mwanzo mwema kwa Wizara na wateja wake na hii inaonesha kwamba sasa Wizara imepata uongozi uliokomaa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, naomba Wizara ya Nishati Tanzania Bara nayo kuishauri Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kufuata mfano huo mzuri wa kuisaidia jamii ya Wazanzibar wakati ule mtapokuwa na vikao vya pamoja vya mashirikiano baina ya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, kodi ya mapato, kauli ya Waziri kuhusu migodi kulipa kodi ya mapato, ni kauli ambayo haiwajawahi kutolewa na kiongozi yeyote wa Serikali na ni kauli ya kuungwa mkono na kila Mtanzania mzalendo. Lazima kampuni hizi zilipe kodi stahili, kodi na tozo zote, msimamo huu usitetereke hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua zinazochukuliwa na Serikali dhidi ya ubadhirifu katika Shirika la *TANESCO,* kuna masuala yanapaswa kuangaliwa pia. Mfano wakati ni kweli kwamba *TANESCO* inapata Tanzania shilingi bilioni 60 na Tanzania shilingi bilioni 70 kwa mwezi na kwamba mishahara ni Tanzania shilingi bilioni 11 tu, bado *TANESCO* inatumia fedha nyingi sana kununua umeme kutoka *IPPs*. Mfano taarifa ya *CAG* ya mwaka 2010 inaonyesha kwamba wakati *TANESCO* walitumia Tanzania shilingi bilioni 39 kama *'staff costs',* Shirika

lilitumia Tanzania shilingi bilioni 212 *(45% of all revenues from TANESCO)* kununua umeme kutoka wauzaji binafsi. Suala hili halijitokezi kwenye hoja za Serikali, mikataba mibovu ndio kiama cha *TANESCO,* mikataba hii ipitiwe upya.

Mheshimiwa Spika, *Malagarasi Hydro.* Mradi wa umeme wa maporomoko ya Malagarasi, ni muhimu sana kwa Mikoa ya Kigoma na Katavi. Naishauri Serikali itekeleze mradi huu kwa haraka kwa kushirikisha taasisi za umma ndani ya nchi. Mradi huo pia unapaswa kuwianishwa na mradi wa '*transmission'* ili umeme utakaozalishwa Malagarasi uweze kuingia kwenye grid au kuweza kuusambaza kwenye Mkoa wa Kigoma na Katavi.

Mheshimiwa Spika, Mererani, ninashauri kwamba eneo la Mererani liwe eneo maalum la Kiserikali kama ilivyo machimbo ya Almasi kule Botswana. Nashauri kwamba *Botswana model* itumike kwenye Tanzanite ili kuwezesha nchi kufaidika na madini hayo ya vito. Kwa kuwa leseni ya *Tanzanite One* imemalizika na Sheria ya Madini ya mwaka 2010, imetaka vito kumilikiwa na Watanzania, nashauri Watanznia hao wawe Serikali au Shirika la Serikali. Tuunde 'Debtswave' yetu kwenye Tanzanite ili kulinda, kuhifadhi na kudhibiti biashara ya vito vya Tanzanite. Leseni zote za Tanzanite ziwe chini ya Serikali na iundwe kampuni yenye hisa za Serikali 50% na '*strategic investor'* 50%, *Botswana model* itatusaidia Mererani.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuunga mkono hoja iliyo

mbele yetu. Katika hotuba hii yenye uwazi mkubwa, imeonekana dhamira sahihi ya viongozi wa Wizara katika kuisimamia. Nawaomba viongozi wa Wizara waweze kusimamia ipasavyo haya yote yaliyoandikwa ili yatekelezwe kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono bado kuna changamoto nyingi ambazo inabidi Serikali/Wizara iziangalie kwa mapana yake ili kuhakikisha kuwa kasoro hizo zinamalizika. Miongoni mwa changamoto hizo ni hizi zifuatazo ambazo zinahusu Jimbo la Kibiti na Wilaya ya Rufiji kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, wakati wa uwekwaji wa bomba la gesi toka Somanga na Dar es Salaam mwishoni mwa miaka ya 1990, Songas kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini waliingia mikataba na vijiji vyote ambavyo bomba hili litapita kwamba watapewa huduma mbalimbali za kijamii pamoja na umeme. Naishukuru Serikali kuwa hilo limefanyika ingawa si kwa asilimia mia. Kwa mfano, katika Jimbo la Kibiti, bomba la gesi limepita kwenye vijiji zaidi ya nane (8) lakini hadi leo hii ni vijiji vitatu tu kati ya vijiji 68 vya Jimbo la Kibiti vina umeme. Vijiji hivyo ni Kibiti Mchukwi (Mchukwi hospital) pamoja na Bungu. Hata hivyo, vijiji vyote hivyo vitatu mahitaji ya umeme ni makubwa mno na wananchi waliounganishiwa umeme si zaidi ya 2%.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iangalie suala hili kwani maombi ya kuunganishwa umeme yapo mengi kwa Afisa wa *TANESCO* Ikwiriri lakini utekelezaji

bado hauridhishi. Kwa mfano, mwezi May mwaka huu katika kijiji cha Kibiti, nguzo 12 zimeteremshwa lakini kinachoendelea hakijulikani, nguzo hizi zitaendelea kutosimikwa hadi lini? Nini sababu zinazosababisha kuchelewa kwa mradi huu ambao tayari Serikali ilikwishaukubali?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa umeme umefika Kibiti sekondari, ni vizuri kwa Serikali kuwaunganishia umeme wananchi wa Kinyanya na Mtawanya badala ya umeme huo kutumika kwa shule hiyo pekee.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni katika kijiji cha Mchukwi, ni kweli umeme umepita katika kijiji hiki lakini ni hospital ya Mchukwi pekee imepata umeme. Ni vizuri basi wananchi wa kijij cha Mchukwi A pia wakaunganishwa kwani kuna shule mbili ya msingi na sekondari, zahanati pamoja na nyumba za wananchi, maombi tayari yapo *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, katika mkataba wa Songas, vijiji vya Kata ya Mjawa (Jaribu Mpakani, Uponda na Mjawa) vilivyopitiwa na bomba la gesi navyo viliahidiwa kupatiwa umeme lakini hadi sasa vijiji hivyo vyenye wakazi zaidi ya elfu kumi na tano havijapata umeme. Mwaka jana aliyekuwa Mkurugenzi wa *TANESCO* aliahidi kuwa; kwa umeme umefika Bungu km.8 toka Jaribu Mpakani, *TANESCO* itapeleka umeme hapa kwa mwaka wa fedha 2012/2013 lakini hakuna chochote kinachoendelea. Naiomba Serikali iangalie upya suala hilo kwa kuwapelekea umeme kabla ya kuanza kupitisha bomba la gesi linguine. Wananchi wa Kata hii wamechoka na ahadi hewa zinazotolewa na

Serikali kuhusu kupelekewa umeme. Wananchi hawa wamesema hawatakubali kupitisha bomba llingine kama umeme hautapelekwa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni upelekaji wa umeme Nyamisati kwa kuwa *tender* ilikwishatangazwa, nilitaka kujua hadi sasa wamefikia wapi? Lini utekelezaji wake utaanza?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, Jimbo la Igalula mwezi June 201 lilithibitishiwa na Bunge (iko kwenye *Hansard*) na pia hotuba ya Rais, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete ahadi aliyoitoa tarehe 29/10/210, Ilolwansimba, Uyui, Tabora kwamba Wizara kupitia Wakala wa Umeme Vijijini (*REA*), vijiji vifuatavyo vitapatiwa umeme. Goweko, Nsololo, Imalakaseko, Kigwa A, Kigwa B na Igalula. Naomba sasa kwa niaba ya wananchi wa Igalula kupitia bajeti hii, mradi hii ya umeme ikamilike.

Mheshimiwa Spika, mitambo ya Kinyerezi II - Mw 240, gharama dola za Marekani milioni 432 (691.2 bilioni). Hii gharama ni kubwa kwa ukokotoaji wa kimkataba, uhandisi, ununuzi, manejiment (*EDC Contract).* Sheria ya Dole Gumba *(Rule of Thumb)* ni kwamba Kimataifa MW 1 (kwenye EDC) ni sawa na $milioni moja. Hivyo basi MW 240 ni sawa na $240 milioni angalau $300 lakini siyo $432 labda kama kuna ziada ya miundombinu, Wizara itoe maelezo.

Mheshimiwa Spika, bei ya mwisho ya umeme kwa mlaji hukokotolewa kwa kuangalia maeneo mawili, *capacity charge*, inaangalia gharama za ujenzi wa mitambo kama ulipaji mkopo au urudishwaji wa uwekezaji *(return on investment), utility charge* (gharama au malipo kufuatana na kiasi cha umeme mteja anavyotumia). Hivyo basi, kama gharama ya ujenzi ni kubwa ($432m) maana yake umeme unaozalishwa utakuwa ghali kwa kipindi cha uhai wa mradi *(project life cycle),* bei hii itazamwe kwa makini ili umeme ukuze uchumi na siyo kuwa mzigo kwa biashara/viwanda na watumiaji wa majumbani.

Mheshimiwa Spika, madini mengi yanayochimbwa nchini yanaongezewa thamani Jaipur India (Tanzanite), Thailand (vito) na kwingineko, ajira na pato kubwa vinapotea nchini. Wizara ishirikiane na Wizara za Viwanda na Biashara na Masoko na Wizara ya Uwekezaji na Uwezeshaji ili viwanda hivi vijengwe hapa nchini kwa ubia na makampuni ya nje. Mikataba iingiwe na maduka makubwa katika majiji makubwa Duniani ili vito, mikufu, bangili, pete, herein, vidani, shanga vitengenezwe hapa Tanzania na kufaidisha hata wachimbaji wakubwa na wadogo hapa nchini na wachenjuaji madini na masonara, bei zitawekwa hapa Tanzania. Matangazo kwa bidhaa hizi sasa yatasomeka katika mitandao, magazeti, *television* na sehemu za maduka ya mitindo Duniani mfano Paris, New York, London, Dar es Salaam, Hongkong, Los Angeles, Bervelly Hills na Casablanca.

Mheshimiwa Spika, Loya, Tura, Nsololo, Goweko ni Kata zilizo Jimboni Igalula. Ziko kila dalili za gesi, petrol

(*Iwembele swamps*), madini ya dhahabu, almas na vito katika maeneo haya. Naomba Wizara ifuatilie maeneo haya ili wachimbaji wakubwa na wadogo waweze kufaidika.

Mheshimiwa Spika, fedha za vinasaba sasa si muhimu kwa sababu ya bei ya mafuta ya taa sasa iko juu hivyo, hakuna uchakachuaji. Shilingi bilioni mbili naomba ziletwe Igalula kupitia *REA* na kupeleka umeme vijiji zaidi ya sita vya Tura, Malongwe, Loya, Lutende, Miyenze na Miswaki (Mpyagula), shilingi bilioni sita zipelekwe Majimbo mengine yanayohitaji umeme.

Mheshimiwa Spika, Wizara iendelee kufanya kazi kwa karibu zaidi kwa miradi ya Mchuchuma, makaa ya mawe-umeme), Liganga (chuma) inayoongozwa na Wizara ya Viwanda na Biashara na Masoko na ujenzi wa bwawa la Stiegler’s Gorge MW 1200 chini ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Wizara itumie utaalam na uzoefu na taasisi zake (*TANESCO*) ili umeme uzalishwe kitaalam na kufaidisha nchi na wananchi. Ikibidi miradi ya umeme ishughulikiwe na Wizara mama ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, Kiwira, deni la shilingi 40 bilioni, mabenki shilingi 37 bilioni yalipwe. *Management fee* ya shilingi 8 bilioni isilipwe kwani imeshindwa utekelezaji wa majukumu yake. Wahusika waitwe mbele ya Kamati ya Nishati na Madini kutoa ufafanuzi kuhusu *Kiwira Coal* na *Tanpower Limited*.

Mheshimiwa Spika, kampuni ya *Pan African Energy* ilipe $20.1 milioni pamoja na riba wanazodaiwa na Serikali, kodi waliyokwepa.

Mheshimiwa Spika, wananchi wapewe *shares* tujenge bomba la gesi.

**MHE. CAPT (MSF) JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kusimamia utekelezaji wa shughuli chini ya Wizara hii. Pamoja na pongezi hizi, ninayo maoni na mapendekezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni mradi wa umeme Manyoni – Bahi. Naishukuru Wizara hi kupitia *REA* kwa kwanza kutekeleza mradi huu. Chini ya mradi huu, vijiji vyote 15 vinavyopitiwa na nguzo vinatakiwa kupata umeme lakini wakati mradi unakaribia kumalizika kama vijiji vitatu vimerukwa kuwekewa *transformer,* vijiji hivyo ni Sukamahela, Mbwasa na Maweni. Je, kurukwa kwa vijiji hivi ni bahati mbaya au imekusudiwa iwe hivyo? *TANESCO* waliahidi kuwa dosari ingerekebishwa lakini hakuna hatua iliyochukuliwa na *REA* wanajiandaa kukabidhi mradi huu wakati vijiji hivyo havijaingizwa katika mpango wa kupata umeme. Naiomba Wizara iwasukume *REA* warekebishe dosari ya kuruka vijiji vitatu kabla hawajakabidhi.

Mheshimiwa Spika, mbili, mradi wa umeme Iringa - Singida (400kv). Mradi huu umepita katika Tarafa tatu za Wilaya ya Manyoni, Kintiku, Kilimatinde na Manyoni Mjini. Wananchi wanaopitiwa na mradi, mali zao

zimefanyiwa tathmini na baadhi wamelipwa. Hata hivyo, kuna wananchi 61 ambao ama hawajalipwa kabisa au wamelipwa kwa kupunjwa kwa vile baadhi ya mali zao hazikuingizwa katika ripoti ya uthamini. *TANESCO* wameandikiwa barua na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ili walipe fidia hizo lakini bado hawajalipa na wananchi hao 61 wanayo malalamiko makubwa.

Mheshimiwa Spika, tatu, mradi wa umeme wa upepo Singida. Mradi huu wa kutengeneza umeme kupitia upepo (50 Mw) na wa pili 100 Mw, unaripotiwa kila mwaka katika hotuba ya Wizara hii, sasa ni mwaka wa tatu lakini utekelezaji hauonekani. Haya ni makampuni binafsi, kama kuna vikwazo vinavyochelewesha mradi kuanza basi Wizara iingilie kati ili kuweka mazingira yatakayowezesha mradi huu kuanza.

Mheshimiwa Spika, nne, umeme wa jua *(solar energy).* Hotuba ya Wizara haikutoa uzito kuhusu chanzo hiki cha umeme. Wizara itafaa iweke mpango mahsusi wa kuwezesha chanzo hiki cha umeme kutumika hasa vijijini. Tatizo la chanzo hiki ni bei kubwa ya vifaa vyake. Serikali iondoe kodi katika vifaa hivyo ili wananchi wa kawaida vijijini waweze kuvinunua na kunufaika na umeme wa jua.

Mheshimiwa Spika, tano, wachimbaji wadogo wa madini (Londoni). Tunashukuru kwa Serikali kuweka utaratibu wa kutoa mikopo kwa wachimbaji wadogo wa Londoni kupitia kampuni ya *Tan Discovery Mineral Consillincy*. Tatizo lililopo sasa ni utoaji na utengaji

maeneo kwa wachimbaji wadogo. Tunaomba Serikali itenge maeneo mahsusi kwa ajili ya wachimbaji wadogo na kuwapa leseni.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa mema yote anayotujalia. Nikushukuru nawe binafsi kwa kutuelekeza tunapopotoka wakati wote ndani na nje ya vikao. Nimshukuru Waziri mwenye dhamana, Manaibu Mawaziri, Katibu na Watendaji wote katika Wizara hii, kwa hotuba nzuri lakini kwa mipango yao mizuri ya 2012/2013 ambayo inaonyesha sasa inakwenda kuleta mapinduzi ya maendeleo Tanzania na hasa kwa wananchi wa Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, umeme wa genereta (Rukwa). Mkoa wa Rukwa *specifically* Sumbawanga Mjini, tangu enzi na enzi wamekuwa wakitumia umeme mdogo kutoka Mbala na Zambia ambao umekuwa haukidhi haja na kwa hiyo ukawa *supplement* na umeme wa *generator* ambao umekuwa ukitumika kwa matumizi ya nyumbani ambapo pia imekuwa ikifika sasa nne usiku unakatika mpaka kesho yake (mara nyingi), mara chache umeme umekuwa ukiendelea kuwaka mpaka asubuhi.

Mheshimiwa Spika, umeme huu hautoshi kuleta maendeleo Mkoa wa Rukwa. Katika mgao wa fedha za Serikali, Mkoa wa Rukwa tumekuwa tukiwa karibu na mwisho mwa orodha ya Mikoa yote kwa vigezo ambavyo ni kutokuwa na vivutio vya maendeleo.

Maendeleo ya Mkoa wa Rukwa hayatakuwepo kwa kuendelea kuwa na umeme wa *generator* ambao pia una *serve population* ndogo sana ya Sumbawanga Mjini na siyo kwa wakazi wote wa Sumbawanga Mjini.

Mheshimiwa Spika, utajiri wa Mkoa wa Rukwa, hakuna Mkoa tajiri hapa nchini kama Mkoa wa Rukwa lakini ndio Mkoa maskini kuliko yote hapa nchini. Nasema hivyo kwa sababu, kilimo Mkoa wa Rukwa unalima mahindi kwa kiwango cha kulisha Mikoa yote hapa nchini. Si hayo tu, hata alizeti, ufuta, karanga na maharage. Mkoa unatakiwa kusaga na kusindika unga, mafuta, maharage na kadhalika. Mkoa unatakiwa kusindika minofu na samaki wa Ziwa Tanganyika na Rukwa. Mkoa unatakiwa kuchimba madini ya aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na makaa ya mawe tuliyonayo.

Mheshimiwa Spika, umeme wa grid ya Taifa. Mkoa wa Rukwa kwa muda mrefu tumeahidiwa umeme wa grid ya Taifa unaotoka Nyakanazi -Kigoma - Katavi - Rukwa – Tunduma - Mbeya – Makambako – Iringa. Ni kwa kuupata umeme huu na barabara itakapoisha, tutakapojengewa kiwanja cha ndege, tutaweza kupata wawekezaji ambao wameshaanza kuonyesha nia pamoja na wawekezaji wenyeji, tutaanzisha na kuendeleza viwanda vikubwa vitakavyoleta maendeleo makubwa kwa wananchi wa Mkoa wa Rukwa na kuinua uchumi wa Mkoa wa Rukwa na Tanzania kwa ujumla. Viwanda hivyo vitasaga na kusindika unga wa mahindi, ngano, mafuta ya alizeti na ufuta na kadhalika. Vitasindika minofu na samaki

watamu wa Ziwa Tanganyika na Rukwa, vitachimba madini ainaaina pamoja na makaa ya mawe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Wizara ya Nishati na Madini, kwa kazi nzuri inayofanywa kwa bidii na kwa utaalamu. Nampongeza Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Wakuu wa Mashirika chini ya Wizara pamoja na watumishi wote.

Mheshimiwa Spika, naomba kumuuliza Waziri, Naibu Mawaziri na Katibu Mkuu, atueleze ni lini watatekeleza ahadi ya vijiji au maeneo 10 kwa Wilaya kuunganishiwa umeme? Mbona utekelezaji unasuasua?

Mheshimiwa Spika, napenda kuona mikataba iangalie pale inapotokea *prospecting rights* zinavyouzwa kwa bei kubwa kuliko gharama ya *prospecting*. Tuangalie Uganda ilivyonufaika baada ya kudai haki yake Mahakamani, *prospecting rights* ya mafuta ya *petrol* yalivyouzwa kwa faida kubwa ili nasi tunufaike.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri tuone kuwa *resource for equity production sharing* iangaliwe. Wawekezaji wanapokuja na mitaji iwe ndiyo *share* yao na nchi yetu *shares* zake zitokane na *resources* zetu kama gesi, dhahabu, mafuta na kadhalika. Inabidi tuangalie upya dhana inayotumika. Ikiwa hatuna fedha za kufanya *prospecting*, tunaweza kuruhusu

wawekezaji wafanye *prospecting* lakini baada ya hapo gharama hizo ziwe *capitalised* ama sivyo tutafute fedha zetu kufanya *prospecting*.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. DKT MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja hii na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri wawili pamoja na Katibu Mkuu, Ndugu Maswi ambaye kwa kweli kwa uzalendo wake na kwa maslahi ya nchi, amethibitisha kuwa anaweza. Pamoja na pongezi hizo hapa juu hata hivyo ningetaka haya machache kwa leo nipatiwe majibu ya kina.

Mheshimiwa Spika, mgodi wa *Kiwira Coal Mine.* Naipongeza Serikali kurudisha mgodi huu *STAMICO.* Kwa mantiki hiyo, ninaamini *STAMICO* watatumia zabuni ya uwazi kwa kuzingati sifa na vigezo ili kumpata mbia anayestahili na kufaa.

Mheshimiwa Spika, ninataka kujua katika historia ya kuingia ubia kati ya Serikali na *Tanpower Resources* ilizingatia vigezo gani? Maana imepelekea mgodi huu kuwa *idle* na kizungumkuti kwa Serikali kudhamini kampuni hii katika mkopo wa shilingi bilioni 16.9 na kushindwa *still* pamoja na riba kufikia shilingi bilioni 32.19. Nahitaji kujua fedha analipwa nani kwa maslahi ya nani na kwa nini? Vinginevyo waliohusika wote wachukuliwe hatua kali za wazi za kisheria na pesa hizo ziende katika shughuli za kijamii kama afya, umeme vijijini na elimu - vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba nielezwe mikakati ya *STAMICO* juu ya kuendeleza mgodi huo wa Kiwira ni ipi? Katika ripoti nzima ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri sijaona mahali popote juu ya Mlima Kabulu ambao ni sehemu ya mgodi wa Kiwira na hazina yake ni kubwa kuliko ya *Kiwira Coal Mine.* Naomba nipatiwe maelezo ya kina taratibu gani zilitumika katika kutenganisha leseni hizi mbili na *what is the way forward on this?*

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuongeza mrahaba *royalty* toka 3% to 4% na makampuni ya madini yenye mikataba kufanya hivyo. Hata hivyo, ningeshauri Serikali tena i-*negotiate* na makampuni yanayo *exist* na yenye mikataba ili *STAMICO* iwe na hisa huko kama *entity* ya Serikali kuliko kusubiri makampuni mapya ambayo hatuna uhakika nayo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mrahaba lakini pia kama Taifa katika madini tunategemea sana *corporate tax.* Kodi hii inalipwa kijanjajanja tu hivyo kulipotezea Taifa pato. Makampuni ya madini kila baada ya muda fulani yanauza ama kubadilisha majina kwa nini? *Corporate social responsibility* za makampuni ya madini *in addition* haziendani na mapato wanayopata. Huu ni ujanjaujanja tu hivyo Serikali kutonufaika ipasavyo. *Capital gain tax* inakwenda wapi?

Mheshimiwa Spika, sekta ya madini ni muhimu sana katika Taifa hili. Nchi yetu ni mojawapo ya nchi tajiri katika Afrika kwa madini lakini ndio nchi mojawapo maskini Afrika, kwa nini? Mchango wa sekta

hii muhimu ya madini umekuwa sio wa kuridhisha kutokana na upungufu mbalimbali kama *unnecessary lobbying* ambapo Taifa linapoteza mapato, mikataba mibovu na kadhalika. Nini mkakati wa Serikali katika kurudisha hali nzuri ya sekta hii ya madini *in order*? Tanzania inapenda sana wawekezaji na inaheshimu lakini hii imekuwa nchi inayopoteza *to the extreme,* inatakiwa iwe *win-win situation.*

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mzee Bomani na *recommendation* zake zimefika wapi? Tunaboreshaje sekta *without this good governance with transparency?* Misamaha ya kodi - *ubelievable*!

Mheshimiwa Spika, *biofuel,* kwa sasa Tanzania sera yake haipo, isitoshe kwa muda huu tunapitia jambo la gesi ambalo nchi tunatakiwa kuwa makini sana, tuondokane na makosa yaliyotokea huko nyuma *for win-win situation,* vinginevyo hao wawekezaji kama wanakuja kutunyonya bila *national interest* basi wasije, madini asili hayaozi. *Biofuel* haina faida kwa Watanzania, imeacha Watanzania *devastated due to their land grabbing* na uongo kwa wawekezaji hao.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu Mawaziri wake kwa hotuba nzuri ya bajeti na naomnba kuunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara kupitia *REA* wasaidie kupeleka umeme katika maeneo haya muhimu Jimboni Singida Kaskazini. Maeneo kama ya Ilongero - Msange – Mangida. Umeme huu uunganishe pia shule za sekondari zifuatazo zilizo katika njia hii, Maghoja sekondari, Murigha girls sekondari, Madasenga sekondari pamoja na Mji Mdogo wa Msange.

Mheshimiwa Spika, eneo linguine ni Singida – Mgori – Ngimu - Pohama pamoja na shule zifuatazo Mwanamwema sekondari, Ngimu sekondari na Pohama sekondari.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Wizara iharakishe mchakato wa kupatikana kwa umeme wa upepo kwa kuanzisha mradi wa umeme Singida. Wananchi wa Singida wanasubiri kwa hamu kuanzishwa kwa mradi huu na kusaidia kuleta ajira.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri inayotia tumaini kwa Watanzania haswa suala la umeme. Umeme ni kitu muhimu sana kwa Taifa letu lakini uwezo wa wananchi kumudu gharama ya kuingiza majumbani umeme na kulipa ankra za umeme ni kazi kubwa kulinganisha na kipato na hata aina ya nyumba za wengi wanazokaa, miundombimu haitoi nafasi nzuri ya wao kuweka umeme huo.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali ni vema ikawa na mpango mbadala kwa wale wasioweza kufunga umeme wa *TANESCO* watumie *solar* na hizo *solar* zitolewe na *REA* na wananchi walipie polepole bila hivyo Serikali nia yake ya kuangaza nchi hii itakwama na hii itazua matabaka kwa wale walionacho na wasionacho.

Mheshimiwa Spika, Wanamissenyi wengi wameshafanya taratibu zote za kuingiza umeme majumbani lakini mpaka leo maeneo mengi hawajapata umeme. Naomba kujua lini umeme huo utaletwa? Japo nimepokea barua ya kuwekewa umeme katika vijiji 24, lini kazi hiyo itaanza?

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waziri na Naibu Mawaziri kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, Serikali inashughulikiaje mashimo yanayoachwa wazi na wachimbaji wadogo na wakubwa wa madini? Inasikitisha sana unapoona mashimo makubwa yameachwa, nini hatma yake?

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja. Hatua za kupunguza gharama za kuunganisha umeme vijijini naiunga mkono sana. Naomba ianze kutekelezwa haraka ili kupunguza gharama za maisha ya wananchi wa vijijini.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana *REA* kwa kazi na kasi ya utendaji uliotukuka na mimi nitashiriki

kikamilifu katika kuisema *REA* ili iendelee kupata fedha nyingi za kutosha.

Mheshimiwa Spika, naamini ratiba ya kuweka umeme Tarafa ya Pawaga ili kuwasaidia wananchi wakulima wa mpunga kukoboa mchele kwa kutumia umeme lakini pia kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa mwaka 2009 na mwaka huu 2012 alipotembelea Pawaga, itatekelezwa mwaka huu 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, nawatakia kila la kheri Katibu Mkuu na Watendaji wote, Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuweza kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu Mawaziri na Watendaji wote wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Eliakim Maswi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Wizara ya Nishati na Madini kwa uamuzi wa kupunguza gharama za kuunganisha umeme hasa maeneo ya vijijini kwa asilimia 61.1. Aidha, naipongeza sana *REA* kwa kuendelea na kazi ya kusambaza umeme katika maeneo mbalimbali ya vijijini. Vilevile naipongeza Serikali kwa kukamilisha taratibu za mkopo kwa ajili ya ujenzi wa bomba la gesi toka Mtwara na Dar es

Salaam, ni kweli bomba la gesi litaleta mapinduzi ya uchumi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. MANSOOR S. HIRAN:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Sospeter Muhongo kuteuliwa kuwa Mbunge na Mheshimiwa Rais na pia kuteuliwa kuwa Waziri wa Nishati na Madini ambayo ni Wizara nyeti. Pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Masele na Mheshimiwa Simbachawene kwa kuteuliwa kuwa Manaibu Waziri wa Wizara hii. Naomba nimpongeze Waziri kwa kusimamia vizuri *TANESCO* na kuhakikisha mgao hakuna, pia kufuatilia ufisadi ndani ya *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, umeme vijijini, Mheshimiwa Waziri, wananchi wa Wilaya ya Kwimba hususani taarifa ya Mwanashimba, upembuzi yakinifu (*feasibility study)* ulishafanyika kuhusu upelekaji wa umeme Mji Mdogo wa Hungumalwa na *ginnery* za Sangu na Mwamala. Naomba mwaka huu umeme ufike, pia hii ni ahadi ya Ilani ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, leseni za madini, naomba nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara kwa maamuzi ya kufuta leseni ambazo hazijafanyiwa kazi kwa muda mrefu. Pia sio hiyo tu kuna makampuni yamehodhi maeneo makubwa sana wakati uwezo wake wa kuyatumia maeneo yote hayo haina lakini amelalia maeneo ambayo wananchi wengi wanataka wayafanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kushauri yafuatayo kwa huu uagizaji wa mafuta ya pamoja.

(i) *EWURA* wapange *cap price* kwenye mauzo ya mafuta ya *diesel* inayouzwa kwenye migodi hii;

(ii) Mafuta ya Jet-Al, yanayouzwa kwenye viwanja vya ndege yapangiwe *cap price* na usimamiwe kwa karibu. Hiyo Jet-Al inaweza kuuzwa kama *kerosene* na huku tunafahamu Jet-Al hailipi kodi;

(iii) *Market share* ya makampuni ya mafuta itumike na *EWURA* ya mafuta ambayo wanayapangia kwenye *cap price;* na

(iv) Mafuta ya *transit* yalipe *windfall tax* wakati wanataka ku-*localize*.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO*, napongeza kwa maamuzi ya Wizara ya kupunguza gharama ya kuunganisha umeme vijijini na mjini. Napongeza pia kwa maamuzi ya kusimamisha uongozi wa juu wa *TANESCO* kwa sababu ya ufisadi.

Mheshimiwa Spika, gesi, naipongeza Serikali kwa kuamuwa kujenga bomba ya kusafirisha gesi kutoka Mtwara kuja Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja hii.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kumtafuta Waziri wa Nishati na Madini Mheshimiwa Profesa Sospeter M. Muhongo na kumteua mtu huyu muhimu kwa Taifa letu hili. Hakika kwa dhati kabisa Wizara imepata watu na siyo watu wamepata Wizara. Nawapongezeni sana Waziri na Manaibu wote wawili Simbachawene, Masele, hakika kabisa Wizara imepata watu na mafiga matatu kweli yamekamilika katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, natoa angalizo (ulinzi), kutokana na mafisadi waliopo katika nchi hii, watu wafuatao wapewe ulinzi mkali sana; Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo, Katibu Mkuu wa Wizara, Ndugu Eliakim C. Maswi na Manaibu Waziri wote wawili ili waweze kutenda kazi yao vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri atakapokuwa anafafanua hoja, anieleze juu ya mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itapeleka umeme Laela, Mji Mdogo kupitia vijiji vyote toka Sumbawanga hadi Laela? Waziri atakumbuka Mji huu ndiyo umependekezwa kuwa Makao Makuu ya Halmashauri ya Kwela, naomba nipatiwe majibu. Aidha, atakumbuka Jimbo lote la Kwela hakuna hata kijiji kimoja kilicho na umeme.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa kupeleka umeme Ukanda wa Ziwa Rukwa. Ukanda huu umekuwa ukisahaulika katika huduma muhimu japokuwa ni eneo lenye uchumi mkubwa na shughuli zinahitaji sana umeme. Eneo hili lina tarafa mbili kubwa, Tarafa ya Mtowisa na Tarafa ya Kipeta. Pia inavyo vijiji 50 vikubwa na kata saba (7) kubwa za mfano wa miji midogo kwa majina kama ya Mfinga, Muze, Mtowisa, Milepa, Ilemba, Kaoze, Kipeta.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anipatie maelezo ni lini maeneo hayo yatapatiwa umeme? Vilevile naomba majibu ni lini kijiji cha Sakalilo kitapatiwa umeme ili mradi wa umwagiliaji uwe na manufaa kwa wananchi kwa kufunga mashine za kukoboa mpunga?

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja iliyoletwa mbele yetu. Aidha, baada ya kuunga mkono hoja, naomba nichangie baadhi ya maeneo kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni uwepo wa umeme wa uhakika na uunganishaji wa Mikoa isiyo kwenye gridi ya Taifa. Ni ukweli usiopingika kwamba bila umeme wa uhakika, hakuna maendeleo kwani bila umeme hakuna uwekezaji unaoweza kufanyika. Naipongeza Serikali kwa kulitambua hili na kuanza mpango wa kuunganisha umeme wa gridi ya Taifa kuanzia Nyakanazi kwenda Kigoma, Kigoma kwenda Mpanda, Mpanda kwenda Sumbawanga, Sumbawanga kwenda Tunduma, Tunduma kwenda

Makambako, Njombe hadi Iringa. Njia hii niliyoitaja itachangamsha ukuaji wa uwekezaji na kuchochea ukuaji wa uchumi kwa Mikoa ya Iringa, Kigoma, Katavi, Ruvuma, Mbeya na Njombe.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia njema ya Wizara ya kuhakikisha kwamba nishati ya umeme ya uhakika inasambazwa nchi nzima, ni vizuri vyanzo vingine vya kuzalisha umeme zisipuuzwe. Katika mchango wangu wa kuzungumza na kuandika, niliainisha chanzo cha nishati kutoka makaa ya mawe ya Namwele yaliyopo Rukwa yakichimbwa na mzalendo ambaye yuko tayari kuzalisha umeme na kuingiza kwenye gridi ya Taifa ili mradi apate uhakika kwamba kiasi cha umeme utakaozalishwa utanunuliwa na *TANESCO*. Naomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana atoe majibu kwamba mpango huu na utayari wa mzalendo huyu unaachwa hivihivi tu na tukawa tunawavutia wawekezaji wa kutoka nje ya nchi?

Mheshimiwa Spika, Jimboni kwangu kuna chanzo cha nishati kinachotokana na joto la ardhi. Hivyo, naiomba Wizara itume watalaam ili kufanya uchunguzi wa kitaalam.

Mheshimiwa Spika, pili napenda kuzungumzia suala la kusambaza umeme Wilaya zote nchini. Kwanza, napenda kupongeza nia njema ya Wizara ya kuhakikisha kwamba Makao Makuu ya Wilaya zote zinafikiwa na nishati ya umeme. Pamoja na nia njema hii, napenda Wizara ikatoa kipaumbele kwa miji ambayo ni Makao Makuu ya Wilaya zote Tanzania.

Inatia unyonge pale ambapo Waheshimiwa Wabunge wa baadhi ya Majimbo wanaongelea na kuomba vijiji vyao vipatiwe umeme wakati baadhi yetu hatuna umeme hata Makao Makuu ya Wilaya achilia mbali Makao Makuu ya Tarafa na Makao Makuu ya Kata. Ili tuhakikishe maendeleo yanafika katika maeneo yetu yote ya nchi ni bora tukazingatia Makao Makuu ya Wilaya zote zinafikiwa na umeme.

Mheshimiwa Spika, tatu, ahadi za Mheshimiwa Rais na Makamu wa Rais. Kazi nzuri iliyoanzishwa na uongozi mpya wa Wizara kwa maana ya Mheshimiwa Waziri na Katibu mpya ni vizuri pia wakakumbuka ahadi za Mheshimiwa Rais na Makamu wake ili kuendelea kuwajengea heshima viongozi wetu hawa kwa wananchi. Naliandika hili kumkumbusha Mheshimiwa Waziri kwamba katika Jimbo langu la Kalambo tulipata bahati ya kutembelewa na Mheshimiwa Makamu wa Rais aliyefika Tarafa ya Kasange mwambao mwa Ziwa Tanganyika na kutuzindulia Soko la Kimataifa la Samaki la Kasange na kujionea umuhimu wa kupatiwa umeme katika bandari na soko lile. Naiomba Wizara kuweka katika mpango wa utekelezaji wa kufikisha nishati hii muhimu kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, nne, *bulk procurement,* uwekaji wa vijinasaba pamoja na *ethanol.* Bunge tulilazimika kupandisha bei ya mafuta ya taa ili kukabiliana na uchakachuaji wa mafuta ya *diesel* na *petrol*. Inashangaza pamoja na hatua hii eti bado vinasaba vimewekwa ili kuyatambua mafuta, huu ni wizi wa

mchana, ukomeshwe mara moja na Wizara badala ya kuendelea kufuja pesa za walipa kodi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, katika mkataba wa kununua mafuta kwa pamoja, kuna kipengele kimewekwa cha kuongeza *ethanol*. Kipengele hiki kimekuwa kikitumika vibaya kwa kuongeza *ethanol* nyingi hivyo kuwa na athari kwa mtumiaji na chombo chake na hasa ukizingatia tabia ya *ethanol* inapokaribiana na maji na bei halisia ukilinganisha na bei ya *petrol* kwenye soko, ni vizuri *clause* hii ikaondolewa ili kuondoa malalamishi kwa watumiaji.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono na ninampongeza Waziri, Katibu Mkuu, Bwana Maswi, najua vizuri utendaji wake wa kazi uliyotukuka tangu akiwa Hazina, naipongeza pia timu ya Manaibu Waziri. Waziri simamia misingi ya haki, usitetereke, safisha nyumba yako imejaa uchafu, anzia Wizarani shuka kwenye taasisi zilizo chini ya Wizara. Waziri simama kwa miguu yako, tembelea miguu yako uwe na msimamo, usiyumbishwe na nguvu ya pesa, yapo majaribu utapambana nayo ukizubaa yatakuteka. Wizara hiyo imefukuzisha mpaka Waziri Mkuu, pana mambo hasa upande wa mafuta, gesi na baadaye *uranium*. Simama kidete na Mungu akuongoze siku zote katika maamuzi yenye hekima na busara ili tuijenge nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naungana na Waziri katika maelezo yote ya hotuba yake, naomba wajipange kwa utekelezaji ili bajeti ijayo waweze kutueleza

utekelezaji wa haya wameyatekeleza kwa asilimia ngapi?

Mheshimiwa Spika ukurasa wa 105 – 187, umezungumzia migodi kulipa kodi ya mapato, nchi inatakiwa inufaike na rasilimali zake na si kunufaisha wawekezaji pekee, lisimamie ili migodi iweze kulipa kodi stahili.

Mheshimiwa Spika, naomba kukumbushia ahadi ya *TANESCO* kuhusu kupeleka umeme kupitia Wakala wa Umeme Vijijini *(REA)* katika maeneo ya Tallo, Ibindo, Kadashi, Nyashama, Maligisu na *Kabila Centre*. Serikali imekuwa ikiniahidi tangu bajeti ya mwaka jana na nimekuwa nikiuliza maswali ya mara kwa mara na mara ya mwisho niliambiwa mradi huo unasubiri kutangazwa ambapo zabuni ilikuwa zifunguliwe Mei mwaka huu, je, umefika katika hatua gani? Pia kupitia *REA* ilitaka iunganishe umeme kutoka Montare, Ishingisha, Mhulya, Ngulle na Nyamatale Wilaya ya Kwimba. Waungwana siku zote ukiahidi tekeleza ahadi kwani Serikali inaponiahidi Bungeni wananchi wangu wanasikia, lakini nami nikienda kufanya mikutano yangu naahidi kufuatilia kauli ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Waziri na Katibu Maswi ni majembe yenye uhakika, najua hawawezi kufanya miujiza lakini wanaweza kuleta mabadiliko ya kiuchumi, nidhamu katika maeneo wanayoyaongoza, watu sasa wanafikia kutokujali wanatumia nyadhifa zao kujinufaisha, hawajali maslahi au dhamana waliyokabidhiwa.

Mheshimiwa Spika, mimi ndiye niliyemwondoa aliyekuwa DG, Dokta Rashidi kwa matumizi mabaya ya madaraka. Tupo pamoja kama mtasimamia vizuri rasilimali zetu tulizozawadiwa na Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, nawatakia kila la kheri siyo lazima wakati unahitimisha kuvitamka vijiji nilivyoviainisha, naweza nikapewa majibu hata kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuzungumzia kuhusu leseni za uchimbaji madini kwa wachimbaji wadogowadogo. Nchi yetu ya Tanzania imebarikiwa kuwa na ardhi kubwa yenye madini ya aina mbalimbali mfano dhahabu, almasi, *tanzanite*, uranium, *bauxite* na kadhalika lakini cha kushangaza maeneo yote yenye madini yamegawiwa kwa wachimbaji wakubwa wenye mitaji mikubwa na kuwa ni laana kwa wachimbaji wadogowadogo ambao wamezaliwa katika maeneo hayo. Badala ya kuwanufaisha wananchi husika wenye eneo hilo maeneo ya madini yamegawiwa kwa wawekezaji tena wengi wakiwa ni wa kigeni, wawekezaji hawa hupewa leseni za utafiti na hata kabla ya kumaliza utafiti wengine huanza kuchimba madini na kuyasafirisha nje kwenye nchi zao. Ni kwa nini Serikali haiwapi wachimbaji wadogowadogo leseni za kuchimba madini ili nao waweze kunufaika na rasilimali ya nchi yao?

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu fidia kwa wananchi. Kumekuwa na migogoro mikubwa ya wananchi wanaoondolewa kwenye maeneo yao yenye madini na ulipaji wa fidia kutokufanywa kama inavyostahili. Wananchi wangu mfano wa Mkoa wa Singida, Wilaya ya Singida Vijijini, Mang'onyi na Sumbaru - Ikungi wanalalamikia unyanyasaji na usumbufu mkubwa wanaoupata toka kwa kampuni ya *Shanta Mining Co. Ltd.* ambayo pamoja na kupewa eneo kwa kukiuka utaratibu bado kampuni hii haijawalipa wananchi husika fidia waliyokuwa wanadai. Nashauri Serikali ifuatilie mgogoro huu kati ya *Shanta Mining* na wananchi wa Mang'onyi Singida kuona uhalali wa wawekezaji hawa, ni matatizo ambapo yamepelekea hata kujeruhiana hasa katika kijiji cha Sumbaru.

Mheshimiwa Spika, tatu, faida ya umeme wa upepo Mkoani Singida. Mkoa wa Singida pamoja na kuwa na hali ya nusu jangwa, umebarikiwa kuwa na upepo mwingi ambao una manufaa makubwa katika kuzalisha umeme wa upepo. Umeme wa upepo utasaidia sana katika utunzaji wa mazingira hasa katika Mkoa huo ambao ni jangwa na hivyo utapunguza uharibifu wa mazingira kwa kukata miti kwa ajili ya kuni na mkaa. Naiomba Serikali iharakishe mchakato wa kuleta umeme wa upepo ili kuokoa mazingira yetu na vilevile kuinua kipato cha wananchi wa Mkoa wa Singida ambacho kiko chini sana.

Mheshimiwa Spika, nne, kashfa ya ununuzi wa mafuta kwenye makampuni ya *IPTL, SONGAS* na kadhalika. Kwa kuwa kumekuwa na manung'uniko

mengi na ukosefu wa maadili katika kutunza fedha au matumizi ya fedha za umma, ni vizuri sasa ukafanyika uchunguzi mahsusi kupitia ofisi ya *CAG* ili kubaini ni hasara kiasi gani *TANESCO* inapata katika ununuzi wa mafuta ya kuendesha mitambo ya kufua umeme. Imeonekana kwamba kuna watu wasio waaminifu kwenye Shirika ambao wanapenda umeme wa dharura kwa maslahi binafsi wanayoyapata kwenye makampuni husika.

Mheshimiwa Spika, hii inapelekea hasara kubwa sana na hivyo kupoteza fedha nyingi za walipa kodi wa nchi hii. Kwa mfano, manunuzi ya mafuta toka *IPTL* na *Symbion* kwa mwezi yanakadiriwa kuwa ni shilingi bilioni 42 na haya manunuzi yatagharimiwa kwa miezi mitano (5) kuanzia sasa. Sasa kwa manunuzi haya ya mabilioni ya shilingi tutegemee nini kwenye mustakabali wa uhai wa Shirika la *TANESCO* na Taifa kwa ujumla? Nashauri Serikali pia kufuata Sheria ya Manunuzi ya Umma katika manunuzi yake.

Mheshimiwa Spika, tano, wawekezaji wa makampuni ya uchimbaji madini. Nchi yetu haijaweza kufaidika kwenye sekta ya madini kwani faida inayopatikana haitoshelezi kulingana na kiasi cha madini yanayochimbwa nchini. Makampuni ya uchimbaji madini yamekuwa yakichukua mchanga na kuupeleka kwao kuufanyia utafiti ili kuona kama kuna madini. Swali, ni nani anafuatilia mchanga huo na kujiridhisha kwamba kiasi kinachotolewa na makampuni hayo ni cha kweli? Ni kwa nini uchunguzi huo usifanyike hapahapa nchini ili kujiridhisha sisi wenye

nchini? Huu mtindo haufai na badala yake umeendelea kuliletea Taifa hasara kubwa.

Mheshimiwa Spika, kama haitoshi, makampuni ya madini hayajafanya vya kutosha kutokana na kile wanachovuna. Wananchi walioondolewa kwenye maeneo ya madini wameendelea kuwa maskini, kwa sababu wawekezaji hawa wanatakiwa waendeleze maeneo waliyoyakuta na sio kufanya vitu vidogovidogo kama ujenzi wa shule zisizokwisha.

Mheshimiwa Spika, tunataka uwazi wa mikataba, miradi ya maendeleo kama shule za kisasa, umeme, barabara, hospitali, maji na nyumba bora za kuishi wafanyakazi. Ni kwa nini Tanzania haifanyi kama Afrika Kusini ilipotoa eneo lake lenye dhahabu kwa wawekezaji na leo tunashuhudia mji mzuri ubaoitwa *Egol the place of Gold*? Kwa nini wachimbaji wa madini wa Tanzania wanaacha mashimo tu na kuchafua vyanzo vya maji kama ilivyotokea kule Nyamongo Mkoani Mara? Serikali ije na majibu ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MATHIAS M. CHIKAWE:** Mheshimiwa Spika, natangulia kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, naomba kumshauri Mheshimiwa Waziri kuhusu suala la umeme vijijini. Wilaya ya Nachingwea ina umeme Makao Makuu ya Wilaya kisha umeme huo unatoka Nachingwea na

kuelekea Rwangwa, ukipita juu ya vijiji kadhaa bila vijiji hivyo kufaidi umeme huu. Naomba umeme ushuke katika vijiji vya Matangini, Ikungu, Rupota, Ruponda na Marambo. Wananchi hawaelewi kwa nini umeme huu upite tu juu bila kuwanufaisha wanakijiji hawa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, narudia kuunga mkono hoja ya Waziri wa Nishati na Madini.

**MHE. RAMADHANI HAJI SALEH:** Mheshimiwa Spika, napenda nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehma ambaye ametufikisha katika Bunge lako Tukufu tukiwa hali ya uzima.

Mheshimiwa Spika, niaze kuchangia bajeti hii katika upande wa madini. Tanzania ni nchi yenye madini mengi lakini hadi leo bado hatujafaidika na rasilimali hiyo. Kwa kuwa bado hatujachelewa katika kulinda rasilimali hiyo, Serikali ichukue hatua ya kurekebisha Sheria ya Madini ili wawekezaji wasiondoke na madini na kutuachia mashimo.

Mheshimiwa Spika, naomba nijikite katika upande wa gesi. Kama tutaitumia gesi vizuri, Tanzania itapata fedha nyingi na itaweza kupunguza hata deni la nje.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Spika, mchango wa madini katika bajeti ya Taifa ni mdogo sana. Hii inaleta hisia kwamba haya madini (utajiri) huu tulionao ni wa kazi gani wakati wanaonufaika ni watu wengine tofauti kabisa. Hakika sisi kama Taifa au nchi

yetu imegeuka kabisa na kuwa shamba la bibi. Wawekezaji kutoka nje wameshatusoma na kutufahamu kiundani udhaifu wetu na sasa wanatumia udhaifu wetu huu kuchuma mali yetu na kuondoka. Kila mtu anajua kwamba tunaibiwa katika sekta ya madini lakini cha kushangaza hatuoneshi mikakati ya kuondoa hali hii. Wizara na Serikali kwa ujumla imejipangaje kuhakikisha kwamba tunaepuka balaa hili?

Mheshimiwa Spika, suala la umeme wa uhakika limekuwa kizungumkuti kisichoeleweka. Hadi sasa kuna giza nene katika Wizara hii ya kuondolewa kwa Mtendaji Mkuu wa *TANESCO* na tuhuma za uwepo wa mikataba ya kijanja kuhusu tenda za kusambaza mafuta. Inaonekana wazi kuwa Wizara hii iko katika hali ngumu sana (haijatulia). Kutokana na mambo yote haya, tusitegemee maendeleo yoyote kuletwa na Wizara hii iliyoko katika hali tete. Maamuzi magumu yanahitajika ili kubadili hali hii na kunusuru nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tusipojipanga vizuri katika suala zima la sera, uongozi, mikakati na kadhalika, utajiri wa gesi unaoleta matumaini makubwa kwa kila Mtanzania utageuka kuwa laana, watu wengi wanatahadharisha, nami naungana nao kutahadharisha juu ya jambo hili. Hatutapenda kuja kujuta baadaye kwani Waswahili husema majuto ni mjukuu. Ni lazima sote tujielekeze katika kuwa na sera, mipango na sheria zitakazotulinda na kutuongoza katika kuifaidi rasilimali hii kwa amani na utulivu. Tusipofanya hivi, itageuka laana na hakuna atakayefaidi.

Mheshimiwa Spika, sasa ni wakati wa kutamka bila woga "Mikataba Mibovu Basi", jamani imetosha sasa. Wataalam wetu nao ifike mahali waone kuwa uzalendo ni muhimu sana, ubinafsi haufai kabisa katika mikataba ndani ya sekta ya madini. Mikataba mibovu inaashiria ulafi, ubinafsi, rushwa na mengine mengi kwa watumishi wasio waaminifu. Waziri na Manaibu wake wote ni wapya katika Wizara hii, tumieni nafasi hiyo kujenga upya Wizara yenye kuleta tija na matumaini kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, suala la uharibifu wa mazingira utokanao na uchimbaji wa madini nalo lisifumbiwe macho. Tunahitaji Tanzania endelevu kwa vizazi vingi vijavyo. Siku hizi kuna dhana maarufu ya maendeleo endelevu ambayo huwezi kuitenga na utunzaji wa mazingira. Ni lazima tuwe na mikakati thabiti ya kunusuru mazingira yetu kwani madini yanaweza kuisha ila mazingira yatabakia hadi mwisho wa nyakati.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimwa Spika, naunga mkono hoja hii, ingawa Waziri ni mgeni, lakini kwa muda mfupi tumeridhika na hatua anazochukua za kupambana na ufisadi katika Shirika la TANESCO na Wizara kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri atatue suala la kukatika umeme katika Wilaya za Rombo na Moshi Vijijini. Kukatikakatika kwa umeme mara kwa mara kunaleta kero kubwa. Najua kuna kazi nzuri inayofanyika Makuyuni, Himo katika Jimbo langu la Vunjo. Naomba wakati wa majumuisho uwaeleze wananchi wa Rombo na Moshi Vijiji kutokana na

uwekezaji unaoendelea pale Makuyuni, Himo watanufaika lini na vipi?

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Vunjo kuna maeneo mengi ambapo TANESCO walipeleka nguzo za umeme katika maeneo hayo lakini kwa zaidi ya miaka mitano nguzo ziko palepale hazijachimbiwa ardhini na wala hawajapeleka nyaya katika maeneo hayo.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja. Nampongeza Mheshimiwa Rais Jakaya kwa uteuzi makini wa viongozi wa Wizara hii ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Waziri na Manaibu Waziri wote wawili, kwa maoni yangu, naridhishwa na timu hiyo tangu imepatikana na kwa majukumu ya muda mfupi yaliyotekelezwa lakini pia kwa namna mlivyopanga hotuba hii ya bajeti ya 2012/2013. Katika utekelezaji wa bajeti hii kwa 2011/2012, kulikuwa na changamoto nyingi mfano kukosekana kwa nishati ya umeme hata hivyo juhudi za kuridhisha zilifanyika kupunguza upungufu huo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilikuwa inatekeleza mradi wake kupeleka umeme Wilayani Nkasi kutoka Sumbawanga ambapo vijiji vyote vya njiani vingeweza kunufaika. Kazi nzuri ilifanyika na tumeahidiwa kupata umeme wakati wowote kuanzia sasa, hata hivyo kuna changamoto zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, wananchi wa vijiji vya Nkundi, Kipande, Kantawa, Mihindikwa, Kasu, Chala na Kacheche katika Jimbo la Nkasi Kusini wanalalamika sana kuwa miundombinu iliyoandaliwa njiani katika vijiji hivyo haijaruhusu kuwapatia umeme wale walioko mita chache tu ndani ya kijiji yaani miundombinu haijasambazwa katika vijiji hivyo. Inaonyesha ni wananchi wachache tu ndiyo watakaobahatika kupata nishati hii muhimu ambayo wameisubiri miaka mingi. Waziri hebu fanya wote watakaohitaji umeme wapate katika vijiji vilivyopitiwa na umeme.

Mheshimiwa Spika, umeme huu utawaka lini hasa Mjini Namanyere, wananchi wanasubiri kwa hamu ahadi ya Rais wao ambaye aliwaahidi kupata umeme haraka iwezekanavyo. Japokuwa kazi inaendelea vema, tunaomba umeme uwake.

Mheshimiwa Spika, mpango wa mwaka 2012/13. Katika mpango huu, nimeona nia njema ya Wizara kuboresha upatikanaji wa nishati mijini na vijijini. Naomba pia nipongeze kupunguza gharama za uingizaji umeme mijini na vijijini kwa 25% hadi 70%. Kwa punguzo hili, lazima Waziri apongezwe.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni uwazi na ukakamavu Waziri anaotoa katika kutumikia Watanzania. Mgao haukubaliki, ni kauli ya kwanza kutolewa na Wizara hii. Kama itakuwa ndivyo, sifa hii itaendelea kutukuka kwa muda mrefu. Kama hakuna umeme viwanda havifanyi kazi, watu watakosa ajira, nchi itakuwa giza, kodi hakuna na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, uthibiti wa leseni za madini. Nakupongeza nalo vilevile kuona uwezekano kuongeza zaidi mrabaha toka 4% ili makampuni yanayochimba wachangie zaidi. Vilevile nashauri kwa kuwa uchumi wetu unakuwa kwa haraka, maeneo *strategic* kwa madini yanaweza kubaki kwa wazalendo (wawekezaji), hata kama hawana uwezo, Serikali iwachangie kidogokidogo hadi hapo nchi itakapokuwa na uwezo.

Mheshimiwa Spika, *REA*, naomba umeme Makao Makuu ya Jimbo la Nkasi Kusini, Tarafa ya Kate. Umeme unaoenda Namanyere umepita kijiji cha Nkundi, ukitoka Kundi kupelekwa Kate ni kazi ndogo kwani unakuwa unapitia vijiji vya Kalundi, Myula, Ntalamila na hatimaye Kate.

Mheshimiwa Spika, mwamko wa Ziwa Tanganyika, Mji Mdogo wa Wampembe wakipata umeme tutaweza kusindika samaki aina ya migebuka ambayo kwa sasa tunapeleka Zambia. Ni aibu Ziwa Tanganyika ambalo tunalimiliki kwa sehemu kubwa kuliko nchi yoyote, mazao yake yanasindikwa Zambia ambapo ni nchi ambayo inahodhi eneo dogo sana, tatizo ni umeme kukosekana kule mwambao.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa uchumi wa nchi yetu sasa hivi umeelekezwa kwenye gesi na madini na pamoja na kuchangia pato la taifa lakini bado pato hili halijamfikia Mtanzania. Mimi tatizo kubwa ninaloliona ni kwamba hatuna sera inayotueleza juu ya usimamizi wa hii gesi na madini ili tuweze kusimamia vizuri kwa kuwa

tunaambiwa tu kuna sheria fulani lakini hatuna mfumo maalum kuwa hizi sheria zinatakiwa zisimamiwe na nchi yenyewe, matokeo yake hizi taasisi zinazoundwa kama *STAMICO* na nyingine zinafanya kazi kama Idara ya Serikali. Tatizo hili naliona ni la msingi, naiomba Serikali ilishughulikie na kulipatia ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wachimbaji wadogowadogo ambao ni Watanzania wananyanyaswa sana na wachimbaji wakubwa ambao ni wageni. Cha ajabu, Serikali huwa haiwachukulii hatua hawa wachimbaji wakubwa na Serikali kila siku inakuwa na kigugumizi kutoa adhabu. Leo ukisikia mgodi umevamiwa na Watanzania hatua kali zinachukuliwa na pale wanapotunyima dhahabu zetu Serikali haichukui hatua. Nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Stephen Julius Masele kwa kuweza kuwatetea wachimbaji wadogowadogo, huu ndio uzalendo, umethubutu, umeweza bado kusonga mbele.

Mheshimiwa Spika, mikataba, naishauri Serikali ipitie upya mikataba na ile iliyokuwa mizuri ambayo inawapa haki Watanzania na Tanzania iendelee na ile mikataba mibovu ifutwe mara moja bila kujali mkataba wa nani na unamalizika lini.

Mheshimiwa Spika, tunao Watanzania ambao wamesoma na hawana kazi yoyote, ni bora tuwawezeshe na hii kazi waifanye wao ya kujaza mikataba pamoja na kufanya utafiti kuliko hawa

wageni ambao hawana lolote kwani 90% ya *information* wanapata kwa hawa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, Mheshimiwa Waziri tunataka tuone hii gesi inapunguza ukali wa maisha.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kwanza kumpongeza Waziri wa Nishati na Madini kwa ujasiri wake na kuthubutu kusema wazi katika hotuba yake juu ya migodi kulipa kodi ya mapato (ukurasa 106-107). Hongera sana na hakikisha hilo linatekelezwa kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, madini, nchi yetu imebarikiwa sana kuwa na rasilimali madini, hii isiwe "balaa" kwa nchi yetu bali iwe "baraka" kwa nchi yetu na watu wake.

Mheshimiwa Spika, Serikali iweke mikataba wazi, mikataba yenye manufaa kwa nchi. Sekta hii ya madini imegumbikwa na "usiri" mkubwa na wananchi kuteseka katika nchi yao.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapaswa kuwawekea mazingira bora wachimbaji wadogo, iwawezeshe kwa kuwanunulia vyombo vya kisasa ili waweze kujipatia riziki yao.

Mheshimiwa Spika, Serikali ihakikishe kupima maeneo yote ya migodi hasa migodi mipya kama

mgodi wa *Murus* Endabash *Gold Mining* Karatu. Sheria, kanuni na taratibu zote zifuatwe na mikataba iwe wazi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na baraka ya madini tuliyonayo, Serikali ihakikishe uharibifu wa mazingira unaotokana na uchimbaji wa madini unadhibitiwa.

Mheshimiwa Spika, haiingi akilini kwa mwekezaji kudai kuwa anapata hasara miaka 5 – 7 na bado anaendelea kuchimba bila kulipa kodi, hili likome mara moja.

Mheshimiwa Spika, kwa habari ya gesi, chondechonde, Serikali isitoe msamaha wa kodi. Baraka ya kuwa na Gesi kwa nchi yetu ni ukombozi tosha kwa uchumi wetu na kwa maisha ya Watanzania. Naitaka Serikali kuhakikisha kuwa mikataba inayofanywa katika mradi huu wa gesi iwe na tija/manufaa kwa Watanzania, angalizo, tusije tukafanya kama kwa madini.

Mheshimiw Spika, nishati, nampongeza Waziri na timu kwa hatua wanazochukua kusafisha Wizara, *keep it up.*

Mheshimiwa Spika, umeme ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi katika nyanja zote. Napenda Serikali iniambie ni lini itakamilisha upelekaji wa umeme Endamarariek, Karatu kazi ambayo inafanywa kwa namna ya ajabu. Wananchi walijitolea kuchimbia nguzo na hatimaye *TANESCO* ilifunga nyaya mwanzo na mwisho wakaacha sehemu ya katikati na mara zote

wamekuwa wakidai watakamilisha hadi leo bado haujakamilika.

Mheshimiwa Spika, *REA*, napenda kujua ni lini Serikali itapeleka umeme Tarafa ya Mbulumbulu wakati ambapo *REA* ilishafanya upembuzi yakinifu kuhusu upelekaji wa nishati hii Mbulumbulu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali kutumia nishati ya umeme wa upepo na umeme wa jua (*solar pawer*) hasa kwa shule zetu za Serikali za Kata na Zahanati katika vijiji vyetu. Serikali iwekeze zaidi katika eneo hilo.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Waziri, Manaibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa kuandaa hotuba hii na kuleta hapa Bungeni. Kwa dhati, napongeza kazi nzuri ambayo imeanza kuonekana ndani ya Wizara hii chini ya Profesa Sospeter Muhongo, mtaalam na *professional* na wasaidizi wake. Wote tumpe nafasi aweze kutekeleza mipango mizuri iliyopangwa na kusaidia Watanzania. Huyu ni mtendaji sio mwanasiasa.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukiomba miaka yote hapa Bungeni Serikali ilete mikataba mikubwa kama vile umeme, madini, gesi, makaa ya mawe Wabunge tupate fursa ya kuipitia ili ilete tija kwa Watanzania. Ni kwa nini Serikali bado inafanya mikataba hii kuwa siri? Kwa nini mikataba muhimu kama hii inakuwa siri hata kwa wawakilishi? Ni nini kinafichwa huko?

Mheshimiwa Spika, Serikali baada ya kuunda timu ya kuunda Tume ya kuangalia mikataba ya madini hapa nchini, ilibadilisha sheria/marekebisho ya vipengele vya sheria kwa lengo la kufanya sekta ya madini inufaishe Taifa na Watanzania wote. Serikali ieleze ni kwa nini viwango vipya vya mrahaba wa madini vilivyopendekezwa kisheria havijatekelezwa mpaka leo 2012? Sheria iliainisha jinsi ya kuwezesha wachimbaji wadogo waweze kuchimba kitaalam na kunufaika na kazi wanayoifanya, kuwapimia maeneo yao ya uchimbaji mdogomdogo na kupatiwa hati miliki. Ni kwa nini mpaka leo bado wachimbaji wadogowadogo wanahangaika na kulalamika kuondolewa kwenye maeneo yao?

Mheshimiwa Spika, kuna kikundi cha wachimbaji wadogowadogo wako Ilejoa, Tarafa ya Ulyankuru, Urambo, wamepewa leseni za utafiti kwa miaka zaidi ya sita. Mwaka 2010 walipoanza kuchimba madini wameingia viongozi wakubwa wamepewa leseni kwenye eneo hilohilo wakiongozwa na Mbunge wa eneo hilo na sasa wale vijana wanaambiwa waondoke. Wizara imewanyima leseni ya kuendelea na uchimbaji kundi la Tumaini. Ni kwa nini Wizara inatoa leseni mpya ndani ya eneo ambalo lina leseni nyingine ya uchimbaji?

Mheshimiwa Spika, pamoja na nchi yetu kugundulika madini ya *uranium* katika maeneo mengi kama Bahi, Kondoa, Namtumbo, na kadhalika, bado kama Taifa hatujapenda kuingia kwenye utafiti na uchimbaji wa *uranium* kwa manufaa ya Taifa. Hatuna utaalam wa kutosha (*capacity building*) kwa watu

wetu hapa nchini kuweza kuingia kwenye *exploration* ya madini hayo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inategemea zaidi wawekezaji kutoka nje kuja kuwekeza kwenye uchimbaji. Tunao uzoefu wa kutosha kwa jinsi ambayo migodi ya almas, dhahabu, tanzanite na kadhalika inavyodhulumu haki za Watanzania. Wakati madini yakivunwa na kusafirishwa nje, wanaoishi kuzunguka migodi yote ni maskini wa kutupa. Je, hili sio somo tosha kwa Serikali iliyoko madarakani?

Mheshimiwa Spika, ni nini kinachoisukuma Serikali kukurupuka hadi kwenye hifadhi zetu kuanza uchimbaji wa *uranium* wakati ikijua fika hatuna uwezo wa kusimamia? Je, Serikali inataka kuchimba kila kilichoko ardhini kwa wakati mmoja huu sio ulafi?

Mheshimiwa Spika, kuanzia Awamu ya Kwanza ya Rais, marehemu Mwalimu Julius K. Nyerere alijua tunazo rasilimali nyingi sana ardhini kama madini, gesi, mafuta na kadhalika, kwa nini Serikali baada ya kujifunza kutokana na makosa isijikite kwanza kujenga uwezo wa ndani? Tuwe na wataalam *professionals* ndani ya nchi yetu watakaosimamia rasilimali zetu kwa manufaa ya Taifa hili?

Mheshimiwa Spika, matokeo ya gesi, umeme, mafuta ya taa, moto poa kuwa ghali sana na hivyo wananchi wengi kushindwa kutumia kama nishati, ni hatari sana kwa uhai wa misitu yetu. Asilimia 80% ya Watanzania wanatumia mkaa kupikia wakati *speed* ya kupanda miti ni ndogo sana na hata ikipandwa

inakauka kutokana na kukosa mvua ya kutosha. Gesi kg.15 ni Tshs.65,000 – 75,000, tunaelewa vipato vya watu wetu. Serikali ipunguze bei ya nishati za kupikia kunusuru nchi na jangwa.

**MHE. ABDALLAH SHARIA AMEIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa Mbunge wa Bunge hili. Pili, napenda kuipongeza Wizara hii na Mawaziri na Katibu Mkuu wake kwa kazi nzuri na kubwa ndani ya Wizara hii kwa faida ya nchi kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi ninaomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, kwa sababu Wizara hii chini ya uongozi mpya, unaonekana uko tayari kufanya kazi kwa ajili ya wananchi na kuimarisha Chama changu cha CCM.

Mheshimiwa Spika, ninamuomba Mheshimiwa Waziri aendelee kuwabana viongozi watendaji wasiofaa kwa manufaa ya wananchi wa Tanzania, hasa wafanyakazi wadogo kwani hawa ndio chachu ya matatizo ya *TANESCO* kuonekana Shirika hili kuwa halifai mbele ya Watanzania kwani wao ndio madalali kwa wakubwa wao katika kutengeneza rushwa za kila siku katika Shirika *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi, nampongeza tena Waziri kwa kazi nzuri aliyoifanya kwa kipindi kifupi. Namwombea Mwenyezi Mungu aendelee kuwapa hekima Mawaziri wetu wote wa Wizara hii na Mtendaji Mkuu wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri kuangalia kwa jicho la huruma umeme vijijini, hizo shilingi bilioni tatu zilizookolewa *TANESCO* zipelekwe kwenye mradi wa umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni vituo vya kuuza mafuta kufunguliwa bila utaratibu maalum. Ukiangalia maeneo ya Kibaha, Dar es Salaam na Morogoro Mjini hasa maeneo ya kituo cha mabasi ya Msamvu, utaona kumekuwepo na vituo vingi ambavyo vinahatarisha usalama wa watu wanaofanya shughuli karibu na maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, inashangaza kuona vituo vya mafuta vimelundikana eneo moja wakati maeneo mengine hasa Mikoani hakuna vituo vya kutosha. Mfano mzuri ni kipindi cha mgogoro wa mafuta ambapo magari mengi yaliyokuwa yanayofanya safari ndefu za Mikoani mfano Singida – Dar es Salaam, yalipata tabu kwani vituo vilivyoko barabarani ni vichache sana ukilinganisha na vile vilivyokuwa Kibaha na Morogoro Mjini na kusababisha abiria kupata matatizo. Nashauri uwekwe utaratibu maalum wa utoaji wa vibali kwa wanaotaka kuanzisha vituo vya mafuta hii ni kuepuka mlundikano wa vituo vya mafuta.

Mheshimiwa Spika, pili, kasi ya kuandaa sera, sheria na *gas master plan* iongezwe ili Watanzania waweze kutoa maoni yao na kujiridhisha namna wakavyofaidika na rasilimali ya gesi. Aidha, wananchi wahamasishwe kuwekeza kwenye sekta ya gesi na kununua hisa kwenye sekta ya gesi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa umeme ni muhimu katika kuinua uchumi wa Tanzania, nimefurahishwa sana na *plans* za kutekelezwa kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Mufindi Kusini ndilo Jimbo pekee linalozalisha nguzo za umeme nchini lakini vijiji vyake vingi havina umeme. Naomba umeme katika vijiji vya Mbalamaziwa – Malangali hadi Ihowanza; Mtambula – Kiliminzowo – Iramba; Ihomasa – Udumuka – Kilolo; Nyigo – Ihawaga; Rugolofu; Nyololo - Maduma – Matanana - Bumilayinga. Naiomba sana Wizara kwa vijiji hivyo vilivyovitaja hapo juu ni muhimu sana kuwa na umeme. Pia Rais alipotembelea Jimbo la Mufindi Kusini aliahidi kuwa vijiji vya Mbalamaziwa – Malangali - Ihowanza watapewa umeme.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PHILIPA G. MTURANO:** Mheshimiwa Spika, Profesa Muhongo, Mheshimiwa Maswi, Mheshimiwa Masele na Mheshimiwa Simbachawene, kazeni buti, kazi yenu imeonekana kwa muda mfupi tu mliokabidhiwa Wizara. *Big up,* tuko nyuma yenu,

msiogope vitisho, tunawaombea kila iitwapo leo, *big up!*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Spika, katika kuchangia, nimegawa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu nishati, kwanza napenda kuchangia kuhusu umeme. Bajeti ya *REA* (Sh.157 bilioni) iongezwe, ni ndogo sana. Naipongeza *TANESCO* kwa kupunguza gharama ya kuunganisha umeme hasa katika maeneo ya vijiji. Hii itachochea kukua uchumi vijijini, itasaidia viwanda vidogo kuanzishwa vijijini, shule na zahanati zitapata umeme kwa ajili ya maabara na majokofu.

Mheshimiwa Spika, pili ni gesi, bei ya uzalishaji na usambazaji wa gesi idhibitiwe ili kuzuia ubandishaji na kuhujumiwa bei na "*supply*" ya gesi.

Mheshimiwa Spika, tatu, ni mafuta, bei ya mafuta ya taa ilipandishwa kwa ajili ya kudhibiti uchakachuaji wa mafuta, hili linatekelezwa. Kwa hiyo, bei ya mafuta ya taa itazamwe upya ili kupunguza matumizi ya mkaa.

Mheshimiwa Spika, nne, makaa ya mawe, naishauri Serikali kuwekeza katika kampuni ya Kiwira ili kuwapatia wananchi bidhaa hii ya umeme kwa bei rahisi.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ambayo napenda kuiongelea ni kuhusu madini. Naishauri Serikali katika kutoa leseni ama kutafuta au kuchimba madini, ishirikishe Halmashauri ya Wilaya ya eneo husika pamoja na Serikali ya kijiji kupata uhakika wa umiliki wa ardhi na kulinda uharibifu wa mazingira. Mapato yanayotokana na leseni yasitufanye tukaharibiwa mazingira. Sheria ya Madini, Ardhi na ile ya Serikali ya Mitaa zinahitaji kuoanishwa (*harmonized*) ili kuondoa mgogoro uliopo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itekeleze uamuzi wake wa kukataza kusafirishwa madini yasiyosafishwa (*unprocessed raw minerals*) hasa dhahabu na *tanzanite*.

Mheshimiwa Spika, mwisho, idadi ya wanafunzi 30 – 50 wanaotegemewa kusomeshwa katika fani ya gesi ni wachache sana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Muhongo na Manaibu Mawaziri, Simbachawene na Masele, mnafanyakazi nzuri.

**MHE. SUSAN L.A KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, napenda nipate majibu ya Serikali, je, ni mkakati gani unaofanywa na Wizara wa kuhakikisha Watanzania wanapewa elimu/taarifa za rasilimali za madini mbalimbali zilizopo katika maeneo yao?

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kushusha umeme kwa Kata 23 za Wilaya Kilombero, Wilaya ambayo ina miradi/migodi miwili (2) ya umeme na

mingine inayotarajiwa kuanzishwa lakini Kata takribani 15 hazina umeme na zilizo na umeme ni baadhi ya vijiji.

Mheshimiwa Spika, katika mradi wa kilimo Morogoro Kusini Mashariki, Kata ya Pangawe ambapo unaendeshwa na Wakorea, ziko tetesi kwamba kuna madini na wanachimba bila Serikali kujua, naomba Wizara ifuatilie.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kilombero pamoja na kuwa na migodi miwili (2) ya umeme, lakini Halmashauri haipati mrahaba wowote. Naomba majibu kama Halmashauri inastahili au la.

Mheshimiwa Spika, Jimbo/Wilaya ya Kilombero, ni Wilaya iliyoteuliwa na Rais kuwa ghala la chakula. Hivyo ni muhimu sana kupatiwa umeme ili wananchi wanaozalisha nafaka waweze kusindika na kukuza kipato.

Mheshimiwa Spika, kwa mara ya kwanza nawapa pongezi Waziri Mheshimiwa Muhongo na Katibu wa Wizara, Ndugu Maswi kwa utu na uzalendo wao katika kuokoa kodi za Watanzania zilizokuwa zinaliwa na mafisadi. Mungu awabariki na awape ujasiri, lakini muikumbuke Wilaya ya Kilombero katika kuwashushia umeme ambapo wamebaki kuangalia nguzo tu kwa miaka mingi. Watanzania wanateseka muwaokoe.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii kupongeza uteuzi wa Waziri mpya wa Nishati na Madini, pamoja

na Manaibu Waziri wawili (2), naamini wataitendea haki Wizara hii muhimu kwa mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kuchukua fursa hii kupata ufafanuzi toka kwa Waziri juu ya maagizo yaliyotolewa na Naibu Spika wakati wa majumuisho ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, maagizo husika yalitaka Wizara ya Nishati na Madini, wakati wa kupitisha makadirio ya mapato na matumizi itoe maelezo juu ya mkataba ulioingiwa tarehe 23 Machi, 2007 kati ya *Uranium Resources PLC* na *Western Metals Limited* na *Game Frontiers of Tanzania Limited*. Mkataba ambao, pamoja na mambo mengine unamhalalishia *Game Frontiers Limited* kupata malipo toka kwa makampuni yanayofanya utafiti katika kitalu cha uwindaji katika kijiji cha Mbarang'andu. Nikiamini Wizara ilipata muda wa kulipitia suala hili kwa umakini mkubwa hivyo kuweza kutoa ufafanuzi stahiki kwa Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa, mmiliki wa kampuni ya *Game Frontiers of Tanzania,* Ndugu Mohsin M. Abdallah, ni mmoja kati ya watu waliotajwa na Tume ya Kuchunguza Kero ya Rushwa Nchini, iliyokuwa ikiongozwa na Jaji Joseph Sinde Warioba wakituhumiwa kuwa washirika wa kulipwa katika rushwa kubwa na ukwepaji mkubwa wa kodi.

Mheshimiwa Spika, tatu, napenda kuchangia kuhusiana na gharama kubwa ambazo Wizara inatumia kwa kukodisha/kutumia Mawakili binafsi. Niungane na mapendekezo ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, wa kuitaka Serikali itoe msimamo

juu ya ushiriki wa Mkono & *Company Advocates* ambao huligharimu Taifa hili mabilioni ya shilingi kwa mwaka. Halikadhalika, naomba Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge hili Tukufu, kampuni binafsi ya Mkono *& Company Advocates* ambayo inasemekana ilianza kazi ya ushauri kwa *TANESCO* dhidi ya *IPTL* tokea mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2010 Bunge hili Tukufu lilipiitisha Sheria ya Madini, ambapo pamoja na mambo mengine, sheria husika pamoja na mambo mengine, ilizungumzia suala la machimbo ya vito katika vifungu 8(3) na 8(4) na kutoa mamlaka ya uchimbaji madini husika kwa wazalendo (Watanzania) na pale ambapo utaalam na uwekezaji mkubwa sana unahitajika kuwe na ubia (50/50) baina ya Watanzania na wageni. Taarifa zilizopo zinaonyesha kwamba kampuni ya *Tanzanite One* inakaribia kumaliza muda wake wa mkataba, naomba kauli ya Serikali kuhusiana na utekelezaji wa sheria husika.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni jambo la kawaida sana kwa watu kuhodhi maeneo makubwa yenye madini pasipo kuyaendeleza. Naomba Wizara kwa kuwa imejitabainisha kama ni Wizara ya uwazi na ukweli ituletee orodha ya watu wote wenye leseni za uchimbaji nchini, lakini hawajayaendeleza.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia kuhusu mikataba mibovu, nashauri Serikali (Waziri na Manaibu wako) mpitie kwa upya mikataba yote ya madini na mfanyie kazi taarifa zote za kamati ambazo zimewahi kukusanywa juu ya

sekta ya madini na mfanyie kazi mikataba yote mibovu mtupilie mbali kwa maslahi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, pili ni nguzo za umeme, nashauri Serikali msiuze nguzo za umeme kwa wananchi, muwakopeshe ili wengi waweze kuvuta na kuunganisha umeme kwenye nyumba zao.

Mheshimiwa Spika, tatu, *REA* (umeme vijijini), bado Watanzania 86% hawana umeme hususan vijijini. Mheshimiwa Waziri mpango huu wa umeme vijijini utatekelezwa lini kwa vijiji visivyo na umeme? Wakati wa majumuisho tuambiwe ni fedha kiasi gani zimetengwa kwa ajili ya *REA* ikiwezekana tuambiwe katika bajeti hii ni vijiji vingapi vitapatiwa umeme mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, nne, ofisi za *TANESCO*, nashauri isibaki kwenye Makao Makuu ya Mkoa kwani wananchi wote wanashindwa kusafiri kwenda Makao Makuu ya Mkoa. Nashauri *TANESCO* wafungue ofisi kila Makao Makuu ya Wilaya ili kurahisisha ulipaji wa bili za umeme ili kupunguza gharama za nauli kwa Watanzania.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, napenda kwanza kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii na Manaibu wake pia Katibu Mkuu, kwa kazi nzuri za kukabiliana na changamoto zilizomo kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo ya awali hapo juu, napenda kushauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mosi, naiomba Serikali kuwa makini sana na tasnia ya gesi na mafuta kwani nchi nyingi hapa duniani wamejikuta badala ya kuwa chanzo cha uchumi, mafuta na gesi yameleta adha na usumbufu kwa wananchi kukosa amani. Ni vyema tuwe makini, wasikivu na waelekevu kwa maoni na matakwa ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, pili, Wizara ya Nishati na Madini ifanye "*advocacy*" ya gesi kwa wananchi wa Mikoa ya Kusini yaani Mtwara na Lindi juu ya kiasi cha gesi kilichopo, umuhimu wa bomba la gesi kulipeleka Dar es Salaam na kwa vipi Mtwara/Lindi bado watanufaika na rasilimali hiyo. Haitoshi kwa viongozi pekee wa Mtwara kupata uelewa kama ilivyofanyika kwenye Baraza la Ushauri la Mkoa (*RCC*) siku chache zilizopita na kuacha wananchi bado hawajui mengi. Ni lazima Wizara iongeze wigo wa kutoa uelewa kwa wananchi huku viongozi (sisi) wa Mkoa wa Mtwara tukishiriki kuwaelimisha wananchi.

Mheshimiwa Spika, tatu, *TANESCO* ni chanzo kikubwa cha matatizo ya Wizara hii. Dawa yake ni Wizara kuisimamia kwelikweli na pia kuanzisha Shirika lingine la Umma ili lifanye kazi kama *competitor* na hivyo kuzalisha ushindani wa maendeleo. Shirika hilo liwe la kizalendo na litakalojikita vijijini tu kwa sasa pengine "*REA*" ingefaa pia kufanya kazi ya *TANESCO* vijijini.

Mheshimiwa Spika, nne, katika mapango wa usambazaji umeme katika Mikao ya Mtwara na Lindi,

napenda kupata orodha ya vijiji vya awali vitakavyoanza kunufaika na mradi huu kwa ajili ya rejea mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja hii huku nikiwatakia viongozi na watendaji wa Wizara hii ufanisi wa kimaendeleo, ahsante sana.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze mchango wangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini yeye na Manaibu wake na watendaji wake wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya na kusimamia kwa umakini mkubwa vyanzo vingi vya umeme vilivyopo Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba Serikali ifanye haraka kuandaa Sera ya Madini kwani vinginevyo hali ya madini yetu Tanzania itaendelea kudhoofika.

Mheshimiwa Spika, mikataba mibovu ipitiwe tena kwa ajili ya uhakiki, lakini ikiwezekana iandikwe upya ili kuondoa huu utata uliopo kwani inawezekana wizi huu ukaendelea.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kupunguza gharama za kuunga umeme, tunaipongeza sana Wizara ila naomba basi ile kazi ya kusambaza umeme vijijini iongezeke ili Watanzania waishio huko nao waweze kufaidika na huduma hii kama wenzao. Pia naomba sana ile gharama ya matumizi ya umeme (bei ya umeme) basi ipunguwe kwani imepanda kiasi ambacho watu wengi watashindwa kumudu huduma

hii, tafadhali Mheshimiwa Waziri tuendelee kuwasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, suala la wachimbaji wadogowadogo, naomba tuwasaidie ili nao waweze kujikomboa kwa kupata stahili zao ipasavyo kwani wanasumbuliwa sana na hawa wawekezaji wakubwa.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Lindi, ni Mkoa wa mwisho katika maendeleo ya miradi lakini hatupaswi kuwa wa mwisho, hii inatokana na ubaguzi wa miradi ya umeme iliyopelekwa ikilinganishwa na Mikao mingine. Katika hotuba ya ofisi ya Waziri Mkuu, ukurasa wa 37 ambapo unaelezea kwamba Serikali imepeleka umeme vijijini katika Mikoa 16, Lindi na Mtwara haipo je? Kulikoni!

Mheshimiwa Spika, kwa mtazamo huo, inakatisha tamaa kuona Lindi ipo nyuma katika kila mradi, inasikitisha! Kwa mfano, tunahitaji umeme Nanganga – Nachingwea; Nanganga – Ruangwa; Ngongo – Milola; Nachingwea – Liwale; Nangurukuru – Liwale; Nangurukuru – Mbwemkulu na Mchingwa – Kitomanga. Maeneo haya niliyoyataja, yanaunganisha barabara za Mikoa hiyo, zinaleta changamoto ya maendeleo hivyo naomba Wizara itoe kipaumbele ili kuwe na ufanisi katika maendeleo haya ya pamoja.

Mheshimiwa Spika, madini, Mkoa Lindi, napenda kutoa angalizo kubwa kutokana na ofisi ya Kanda ya

Madini kuwa Tanga kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara. Naomba ibadilishwe iende Lindi au Mtwara kurahisisha kazi ya utoaji leseni.

Mheshimiwa Spika, watendaji wa Wizara kujihusisha na ufisadi wa kugawa vitalu kwa wageni na wao kuwa madalali wa vitalu, kama Wizara haitakuwa makini, nchi itaingia kwenye hasara kubwa. Kitendo cha wageni kupewa maeneo kinyemela na wengi wao kuwa vinara wa uharibifu na kuipeleka nchi kubaya.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani kwa kumalizia na kuunga mkono hoja.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Profesa Sospter Muhongo, Naibu Waziri, Mheshimiwa George Simbachawene na Mheshimiwa Stephen Masele, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kuwasilisha bajeti ya Wizara yao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni nyeti na ina changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo wamekuwa na matatizo makubwa kutokana na changamoto nyingi sana wanazokumbana nazo katika mradi wa uchimbaji. Ni vyema Serikali ingeanzisha mfuko ambao ungeweza kuwasaidia katika kupata mitaji na kununua vifaa vya uchimbaji.

Mheshimiwa Spika, vilevile wachimbaji hawa wadogo hawana elimu ya kutosha ya kuendeleza miradi yao. Hivyo Serikali ingetenga pesa kwa ajili ya kusaidia kuwapatia elimu.

Mheshimiwa Spika, pia wachimbaji hawa wanakabiliwa na tatizo kubwa la kuvamiwa na wachimbaji wakubwa na mbaya zaidi wapo wawekezaji wenye maeneo mengi na bado hawafanyi kazi yoyote. Hii inawanyima fursa wawekezaji wadogo ambao ni wazawa.

Mheshimiwa Spika, Shirika la *TANESCO* linakabiliwa na matatizo makubwa sana hasa wananchi kulilalamikia sana Shirika, kwanza kukatikakatika bila taarifa kwa umeme, kuongezewa gharama za bili kwa malipo ya umeme, kuna baadhi ya watendaji wamekuwa na mtandao wa kulihujumu Shirika kwa kuwaunganishia umeme visivyo halali, kunapotokea tatizo la hitilafu katika eneo fulani ukitoa taarifa huduma haipatikani kwa uharaka.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali ingeangalia gharama za kufunga umeme katika majumba yao. Wananchi wengi wanashindwa kutumia huduma hii kutokana na gharama kubwa na usumbufu wa kupata huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, pengine Serikali ingelenga kutumia rasilimali tulizonazo kama milingoti ya umeme. Wilaya ya Mufindi katika Mkoa wa Iringa kuna msitu ambao unatoa hiyo milingoti, je, ni kweli milingoti hiyo ikitoka nje ya nchi ni bei rahisi kuliko inayotoka hapa

kwetu? Ni vyema sasa hili lingeangaliwa ili kuendelea kukuza uchumi kwa kutunza rasilimali zetu wenyewe.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Nishati vijijini – REA ilianzishwa, lengo kubwa ilikuwa kuboresha, kuhamasisha na kuwezesha upatikanaji wa matumizi ya nishati bora vijijini. Pamoja na mpango huu mzuri, Serikali ingekuwa na mkakati wa kuhakikisha vijiji vyote vinapata umeme. Sababu vijiji vingi sana havina umeme na hata havina uhakika kama lini umeme utafika na bajeti ya Wakala huu iongezwe ili waendelee kufanya kazi kwa kasi zaidi.

Mheshimiwa Spika, madini, kwa kuwa nchi yetu imeanza kuzalisha gesi tena ya kutosha, je, gesi hiyo inayozalishwa ni kiasi gani na kiasi gani kinafika kutoka inapozalishiwa hadi Ubungo kwenye mitambo? Kwa sababu gesi nyingi inapotea njiani wakati wa kuisafirisha hadi kwenye mitambo Ubungo.

Mheshimiwa Spika, je Serikali haioni ilishauriwa vibaya na wataalam, kwani umeme ungezalishwa palepale jirani na sehemu inapozalishwa gesi ili yenyewe isafirishe umeme badala ya kusafirisha gesi? Je, haioni kama umeme ungeanzia kule inakotoka gesi vijiji vingi vingefaidika kwa kupata umeme?

Mheshimiwa Spika, niwapongeze Waziri, Katibu Mkuu na timu yake kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kipindi kifupi toka wapate madaraka.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza sana Profesa Muhongo, Waziri wa Nishati na Madini pamoja na Manaibu Mawaziri wake na uongozi mzima wa Wizara hii kwa hotuba nzuri sana na naunga mkono.

Mheshimiwa Spika, nianze mchango wangu katika eneo la umeme. Nchi hii imekuwa na mgogoro wa mikataba iliyoingia na nchi hii katika kutafuta umeme wa dharura, je, dharura huwa ya miaka mingapi? Naomba sana Profesa uone namna ya kuifuta mikataba hii ambayo si endelevu, mkataba wowote kama hamna namna ya kutoka au kuisha basi huo ni mkataba mbovu na ifike muda tuachane nayo.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Umeme Vijijini liende Mikoa yote, tupewe ratiba ya vijiji vyangu vya Jimbo la Njombe Magharibi vikiwemo Ulembwe, Egagala, Makoga, Kipengale, Wangana, Uhekule, katika Tarafa ya Imalinyi, vijiji vya Itulalumba, Ihanja, Dulamu, Palagawamu, Kirinto, Kanani, Mambegu, Ludunga zikiwemo sekondari za ulembwe, Makuga, Philijio Magula, Wamike, Ludunge na Ilembula.

Mheshimiwa Spika, naomba *REA* wafike Wilaya mpya ya Wagungumbe na hasa Makao Makuu ya Wilaya hiyo ya Igwachanya na watupe ratiba ni lini umeme utapatikana katika vijiji hivyo na Makao Makuu ya Wilaya ambapo umeme upo hauna nguvu na sasa ni mji, maeneo mengi hayana umeme. Pia pale Ilembule ni mji mdogo, maeneo mengi hayana umeme.

Mheshimiwa Spika, eneo la madini nalo lina mengi yanatakiwa kufanyiwa kazi. Mikataba ya uchimbaji madini iwe yenye maslahi kwa Taifa kuliko kuwa kwa kikundi kidogo. Napendekeza mikataba hiyo ipitiwe upya kwa lengo la kuboresha na kulinda maslahi ya Taifa.

**MHE. ABDULSALAAM SELEMAN AMER:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri kwa uteuzi weo huu katika Wizara nyeti yenye msukosuko katika kuendeleza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwao ni kukaza buti, kwa juhudi wanazozifanya katika Wizara hii na Mwenyezi Mungu awalinde.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kuhusu *REA*, naomba waibane Wizara ya Fedha kupata pesa ambazo Bunge lilipitisha katika kodi ya *kerosene* ili waweze kufanya kazi yetu vizuri kupitia *REA* ili wananchi walio vijijini nao wapate haki yao ya umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia *REA,* naomba sana waweze kutupatia umeme vijiji vilivyo jirani na mtambo wa Kidatu. Toka mradi huo uanze zaidi ya miaka 20 iliyopita kuna baadhi ya vijiji kama Kidogobasi, Msowero, Iwembe, Rumango, Vidunda na Kidezo. Naomba msaada wake Mheshimiwa Waziri ili wananchi waliozunguka mradi huo wapate umeme

huo. Nyaya zinapita mbele yao na kwenda Miji ya mbele, wao wanaambulia kulinda na kuona nguzo na waya zinapita mbele yao.

Mheshimiwa Spika, chonde chonde ombi langu hilo Mheshimiwa Waziri alipe kipaumbele angalau kelele za mitambo ziwapoze kwa kuwapatia umeme kwani ni haki yao kimsingi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Waziri, Naibu Mawaziri na Katibu Mkuu kwa namna Wizara ilivyoanza kushughulikia matatizo sugu ya upatikanaji wa nishati ya umeme.

Mheshimiwa Spika, miradi ya kupeleka nishati ya umeme vijijini na ile miradi ya kupeleka nishati ya umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya ni jambo la ukombozi kwa wananchi wetu. Katika sehemu hii naomba maeneo ya Sikonge ambayo kwa muda mrefu yamekuwa yakiomba nishati hii bila mafanikio mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara iangalie eneo la Kiyombo lililoko Kata ya Kipiri jirani na Kata ya Mgandu Wilaya ya Manyoni.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa upo mradi unaoendelea pale Mgandu, naiomba Wizara iweke uendelezo wa mradi huu kwenye maeneo yote mpaka Kilumbi, Mwamagembe na Rungwa.

Mheshimiwa Spika, eneo la Tarafa ya Sikonge, naiomba Wizara iangalie uwezekano wa kushusha umeme maeneo ya Mpombwe, Mkolye na Mlogolo kwenye njia ya kuelekea Sikonge toka Tabora. Aidha, Kata ya Chabutwa na Ipole pamoja na Kata ya Mibono na Usunga ni maeneo ya Kata zenye mahitaji ya nishati hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, niiombe Wizara Kata ya Mole ipelekewe umeme kama ambavyo Serikali imekuwa ikiahidi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. PROF. PETER MSOLLA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Manaibu Waziri, katibu Mkuu na Wakurugenzi wa Wizara kwa kuwasilisha bajeti nzuri na yenye kuleta matumaini kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, aidha, naipongeza Wizara kwa dhati kwa kupunguza gharama za uunganishaji umeme kwa asilimia kubwa jambo ambalo lilikuwa ni tatizo kubwa kwa Watanzania walio wengi na hususan wale waishio vijijini.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kuna tatizo la baadhi ya wananchi wanaojiunganishia umeme majumbani bila kufuata taratibu. Je, Wizara ina mkakati gani wa kupambana na tatizo hili ambalo sehemu nyingine vitendo hivi vimesababisha moto na kuleta hasara kubwa?

Mheshimiwa Spika, nasikitika kueleza kwamba licha ya umeme kuvutwa kutoka Iringa kwenda Kidabaga (Kilolo) mwaka 2009, vijiji saba na sekondari tatu zimepitwa bila umeme kuteremshwa. Aidha, umeme kutoka Ilula hadi Ruaha Mbuyuni, Wilayani Kilolo umekwisha vutwa, lakini umeme haujawashwa na vijiji nane havijapata umeme licha ya watu wengi kujiandikisha kupata umeme. Ni lini umeme utapatikana katika vijiji na shule hizi?

**MHE. NAOMI MWAKYOMA KAIHULA:** Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena naomba nichangie kwa uchache hoja hii ya umuhimu mkubwa kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, bila ya unafiki wa Chama au vipi naomba nipongeze sana uteuzi wa Profesa Sospeter M. Muhongo ambaye umahiri na umakini wake umejidhihirisha katika hotuba yake yenye ufasaha wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, naomba kusisitiza baadhi ya mambo ambayo yeye kama kiongozi mkuu wa Wizara hii ya Nishati na Madini anapaswa kuyazingatia katika utendaji wake wa kuikomboa nchi kutokana na janga kubwa la ufisadi wa madini na umeme.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa la uchumi wa Tanzania ni uhujumu wa uchumi unaofanywa na *syndicates* ambazo zimesukwa kitaalam sana kiasi cha kufanya iwe vigumu sana kutambua nani anafanya nini na ana maslahi gani katika masuala ya mikataba.

Mheshimiwa Spika ili nchi hii upone inahitaji watu au viongozi wajasiri wa kutoa maamuzi magumu kama yaliyofanywa na Waziri kutupilia mbali makubaliano yasiyokuwa na maslahi kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, suala linalohitajika pia ni hatua zaidi ya kutambua wahujumu hawa na kuchukuliwa hatua za kuwafilisi badala ya kuwaacha tu, wawe *exposed* ili wawe mfano kwa wale wengine wanaotaka kufuata mfano wao.

Mheshimiwa Spika, suala la gesi si la mchezo tunahitaji Sera haraka na Sheria mbalimbali ili tuweze kuisimamia vizuri sekta hii.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine muhimu ni kwamba tunaomba ramani inayoonesha vitalu na mgao wake kwa watu mbalimbali, ufanyiwe mkakati wa kuipitia ikiwezekana Bunge lihusishwe katika kutengua sehemu zote za madini zilizomilikishwa bila mpangilio wa fisadi kwa wageni irudishwe kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sana kwa Taifa sasa hivi kuona kuwa vijana wetu wanafanyiwa mkakati wa kumiliki vitalu kwa kudhaminiwa na Serikali yao. Pia tuhakikishe kwamba wananchi wanaohamishwa kwenye sehemu za madini, pia wanachukua hisa katika sehemu wanazozihama na wahakikishiwe kuhamia kwenye nyumba yenye miundo mbinu ya msingi kama maji, barabara, umeme na kadhalika.

Zaidi zaidi iwe ni marufuku kuwamilikisha wageni ardhi bali wakodishiwe tu kwa kushirikiana na wazalendo.

Mheshimiwa Spika, naamini kuwa uongozi wa Mheshimiwa Muhongo utayatafakari na kuyazingatia mapendekezo niliyoyatoa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utoaji na usimamizi wa leseni za madini, Serikali inaeleza kuwa kupitia Hotuba ya Waziri shughuli za utoaji wa leseni za madini nchini zimeendelea kuimarika na kuboreshwa. Sikubaliani na Serikali katika hoja au taarifa hii kwa kuwa katika migodi mipya inayoibuka utoaji wa leseni za uchimbaji kwa wachimbaji wadogo, umekuwa na urasimu na *double standard* au *double allocation* ya *plot* za uchimbaji hivyo kupelekea wazawa au wenyeji wa eneo inapogundulika madini hawapewi nafasi za awali za umiliki wa maeneo ya uchimbaji. Mfano, wa eneo lenye matatizo kama niliyoainisha hapo juu ni eneo jipya la uchimbaji lililopo Endabash – Karatu. Tunaomba Wizara iingilie kati na kumaliza matatizo yaliyopo eneo hilo jipya la uchimbaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuendeleza uchimbaji mdogo wa madini unaofanywa na wachimbaji wadogo, mojawapo ya vyanzo muhimu vya ajira nchini hususan maeneo ya vijijini. Hivyo basi, Serikali ni vema iwape nafasi ya kwanza wachimbaji hawa wadogo leseni kwa wakati ikiwa ni pamoja kuwaanishia maeneo sahihi ya uchimbaji.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kutokana na hali ngumu ya uchumi inayowakabili vijana hawa, Serikali ianzishe Mifuko Maalum kwa ajili ya kuwapatia mitaji na mikopo wachimbaji hawa ili wapate vifaa vya uchimbaji, jambo ambalo litasaidia wachimbaji hawa katika kumudu gharama za ukodishaji wa zana, hivyo kuwafanya vijana hawa kuendelea na kazi hii ambayo huwapatia ajira.

Mheshimiwa Spika, Wizara iendelee kutoa mafunzo kwa wachimbaji wadogo ili kufahamu mbinu mbalimbali za kukabiliana na changamoto wanazokutana nazo sambamba na kuimarisha afya zao na usalama wao, hasa waweze kujikinga na maambukizi ya UKIMWI, hii ikiwa na utunzaji wa mazingira katika migodi ili kupunguza uharibifu mkubwa wa mazingira unaofanyika katika maeneo ya migodi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nishati ya mafuta, Serikali lazima ichukue hatua za dhati dhidi ya upatikanaji wa bei ya mafuta ya taa. Mafuta haya hutumiwa na wananchi walio wengi wa kipato cha chini, jambo ambalo humzidishia mwananchi mzigo mkubwa na kusababisha bidhaa za kuni na mkaa kuwa kubwa na kupelekea uharibifu mkubwa wa mazingira, Serikali ituambie ina mkakati gani wa kumpunguzia mwananchi mzigo.

**MHE. ALPHAXAD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Rais kwa kuwateua Waziri na Manaibu wachapa kazi ambao wameanza kwa

muda mfupI kuonesha kwamba nchi yetu ina mwelekeo wa kutatua matatizo ya mgao wa umeme pamoja na matatizo katika sekta ya madini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo napenda kusema yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, gharama za kuunganisha umeme Vijijini pamoja na kuwa sasa 170,000/=, bado wananchi wetu vijijini kutokana na kipato chao kuwa kidogo hawataweza kuzimudu. Nashauri kuwa wananchi waunganishiwe umeme na gharama ya kuunganishiwa ziwe zinalipwa kidogo kidogo kupitia ankara ya mwezi hadi fedha ziishe. Naomba majibu.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo wadogo Jimboni Mwibara wanahitaji semina na mafunzo ya muda mfupi kwa ajili ya kujua angalau kwa uchache, sekta ya madini ili wajue namna ya kutafuta masoko, kupata vifaa na zana za uchimbaji, taratibu za masuala ya leseni za utafiti na kadhalika. Aidha, nashauri Wizara iwasaidie kwa kuwapatia vifaa kama *crashers* na *mercury.* Naomba majibu.

Mheshimiwa Spika, umeme vijijini Mwibara ambao mmetenga fedha, ni vema mkazingatia suala la fidia kwani hatujafidiwa kwa wale ambao waliathirika wakati wa kupitisha umeme kutoka Bunda kwenda Ukerewe. Naomba majibu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo kwa juhudi kubwa aliyoionesha kwa kipindi kifupi alichofanya kazi katika Wizara hii. Nawapongeza Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu kadhalika na wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa jitihada zao za kuhakikisha kwamba wawekezaji wanakoma kutuibia katika migodi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo naomba kuchangia mambo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kuokoa sh. Bilioni 6,282,900,000/= kila mwezi baada ya uamuzi wa kuvunja mkataba wa Tanesco na kampuni ya *Oryx* na *Camel Oil.* Nawapongeza sana. Naishauri Wizara kuendelea kupitia mikataba mbalimbali ndani ya Wizara inawezekana yakagundulika mengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, madini ya urani yamegunduliwa Namtumbo, Manyoni na Bahi na hivi karibuni mradi utaanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanaozungukwa walioko kwenye maeneo yenye madini ya urani hawajaelimishwa athari za madini hayo, naiomba Serikali kwanza kutoa elimu kwa wananchi kuhusu madini ya urani kabla ya kuchimbwa kwani ni madini yenye athari kubwa kwa afya ya wanadamu, mimea na wanyama.

Mheshimiwa Spika, naomba kujua mradi wa umeme wa upepo umefikia wapi, kwani ni umeme wenye gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, umeme unaopotea njiani kutokana na uchakavu wa miundombinu ni mwingi. Serikali ina mpango gani wa kutengeneza miundombinu kabla ya kuingiza *MW* nyingi zinazotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, mradi wa kufua umeme wa *Stigler's Gorge MW* 2100 ni wa muda mrefu sana na wananchi hawaelewi ni kwa sababu gani haujaanza kutekelezwa. Bajeti ya mwaka 2011/2012 tulielezwa kuwa mradi huu utakamilika mwaka 2014. Bajeti hii ya 2012/2013, Mheshimiwa Waziri hajasema mradi huu utakamilika lini? Kama Serikali haina fedha za kutosha ni bora kuwa na miradi michache inayotekelezeka kuliko kubeba miradi mingi tusiyoweza kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, nina imani na Serikali kuwa mradi wa gesi asilia itawanufaisha wananchi bila kuzongwa na kelele za wananchi kwamba, tunaibiwa na wawekezaji. Serikali irudishe imani kwa wananchi kwamba kuibiwa na wawekezaji hakupo tena.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa sababu tulikubaliana kwamba saa tano na nusu tunawaita wanaojibu hoja kwa dakika ishirini ishirini kwa kila Naibu Waziri, halafu Waziri mwenyewe atapewa dakika 50. Hiyo itatupeleka mpaka saa saba, halafu tutaingia

kwenye Kamati ya Matumizi. Kwa hiyo, namwita Naibu Waziri Mheshimiwa Maselle.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELLE):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kusimama katika Bunge lako Tukufu. Niwatakie heri Waislam wote wanaoshiriki ibada hii ya Ramadhan Mbaraka. Pia natoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki kwa kupoteza wapenzi wao katika ajali ya meli iliyotokea 18 Julai, 2012 huko Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais Daktari Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuniamini kuitumikia Wizara hii kama Naibu Waziri wa Nishati na Madini kuisimamia sekta ya madini. Kwa mara nyingine ameonesha imani yake na jinsi anavyothamini vijana wa Taifa hili na kuidhihirisha falsafa yake ya kuwaandaa vijana kupata uzoefu wa uongozi kwa manufaa ya baadaye ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais, Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Pinda kwa maelezo na miongozo yake mbalimbali ambayo wamekuwa wakinipatia tangu nimeingia katika Bunge hili. Nimshukuru sana Waziri wangu Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo kwa kuniongoza vyema na kuhamishia uprofesa wake kwangu.

Mheshimiwa Spika, pia nimshukuru sana kwa dhati Naibu Waziri mwenzangu, kaka yangu Mheshimiwa George Simbachawene, Katibu Mkuu Eliakim Maswi, Makamishna, Wakurugenzi na watumishi wote wa Wizara kwa ushirikiano walionipa katika utekelezaji wa majukumu yangu na wamenifanya nizoee mazingira mapya ya kazi kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikupongeze wewe binafsi kwa kusimamia na kuliongoza vyema Bunge letu. Kwangu naamini kwamba wanawake na wasichana wengi hapa utaendelea kuwa mfano bora kwao. Nakumbuka ulivyonipigania nichaguliwe kuwa Makamu wa Rais kijana zaidi kuwahi kutokea katika Bunge la Afrika kabla ya kujitoa hatua za mwishoni kufuatia uteuzi wangu katika nafasi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, niwashukuru pia Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge, Mawaziri, Manaibu Waziri, Katibu wa Bunge na kwa kipekee kabisa niwashukuru Wabunge wote kwa ushirikiano wao mzuri kwangu, nasema ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mkoa wa Shinyanga ndiyo waliyoniwezesha kuwemo katika Bunge lako Tukufu, hivyo napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru kwa ushirikiano wao mkubwa wanaoendelea kunipa na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu. Naahidi kuendelea kushirikiana nao katika kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili na kuleta maendeleo ya kweli katika Mkoa wa Shinyanga na Taifa kwa ujumla. Familia yangu imeendelea kuwa mhimili mkubwa wa utendaji mzuri

wa kazi zangu. Kwa namna ya pekee napenda kumshukuru mke wangu mpenzi Pauline kwa kunipa moyo na watoto wetu Lisa na Fernando.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa nichangie hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini iliyowasilishwa jana hapa Bungeni kwa kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge, majibu yangu yatajibu hoja zilizoelekezwa kwenye sekta ya madini.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi wamechangia kwenye suala la mrabaha na mapato yote yanayotokana na sekta ya madini kwa kuwatambua, najua wengi wamechangia. Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Hamis Kigwangala, Mheshimiwa Selemani Zedi, Mheshimiwa Deogratias Ntukamazina, Mheshimiwa Daktari Mary Mwanjelwa na wengine wote waliochangia katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Watanzania wengi wamekuwa na kilio cha siku nyingi kwamba sekta ya madini pengine haichangii vizuri kwenye pato la Taifa na tungependa tupate zaidi ya hiki tunachokipata. Napenda kukiri katika Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imejitahidi kupiga hatua kubwa muhimu katika kuongeza mapato yanayotokana na sekta hii ya madini ukilinganisha na kule tulikotoka.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kwamba sekta hii hasa uwekezaji mkubwa wa madini una umri wa miaka isiyozidi 15 hapa nchini. Kwa hiyo, kweli kule mwanzo tulikosa uzoefu na sasa Watanzania wengi

wameendelea kuelewa na kujifunza na Sheria 2010 baada ya Tume ya Bomani na maoni mbalimbali ya wadau likiwemo Bunge lako Tukufu ilileta mapendekezo ambayo Sheria ile imeboresha mambo mengi ambayo kwa sasa kwa kweli yanalinufaisha Taifa kwa kiwango. Lakini sisi kama Wizara hatujaridhika bado tunataka tupate zaidi ya hapo.

Mheshimiwa Spika, mrabaha ulikuwa ukilipwa asilimia tatu ya *net,* lakini sasa tumeanza kupokea asilimia nne baada ya majadiliano na makampuni makubwa ya migodi japokuwa majadiliano hayakuwa mepesi, lakini tunashukuru vijana wazalendo wanaofanya kazi kwenye migodi hiyo kwa kuwatambua Ndugu Deo Mwanyika wa *Barrick, Vice President* Bwana Gerald na Bwana Victor kwa ushirikiano ambao wametoa katika Wizara yetu kuhakikisha kwamba Serikali kama vijana wazalendo wa Taifa hili wanatoa msaada wa kuona kwamba wananufaika zaidi katika sekta hii ya madini.

Mheshimiwa Spika, sasa Watanzania wengi wanafikiri tunapopata mrabaha asilimia nne ya *growth* ya mapato yote wanayopata wanafikiri ndiyo hicho tu tunapata. Hili tumekutana nalo sehemu mbalimbali, wanafikiri ile sasa asilimia 96 inakwenda wapi? Ina maana huyu mwekezaji anaondoka na asilimia 96. Ndugu zangu Watanzania sio hivyo.

Mheshimiwa Spika, mrabaha sio kodi, mrabaha kama vile mahari inayolipwa kwenye familia baada ya kumtunza binti na anapoolewa. Ni kama shukrani kwa maana kwamba Taifa hili limebarikiwa kuwa na

rasilimali hizo. Lakini tunazo kodi mbalimbali ambazo Taifa linapata.

Mheshimiwa Spika, ningependa Watanzania waelewe kwamba sio asilimia nne ya mrabaha ndiyo tunachokipata peke yake. Naomba nizitaje kodi zingine ambazo tunazipata kama Serikali ikiwemo *PAYE*, kuna kodi ya *withholding tax*, kodi ya zuio, kodi ya *VAT*, *stamp duty, import duty excise duty, corporate tax, income tax, road toll, local levy* na kodi zingine. Kwa hiyo, hizi kodi zingine ambazo zipo kwa mujibu wa Sheria ukizikokotoa zote Serikali inapata mpaka wastani wa asilimia 52 ya mapato yanayotokana na uzalishaji wa migodi ya hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, migodi mikubwa tangu imeanza shughuli za uzalishaji mpaka sasa imeweza kulipa Serikalini, jumla ya bilioni 951 katika Serikali Kuu. Lakini kuna suala ambalo wengi wamezungumza, nitazungumza baadaye kidogo la *service levy*. Kweli kwa mujibu wa Sheria ya mwaka 1982, *Local Government Finance Act, 1982* inaeleza wazi na kuipa mamlaka Halmashauri kukusanya mapato kiwango kisichozidi 0.3 *percent* na hiyo ndiyo Sheria mama.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa bahati mbaya kama nilivyosema inawezekana tulivyoanza, tulikuwa hatujapata uzoefu wa kutosha migodi hii ilikuwa hailipi hiyo na mgodi wa kwanza *Resolute* ulianza mwaka 1997, ukafuatiwa na *GGM* mwaka 1999, lakini kwa kipindi chote hicho hawakulipa *service levy* kwenye Halmashauri zetu, wanakofanya kazi na hoja yao

ilikuwa kwamba Halmashauri hazijatayarisha *by laws* na *GN* ambayo ilifuata mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na vikao vingi sana na migodi hii na kwa kweli kama Mheshimiwa Profesa Kahigi alivyosema kwamba sio kutoa rai tumeshaagiza na naagiza tena migodi yote lazima izingatie Sheria mama. Kisingizio cha kusema kwamba *GN* haikuwepo, *by laws* hazikuwepo, lakini hakuna *GN* na *by laws* ambazo zinaweza kufuta Sheria mama. Kwa hiyo, ni haki yetu kama Watanzania, Halmashauri zetu ni haki ziweze kulipwa madeni yote ya nyuma kama stahili yetu kwa mujibu wa Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tayari nimeshaanza mazungumzo tangu nilipoingia Wizarani mwezi wa Tano na migodi hii mikubwa napenda kukiri mazungumzo hayakuwa mepesi, yalikuwa mazito. Lakini nataka kulihakikishia Bunge lako Tukufu na Watanzania kwamba tumeweza ku-*cross deal* la *GGM* kulipa madeni yote ya nyuma tangu walipoanza. Wataalam wetu wamesha-*establish* ni kiasi gani cha pesa ambazo walikuwa wanakwepa kulipa tangu walipoanza mpaka mwaka 2005 ambapo *GN* ilitoka.

Mheshimiwa Spika, vile vile tumeweza kupata suluhisho la mgogoro uliodumu muda mrefu wa *Resolute* na ulimhusisha hasa ndugu yangu Mheshimiwa Kigwangala, amepambana kuhakikisha kwamba Halmashauri ya Nzega inapata kile kitu ambacho inastahili.

Vita hiyo tumeweza kuishinda kwa pamoja na ninawashukuru sana kwa ushirikiano walionipa katika majadiliano yale na migodi hii imeenda kukaa kwenye bodi zao kuhakikisha kuwa madeni yote ya nyuma ambayo walikuwa hawalipi kuanzia 1997 mpaka 2005 yanalipwa.

Mheshimiwa Spika, nimemsikiliza Mheshimiwa Maige, amezungumzia pia Bulyan'hulu. Nataka nimpe taarifa tu kuw, kesho nitakuwa na kikao na Bulyan'hulu kwa maana ya Barrick, kwa wembe ule ule kuhakikisha kuwa haki ambayo ilikuwa imepotea siku nyingi inapatikana. Kwa hiyo, niwahakikishie ndugu zetu kule kwenye Halmashauri kuwa, nina hakika Barrick ilitoa mfano wa kukubali kwenda mapema ku-*immigrate* kutoka mrabaha wa asilimia tatu kwenda asilimia nne na ilionekana kulaumiwa na migodi mingine. Migodi hiyo mingine nayo imekuwa ya kwanza kukubali kulipa madeni ya nyuma. Natumaini na Barrick nao watakubali kulipa madeni ya nyuma. (*Makofi)*

Kwenye Sheria Mpya ya 2010, yapo mambo ambayo yameboreshwa ambayo Watanzania wengi hawayaelewi. Huko nyuma migodi hii ilipokuja kuwekeza tukiri kuwa ni uwekezaji mkubwa sana.

**SPIKA:** Naomba jielekeze kwenye *mike*, kadiri unavyokwenda pembeni *mike* inakuwa mbali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Spika, ni uwekezaji mkubwa. Sasa migodi ilipokuwa ikija ilikuwa inaleta mkopo wa asilimia 100, kwenye Sheria mpya

tumeboresha kuwa *debit* na *equity* lazima iwe asilimia 70 kwa asilimia 30. Kwa hiyo, inatusaidia kupunguza muda wa kulipa *Corporate Tax,* kwa sababu watu wengi wamekuwa wakizungumza migodi mingi na hailipi *Corporate Tax* lakini hiyo ilitokana na *investment* ambazo wameweka pale sasa ile *payback period* inakuwa ni ndefu sana kama umekuja na mkopo wa asilimia 100. Kwa hiyo, unapopunguza mkopo kwa kutumia utaratibu mpya kwenye Sheria yetu ni kwamba, inapunguza ule muda wa *payback,* kwa hiyo, migodi mingi imeanza kulipa *Corporate Tax,* nafikiri kama kuna mgodi ambao haujalipa ni Buzwagi.

Hiyo inakwenda sambamba na kurekebisha, *reinforce,* hii migodi. Barrick zamani walikuwa wanachuliwa kama Barrick Tanzania. Kwa hiyo, kama Buzwagi imeanza leo na Bulya'nhulu imeanza zamani na inapata faida, Tulawaka au Buzwagi ikiwa inapata hasara, hasara ile inabebwa na Bulya'nhulu; kile kitu kimerekebishwa kila mgodi utasimama wenyewe. Kwa hiyo, kama Bulya'nhulu inapata faida ni faida kwa Bulya'nhulu lakini pia Sheria imerekebisha *rehabilitation bond* hasa mgodi unapokuwa unaelekea kwenye kufungwa, kunakuwa na ile *closure plan* imerekebishwa wataweka *bond* kiasi kisichopungua Dola milioni thelathini kama *security* ya Serikali ikitokea kuwa migodi ile haitafanya chochote katika uwekezaji ambapo wamechimba mashimo.

Mheshimiwa Spika, *procurement and service* tumepigia kelele sana kuwa migodi inanunua vyakula nje, mchicha na kila kitu, sasa hivi Sheria yetu inawalazimisha wanunue ndani ili kutoa kipaumbele

kwa makampuni ya ndani na kuweza kutoa *supply* katika migodi hii. Hili la *service levy* linakwenda sambamba na makampuni mengine ambayo yamekuwa yanatoa zile huduma, *sub-contracting.* Ninapenda kutoa rai kwa Halmashauri zote nchini zinazotoa huduma ndani ya migodi, zinapaswa kulipa *service levy* kwa sababu msingi wa *service levy* pia ni kuchangia huduma ambayo wanaitumia katika maeneo husika. Kama wanatumia barabara zetu, wanakanyaga, wanatumia ofisi zetu, kwa hiyo, nao wanapaswa kulipa. Nawapongeza Kampuni ya *BP* ambayo sisi Serikali tuna *share,* wao wanalipa kule Geita na makampuni mengine yote yanapaswa kulipa.

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye migodi mipya itakayoanza na kwa Sheria mpya, tumeweka kuwa lazima Serikali tutakuwa na *shares* zisizopungua asilimia 15 na hii itatokana na *powers* zetu za ku-*negotiate.* Kwa hiyo, mgodi wowote mpya utakaoanza kabla hatujatoa leseni, sisi tunakuwa na *share* zisizopungua asilimia 15 kama *free carried interest* na ambayo tutakuwa tunapata gawio mwisho wanapopata faida. Ukiachia mbali kodi ambazo tutapata Waheshimiwa Wabunge, napenda hili lieleweke vizuri na Watanzania waweze kuona tumepiga hatua kubwa sana toka tulipoanza mpaka sasa, lakini dhamira yetu kama Wizara tupate zaidi ya hapo.

Utatuzi na usuluhishi wa migogoro maeneo ya migodi: Kumekuwa na migogoro mingi sana kwenye sehemu za migodi na nimefanya ziara katika baadhi ya maeneo ya Kanda ya Ziwa na Arusha. Migogoro mingi imetokana na aidha baadhi ya watumishi wenye

tamaa ya kutaka kushiriki katika shughuli hizi za madini. Kulikuwa na mgogoro kule Ushirombo, Halmashauri ilikuwa inataka kuchukua leseni, tukaushughulikia. Kubwa zaidi, nilitaka kuzungumzia hapa tabia iliyotaka kujitokeza ya migodi kushiriki vitendo vya kuua raia.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Serikali hatuwezi kuvumilia mauaji ya wananchi yatokee na tuna wajibu wa ku-*guarantee* usalama wa Watanzania wote wanaoishi maeneo ya migodi na pia tuna wajibu wa ku-*guarantee* usalama wa makampuni ya uwekezaji. Kwa hiyo, sote kwa pamoja tumekaa vikao kuona namna nzuri ya kufanya kuhakikisha tunapata njia sahihi ya ku-*deal* na migogoro na kuuwa isiwe kimbilio la kwanza. Kwa hiyo, ndugu zangu maeneo ya Geita, Nyamongo, Mheshimiwa Nyambari Nyangwine, umekuwa ukipiga kelele sana, Amar Kassu kumekuwa na mgogoro kule wa Geita - Bulya’hulu wameingia katika eneo la Wilaya ya Nyang’hwale. Hili napenda niliweke wazi kuwa, tulipoomba taarifa katika Mgodi wa Bulyanhulu hawakutoa taarifa sahihi namna walivyokwenda kule chini kuvuka mpaka wa Kahama na kuingia upande wa Geita wakati ule ikiitwa na sasa inaitwa Nyang’hwale. Kwa hiyo, Wilaya ya Nyang’hwale inazo sababu zote za msingi za ku-*claim* haki yoyote inayopatikana kutokana na mapato kama Wilaya zingine zenye migodi.

Vijiji ambavyo vipo karibu na mgodi ule vimo ndani ya leseni ya Barrick, Kwa hiyo, tunaangalia na kesho kwenye mazungumzo yetu tutajadili namna ya kuwafidia kama Mheshimiwa Mbunge alivyopendekeza, ikiwezekana wale wananchi

wafidiwe wahamishwe pale na Nyang'hwale, kama Wilaya ianze kuangalia ni namna gani nayo itanufaika na uwekezaji ule. Kwa sababu *underground* mgodi wa Bulya'hulu umeshafika Wilaya ya Nyang'wale kwa zaidi ya kilometa moja.

Wachimbaji wadogo ndiyo imekuwa *focus* yetu kama Wizara, tunatambua mchango wa Watanzania na kuwa nchi hii itajengwa na Watanzania wenyewe. Sisi kama Wizara, ninamshukuru Mheshimiwa Waziri, ameshaelekeza kuwa lazima tuwasaidie wachimbaji wadogo wa maeneo ya Nyarugusu, Mgusu, Ushirombo, Ushokerahela, Misungwi na Igalula kule kwa ndugu yangu Mheshimiwa Mfutakamba na akina Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa Charles Kitwanga, Mheshimiwa Moza Abedi Said, Mheshimiwa Ezekiel Maige na Mheshimiwa William Ngeleja, wote wamezungumzia suala hili.

Nataka niseme kuwa, hiki ni kipaumbele chetu na tumeshaanza kuwatengea maeneo wachimbaji wadogo. Nchi yote imegawanywa, ukiangalia kwenye ramani utaona sehemu zote zina leseni. Kwa Sheria ya Madini hasa eneo la leseni ya utafiti, inapomaliza muda wake yule mwenye leseni anatakiwa aachie eneo nusu kwa Kamishna wa Madini. Kamishna ataangalia kama hilo eneo linafaa kwa matumizi ya wachimbaji wadogo, tunawagawia. Kwa hiyo, leseni zote tulizotangaza ambazo hazijatimiza masharti na ambazo tumetangaza kwa mujibu wa Sheria, ninawaomba wenye leseni hizo wafuate masharti; vinginevyo, tutazifuta kwa mujibu wa Sheria na tutazigawa kwa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu kwa eneo hilo ieleweke hivyo na ule mgogoro wa kuwa wachimbaji wadogo wanagundua halafu mwekezaji anakuja, shida kubwa pale ni elimu. Unapokuwa unamiliki ardhi haitoshelezi kuwa ndiyo tayari unamiliki leseni ya uchimbaji na haimzuii mtu mwingine kuja ku-*apply* leseni ya uchimbaji katika eneo hilo. Kwa hiyo, nawaomba ndugu zangu Watanzania, mnaoona kwenye maeneo yenu ya asili yana madini, nendeni mkaombe leseni, mnapochelewa mtu mwingine akiomba leseni ya utafiti na wewe unapokwenda kuomba unakuta tayari lile eneo kuna mtu amekwisha *apply,* utaratibu ni kuwa, anayeanza ku-*apply* ndiyo anayehudumiwa. Kwanza, ni suala la elimu; tunaendelea kuitoa ili watu waelewe kumiliki ardhi siyo leseni ya uchumbaji na kumiliki leseni ya uchimbaji siyo kumiliki ardhi. Lazima umfuate mtu mwenye ardhi mkubaliane naye na aridhike, kwa maana ya ku-*compensate* na upate *consent* yake. Kwa hiyo, kwenye suala la *compensation* kumekuwa na malalamiko mengi na hili ndugu zangu tukiri kuwa Sheria yetu ya Ardhi inafidia *surface.*

Mtu akikuta madini sehemu anaangalia kama una shamba, una mihogo, miembe, nyumba, ndiyo anafidia *surface.* Kwa hiyo, nafikiri Bunge hili na sisi Wizara tutapenda kupokea mapendekezo na ushauri tuone namna wenzetu wa ardhi wanavyoweza ku-*review* Sheria yao ili kama kuna uwezekano tuanze kufikiria na kule chini kuna nini, kwa sababu inakuwa ni kelele kuwa mtu anapisha uwekezaji, analipwa mihogo yake na chini anaacha dhahabu. Hilo

tumekwishaliona na tunalifanyia kazi, lakini zaidi, Sheria ya Ardhi inatakiwa iangalie kwenye *compensatio*n.

Mheshimiwa Spika, Udhibiti na Utoroshaji wa Madini. Mimi nilikuwa muumini wa udhibiti na utoroshaji wa madini na nilipokuwa kwenye Kamati ya *PAC* nilikuwa ninagombana sana na Kamishna. Watanzania wengi tunaamini kwamba, udhibiti ule hauko sawasawa lakini ninataka kuwahakikishia ndugu zangu kuwa, nilikuwa ninagombana kwenye ukaguzi, lakini nimefuatilia nimeona kwa umakini na ndiyo nikaja kugundua *Agency* yetu ya *TMAA*, inafanya kazi kubwa sana ya kubaini upungufu mbalimbali. Haya madeni ya nyuma tunayozungumza, *TMAA* ndiyo iliyofanya zile hesabu na kugundua *Tanzanite One* Arusha walikuwa wana-*under declare* mrababa kuanzia 2004 – 2008, jumla ya Dola za Kimarekani milioni mbili na nusu zilikuwa hazijalipwa. Hivi sasa tunavyozungumza, ninapenda kulihakikishia Bunge lako kuwa, pesa zile zimelipwa baada ya kukabana na *Tanazanite One.* Niseme tu kwamba, Mheshimiwa Kahigi alisema kuwa, tunatoa rai siyo tu rai tuko *serious* na tunakaba kwelikweli. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kengele ya pili.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, kwa heshima kubwa, ninawashukuru

sana Waheshimiwa Wabunge, kwa kipekee kabisa kwa jinsi walivyotupa nguvu ya kuchapa kazi.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa zawadi ya uhai na kuniwezesha leo hii kuwepo na kuongea mbele yenu. Kwanza, ninawatakia Waislamu wote, *Ramadhani Kareem*.

Naomba kutumia fursa hii, kuungana na Watanzania wenzangu, kuwapa pole ndugu zetu wote waliopoteza maisha katika ajali ya meli iliyotokea Zanzibar, tarehe 18 Julai, 2012. Mwenyezi Mungu, azilaze roho za marehemu wote mahala pema peponi na wale waliopata madhara waweze kupata nafuu.

Kwa namna ya pekee, naomba nimshukuru Rais wangu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, ninayeshughulikia Nishati. Ninaomba kumwahidi na niwaahidi Watanzania wote kwamba, nitakuwa mwadilifu na nitatumia umakini mkubwa katika kufanya kazi yangu na sitamwangusha Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Pia nashukuru sana kwa ushirikiano ninaopewa na mafundisho na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa malezi yake na Mawaziri wote, kwa namna wanavyonisaidia katika kutekeleza wajibu wangu. Ninapenda

kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote walioteuliwa. Kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama hap, nawapongeza na Waheshimiwa Wabunge, kwa kuchaguliwa pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru Wananchi wa Jimbo la Kibakwe, kwa ushirikiano wanaonipa na hasa katika kipindi hiki ninapotekeleza majukumu yangu ya Unaibu Waziri na Jimbo pia. Ninapenda kuwaahidi kuwa, sitawaangusha na nitafanya kila linalowezekana kuleta maendeleo katika Jimbo letu la Kibakwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, wa Vyama vyote, kwa ushirikiano wanaonipa hadi kufikia hatua hii, kwa kuniwezesha kukulia ndani ya Bunge hili. Nikiri kwamba, kisiasa mimi nimekulia ndani ya Bunge hili; nawashukuruni nyote kwa ushirikiano huu.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru wewe binafsi kwa malezi yako na hata kuniwezesha leo nikaonekana kuwa ninastahili kufanya kazi hii ya Unaibu Waziri na kumsaidia Mheshimiwa Rais. Mwisho lakini siyo kwa umuhimu, nawashukuru familia yangu yote na hasa mke wangu Mariana, kwa kunitia nguvu na ushauri katika kutekeleza majukumu yangu.

Nachukua nafasi hii ya mwisho katika kushukuru kumshukuru sana Mheshimiwa Profesa Muhongo, kwa namna ambavyo anatufanya tufanye naye kazi kwa raha sana. Ukifanya kazi na Profesa unapaswa kuwa

na kasi na kufanya maamuzi na kuthubutu kila wakati na yeye yupo tayari kukusahihisha; Mheshimiwa Waziri wangu ninakushukuru sana. Namshukuru sana pia ndugu yangu Mheshimiwa Masele, kwa ushirikiano anaonipa, lakini pia Katibu Mkuu wetu Ndugu Maswi na Makamishna wote Wizara ya Nishati na Madini, tuendelee kuchapa kazi, tumepata *support* kubwa ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaingia kwenye hoja zilizochangiwa na Wabunge, labda niseme nimetafsiri nini leo na jana, kwa muda ambao nimekuwepo katika Bunge kwa miaka takriban saba. Nimeona kitu tofauti kwamba, sasa sauti ya Mwenyezi Mungu, imejidhihirisha ndani ya Bunge hili. Kwangu mimi siyo sababu ya kujidai, siyo sababu ya kujiona, ninaweza au tunaweza Wizara yetu lakini ninaamini kupitia kwenu, Mwenyezi Mungu ameamua kujitokeza na hivyo tutajitahidi kufanya kazi kwa niaba ya Watanzania kuhakikisha kuwa wanaona ile furaha waliyoitarajia wakati wote.

Wizara yetu ina mambo mengi makubwa; ni Wizara ambayo inakamata Uchumi. Ukizungumzia umeme unazungumzia Uchumi wa Nchi. Ukizungumzia umeme unazungumzia uhai na usalama wa Uchumi. Ukizungumzia umeme unazungumzia uhai na usalama wa kisiasa na uhai na usalama wa kijamii. Kwa hiyo, umeme ndiyo kila kitu katika nchi. Wabunge wengi wamechangia kwa hisia mbalimbali; wengine wamesema mambo mengi lakini niseme tu kwamba, haya yote mliyoyasema kwetu sisi ni changamoto tupu; yote yalikuwa yanatusaidia ili kutekeleza majukumu

yetu. Kubwa kuliko yote ambalo limesemwa na Wabunge wengi ni lile linalohusu *TANESCO* na masuala ya umeme kwa ujumla; hili limesemwa na takriban Wabunge wote.

Mheshimiwa Spika, wapo waliochangia kwa kuandika, wapo waliochangia kwa kuzungumza Bungeni na wapo ambao kwa kupiga makofi tu huo ni mchango tosha, lakini wapo ambao kwa hisia zao tu utaona ni mchango tosha kabisa. Mimi ninaamini kuwa wote humu ndani mmechangia kwa kiasi kikubwa jambo hili, kwa hiyo, sihitaji hata kutaja majina kwa kuwa wote nina *register* rasmi kuwa mmesema jambo linalohusu *TANESCO* na umeme. Labda niseme mambo mawili, matatu, katika sehemu hii.

Tulipoingia pale Wizarani tukiongozwa na Mheshimiwa Profesa Muhongo, mimi nimwite jembe; tulipoanza kazi kazi yetu kubwa tulianza na *TANESCO*. Tuliwaita *TANESCO* ofisini kwetu asubuhi, mchana na jioni, lakini kila wakitueleza hatuwaelewi tukasema kuwa labda elimu tunatofautiana hapa mimi sielewi tu. Ukiuliza mapato yanayopatikana huelewi, ukiuliza kuna matatizo gani huelewi, lakini kila unapokaa siku mbili unaombwa kukubaliana na mgao wa umeme na mkizungumza mezani mgao unatoweka. Kumbe umeme wa Tanzania ni suala la kuzungumza mezani halafu mnakubaliana kuwa unakuwepo mgao au haupo; hii haikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii haiwezi kukubalika na ninaamini kwa Waziri wangu Mheshimiwa Profesa Muhongo na ndugu yangu Mheshimiwa Masele na

Katibu Mkuu Maswi, nawaambieni na niwahakikishieni hakuna kitu; wafikirie *formation* mpya, lakini kwa hilo hawawezi. Hisia zilikuwa ni kubwa zinazohusu bei ya umeme, lakini wananchi wengi na Wabunge mmefurahia sana juu ya kupunguza gharama za uwekaji umeme. Sisi tunafurahi pia, lakini jambo hili tumelifanya kwa kazi kubwa kweli kweli, limetuchukua takriban vikao 10 mpaka 15 kuzungumzia kuhusu jambo hili tunaambiwa haiwezekani, lakini tunamshukuru Mungu wa Haki leo limewezekana. *(Makofi)*

Kazi kubwa ni kututia moyo ili tuweze kulisimamia, lakini pia kuna suala ambalo Waheshimiwa wengi wamelizungumza; Mheshimiwa Anna Kilango Malecela, Mheshimiwa Joseph Selasini, Mheshimiwa Alphaxard Lugola, Mheshimiwa David Kafulila, Mheshimiwa Magale Shibuda na Mheshimiwa Ezekiel Maige kwamba tuibane *TANESCO*. *TANESCO* ndiyo kila kitu; kwa hiyo, kwa kuwa ninyi ndiyo mnaagalia *accountability* ya Serikali kama Bunge, mkituruhusu tuwe tunaingilia kwa kibali chenu kinachofanyika ndani ya *TANESCO* hatutashindwa. Umeme unaibwa *TANESCO* na wanaoiba wanajulikana hawafanywi chochote. Wizi mkubwa wa umeme acha wa vishoka, upo wizi wa kutumia mita hizi za LUKU, mtu anakuwa na *units* nyingi haijulikani anazipata wapi. Kwa hiyo, haya yote ni matatizo makubwa ambayo yapo. Nguzo zinatoka Mufindi hapa Nchini tunanunua kwa shilingi 270,000; kwa nini?

Kwa hiyo, nasema sisi tumejipanga, tunaogopa tu kwa sababu tatizo ni kubwa sana, tusije tukakurupuka,

tunaenda tukiwa *very analytical*. Tunataka twende kwa hatua, tumeanza na hatua hii lakini tutaenda kimoja baada ya kingine na ninawahakikishieni Watanzania wataonja raha ya maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nielezee suala la gesi. Suala la gesi nalo limechangiwa na Wabunge wengi kwa hisia kubwa, lakini walioongoza kwa hili pamoja na Kamati zote mbili ni Wabunge wanaotoka Mikoa ya Mtwara na Lindi, wamelisemea jambo hili sana. Wanataka kuona manufaa ya gesi katika maeneo yao. Ni vizuri nikawataja ambao ni Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa George Mkuchika, Mheshimiwa Dunstan Mkapa, Mheshimiwa Jerome Bwanausi, Mheshimiwa Anna Abdallah, Mheshimiwa Agnes Hokololo, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Mathias Chikawe, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Mheshimiwa Faith Mitambo, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, Mheshimiwa Riziki Omary Juma, Mheshimiwa Riziki Lulida, Mheshimiwa Diana Mwatuka, Mheshimiwa Maulida Anna Komu, Mheshimiwa Mariam Kasembe, Mheshimiwa Jabir Marombwa na Wabunge wengine wengi wamelizungumzia jambo hili.

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie kwamba, jambo hili Serikali imejipanga kuhakikisha gesi inasaidia Taifa, lakini gesi inayotoka Mtwara na Lindi ni lazima na maeneo ambako gesi inatoka waone utamu huo. Kwa hiyo, tuwahakikishie kwamba tumejipanga na tunatambua kuwa zipo ahadi nyingi zilizotolewa na Serikali, wakati wa kuzitekeleza sasa umefika na kama

mnabisha angalieni tunafanya nini kuanzia tutakapopitisha Bajeti yetu leo. Tusaidieni tupitishe bajeti na tunawahakikishia kwamba, tutaanza kuchukua hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawafahamisha Wabunge hawa kwamba, yaliyofanywa kule ni mambo mengi, sasa hivi tuna transfoma 37 tulizozipeleka kule, hapo tuna uhakika wa vijiji vingi sana kupata umeme. Pia vijiji vyote vinavyopitiwa na bomba lile tunataka viwe na umeme. Hapa kama Serikali hatuzungumzii suala la umeme kwamba wapate umeme, kwa sababu gesi inatoka kule tunataka tuzungumzie na miundombinu mingine yote, kama barabara na viwanda kwa ujumla wake. Kwa sababu mtu akiweka viwanda kule Mtwara ni dhahiri kwamba, ataweza kuzalisha kwa bei ndogo, kwa sababu umeme wa kule utakuwa na *special tariff.* Pamoja na hali ilivyo sasa, leo hii umeme uliopo Mtwara bado ni mwingi na tunahitaji kuuendeleza zaidi kwa matumizi na bado uchumi wa Mtwara upo chini kwa sababu bado tunahitaji kuweka viwanda. Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kwa niaba ya Serikali kutoa wito kwa wawekezaji mahali popote kwenda kuwekeza pamoja na kwamba nchi nzima panafaa, lakini Mtwara na Lindi panafaa zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, gharama ya umeme wa Kusini na mipango ya umeme kwamba *REA* haipo kule Kusini, jamani ninyi watu wa Kusini ni *Special Zone,* msizungumzie habari ya *REA.* Ninyi mnazungumzia *Special Program* ya Serikali, namna ya kupandisha hadhi na maisha ya watu kwa kupitia umeme, barabara na kila kitu. Ninawaomba sana Wabunge

wote wa Lindi na Mtwara, Jumatatu, saa saba, baada ya Bunge, tukutane ili tuweze kufundana vizuri na tuoneshane ni nini Serikali inataka kufanya katika Mikoa yenu.

Mheshimiwa Spika, lilizungumzwa pia suala la kukatika umeme katika Majimbo mbalimbali. Matatizo haya yanatokana na uchakavu wa laini na Mzee wa Vunjo na Rombo Mheshimiwa Selasini alisema hili na Wabunge wengi wamesema katika maeneo yao kwamba, sehemu hizo umeme unakatika sana. Naomba niwahakikishie kwamba, kama tutaibana mianya ya fedha inayopotea *TANESCO*, kama tutabana matumizi na mikataba mibovu na kama kweli tutahakikisha tunaifanya *TANESCO* ikae mahali panapotakiwa, marekebisho ya vitu hivi ni madogo sana na ya hela kidogo sana. Kwa hiyo, marekebisho haya yatakuja na mimi niwahakikishie kwamba, tutarekebisha sehemu zenye umeme ili uweze kutulia.

Mheshimiwa Spika, yapo mengine yaliyosemwa na Mheshimiwa David Kafulila, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Gosbert Blandes na Mheshimiwa Deogratias Ntukamazina kwamba, Mikoa ya Kigoma, Katavi na Rukwa, ule Mradi ambao tunautarajia wa njia ya *electricity five*, ninyi kule mpo salama isipokuwa tu bado Serikali hatujafikia kwenye *stage* za kupata fedha. Tungeweza kusema *stage* tulizofikia lakini siyo vizuri kusema jambo ambalo lipo kwenye *process*. Kwa hiyo, *program* ile itatusaidia, lakini itaenda sambamba na Mradi wa Malagarasi wa *42 Megawatts* na Mrongo Kigakata *16 Megawatts*. Hii itaenda pamoja katika *package* hiyo.

Mheshimiwa Spika, pia nizungumzie suala zima la changamoto za utekelezaji wa mfumo wa uagizaji mafuta kwa pamoja. Mfumo huu wa uagizaji wa mafuta umetusaidia sana Serikali katika kuhakikisha angalau tunadhibiti mapato na kupata mapato makubwa. Mfumo huu wa kuagiza mafuta kwa pamoja umeisaidia hata *TRA* kukusanya fedha nyingi za kutosha. Mfumo huu umetusaidia kudhibiti uchakachuaji, lakini pia nirudie kusema hata suala zima la vinasaba ambalo Wabunge mmelisema sana hapa.

Mkataba wa Vinasaba unaisha mwezi wa nane mwishoni; tuache uishe tukae tutafakari tutashauriana na Bunge tuone njia bora ni ipi ya kufanya, kwa sababu imeelezwa hapa na hoja hii ni ya msingi kwamba, vinasaba vinaongeza gharama ya mafuta. Hatuwezi kukataa moja kwa moja, tutaangalia *the best way.*

Mheshimiwa Spika, yapo mawazo pia katika Wizara kwamba, kwa nini tusitafute njia ya usafirishaji wa mafuta kwa kutumia *monitoring* ya magari ya *electronic.* Siku hizi teknolojia zimepanda, unaweza ukafunga vifaa na wanaosafirisha mafuta na *export* ikajulikana au *under escort*, kwa namna yoyote ile tutakubaliana lakini dhamira ya Serikali ni kupunguza gharama kwa mwananchi wa kawaida. Kwa sababu gharama ya mafuta huwa inahamia kwa mwananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, suala zima la kufufua Kampuni ya Mafuta ya *OPEC*, Serikali imeshaanza kuchukua hatua na tunadhani kufanya *downstream business* ya mafuta ni muhimu kwa Serikali. Kuwa na kampuni inayoshiriki na *Private Sector* ni muhimu kwa sababu inatusaidia kupata *information* ya *industry* ya mafuta inakwendaje, ingawa kuna gharama lakini hatua zimeshaanza kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, lilizungumzwa suala lingine la kwamba, Serikali inachukua hatua gani kuhusu tatizo la kuingiza nchini mafuta yasiyokidhi viwango. Niseme tu kwamba, *EWURA* wameshauri, *TBS* uwezo wao wa kupima mafuta kama tulivyoweza kupata taarifa mbalimbali ni mdogo, wanapima vipimo vichache tu kati ya vipimo vingi wanavyotakiwa kuvipima. Kwa hiyo, tumeshauri *EWURA* wenyewe waanzishe maabara waweze kupima wenyewe mafuta. Pia tunafikiria urekebishaji wa Kanuni za Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja ili kuhakikisha tunaziba mianya katika kutekeleza mfumo huo.

Mheshimiwa Spika, uandaji wa Sera ya Gesi tunawahakikishia kwamba, mwezi huu tisa Sera itakuwa imekamilika na mchakato wa *consultation* unaanza mapema kabisa baada ya Bunge hili. Kwa hiyo, niwahakikishie kwamba, Sera ya Gesi itakuja mapema na kwa hiyo hadi Bunge linalokuja Sheria inaweza ikawa Mezani kwa ajili ya kujadiliwa. Hapo ndipo tutakapotakiwa kusema ni namna gani tunaweza kulinda maslahi yetu.

Mheshimiwa Spika, wapo wengine wameleta dhana hapa kwamba, eti Serikali tumeshaingia mikataba mibovu. Nataka niwahakikishie kwamba, katika gesi bado hatujapoteza, tukijilinganisha sisi na nchi za wenzetu, kwa mfano, Afrika Kusini, sisi tumewazidi. Ukiangalia *fiscal regime comparison* ya kwetu sisi Tanzania ambao hatujaanza hata kufanya *production,* tupo *at 72 percent* ya *Government take*, Serikali inachopata ni 72 *percent*. Kwa hiyo, tunawazidi Afrika Kusini, tunawazidi Mozambique, tunawazidi Namibia na pengine tunaweza tukaenda zaidi ya hapo kwa sababu suala la biashara ya gesi, *investment* inapoanza inakuwa kidogo, mzani una-*balance* lakini kadiri miaka inavyokwenda na tunavyozidi kuzalisha, Serikali inazidi kuwa na hisa nyingi zaidi na baadaye inaweza ikawa na hisa nyingi kuliko hata kampuni.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tusiwe na wasiwasi hatujapoteza, *we are in 72 percent of Government take*. Tukae tusubiri Sera ije, tufikirie tuweke namna gani. *72 percent* siyo mbaya, huko kwingine Afrika Kusini wenyewe wapo kwenye *almost 30 percent*.

Mheshimiwa Spika, najua muda wangu ni mdogo na pengine siyo rahisi kujibu hoja zote. Niwahakikishie Wabunge yale maombi yao yote ya Vijiji vyao na maeneo inapopita Miradi ya *REA* na marekebisho wanayotaka, kama kuna maombi mapya, sisi Wizara yetu haina usiri, njoo tukae tukubaliane umeme upite wapi, wapi uliruka na wapi tufanye nini. Niwahakikishie kwamba, Wizara imeagiza transfoma 370, kazi ya transfoma hizo ni kwa ajili ya kutatua matatizo ya wale ambao nyaya zinapita juu. Wananchi wanauona

umeme unapita, tunataka kote kwenye maeneo hayo ambako umeme unapita juu transfoma 370 ni kushusha tu kila mahali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaamini *target* ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi itafikiwa, asilimia 30 ya Watanzania watakuwa na umeme.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuwashukuru sana, kama nilivyosema, siyo rahisi sana kutumia muda huu wa dakika 20 kujibu hoja hizi zote, maana ili nijibu hoja zote nilipaswa nisome karatasi zote, siyo rahisi sana. Kwa hiyo, niwahakikishie tu kwamba, tutatoa majibu yote, tutaweka kwenye *pigeon hall* na pengine wale Wabunge ambao wanataka kupata ufafanuzi wa mambo yao, *this Ministry should be a friendly Ministry*. Wabunge muwe na urafiki na Wizara hii; mmeanzisha ukombozi wa Tanzania katika Wizara yetu, sisi hatutawaangusha. Ni changamoto kwetu kuhakikisha kwamba, tunafanya kazi nzuri kwa Watanzania na kuhakikisha kwamba, tunakuwa karibu na Wabunge maana mmeamua kutuonesha maajabu ya Mungu kupitia Wizara yetu. Tunawaahidi huduma iliyotukuka na uaminifu mkubwa na Mwenyezi Mungu atatusaidia katika hili.

Mheshimiwa Spika, nisingependa kengele inigongee, nawashukuru Wabunge wenzangu, naomba kuunga hoja mkono. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, sasa nitamwita mtoa hoja.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kuniwezesha kufika siku ya leo ninapohitimisha hoja yangu kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2012/13.

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Selemani Zedi, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini na Mheshimiwa John Mnyika, Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Kwa namna ya kipekee kabisa naomba niwashukuru sana Wabunge wote bila kujali itikadi zetu, tumepokea, tumejadili na kutoa maelekezo kwa Wizara yangu. Maelezo na ushauri wenu ni chachu ya utendaji ambao wenzangu wanapaswa kuanza kuuekeleza mara moja.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hoja hii, Wabunge wamepata nafasi ya kuchangia kwa maandishi ambao jumla yao ni 194. Waliochangia kwa kuzungumza ni 30.

Mheshimiwa Spika, nitaanza kuwatambua kwa majina muda si mrefu, ambaye sitamtaja jina lake anisamehe kwa dhati kwani sikukusudia ila nikikumbushwa nitataja jina lake kabla sijahitimisha hoja yangu.

Mheshimiwa Spika, orodha ya Wabunge waliochangia kwa kuzungumza ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mussa Zungu Azzan, Mbunge wa Ilala, Mheshimiwa Said Bungala, Mbunge wa Kilwa Kusini,

Mheshimiwa Rachel Mashishanga Robert, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Hasnain Mohamed Murji, Mbunge wa Mtwara Mjini, Mheshimiwa Shaffin Ahmedali Sumar, Mbunge wa Tabora Kaskazini, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Christopher Ole Sendeka, Mbunge wa Simanjiro, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mbunge wa Rombo, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mbunge wa Karagwe, Mheshimiwa Hamis Missanga, Mbunge wa Singida Magharibi, Mheshimiwa Vick Kamata, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyang'hwale, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mbunge wa Jimbo la Busanda, Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangalla, Mbunge wa Nzega, Mheshimiwa Alphaxard Lugola, Mbunge wa Mwibara na Mheshimiwa Subira Mgalu, Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengine waliochangia ni Mheshimiwa Moza Abedi Saidy, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa John Shibuda Magalle, Mbunge wa Maswa, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mbunge wa Msalala, Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, Mheshimiwa Said Mussa Zubeir, Mbunge wa Fuoni, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Prof. Kulikoyela Kahigi, Mbunge wa Bukombe, Mheshimiwa Abia Nyabakari, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Joseph Kandege Mbunge wa Jimbo la Kalambo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuokoa muda na kwa kuwa Majimbo yenu mnayafahamu, naomba nisitaje Majimbo.

Mheshimiwa Spika, orodha ya Wabunge waliochangia kwa maandishi ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba, Mheshimiwa Anna MaryStella Mallac, Mheshimiwa Deogratias Ntukamazina, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mheshimiwa Nyambari Nyangwine, Mheshimiwa Hezekia Chibulunje, Mheshimiwa Abdul-Aziz Abood, Mheshimiwa Sylvester Kasulumbayi, Mheshimiwa Rebecca Mngodo, Mheshimiwa Shukuru Kawambwa, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Augustino Massele, Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee, Mheshimiwa David Kafulila, Mheshimiwa Betty Machangu, Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mheshimiwa Henry Shekifu, Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Mheshimiwa Juma Nkamia, Mheshimiwa Dkt. Kebwe S. Kebwe, Mheshimiwa Moshi Kakoso, Mheshimiwa Charles Mwijage, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Vincent Nyerere, Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Amos Makalla, Mheshimiwa Mwigulu Madelu, Mheshimiwa Hussein Nassor Ama, Mheshimiwa Vita Kawawa na Mheshimiwa Modestus Kilufi.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu, Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Dkt. Seif Seleman Rashid, Mheshimiwa

Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Edward Lowassa, Mheshimiwa Rita Mlaki, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Josephine Chagulla, Mheshimiwa Azza Hamadi Hilal, Mheshimiwa Ismail Rage, Mheshimiwa Brig. Jen. Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye, Mheshimiwa David Malole, Mheshimiwa Mariam Kasembe, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani, Mheshimiwa Sabreena Sungura, Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Abdul Jabiri Marombwa, Mheshimiwa Athumani Mfutakamba, Mheshimiwa Deo Filikunjombe, Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Mheshimwia Rosweeter Kasikila, Mheshimiwa Mary Nagu, Mheshimiwa Mary Mwanjelwa, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Assumpter Mshama, Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa William Lukuvi, Mheshimiwa Mansoor Hiran, Mheshimiwa Ignas Malocha, Mheshimiwa Joseph Kandege, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Mheshimiwa Mathias Chikawe, Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa, Mheshimiwa Dkt. Augustine Mrema, Mheshimiwa Desderius Mipata, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mheshimiwa Mch. Israel Natse, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Abdallah Sharia Amer, Mheshimiwa Sara Msafiri Ally, Mheshimiwa Mendrad Kigola, Mheshimiwa Philipa Mturano, Mheshimiwa Mustapha Akunaay, Mheshimiwa Susan Kiwanga, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Pauline Gekul, Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa Riziki Lulida na Mheshimiwa Rita Kabati.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Eng. Gerson Lwenge, Mheshimiwa Abdulsalaam Selemani Amer, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Prof. Peter Msolla, Mheshimiwa Naomi Kaihula, Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mheshimiwa Alphaxard Lugola, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Livingstone Lusinde, Mheshimiwa Tundu Lisssu, Mheshimiwa Mwanamrisho Taratibu Abama, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Mahamoud Mgimwa, Mheshimiwa Dkt. Haji Hussein Mponda, Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mheshimiwa Highness Kiwia, Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mheshimiwa Gregory George Teu, Mheshimiwa Zahra Ali Hamad, Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya, Mheshimiwa Dkt. Binilith Mahenge, Mheshimiwa Moses Machali, Mheshimiwa Albert Ntabaliba, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa Saleh Pamba, Mheshimiwa Prof. Kulikoyela Kahigi, Mheshimiwa Maryam Msabaha, Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya, Mheshimiwa Moza Abedi Saidy, Mheshimiwa Haji Juma Seleweji, Mheshimiwa Martha Moses Mlata, Mheshimiwa Omari Rashid Nundu, Mheshimiwa Dustan Kitandula na Mheshimiwa Fatma Mikidadi.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mheshimiwa Zarina Shamte Madabida, Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Catherine Magige, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa Dkt. Dalali Kafumu, Mheshimiwa Joshua Nassar, Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Mheshimiwa Luhaga Mpina,

Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli, Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mheshimiwa Rashid Ali Omar, Mheshimiwa Haroub Muhammed Shamis, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Haji Khatib Kai, Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa David Silinde, Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mheshimiwa Meshack Opolukwa, Mheshimiwa James Mbatia, Mheshimiwa Dkt. Terezya Huviza, Mheshimiwa Deo Filikunjombe; huyu labda ameandika mara tatu tatu, Mheshimiwa Eugen Mwaiposa, Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Mheshimiwa Chiku Abwao, Mheshimiwa Faith Mitambo, Mheshimiwa James Mbatia, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Dkt. Abdulla Juma Abdulla Saadalla, Mheshimiwa James Lembeli, Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed, Mheshimiwa Omary Badwel, Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogela, Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mheshimiwa Ester Matiko, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Waride Bakari Jabu na Mheshimiwa Herbert Mntangi.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa George Huruma Mkuchika, Mheshimiwa Ezekia Wenje, Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu, Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mheshimiwa Dkt. Kebwe S. Kebwe, Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Salum Barwany, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar, Mheshimiwa

Dunstan Mkapa, Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mheshimiwa Abdalla Haji Ali, Mheshimiwa Said Mussa Zubeir, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Eng. Hamad Yussuf Masauni, Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mheshimiwa Nassir Yussuf, Mheshimiwa Jenista Mhagama na ndugu zangu waliowakilisha hapa Mheshimiwa Steven Maselle na Mheshimiwa George Simbachawene.

Waheshimiwa Wabunge, napenda kusisitiza fursa niliyowapatia kwamba, huenda muda hautoshi na maswali mnayo mengi sana. Wizara yetu inataka kufanya kazi karibu sana na ninyi. Kwa hiyo, nimewaagiza wafanyakazi wote ambao wapo hapa kwa ajili ya bajeti wakiwa na Wakuu wao wa Vitengo, kuanzia kesho watasikiliza hoja zenu ambazo mnazo. Kwa hiyo, kesho Jumapili, kati ya saa tatu asubuhi mpaka saa saba, tafadhali kama una tatizo lolote hasa ukiangalia ile michoro, tuliwapatia njooni ofisini kwetu, ofisi ipo nyuma ya Dodoma Hoteli. Watakaa hapa hapa Jumatatu na Jumanne kuanzia saa mbili asubuhi mpaka saa 12 jioni. Kwa hiyo, jamani wenye kiu ya maswali tunawakaribisha sana. *(Makofi)*

Pili, napenda sasa niwaeleze kidogo tatizo ambalo limeleta mambo mengi, la *TANESCO* nadhani ni vizuri mlisikie kutoka kwangu mwenyewe. Kabla sijalisema hilo, kuna vitu viwili ambavyo ni vya muhimu sana. Napenda niwaeleze Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote wanaotusikiliza hapa; alikuwepo Mwanafilosofia mmoja, mwenyeji wa Scotland, walikuwa kwenye majadiliano mengi sana ya mambo

ya filosofia. Mwaka 1852 alisema nitayatafsiri kwa Kiswahili baadaye.

Alisema *truth like a touch, the more it shock it shines,* narudia tena hii ni lugha ya zamani kidogo, siyo Kiingereza chepesi cha siku hizi. *Truth like a touch, the more it shock it shines,* yaani ukweli ni kama tochi au kurunzi yenye betri, ndani unavyozidi kuitingisha ndivyo jinsi ambavyo mwanga unazidi kuwaka. Unajua tafsiri hizi unamwachia mtu mwenyewe huwezi ukamtafsiria. *(Makofi)*

Wa pili, alikuwepo Mwandishi maarufu sana wa Kimarekani alikuwa anaitwa Walter Lipman, tarehe 14 Aprili, 1945 alikuwa Mwandishi wa *New York Herad Tribunal,* Gazeti la New York lile, ni kubwa sana mpaka sasa hivi bado lipo. Tarehe 14 Aprili, 1945 alisema haya: "*The final test of a leader is that he lives behind him in other men the conviction and the will to carry on.*" Naomba nirudie tena: *"The final test of a leader is that he lives behind him in other men the conviction and the will to carry on."* Kwa maneno mengine, ukitaka kujua mafanikio ya Kiongozi yeyote ni yule ambaye ameacha kitu nyuma, amewaacha watu nyuma ambao wanataka kuyaendeleza yale aliyoyaacha. Kwa siku chache nilizokaa hapa Bungeni, hapa ndugu zangu mtakapokuwa mnafanya hii tafsiri kuna makundi ya watu wawili; kuna kundi la Mwalimu Nyerere, kuna kundi la Marehemu Sokoine na kuna kundi la Kawawa. Utakavyokuwa unafanya tafsiri, kuna kundi lingine la Mobutu, kuna kundi la Bokasa na kundi la Abani. *(Makofi/Kicheko)*

Mimi nilipata bahati kusoma shule yetu ilikuwa nzuri. Mimi kwetu ni Musoma Mjini pale, kwanza, Ndugu Maswi hata hatusikilizani lugha, yeye anatoka Tarime mimi natoka Musoma Mjini. Huyu kijana Nyerere ni mpwa wangu, kutoka kwao na kwetu ni nyumba tano tu, ni mpwa wangu wa karibu sana. Mwalimu Nyerere wakati nikiwa *form one,* mnamjua Neil Armstrong, mtu wa kwanza kutembea kwenye mwezi ilikuwa tarehe 20 Julai, 1969 na mimi nilikuwa *form one*, bahati nzuri nilisoma Shule ya Wamarekani tukaona Armstrong anatua mwezini. Mwalimu alikuwa mwepesi sana kutufanya wakati huo tusipoteze na kujidharau, alisema hivi: "Wakati wengine wanakwenda mwezini, sisi twende vijijini. Je, Wabunge na Serikali tulimsikiliza Mwalimu? (*Makofi*)

Sasa nije *TANESCO.* Mtu anayeitetea *TANESCO* au anayewaumiza *TANESCO*, msichukue *the short history* kama kile kitabu tulichokuwa tunakisoma; *Short History of Tanganyika,* chukua *Long History.* Hili Shirika lilianzishwa mwaka 1930, yalikuwa makampuni mawili yakaja pamoja. Sasa toka mwaka 1930 hata kama inabadilisha watu wanaoiendesha hamuwezi kulikubalia hadi leo hii, asilimia chini ya 20 ya Watanzania hawana umeme. Unatetea nini; unatetea upuuzi tu? (*Makofi*)

Isitoshe ni kwamba, *TANESCO* ni asilimia 100, ni Shirika la Umma la Serikali. Yeyote anayejidanganya kwamba halitaingiliwa anapoteza muda, tutaliingilia tu. (*Makofi*)

Sasa basi kama ni hisa 100 na ninyi Watanzania mmejua mambo ya hisa siku hizi, sote hapa tumenunua hisa huku mbili, tatu, si kila mwisho wa mwaka mnapata gawio (*dividend*)? Nitaongea na Waziri mwenzangu wa Fedha, tuanzie *TANESCO* na Mashirika yangu yaliyoko chini yangu nayapa maagizo, Januari mwakani lazima tufanye kikao. Wao watakuwa wanatoa fedha ngapi kurudishia wenye hisa? Hamuwezi kuja hapa kila siku bajeti hazitoshi mnasema vyanzo mnapeleka kwenye bia badala ya kwenda kuchukua hela *TANESCO. (Makofi)*

Mwisho, muundo mpya wa kutatua matatizo ya Wizarani kwangu; mimi nilikuwa Mwenyekiti wa Bodi ya *STAMICO,* nilikuwa Mwenyekiti wa Tume Teule iliyokwenda kuchunguza vifo vya Mererani mwaka 2002, lakini wengi nadhani hiyo ripoti yangu hamjaiona. Sasa tunakuja na mtindo mpya, lazima tubadilike. Nami nasema Wizara yangu haya mambo ya Tume siyataki. Kitakachotokea kuanzia sasa tujaribu huu mtindo tukishindwa tutarudi kwenye Tume, kama tatizo limetokea kwa sababu Wafanyakazi wa Wizara wanalipwa kwa ajili ya shughuli hiyo, watakwenda na kushughulikia hilo tatizo, watatengeneza ripoti halafu tutakuwa na kitu kinachoitwa *public hearing,* yaani hiyo Ripoti kama Ripoti ni watu wa Mererani, tutakwenda nayo na mimi mwenye nitakuwepo itawasilishwa tutaijadili tutamaliza hapo na Watanzania wanasonga mbele. (*Makofi*)

Sasa kwa sababu sitaki kukosa neno, naomba nizungumzie utendaji wa Mkurugenzi Mtendaji wa *TANESCO.* Tangu kuteuliwa kuiongoza Wizara ya Nishati

na Madini, tumeona uwajibikaji usiokidhi matakwa ya Kanuni za Utumishi katika uendeshaji wa Shirika la Ugavi na Umeme nchini.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* ni Shirika la Umma kwa asilimia 100; hivyo, linahitaji kuangaliwa kwa karibu sana na kuchukua hatua za haraka ili kuwezesha ustawi wa Watanzania. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, tumeamua kwa dhati kabisa kurejesha heshima ya Serikali katika eneo hili. *(Makofi)*

Kama *TANESCO* watafanya kazi kulingana na taratibu, hatuna tatizo, kinyume chake lazima tuchukue hatua bila kusita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, wameshauri tuongeze juhudi na turudishe heshima katika *TANESCO*, nami nasema hili linawezekana kwa kuwa tumedhamiria, nia tunayo na uwezo tunao. *(Makofi*)

Uamuzi wa kumsimamisha Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa *TANESCO*, ulichukuliwa na Bodi ya Wakurugenzi katika Kikao cha Dharura cha tarehe 13 - 14 Julai, 2012. Kwa mujibu wa maelezo ya Bodi, amesimamishwa kutokana na tuhumu za ubadhirifu na matumizi mabaya ya madaraka. Bodi ya Wakurugenzi imemwomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya uchunguzi wa kina kuhusu tuhuma hizo.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya tuhuma zilizo dhahiri na zitafanyiwa kazi na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni pamoja na hizi hapa: Kwanza, kukiuka, maadili ya utumishi wa umma kwa kuingia

mkataba ambao yeye mwenyewe ana maslahi na mke wake Eva akiwa Mkurugenzi. Aidha, Wakurugenzi wengine ni watoto wake; Fred na Veronica William. Ni kweli kabisa, kampuni yao iliyoanza kazi Aprili, 2012, kwa mtaji wa shilingi milioni kumi, miezi minane baadaye ilipata mkataba wa zaidi ya shilingi milioni 880 *TANESCO.* (*Makofi*)

- Kuwepo kwa manunuzi mengi yasiyokidhi vigezo ni tatizo lingine kubwa katika *TANESCO.* Wakati nafanya kikao na Wafanyakazi wa TANESCO walioandika tuhuma zilikuwa zimejaa kasha. Moja, iliyonifurahisha sana na kunisikitisha ni kwamba, waliagiza *spare part* kutoka Uingereza wakalipia Pauni 50,000 kumbe lilikuwa *box* la misumari.

- Kukumbatia wafanyabiashara ambao walichangia sana kushindwa kwake kutenganisha maslahi binafsi na maslahi ya Shirika.

Waheshimiwa Wabunge, kuna Wabunge wawili, watatu siwezi kuwataja.

**WABUNGE FULANI:** Wataje.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Hawapo huko, wao walinipatia *information* nzuri nikaimeza; ni kwamba, mimi mwenyewe nilikuwa najua kwamba hizo nguzo ambazo tunapigia kelele zinatoka hapa hapa nchini huko Iringa, zinasafirishwa kwenda Mombasa halafu zinarudishwa nchini zikiwa nguzo za South Africa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunao ushahidi usio na shaka wa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kufanya biashara na *TANESCO*. Ni kazi ngumu kweli kweli kumsimamia anayekupa biashara na hawezi kukuheshimu kwa kuwa anakufahamu na anakufadhili.

Baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, wameingia mkataba wa kuiuzia *TANESCO* matairi na kushinikiza kubadili bei ya matairi hayo baada ya mkataba kufungwa na hili lilifanyika pamoja na kuwa matairi hayo hayakuwa na viwango. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niwashauri na kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, kwa dhati kabisa, waache kufanya biashara na *TANESCO* ili wawe na uhuru wa kuisimamia na kuiwajibisha pale inaposhindwa kutekeleza majukumu yake; kufanya vinginevyo ni kujiweka katika mazingira magumu sana ya kimaslahi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu pendekezo kuwa iundwe Tume Teule, ni maoni yangu kuwa hakuna umuhimu wa kufanya hivyo, kwa vile tayari *CAG* alishapewa kazi hiyo. Kwa hiyo, Watanzania na magazeti yote tufunge huu mjadala tufanye mambo mengine ya muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niruhusu nijibu hoja chache kwa kufuata maudhui yanayofanana. Nawashukuru sana Naibu Mawaziri wa Madini, kwa kujibu vizuri hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, sasa niruhusu nijibu hoja chache kwa kufuata maudhui yanayofanana. Nawashukuru sana Waheshimiwa Naibu Mawaziri wa Nishati na Madini kwa kujibu vizuri hoja za Waheshimiwa Wabunge. Wamenirahisishia kazi. Nianze na Hoja za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, Sera, Sheria na Mpango Kabambe wa Gesi Asili. Umuhimu wa Sera, Sheria na Mpango Kabambe uko wazi. Wizara imekamilisha maandalizi ya Sera hiyo na nadhani Naibu Waziri ameieleza kwa ufasaha kabisa.

Mheshimiwa Spika, hofu ya mgawo wa umeme. Hofu isiyo ya lazima imetanda miongoni mwetu na kukuzwa na baadhi ya vyombo vya habari kuhusu uwezekano wa kuwa na mgawo wa umeme. Nadhani na hili limeelezwa vizuri kwa sababu *capacity* ya kuzalisha tunayo na matumizi yetu yako chini zaidi.

Mheshimiwa Spika, *TPDC* kusitisha ugawaji wa vitalu. Kuna ukweli kuwa Sheria na Sera za Gesi zikikamilishwa, mikataba ya utafutaji inaweza kuwa bora zaidi. Hata hivyo, Sera ya Nishati na Madini, Sheria ya Utafutaji wa Mafuta na Gesi ya mwaka 1980 na *Model PSA,* vinatosheleza mahitaji ya sasa. Pamoja na hayo, suala la ugawaji wa vitalu vya kutafutia mafuta na gesi asili katika maeneo ya baharini, linaanza kuonekana kuwa tete. Hapa inabidi tuchukue hadhari kubwa kwani ni vema tusichukue uamuzi wa kudumaza utafutaji nchini kama tulivyofanya miaka ya nyuma.

Waheshimiwa Wabunge, niwaeleze kwamba dunia ya leo hii, ni mambo ya ushindani. Siku nyingine nikiongea, nitawaeleza vigezo 12 ambavyo vinafanya nchi iweze kushindana na nchi zingine. Kwa hiyo, sisi anayeshauri tusimamishe utafutaji wa mafuta, tutakuwa tumefanya kosa kubwa sana kwa sababu Msumbiji wanatafuta, Kenya wanatafuta, Congo wanatafuta, Kenya wamegundua juzi mafuta kule juu, Uganda wamegundua mafuta, kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge, ni lazima tuendelee na zoezi la kutafuta mafuta na gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *PAT* kulipa Dola za Marekani Bilioni 20.1 na hizi nadhani Waheshimiwa Manaibu Waziri wameeleza vizuri na ukweli ni kwamba tumeagizwa mikataba hiyo tuichunguze upya na mikataba ya *Songas* tuipitie upya. Kwa hiyo, muwe na imani kwamba hiki kitu tunakifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Uagizaji wa Pamoja wa Bidhaa za Mafuta. Nadhani hii aya ya 161 ya hotuba yangu, maelezo yanajitosheleza na hata hivyo tunazidi kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya hoja zilizotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini zimetolewa pia na Kambi Rasmi ya Upinzani. Ninatoa majibu kwa hoja zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kutayarisha wataalam watakaohitajika katika sekta ya gesi. Mimi mwenyewe nashukuru nimesema, pale Wizarani tumeanzisha

*marshal plan,* hata mkisoma kwenye kitabu chetu hicho kuna *marshal plan*. Tunataka kati ya mwaka huu na mwaka 2016 tuwe na vijana wataalam kati ya 30 na 50 na isitoshe hawa watasomeshwa kwa hela zetu, zile pesa ambazo zilizokuwa zinaingia Wizarani, mnasema hamjui zinavyotumika na zile za kule *TPDC,* sasa sisi kama Wizara tunatoa *scholarships*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kusitisha uwekaji wa vinasaba kwenye mafuta, Naibu Waziri ameliongelea.

Mheshimiwa Spika, mikataba ya bomba la gesi la Mtwara, tumeliongelea kwa kirefu sana.

Mheshimiwa Spika, sasa nije kwenye hili la *TANESCO* na wizi wa *TANESCO*. Kuna jambo muhimu kulisemea kwani halikubaliki ambalo ni wizi wa umeme nchini kwa kutumia mitandao ya Luku isiyosajiliwa na *TANESCO* (*ghost vending system*). Katika zoezi linaloendelea la ukaguzi wa mita za *TANESCO* pamoja na ukusanyaji wa madeni, tayari wateja watano wakubwa wamekamatwa na kufikishwa Polisi. Wateja hao wamekutwa na *unit* za umeme ambazo hazikununuliwa kihalali kupitia mtandao wa mauzo ya Luku wa *TANESCO*. Naelewa wapo wengi wa aina hii. Wateja ambao mpaka sasa tumethibitisha kwamba wanaiba umeme ni pamoja na hawa:-

(i) *St. Marys International School*;

(ii) *Access Bank* iliyoko Tabata Matumbi;

(iii) *Shree Shyam* wenye duka linalojulikana kama *Malick Bhachool* lililopo Mtaa wa Aggrey/Market Karikoo; na

(iv) *Akubu Paradise Hotel* iliyopo Mtaa wa Magira, Kariakoo.

Mheshimiwa Spika, hawa wote; St. Mary's ni thamani ya shilingi milioni 10.5, *Access Bank* ni thamani ya shilingi milioni 13.8, *Shree Shyam* ni thamani ya shilingi milioni 8.1, Philipo Gunda mwenye Hoteli inayojulikana kwa jina *Akubu Paradise Hotel* iliyopo Mtaa wa Magira, Kariakoo huyu *unit* zake ni za thamani ya shilingi milioni 25.3. Baadhi ya wateja hawa wamekwishafikishwa Polisi kwa ajili ya kutoa maelezo na hatua zingine zitachukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mpango wa Serikali wa kupunguza matumizi ya fedha za umma hasa katika ununuzi wa magari yenye gharama kubwa, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu itatekeleza kwa dhati agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu la kudhibiti matumizi ya magari ya bei mbaya kuanzia mwaka huu wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji huo, Viongozi Waandamizi wa Wizara wakiwemo Makamishna na Wakurugenzi waliokuwa wanahudumiwa na magari ya gharama kubwa, wataanza kutumia magari ya kawaida, ambayo ujazo wake hauzidi (CC) 3,000 na hizi ni gari zao za mkopo. Hili zoezi litatufanya tuwe tunaokoa shilingi bilioni 1.4 kila mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sekta ya madini. Hapa Naibu Waziri ameongelea mambo ya *corporate tax* kwamba tumeanza kulipa na hili la Merareni nalo limeongelewa na Ndugu zangu wale rafiki zangu wa *Tanzanite One*, hili jambo liko mezani kwangu. Kwanza, tumeshatoa ile leseni ambayo ilikuwa ni *special minning license* imebaki *mining licence* ya kawaida na yenyewe haijatolewa kwa sababu hatuwezi kufanya nao maongezi mpaka wawe wamemaliza kulipa fedha zetu za nyuma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, suala la Kiwira limeongelewa kwa undani na mimi niseme kwa muda niliokaa pale, tumelichunguza kwa undani sana, lakini niwaeleze tu kwa kifupi, iwapo tunataka mgodi huo uchukuliwe na *STAMICO* na zile asilimia 70 ya hisa zilizoko kwenye kampuni ya Kiwira, ni lazima tulipe madeni ya kule walipokopa fedha. Ukichukua deni, hata ukichukua urithi wa mzazi wako, nadhani unachukua urithi wa nyumba na madeni yake. Kwa hiyo, ndiyo hali halisi hiyo. Tunaweza tukawa wachungu kweli lakini kurithi mali lazima urithi na madeni na uzuri ni kwamba wanaodai kwa wingi ni Mashirika ya Umma. Ni *NSSF*, *PSPF* pamoja na *CRDB*. Kwa hiyo, tukiwalipa hao, hata hii mijadala mikubwa ya fedha za wafanyakazi, tutakuwa tumesaidia sana hayo mashirika. Kwa hiyo, Ndugu zangu, kila kitu kinaenda vizuri kwenye hilo.

Mheshimiwa Spika, sasa kuna hili la kupeleka mchanga nje, labda wakaoteshe kule, sawa inaweza ikatokea miujiza ya kijiolojia lakini sidhani kama hiyo ipo kwamba madini yanaota kwa sababu kama dhahabu

ya kule Mwanza ilitengenezeka miaka 2.7 *billion years ago*. Kwa hiyo, ni *process* ndefu ya kutengeneza madini sio ya kuotesha mara moja kama uyoga. Hata hivyo, Waheshimiwa, kitu ambacho vilevile mimi nimeshaagiza na *project* inaanza nakubaliana na nyie. Katika ule mchanga, kuna madini tusiyoyafahamu na kwa vifaa vilivyoko hapa nchini, hatuwezi kuyafahamu na haya madini yamekuja kuwa na uthamani hivi karibuni, haya sasa yanaitwa *technology metals* au *strategic metals*.

Mheshimiwa Spika, kuna ugomvi kati ya China na Marekani kwa sababu China ina-*control* 95% ya madini ya aina hiyo duniani, halafu anakuwa mjanja, hatumii, anakwenda nje, lakini ndiyo ujanja wa kibiashara. Sasa nimeagiza, bahati nzuri katika mwanafunzi wangu mmoja ambaye alionekana kutimiza *conditions* zangu za kufanya utafiti, nimempatia Profesa Mruma ambaye ndiye *CEO* wa *Geological Survey,* tunaanzisha mradi wa, je, haya madini yako wapi? Hizo ramani tulizowapatia baada ya muda tuonyeshe hizi *strategic metals* ziko wapi. Kwa hiyo, ni kitu kipya, hatuwezi kulaumu *technology* inabadilika. Madini kama hayo ni kama *indium* yaani hizi *electronics* zote mnazotembea nazo zinahitaji hiyo na wengine mnafahamu ule wizi wa *coltan*, ile *coltan* ni *crom byte* na *tantalum*. Ile *tantalum* ni ya muhimu sana kwenye mambo ya *computers* na *semi-conductors*. Halafu kuna mengine kama *palladium***,** haya yote ndiyo yanayotumika kutengeneza *exhausts* za *pipe* za gesi. Sasa ni kweli nakubaliana na hilo na sisi tunalifanyia kazi. Haya mambo mengine ya madini, mwenzangu ameyaongelea kwa kirefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine lililoulizwa na Kambi ya Upinzani hasa Mheshimiwa Mdee, huu mkataba wa siri, kweli tumeufuatilia mkataba wa siri, ule wa uchimbaji wa *uranium*. Sasa hapa ile kampuni ya kutoka Australia, imeingia mkataba na kampuni ya Kitanzania inaitwa *Game Frontiers* ambayo kazi yake ni kuwinda kule karibu na *Selous*, lakini ukiangalia kwenye ramani kile kitalu kiko nje ya *Selous*. Sasa wakaingia mkataba wa kulipana, huo mkataba ni kwenye dola milioni sita (6 milioni) kila mwaka walipane halafu wakianza kuchimba vilevile malipo yatakuwepo. Sasa sijui kama *TRA* ilipata chochote. Nimetuma watu Wizara ya Ardhi kulifuatilia na nimetuma vijana kwenye *field* wakiwa na *GPS* waweze kuangalia kama kuna *coordinates* na hilo kweli lipo na tunalifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kuna wengine walisema kwamba, nadhani huyu ni Mheshimiwa Mnyika, alitoa pendekezo zuri sana kwamba inabidi na sisi tuanze kuwa na *gold reserves*, lakini hiyo ni kitu muhimu, hakuna nchi iliyoendelea na yenye uchumi mzuri ambayo haina hazina ya dhahabu. Kama kuna Mchumi anasema hatupaswi kuwa nayo, hata sisi ambao siyo Wachumi tutaanza kuweka alama ya kuuliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaonyeshe tu kwa mfano, nchi kubwa duniani kama Marekani, Januari mwaka huu, Marekani *reserve* yake ya dhahabu ilikuwa ni tani 8133.5, dhahabu waliyoweka *reserve*. Namba mbili duniani ni Ujerumani, ina tani 3396.35 na tatu ni *IMF,* ina tani 2811.1. Sasa Waheshimiwa Wabunge kama *IMF*

inayotushauri kila siku na yenyewe ina *reserve*, wewe unayeshauriwa kwa nini usiwe na *reserve*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namba nne ni Italy, ina *reserve* ya tani 2451.8. Ya tano ni France, ina tani 2435.4; ya sita ni China, ina tani 1054 na sisi bingwa wetu Afrika Kusini anashika namba 29, ana tani 125. Niliangalia na Malawi alikuwa na tani 0.3, sasa hata Malawi itushinde jamani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hitimisho, si rahisi kujibu kila hoja iliyopokelewa. Hata hivyo, naahidi kuwa nitaandaa majibu ya hoja zote na kuyawasilisha kwa Waheshimiwa Wabunge kama kitabu. Nitashirikiana na Bunge lako Tukufu ili kuhakikisha kuwa sekta ya madini na nishati zinaongeza mchango wake katika ukuaji wa uchumi wa nchi na kamwe sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba, iwapo Dira yetu ya Maendeleo ya 2015, inasema kwamba sisi tutoke kwenye nchi ambazo ni maskini twende kwenye *middle income country.* Maana ya kuingia kwenye nchi za katikati, ni kwamba kipato chako kinapaswa kuwa kati ya dola 3800 na dola 12,500. Sasa kufika huko Waheshimiwa Wabunge, ni lazima tuwe na umeme ambao ni zaidi ya *megawatt 3500*. Kwa hiyo, tunaomba hili Bunge litusaidie tutimize malengo yetu tuliyoainisha kwenye dira yetu ya maendeleo.

**SPIKA**: Mheshimiwa Waziri, naomba usubiri kidogo. Kuna suala lilikuwa linazungumzwa hapa kwamba mafuta yalivunja utaratibu, hukutupa faida ya hiyo kitu;

kwamba ununuzi wa mafuta sijui umevunja taratibu na nini. Naomba utumie dakika chache kueleza suala hilo.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, utaratibu huo, kwanza Waheshimiwa Wabunge tuangalie tu mantiki iliyo ya chini kabisa, *simple logic*. Mimi hapa ninaumwa njaa na sina fedha ya kununulia chakula, Mheshimiwa Mbunge hapa anasema Ndugu yangu huwezi ukafa njaa, naomba nikusaidie. Ni uamuzi wake *either* anipatie chakula au fedha. Hivi kweli mimi ninayeumwa njaa nitamwekea masharti? Sasa *TANESCO* haina fedha, mafuta, lakini inataka iweke masharti kwa anayempatia fedha. Kwa hiyo, nadhani hiyo tu kwanza haina mantiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili ni hivi, ile siku ambayo waliweka mgao nchi nzima, mimi sikupewa taarifa, Manaibu Mawaziri hawakupewa taarifa, Katibu Mkuu hakupewa taarifa. Tukasema potelea mbali hakuna sababu ya kukasirika, mimi nilikuwa nimeitwa na Mkuu wangu, Waziri Mkuu niwe Dar es Salaam siku ya ijumaa, tumefanya kazi mpaka karibu saa tisa usiku, tunaambiwa umeme umerudi, ndipo na mimi nikaenda kitandani. Asubuhi nimesafiri kutoka Dodoma mpaka Dar es Salaam, nikafika kwenye jengo la *TANESCO* pale Ubungo, nikawapigia simu Waheshimiwa mmeshaenda kuchukua mafuta? Walikuwa bado hawajaenda kuchukua mafuta. Sasa fikirieni Waheshimiwa kama kweli ni mgao ambao ni halali na wana nia ya mafuta, mtu kasafiri kutoka Dodoma mpaka Dar es Salaam Ubungo, watu wa Dar es Salaam hawajaenda kuchukua mafuta, nadhani hiyo ni tafsiri ya ajabu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mbali ya hapo, ieleweke kwamba, sisi fedha tulizowapatia hatujaingilia, hiyo ya kusema tumeingilia Kanuni, Wizara haikuamka ikaenda kuingilia fedha za *TANESCO* na kuingilia zile *tendering system* zao, hayo ni kazi yao. Hatukuingia huko, sisi tulikuwa tunawapatia wao, tunawasaidia. Kwa hiyo, siyo kweli kwamba tumekiuka, ingelikuwa tumekiuka na kama tungevuka mpaka, tukaingia ndani ya *TANESCO* na kuwalazimisha kwamba acheni hao, chukueni hawa PUMA, hatukufanya hivyo. Kwa hiyo na sisi kama Wizara kisheria, tuna haki ya kuweza kununua chochote kwa upande wetu na wale *TANESCO* wana haki hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hakuna kosa limefanyika kwa sababu wao wana haki kisheria ya kununua chochote kama wana hela zao na sisi huku tunaruhusiwa kisheria. Kwa hiyo, hiyo nayo haionyeshi chochote tulichokiuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine tena ni kwamba, hii *PUMA* ni Kampuni yetu, tuna 50%. Sasa uangalie jinsi ambavyo tunajimaliza wenyewe; kwanza tukinunua kwenye kampuni yetu kama ambavyo wafanyabiashara wengine hapa wanaambizana kanunue kwenye maduka ya ukoo wako, utakuwa unaacha biashara ndani ya familia, moja hiyo. Kwa kuwa, tuna 50%, inamaanisha kwamba, biashara hiyo ikifanikiwa na sisi *dividends,* pato letu, gawio letu, tutafaidika! Lakini zile kampuni nyingine tukizipatia, hata kama zingekuwa na bei ya chini, hela hizo

tumepeleka lakini hizi za *PUMA,* faida yake bado tutaipata kwenye gawio na isitoshe, yenyewe ndio imetoa bei ya chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu uchunguzi wetu umeonesha kwamba, hata huyu anayeuza kwa 1,850/= kwa lita, kumbe anaenda kununua *PUMA* na *PUMA* sio 1,500/= ni 1,460/=. Sasa hapa Waheshimiwa Wabunge, kwanza tumeokoa shilingi bilioni tatu (3) kila baada ya wiki mbili, inamaanisha shilingi bilioni sita (6) na isitoshe tumeongeza gawio letu wakati tukija kukaa chini kuwekana sawa kimahesabu. Pia isitoshe huyu *PUMA* mpaka sasa hivi, Waheshimiwa, sisi hatujalipa hata senti moja, ametudhamini kwa mkopo na sio kweli kwamba tumepeleka fedha, haijalipwa senti hata moja kwa sababu, sisi ni wabia, ni kampuni yetu. Kwa hiyo, kuna sababu nyingi sana ambazo zinaonesha kwa nini tumefanya tulivyofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho kabisa, unajua mimi sikusoma Sheria, lakini ukiwa unasomasoma vitabu na magazeti na nini, unaweza ukajikuta unakuwa *Bush Lawyer.* Ni kwamba, tumeenda kupata barua na makubaliano kwa sababu, *IPTL* bado ipo chini ya mufilisi. Imeandikwa kabisa na barua tunayo na hiyo sisi ndio tulingoja ndio ingekuja kuniokoa mimi na Maswi, kama hii kitu ingekuja hapa Bungeni. Ndio tulikuwa tumeificha, tunangoja, kama nondo ya mwisho hiyo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hiyo barua inasema kwamba, atakayeinunulia *IPTL* mafuta ni Wizara. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote, hili

jambo nadhani limefikia tamati. Tusonge mbele na tufanye kazi kwa manufaa mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa unajua mambo ya kujifunza hayana mwisho, nilisharukia mambo mengine kabisa, naomba kutoa hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI:** Mheshimiwa Spika, Naafiki. *(Makofi)*

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mwongozo wa Spika!

**SPIKA:** Naomba tuendelee, wakati wa uamuzi hatufanyi mwongozo. Nimetoa maamuzi kwamba, tunaingia kwenye Kamati ya Bunge Zima.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**FUNGU 58 – WIZARA YA NISHATI NA MADINI**

*(Hapa Wabunge wanaotaka kuuliza maswali walisimama kabla ya kifungu husika kusomwa)*

**MWENYEKITI:** Naomba mkae kwanza. Utaratibu ni kwamba, atasoma kile kifungu kinachohusika, atasoma ile hesabu inayohusika, halafu ndio mtasimama. Naomba uanze tena.

Kif. 1001- *Administration and HR Management* … Shs. 8,027,554,000/=

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi.

**MWENYEKITI:** Mkumbuke, tunaingia kwenye Sera, sio kijijini kwangu hakuna umeme, sijui kikaenda hapa, hivyo sivyo; Sera, Mheshimiwa!

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, Serikali, imetenga jumla ya shilingi bilioni 8.9 kwa ajili ya kuendeleza wachimbaji wadogo, ikiwa ni pamoja na kuwapa mikopo. Je, hii pesa, shilingi bilioni 8.9, itagawanywa kwa wachimbaji wote Tanzania ama katika maeneo ambayo yamewekwa kwa ajili ya kugawanya viwanja kwa ajili ya wachimbaji wadogowadogo, ambayo imeoneshwa hapa kwenye hotuba ambayo ni kama maeneo 12 hivi?

**MWENYEKITI:** Hebu uliza vizuri swali lako. Acha kwenye Mafungu, wewe uliza Sera yenyewe ikoje? Ukiingia kwenye Mafungu, sisi hatujaingia huko.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naulizia kwamba, Wizara imetenga takribani shilingi bilioni 8.9 kwa ajili ya kuendeleza wachimbaji wadogowadogo. Je, pesa hii inagawanywaje, kwa kufuata uwiano wa maeneo yote ya wachimbaji wadogowadogo?

**MWENYEKITI:** Sera ya Wizara, kuhusu wachimbaji wadogowadogo na viwanja, ndio unachotakiwa kujibu, tafadhali!

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi ukisema uzigawe kwa wachimbaji wadogowadogo mmoja mmoja, haziwezi kutosha. Tulichokifanya, tumeagiza Mikoa yote kuwa na Vyama vya Wachimbaji Wadogo na pia kuwa na Chama cha Kitaifa. Kwa hiyo, tunapotoa mkopo kwa wachimbaji wadogo, tutaelekeza kwenye vyama vyao ambavyo ndio vitakuwa vinawatambua wanachama wa vyama vile.

**MHE. ENG. HAMAD YUSSUF MASAUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Maana mbali ya kwamba mimi ni Mjumbe wa Bodi ya *PUMA* lakini Wizara hii ndio imenilea, ajira yangu ya kwanza, nilianzia hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, nilizungumzia na bahati nzuri Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, walieleza kwamba, Mpango na Sera karibu zitafika hapa Bungeni. Sasa nilitaka kujua tu kwamba, je, kwa kuwa bado suala la gesi tunapolizungumza sasa hivi ni suala la Muungano; Mipango hii na Sera hii, imezingatia ni jinsi gani Zanzibar, itafaidika? Kwa sababu, hata kama itaamua baada ya mabadiliko ya Katiba, pengine gesi iondoke, lakini tunapozungumza sasa hivi gesi ni suala la Muungano. Kwa hiyo, naomba ufafanuzi katika hili?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI – MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Masauni kwamba suala la gesi bado ni suala la Muungano kwa sasa hivi, suala la Katiba inabakia vilevile; hatuwezi kusema chochote kile, labda tusubiri wakati huo tuone itakuwa nini.

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi katika mchango wangu wa maandishi, nilikuwa nataka nisikie chochote kuhusu Sera ya Gesi kwa upande wa Zanzibar lakini kwa bahati mbaya, sikumsikia Waziri akisema chochote, naomba majibu.

**MWENYEKITI:** Hili liko sawasawa na lile lililopita?.

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR:** *Yes!*

**MWENYEKITI:** Sasa itakuwa ni kurudia, Mheshimiwa Mkiwa.

**MHE. MKIWA ADAM KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi, nilipenda kujua ni nini Sera ya Madini pale ambapo wawekezaji wanakuja kuhitaji eneo na eneo hilo likathamanishwa na wananchi wakazuiwa kufanya maendeleo yao au kufanya shughuli zao za kijamii na baada ya muda wawekezaji wale wakaahirisha kuchukua eneo lile, takribani yapata miaka 8 au 7. Nimetolea mfano, Kata ya Mtakuja, Kijiji cha Nyakabale; nilitaka nijue Sera inasema nini na ni nini hatma ya wananchi hawa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Madini iko wazi, mwekezaji anapokuja kutaka eneo lolote kwa ajili ya uwekezaji, wawekezaji wakubwa kwanza wanaanza kwa kuomba leseni za utafiti na leseni ile anapoipata kwanza, kabla hajafanya chochote ni lazima apate ile *right of entry;* apewe *consent* ya lile eneo ambalo anakwenda. Kwa hiyo, kwa suala la Nyakabale, tunafahamu kuna leseni pale ya Mgodi wa *GGM,* wameshikilia baadhi ya maeneo na kwa sasa tuko kwenye mazungumzo kwa sababu hawayatumii ili waachie maeneo hayo kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuzingatia Mikataba mingi ya Kimataifa inayoweka msisitizo kumuendeleza Mwanamke Duniani, naomba Wizara, kupitia kwa Mheshimiwa Waziri, atupe maelezo ni jinsi gani bajeti ya Wizara yake imezingatia kumwendeleza mwanamke kielimu, kiuchumi na kijamii?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwenye Wizara yetu, maana najaribu kutafuta Sera hapa, siipati sawasawa lakini tunatambua mchango wa wanawake katika sekta ya madini na tunasimamia kwenye ajira. Ukitembelea kwenye migodi, wanawake wanapewa nafasi na hata kwenye madini pia, kwenye nishati ya gesi, tumetoa kipaumbele pia wanawake waweze kupata ajira.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nilitaka kujua kwamba, baada ya uwekezaji, wananchi wa kwenye migodi sehemu mbalimbali Tanzania, imesababisha wakakosa ajira. Hii imesababisha kushuhudia wananchi wanauwawa, wengine wanakuwa vilema, wengine wanapelekwa gerezani. Mwaka jana mwezi wa Mei, 2011, Serikali ilisema mojawapo ya njia ya kutatua kero hiyo ya ajira kwa wananchi hawa wanaozunguka migodi itawatengea maeneo maalum pamoja na kuwapa mitaji na mafunzo. Lakini katika hotuba ya Waziri, hakuainisha ni katika hatua zipi wamefikia, badala yake amesema tu watatoa leseni kwa wachimbaji wadogo na tunajua leseni za wachimbaji wadogo zina masharti ambayo wananchi hawa hawawezi kutimiza. Kwa hiyo, napenda kupata kauli ya Serikali, kuhusu kauli yao waliyoitoa mwaka jana.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli ya Serikali iliyotolewa mwaka jana, siwezi kufanya *reference* kwa sasa lakini ninachoweza kumueleza Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, katika Sera ya Madini, inatoa kipaumbele, hata kwenye Sheria ambayo nimeieleza hapa wakati najibu hoja, inatoa kipaumbele kwanza kwa ajira za vijana na hasa kwenye maeneo ambayo yanazunguka migodi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa limetokea tatizo kwamba kuna baadhi ya sifa ambazo zinahitajika kwa vijana wa eneo lile, wanazikosa. Kwa hiyo, migodi inalazimika kwenda kupata vijana wa maeneo

mengine ambao wana sifa zinazokidhi mahitaji ya migodi.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika mchango wangu wa maandishi, nilitaka kujua kuhusu uendeshaji wa Shirika la *TANESCO.* Kwa kuwa, tarehe 13 na 14, Bodi ilikaa na ikafanya maamuzi dhidi ya Menejimenti na Bodi hiyohiyo haikuwa na usafi wa kuweza kufanya maamuzi waliyofanya dhidi ya Menejimenti; na kwa kuwa, baadhi ya Wajumbe, waliofanya maamuzi ya kuwasimamisha hao Watendaji wa *TANESCO,* nao walikuwa na mgongano wa kimaslahi katika utaratibu mzima wa kuendesha Shirika hilo. Nikaomba Waziri anipatie majibu, kwa nini asivunje Bodi ya *TANESCO* vilevile ili iweze kukaa pembeni wakati huu uchunguzi unapofanyika ili haki itendeke kwa wote? Kwa sababu, Bodi ni chafu na Menejimenti ni chafu na hili ni Shirika la Watanzania wote. Kwa hiyo, nilitaka kupata majibu kutoka kwa Waziri.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, alichokisema Mheshimiwa Mbatia, ni kweli na sisi tunapenda kwenda taratibu na sio kwa jazba. Kwa hiyo, ukweli ni kwamba, tunakokwenda, inabidi Bodi ivunjwe, lakini inabidi twende kwa taratibu badala ya kwenda kwa haraka. Nashukuru kwamba Mheshimiwa Mbatia anayoyasema ni kweli kwamba Bodi ina matatizo na Menejimenti ina matatizo, Menejimenti sehemu wameshasimamishwa, Bodi wanasema ikae pembeni, hata kabla ya haya yote kutokea, tulishaanza kuweka alama ya kuuliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme tu hivi, kwenye mashirika na kampuni zote ambazo ziko chini ya Wizara yangu na nilivyowaeleza kwamba Mheshimiwa Rais ndiye anateua Mwenyekiti wa Bodi na wale Wajumbe wa Bodi kama mlivyoona *TPDC* kwa kujaribu kuwashirikisha Watanzania wote, uamuzi wangu ni kwamba nitakuwa ninatangaza kwenye magazeti Mtanzania yeyote anayejipima na kuona ana uwezo wa kuingia kwenye Bodi analeta maombi yake. Tumeshaanza kufanya kwa *TPDC,* naona mmeona wameomba watu 72 na tutachuja. Kwa hiyo, yote yale badala ya kukaa mimi wale Wajumbe wa Bodi, ni mimi napaswa kuwateua, lakini nadhani kwa kutenda haki kwa wataalam wa fani mbalimbali, siyo vizuri mimi nijifungie mwenyewe chumbani halafu ninateua rafiki zangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hizo ndizo taratibu mpya za Wizara yangu na wote hata awe Mbunge, awe tayari kushindana. Ukiona kwamba una ubavu wa kushindana, leta maombi. Ahsante. *(Vigelele/Makofi)*

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi kwa Wizara hii, nilimwomba Waziri afafanue sera ambayo itatumika kule Vunjo, Moshi Vijijini na Rombo kwa sababu ule umeme tunaotumia sasa hivi una matatizo makubwa sana. Unatoka pale Kiyungi ukija Vunjo unazima, ukipata matatizo yanasambaa mpaka Moshi Vijiji mpaka Rombo. Sasa nataka kujua mpango kabambe, mpango mpya, sera ambayo itaweza

kutukomboa eneo hilo ili tuweze kupata umeme wa kudumu ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mrema, huwa tunakuheshimu lakini hilo siyo suala la kisera.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Madini ya *nickel* ni madini muhimu sana katika utengenezaji wa ndege, chuma cha pua. Sasa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ni hotuba muhimu sana na ni *road map* inayoonyesha dira lakini nimesikitika kuona mgodi mkubwa ambao ni wa pili duniani katika *deposit* za *nickel* haukuguswa kabisa na hotuba hii. Sasa napenda kujua Mheshimiwa Waziri, Serikali ina mpango gani na mgodi wa *Kabanga Nickel*?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nimemuomba radhi, ukweli ni kwamba hatukuweka kwenye hotuba lakini nimeshaonana na watendaji wote na ile kampuni wamenieleza, ni kupitiwa lakini ni mgodi mzuri sana. Lakini usisahau Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa muda fulani walisimamisha shughuli kwa sababu ya mambo ya kifedha na kitu kimoja ambacho mimi nitakifuatilia kwenye *Kabanga Nickel,* kwanza ni mgodi mkubwa kweli, halafu ile *nickel* na *cobalt* haiko tu upande wa Tanzania, inaenda mpaka kule Burundi sehemu za Msongati. Kwa hiyo, kuna jambo moja nilikaa nikawauliza, hivi tukifika pale mpakani kama huko kuna Burundi, Tanzania tutaonaje, lakini nadhani hilo wataalam wataifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho niliongea na *CEO,* nilimueleza nadhani Kamishna anayeshughulika na leseni, kabla ya kutoa ile leseni ya kuchimba, kitu inachobidi tukifanyie kazi ni kwamba yeye ameomba leseni ya *nickel* na *copper* peke yake lakini kutokana na rafiki yangu aliyekuwa anafanya *PhD* yake upande wa Burundi, hiyohiyo inaonekana kuna *vanadium***,** kuna *PGE* ambayo inathamani zaidi kuliko *nickel* na *copper*. Kwa hiyo, nadhani nitatuma watu, nikachukue *sample,* tutaenda kwenye maabara kubwa duniani waweze kutueleza kama kweli yeye anasema *vanadium* na *PGE* haipo ambayo ina thamani kuliko *nickel* na *copper*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, isitoshe nimeongea na Mheshimiwa Waziri anayeshughulikia mambo ya reli, kitendawili kingine ni kwamba wakishaanza kuzalisha, kuanza kuvuna *nickel* na *copper,* wao wanasafirisha tani zaidi ya 250,000 na ukichukua reli yetu ya kati, nadhani ndiyo ujazo wake huo na yenyewe inasafirisha karibu tani 250,000 kwa mwaka. Kwa hiyo, vilevile inabidi tukae chini na Wizara inayohusikana na reli kabla huo mradi haujaanza lakini tunaufuatilia na tunajua ni mradi muhimu sana, samahani kwa kuwa haipo kwenye kitabu.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kupata nafasi lakini kwenye mchango wangu wakati nilipokuwa nachangia kwa maandishi, nilimwomba Mheshimiwa Waziri anieleze au awaelezee Watanzania utaratibu au sera ya kupata wanachama wapya wa *TANESCO.* Nilimwelezea kwa kirefu ni jinsi gani wananchi wengi wanaotaka umeme

wanapata usumbufu mkubwa hata baada ya kukamilisha yale mahitaji yanayohitajika kwa mfano kujiandaa labda kujiandikisha katika kijiji husika wanakuwa 200 au 100 lakini wanakuwa wanakwenda na kurudi hadi kufikia miaka mitatu. Kwa hiyo, nataka tu kujua sera ya *TANESCO* ya kupata wateja wapya inasemaje kuhusu muda na utaratibu kwa ujumla?

**MWENYEKITI:** Uenezaji wa umeme, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni kweli Mheshimiwa Mwaiposa anachokisema na hili linatokana na yale maandalizi yaliyokuwa siyo mazuri ya kukosa vifaa kama mita, *wire*, nguzo na vitu vingine na hii inatupelekea kwenye msingi wa tatizo lenyewe la *TANESCO* lakini sisi kama Wizara tulishatoa tamko kwamba tunadhani mpaka tarehe 30 Juni, Mheshimiwa Waziri aliagiza wawe wamemaliza kuwafungia wateja wa zamani wote ili tuanze kushughulika na hawa wapya. Tunafikiri kwa sababu jana tumetaja tarehe ya kuanza kutumika hivi viwango vipya, tutakapofika kwenye viwango vipya, basi waanze wateja wapya wale wa zamani wote wawe wameshafungiwa. Hivi tunavyosema, *TANESCO* wana mita karibu 50,000 ambazo zimeingia, kwa hiyo, hakuna Mkoa ambako shughuli za ufungiaji wateja haziendelei, kila Mkoa wanaendelea kwa ushindani, kwa mfano hapa Dodoma hapa ni karibu wateja wote wameshafungiwa.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Katika mchango wangu wa maandishi, nilitaka kujua tu sera ya Wizara kuhusiana na usambazaji wa gesi ambayo imepatikana katika nchi hii kwa miji ile mikubwa kama Mwanza, Mbeya, Arusha, maana miji imeonekana kwamba sasa inatumia mkaa kwa wingi na matokeo yake inakuwa inachangia kwa kiasi kikubwa…

**MWENYEKITI:** Katika miji mikubwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru tumeanza kwa kiasi fulani, Dar es Salaam kuna mradi ambao unaendelea kusambaza Dar es Salaam lakini uendelezaji wa matumizi ya gesi ni jambo ambalo tunalitarajia na hii itakwenda kwa kasi, itatusaidia kuokoa mazingira. Lakini yote haya yatatimia tu endapo kwanza lile bomba litakamilika na bomba lile tumepanga likamilike ndani ya miezi kumi na nane kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam ambako tunaamini tutaanzia na hiyo program iliyokwishaanza na baadaye tutaona namna ya kusambaza gesi sehemu zingine.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mimi napenda kuuliza, katika mchango wangu wa maandishi, nilizungumzia suala zima la sera ya Serikali kuhakikisha inafikisha umeme vijijini. Nikaielekeza na kuishauri Wizara kwamba kule kijiji cha Titye tuna maporomoko makubwa sana ambayo tunayatumia hata katika kilimo cha umwagiliaji. Je, Wizara iko tayari

kuagiza wataalam wakapitie maporomoko yale na kuangalia ili kuweza kupata umeme katika maeneo ya vijiji vya Titye, Lalambe na maeneo mengine? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakushukuru. Ni kweli anachokisema Mheshimiwa Buyogera. Kwanza, ndiyo sera ya Wizara yetu kwa sasa kwamba tusitegemee tu kila mtu akasema *grid, grid*, vyanzo hivi vya maeneo husika ni vyanzo muhimu na pengine kunaweza kukaanzishwa hata ushirika wa watumiaji wa vyanzo hivi. Kwa hiyo, *REA* wanafanya kazi nzuri, mpaka sasa wamesha-*identify* vyanzo zaidi ya 50 nchini na wanaendelea kufanya hivyo na kwenye bajeti yetu mkisoma kwenye hotuba ile tumetenga kiasi cha fedha kwa ajili ya *identification* na baadaye kuendeleza. Baadhi ya maeneo tayari tumetoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyanzo hivyo vinavyojitegemea na wanaanzisha ushirika na watumiaji na hata mkawa na *tariff* ya kwenu wa eneo hilo. Kwa hiyo, niseme tu kwamba Waheshimiwa Wabunge tuwe wa kwanza katika kuhakikisha kwamba tunatunza mazingira ya maeneo yanayoweza kuwa na vyanzo hivyo vya maporomoko ili vyanzo vile vitusaidie kuzalisha umeme katika maeneo yetu, wazo la *grid, grid,* ni wazo ambalo kwa kweli haliendani na wakati wa sasa.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ukienda ukurasa 89 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, tunashukuru kwamba gharama za kuunganisha umeme zimepunguzwa kwa *single phase* kutoka shilingi milioni moja laki tatu mpaka laki tatu na

kwa nguzo mbili kutoka shilingi milioni mbili mpaka laki nne na hamsini vijijini lakini hatujaambiwa kwa wale ambao nguzo zinazidi idadi hiyo hapo inakuwaje gharama yake?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio yetu haya yanatokana na ukweli kwamba ni wajibu wa Shirika lenye kazi hii kufikisha hata karibu na umbali huo mdogo kwamba wakifikisha umbali ule, sasa ndiyo ibakie jukumu la mteja. Lakini mahali ambapo panazidi nguzo zikawa nyingi kumi, kumi na ngapi panahitaji sasa *program* maalum. Huu ni umbali mkubwa ambao unahitaji kwa kweli kuwa na mpango maalum lakini tunataka *TANESCO* tunaposema wamefikisha umeme basi angalau unazungumzia nguzo moja, mbili au hakuna nguzo kabisa. Kwa hiyo, hapa ndiyo maana hatukusema chochote. Kwa hiyo, ni jukumu la *TANESCO* kusogeza kwa umbali huo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nami naomba kuuliza kuhusu sera inasemaje kuhusu umiliki wa nguzo kwa sababu unakuta mtu amevuta labda nguzo tatu halafu wengine wanakuja kuchukua umeme bila nguzo yoyote lakini yule mateja wa awali hapati *compensation* yoyote. Naomba kujua sera inasemaje ili tuweze kujua wanasaidiwaje wale waliovuta mwanzoni? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge analeta hoja ambayo kwa kweli

na sisi tumeijadili sana na ni kweli kwamba haina *logic* kwamba mtu unavuta nguzo kwako tano halafu mtu mwingine anakuja kuchukua pale na wewe ulilipia halafu hurudishiwe fidia yako na hili kwenye sheria na sera zimetambua kabisa kwamba huyu mteja aliyevuta kwa kiasi hicho wanaokuja wengine lazima wamlipe au shirika li-*negotiate* naye kuona namna gani wanaweza kufidiwa. Kwa hili tumewaagiza *TANESCO* kwamba wasifanye kiholela, lazima wafanye kwa mujibu wa kanuni zilizopo na ni kanuni ambazo zipo kabisa kwamba lazima wana-*mediate* pale kuhakikisha kwamba huyu mteja naye anapunguziwa ule mzigo alioupata mwanzo.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Katika mchango wangu wa maandishi nilitaka kujua kwamba mwaka 1983 kuna mradi wa bomba la mafuta ulianza kufanyiwa utafiti kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza. Ilipofika mwaka 1998, Rais aliyekuwepo aliidhinisha huu mradi kuanza kutekelezwa, wa bomba la mafuta kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza kusaidia Kanda ya Ziwa lakini mpaka sasa huu mradi haujawahi kuanza. Sasa napenda kujua sera ya Serikali inasemaje kuhusu mradi huu wa bomba la mafuta kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza kusaidia Kanda ya Ziwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, tunajua kwamba ulikuwepo mradi huo lakini kama unavyojua nchi imepitia vipindi mbalimbali vya kiuchumi na wakati mwingine sera za dunia zinatukumba tunafikiri pengine hiki na hivi na hivi. Sisi

tunafikiri tulichukue hili tuweze kwenda kulifuatilia tuone kama bado ni *viable* au ni vipi, ahsante sana.

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi nimetaka kujua, katika kurasa wa 51 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri ametamka mpango wa kuwaendeleza wachimbaji wadogowadogo kwa kuwapa mikopo, mitaji pamoja na kuwatengea maeneo. Sasa swali langu ni kwamba maeneo mengi karibu Tanzania nzima, aidha yana leseni za utafiti ama uchimbaji, hawa wachimbaji wadogowadogo wa madini watatengewa maeneo yapi wakati maeneo mengi yameshachukuliwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati najibu hoja hapa nilieleza kwamba kweli maeneo mengi yameshikiliwa na leseni za utafiti na makampuni makubwa na wale wadogo lakini Sheria ya Madini inaeleza wazi kwamba leseni zile zinapo-*expire,* zinapofika mwisho yule mwenye leseni anapaswa aachie nusu ya eneo lile, hiyo ni kwa mujibu wa sheria. Kwa mantiki hiyo sasa, sisi tumekubaliana kwenye Wizara kwamba maeneo yatakayoachiwa nusu tutayaangalia kiwango cha mashapa yaliyopo pale kama yanafaa kwa kupewa wachimbaji wadogo. Tunawahamasisha wachimbaji wadogo wawe kwenye ushirika ndiyo inakuwa rahisi kuwagawia maeneo kuliko mtu mmoja mmoja kwa sababu maeneo kweli si mengi sana na kwa mtu mmoja mmoja hayawezi kutosheleza. Kwa hiyo, tutatumia yale ambayo leseni za utafiti zitafika mwisho na anapo-*renew* lazima afike mwisho.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika mchango wangu wa maandishi, nilikuwa nimependekeza kwamba pengine Serikali ituletee mapendekezo ya kubadilisha Sheria ya Madini ya mwaka 2010 ili tuweze kufuta *possibility* ya kuwa na *fiscal stability clause* lakini pia tu-*introduce* kodi nyingine mpya kama *win for gain tax* pamoja na kufanya *ring facing,* Serikali inasemaje kuhusu hilo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nililikaribisha hili nilivyokuwa nikijibu hoja kwamba yako mambo ambayo lazima sasa tuyaangalie tena. Kwa mfano, amelizungumza hilo lakini pia tulizungumzia *compensation,* bado kuna mjadala mkubwa unaendelea kwenye maeneo mbalimbali yenye madini na kama nchi sasa hivi ndiyo tunaelekea kwenye kufahamu vizuri hii *industry* ya madini. Kwa hiyo, ninakaribisha mawazo hayo na kwa sababu mchakato wa kuleta mabadiliko ya sheria humu Bungeni unafahamika na sisi tutaliangalia na wataalam wetu.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Imeonekana hujuma ndani ya Shirika la *TANESCO,* ni tatizo kubwa sana kiasi kwamba kumekuwa na mgao wa umeme ambao sio wa lazima na hata Mheshimiwa Waziri amejaribu kueleza hata baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakijuhusisha na hujuma ndani ya Shirika la *TANESCO* kiasi kwamba Bunge leo hii linaonekana kuwa na sura

mbaya machoni pa wananchi wote ambao wamesikia mijadala ambayo imekuwa ikiendelea tangu jana.

Sasa naomba ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Katika kutekeleza sera au falfasa ya ukweli, uwazi na uwajibikaji, ni kwa nini Waziri asilieleze Bunge na umma wa Watanzania Waheshimiwa Wabunge ambao wamejihusisha moja kwa moja kwenye suala la kuhujumu *TANESCO* na ku-*support* mambo ambayo yameonekana hayana tija kwa Taifa leo? Naomba ufafanuzi ni kwa nini wasitajwe ili isionekane kwamba Bunge zima wanashirika au ni sera ya Wizara kuwaficha wahujumu wa uchumi ambao walistahili kunyongwa hadharani ili kuweza kutoa fundisho kwa watu wengine? Naomba ufafanuzi. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niweke vizuri rekodi kwamba Mheshimiwa Waziri hakusema kwamba wapo Wabunge wanaohujumu *TANESCO* amesema wapo Wabunge wanaofanya biashara na *TANESCO* na katika kufanya biashara hakuna Mbunge anayezuiwa kufanya biashara.

Sasa tatizo ni kwamba, unafanya biashara na nani? Una maslahi gani huko unakofanya biashara ukiwa Mbunge? Hilo ndilo linalokuwa tatizo. Sasa kwa msingi huo, na kwa kuwa Waziri ameshasema na ameshatoa wito kwamba anawaomba waache kufanya biashara, lakini hatuwezi kuzuia haki ya wao kufanya biashara kwa sababu hiyo ni haki yao, ila tu kwamba wanafanya biashara wakati huo wengine

wakiwa kwenye Kamati na wengine wakiwa wanaisimamia hiyo hiyo Serikali, hapo ndipo kuna mjadala, na hilo pia ni suala ambalo linahusu sana Bunge lenyewe kufanya maamuzi. Kwa hiyo, sisi kama Serikali tunafikiri kwamba ni vizuri wakaacha tu kufanya hiyo biashara na *TANESCO*.

**MWENYEKI:** Mheshimiwa John J. Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani tulieleza umuhimu wa Wizara kusafisha Wizara na Taasisi zake na ninashukuru Mheshimiwa Waziri ametoa kauli kuhusiana na *TANESCO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, kwenye hotuba tulitaka vilevile kauli ya Serikali, kwani msingi wa matatizo kwenye Taasisi ya Wizara ya Nishati na Madini ni pamoja na mambo ndani ya Wizara yenyewe; na kwa kuwa, kuliundwa Kamati mbalimbali za Bunge kama Kamati iliyochunguza ukusanyaji wa pesa maarufu kama Kamati ya Suala la Jairo na Kamati ya Masuala ya Gesi ya Asili; na kwa kuwa, ndani ya taarifa za Kamati kuna Maazimio ya Bunge yaliyotokana na taarifa hizo, kuna hatua ambazo zilipaswa kuchukuliwa za kusafisha Wizara ikiwemo baadhi ya Watendaji wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kupata kauli ya Serikali kuhusu utekelezaji wa maazimio ya Kamati hizi mbili muhimu ambazo zimekuwa zikisuasua kwa kipindi kirefu.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mitindo mingi sana ya kufanya kazi, lakini mimi nadhani mtindo wangu huwa ni wa kujiridhisha kwanza. Labda kidogo tunatofautiana, kwani Mheshimiwa, yeye ni mwanasiasa *per se* na sisi kidogo sayansi huwa zinataka *evidence.* Sasa mimi siwezi kukurupuka tu nawatoa watu bila kuwa na *evidence*.

Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kazi hii tunaifanyia kazi, lakini vilevile mtu asije akaonewa, lazima tuwe na vithibitisho na tunavyofanya kazi kwa mtindo wetu hatufanyi kazi kwa redio na magazeti, sisi huwa tunafanya kazi kwa kuona matokeo. Naomba niseme kwamba tumeanza, na siyo hivi, tumeshaanza na katika kikao changu na wafanyakazi wa Wizara tuliongea kwa kirefu na kwa undani sana *Water Front* na mwisho wake tulitaka kuonyesha kwamba kweli mambo tuliyokubaliana, tumekubaliana nayo kwa uzalendo wa hali ya juu. Tulikula kiapo ambacho hatukutumia Biblia wala *Quran.* Baada ya kula kiapo tukaimba Wimbo wa Taifa, kwa hiyo, ambaye atakiuka kiapo chetu, basi yatampata hayo yanayopaswa kumpata.

Kwa hiyo, tunachukua taratibu za kusafisha Wizara, na zipo, lakini lazima twende kwa taratibu ambazo hazitamwonea mtu yeyote.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea na Mheshimiwa Mgimwa.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka kujua, Sera ya Wizara kuhusu kuvipatia vijiji vyote vinavyozunguka maeneo ya miradi ya umeme kama vile Bwawa la Mtera na Kihansi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa swali la Mheshimiwa Mgimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya sasa ya Wizara na utaratibu tuliouandaa ni kwamba kupitia miradi ya *REA,* tutahakikisha maeneo yote ambayo ni wadau wa karibu sana wa vyanzo muhimu vya umeme nchini, wanapatiwa umeme, na hii unaiona inakwenda sambamba na wenzetu ambako kunatoka bomba la gesi. Kwa wale wote ambao kunatoka gesi bomba linapita na wenyewe wanapatiwa *priority* ya kupata umeme, na kwa hiyo, tunaendelea na sehemu zote zenye vyanzo muhimu katika nchi wapate umeme kwa sababu ndiyo wanaotazama maeneo yale. Kwa hiyo, tutajitahidi kama kwako Kihansi na Mtera ambako ni kwangu nao wanapata *privilege* hiyo na wako katika mpango mzima nafikiri tuwasiliane ili nikuonyeshe vijiji tulivyoviainisha.

**MHE. ALHAJI MOHAMMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Katika mchango wangu wa kuzungumza, nilijaribu kuikumbusha Serikali kwamba, kama kumbukumbu yangu iko sawasawa, Sheria ya *REA* ya mwaka 2005 inaelekeza kwamba tozo ambazo watapewa *REA* ni 5% lakini hivi sasa tozo inayotozwa ni

3%. Kwa hiyo, nikasema, ili tuipe *REA* fedha za kutosha, ni angalau hili ambalo lipo kwenye sheria ya kutoa tozo ya 5% litekelezwe wakati hatua nyingine zinafikiriwa.

Je, Mheshimiwa Waziri unasemaje juu ya hilo?

**NAIBU WAZIRI WANISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba inawezekana tozo hiyo ni 5%, lakini wakati mwingine tunasema isizidi 5%, maana sasa ukisema uweke kabisa kwenye 5%, inabidi wakati mwingine uangalie *economics* za nchi na uangalie hali ikoje. Kwa sababu hata mafuta yenyewe tusije tukayapandisha bei sasa yakawa tena hata wananchi hawawezi kumudu na kuongeza gharama za maisha.

Kwa hiyo, tunakwenda kwa umakini mkubwa, lakini pale itakapobidi, basi Serikali itafanya maamuzi ya kuongeza.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Katika mchango wangu wa maandishi, nilitaka kujua juu ya sera ya usambazaji umeme vijijini inayotekelezwa na *REA,* kwa nini wanapopita kwenye kijiji hata kama kuna watu wamejiandikisha, vizuri lakini hawasambazi kwa watu wote wenye kiu, wanaweka kidogo kwa watu wachache na kuendelea. Jambo hili linaleta usumbufu na watu wanakuwa wameshasubiri muda mrefu.

Nilitolea mfano juu ya maeneo mbalimbali yanayotoa umeme, kwa mfano, mradi unaotoka Sumbawanga kwenda Namanyele, sasa hivi watu

wamejiandikisha na walisubiri sana muda mrefu ahadi ya Mheshimiwa Rais, lakini sasa umeme unapita, lakini inaonekana maeneo mengine yataachwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua hilo!

**MWENYEKITI:** Sera ikoje?

**NAIBU WAZIRI WANISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa swali la Mheshimiwa Mipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba *REA* wanasambaza umeme na angalau tunakuwa na nyumba za kuanza nazo kwa wale watakaochangamka kujiandikisha mwanzo, lakini siyo kwamba tunaishia hapo. Kwa hivi sasa kwa sababu mazingira yamebadilika kwamba hata bei ya kuunganishiwa umeme tumeishusha, hii yote ni kwa ajili ya kuwafanya wananchi wa maeneo ya vijijini ambako tunaamini kwamba uwezo wao siyo mkubwa, waweze kumudu gharama.

Pia, kwa maeneo kwa mfano, kutoka Sumbawanga kwenda Namanyele ambapo mradi huu umepita na kwamba vipo vijiji ambavyo wamejiandikisha na umeme haujashushwa, tayari tumeshaliona hilo na tumeagiza *transformer* 370 ambazo Wizara imeagiza na itawakabidhi *TANESCO* ili waweze kushusha sehemu zote ambapo umeme unapita ili wananchi wasione tu waya zinapita juu.

**MHE. MAGALLE J. P. SHIBUDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wilaya ya Maswa ina ahadi ya kusambaziwa umeme katika vijiji kwa zaidi ya miaka mitano. Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kufunga safari kwenda Maswa akatusaidie kukwamua vizuio vya kupata umeme vijijini kwa sababu ya urasimu uliojitokeza, ni wa kila mbuzi hula kwa urefu wa kamba yake?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shibuda sisi tunazungumzia sera, sasa tena tukienda Maswa…

**MHE. MAGALLE J. P. SHIBUDA:** Namwalika, maana yake ndiyo swali lenyewe lilikuwa …

**MWENYEKITI:** Anasemaje?

**WABUNGE FULANI:** Anamwalika!

**MWENYEKITI:** Ah! Basi atakuja. Mheshimiwa Dkt. Kebwe.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii. Napenda nipate maelezo ya Serikali katika maeneo ambayo kuna mwingiliano kama Waziri alivyotoa maelezo, yaani mwingiliano wa Nyang'wale na Geita, lakini hakutoa maelezo kwamba baada ya hapo ni nini kinafanyika katika nchi nzima ya kufanya *mapping* ikiwemo sehemu ya mgodi wa *North Mara* jinsi ambavyo umeingiliana na Serengeti, lakini Serengeti haipati mapato katika kijiji cha Nyiboko pamoja na Borenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELLE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna maeneo mengi sana nchini yanaingiliana kwa sababu mtandao wa madini au miamba ya madini haifuati mipaka ya kiutawala. Kwa hiyo, mambo haya maamuzi yake mara nyingi huwa ni ya majadiliano na kama nilivyosema wakati najibu hoja kwamba tutakuwa na kikao na Kampuni ya *Barrick* kwa ajili ya kujadiliana na uongozi wote, wanaotoka katika maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimetambua alivyosema hili la Serengeti kuingiliana na Nyamongo na lenyewe tutalitatua kwa majadiliano. Lakini pia yapo matatizo katika mpaka wetu wa Kusini kati yetu sisi na Malawi na lenyewe kuna Tume maalum inaendelea kulifanyia kazi ili kuangalia ile miamba inayovuka upande wa pili wa Malawi na inayokuja upande wetu Tanzania. Kwa hiyo, haya yanatatuliwa kwa majadiliano.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi niliomba kupata msimamo wa Serikali kutokana na kwamba, baada ya kuzinduliwa bomba la gesi kutoka Mtwara mpaka Dar es Salaam imebainika kwamba mwekezaji ameomba kuweka baadhi ya visima vya Songosongo rehani ili kuomba fedha katika taasisi za nje. Sasa ninapenda kujua, ni kweli kwamba jambo hili lipo? Nini msimamo wa Serikali

kuhusu kuweka visima vya gesi vya Songosongo rehani jambo ambalo ni aibu na ni hatari sana kwa nchi yetu?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna Kampuni moja ilitoa pendekezo hilo na hii imetokana na kwamba *TANESCO* imetumia umeme wake mwingi na *TANESCO* ilikuwa hailipi deni. Sasa kampuni inataka kuendelea na shughuli zake, kwa hiyo inataka kwenda kukopa fedha nje. Sasa kwenda kukopa fedha nje, ikatoa pendekezo kwamba iweke kisima kimoja rehani ambacho kina gesi karibu milioni *880 billion cubic feet* na vilevile akapendekeza kwamba *assets* zisizohamishika likiwemo bomba la gesi la Dar es Salaam. Lakini kwa kifupi ni kwamba, haikubaliki wala haitekelezeki, haiwezekani! Msimamo wa Serikali ni kwamba tumekataa na haliwezi kufanyika hilo. *(Makofi)*

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Watanzania wanafahamu kwamba Taifa letu kwa sasa linakwenda kuwa Taifa lenye uchumi wa gesi na mafuta miaka michache ijayo, na kuna Makampuni mengi kutoka duniani yanafanya tafiti za mafuta na gesi. Lakini changamoto kubwa katika eneo hili ni uwazi kuhusu kiasi ambacho kinapatikana, lakini uwazi katika gharama ambazo wanazitumia. Zipo taarifa kwa baadhi ya Makampuni ikiwemo *Mare and Prom*, zina *over estimate,* yaani zina *report* gharama kubwa sana au zina *inflate,* wanatumia Dola za Kimarekani milioni 60 lakini wanasema wanatumia Dola za Kimarekani milioni 240.

Sasa nataka kujua, Serikali yetu inachukua hatua gani kuweza kudhibiti mwenendo wa Makampuni ambayo yanafanya tafiti za mafuta na gesi nchini ili tusije kutumbukia katika tatizo lile lile ambalo linajitokeza kwenye Makampuni ya Madini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, tena kwa kifupi kwa sababu nina dakika nne tu.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anachosema kinaweza kuwa ni kweli, kwani sina uhakika. Lakini lazima tufahamu kwamba haya Makampuni ambayo yanatafuta gesi na mafuta, ni hayo hayo Makampuni ambayo yanatafuta gesi na mafuta popote duniani. Hicho ni kitu cha msingi, kwani siyo tu yamekuja kwa ajili ya Tanzania.

Jana niliagiza *TPDC analysis* ya matumizi ya kwao, Kampuni kwa Kampuni na mimi napenda kumkaribisha Mheshimiwa Mbunge kati ya kesho, Jumatatu na Jumanne, timu ya *TPDC* ipo hapa, ina hizo nyaraka, aweze kuja tujaadiliane ana kwa ana kwa sababu hii ni ndefu sana.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nataka kujua sera ya zabuni pamoja na utoaji wa leseni kubwa za madini zinapokuwa ni moja, tangu moja zikagawanywa inakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilielezea mfano wa mlima Kaburu katika mgodi wa Kiwira. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Naomba ujibu kwa kifupi sana, kwani nina dakika chache sana.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELLE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa *reference* aliyoizungumza ya Kaburu, kuna taratibu zilikiukwa nyingi kwenye sera na sheria. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri alipokuwa anajibu, alieleza kwamba tumefaya uchunguzi na uchunguzi unaendelea. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge, kwa hizi siku tulizozitoa baadaye tunaweza tukampa ufafanuzi kwa sababu ni suala refu sana.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wa maandishi niliieleza Wizara kwamba, miradi ya gesi ni jambo muhimu sana katika ustawi wa uchumi na kukuza sekta nyingine katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umezuka upotoshaji mkubwa sana kwamba miradi hii haielekei kuisaidia nchi. Nilitaka Wizara ionyeshe jitihada za dhahiri kabisa kuelimisha wananchi na hasa wa Mikoa ya Lindi na Mtwara. Nini manufaa ya gesi katika uchumi wa nchi yetu na yale ambayo wao watanufaika nayo?

**NAIBU WAZIRI WANISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanza kufanya hivyo na tulikuwa tumeanza na Mkuu wa Mkoa wa Mtwara na tunaendelea na kwa kweli wananchi watambue kabisa kwamba gesi ina manufaa makubwa, inasababisha mbolea,

inasababisha uzalishaji wa umeme, inauzika yenyewe kama bidhaa na kwa hiyo, kuna manufaa makubwa na kwa kweli viwanda vitakua na kilimo kitakua kwa sababu ya gesi.

Kwa hiyo, nikubaliane na Mheshimiwa Mangungu na nimpongeze kwa jitihada kubwa anazofanya katika kutetea suala la gesi katika maeneo ya Mikoa ya Lindi ya Mtwara.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu wa maandishi nilieleza kuwa ni haki ya Mtanzania yeyote kupatiwa umeme, lakini nikaeleza kwamba yapo maeneo yanasahaulika kupelekewa umeme japokuwa yana fursa nyingi za kiuchumi yanayoweza kusaidia Taifa letu na nikatoa mfano wa Ukanda wa Ziwa Rukwa na nikaiomba Serikali ijaribu kutuma wataalamu kupita katika ukanda huo ili waweze kubaini fursa zilivyo nyingi zinazoweza kusaidia uchumi wa nchi hii.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nitatumia kifungu namba 104 kuongeza dakika ili tumalize wale walioomba. Haya, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba yapo maeneo yenye fursa nzuri na muhimu sana za kiuchumi kama maeneo ya umwagiliaji na maeneo ambayo yana rutuba. Sisi katika Sera ya Umeme ya Taifa, ni kwamba, maeneo hayo yenye fursa za kiuchumi, kilimo cha umwagiliaji na mabonde makubwa ni lazima yapelekewe umeme,

kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Malocha kwamba hata Laela na hata maeneo ya mradi wa umwagiliajia kote tunapeleka umeme.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika uwekezaji wa migodi mikubwa uliofanyika awali ambao ulishahamisha wananchi, umewaacha watu wengi katika umasikini, lakini katika baadhi ya migodi, ni watu wanapambana na wawekezaji na hatimaye uuaji.

Katika uwekezaji mkubwa ambao utakuja kama ambavyo nilitoa mfano wa Ngasamo ambapo kuna *Nickel* nyingi, imeonekana kwamba wananchi sasa hawatahamishwa mpaka wapewe thamani halisi ya maeneo yao pamoja na mali zilizopo ili wasiondoke wakiwa masikini. Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELLE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge ameuliza, lakini alichokieleza ni kama ametoa jibu moja kwa moja kwamba lazima kuwe na *compensation* kama wananchi walikuwepo eneo husika na lazima mwekezaji apate *right of entry,* yaani lazima apate kibali na makubaliano ya kufanya shughuli pale. Kwa hiyo, huo ndiyo utaratibu na sheria inaelekeza hivyo. Kwa hiyo, kilichopo ni kusimamia na kuhakikisha kwamba tusingoje madhara yatokee ama kumkaribisha mwekezaji halafu baadaye ndiyo tunageuka. Lakini lipo tatizo, kwani kuna watu ambao wanavamia maeneo ambayo mwekezaji anakusudia kufanya *compensation.* Wakihisi hivyo, wanawahi kwenda kule kuchukua yale maeneo ili nao wafidiwe.

Kwa hiyo, wanasababisha usumbufu mkubwa kwa wawekezaji.

**MHE. JOELSON L. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwa kuwa, katika aya ya 190 Mheshimiwa Waziri ametoa agizo zito la kutaka kampuni zote zinazochimba madini kwa miaka mitano na kuendelea, ambazo hazijaanza kulipa kodi ya mapato, zianze kulipa bila visingizio na wale watakaoshihdwa, basi wafunge migodi na kuondoa. Lakini sasa swali ni kwamba, Makampuni haya ni Makampuni gani kwa majina na amri yake hii inatekelezwa msimu gani sasa? Ni msimu huu wa fedha amri hii inaanza kutekelezwa au itatekelezwa kipindi gani?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Waziri ameagiza yote yaanze kulipa *corporate tax*. Hivi sasa Makampuni ya Barrick na mengine yote kwa mfano, TULAWAKA, Bulyanhulu, na *North Mara* wanalipa, kasoro Buzwagi ambayo uwekezaji wake siyo wa muda mrefu sana. Lakini pia Makampuni kama *GGM* na *Resolute* pia wanalipa sambamba na *Tanzanite one*. Kwa hiyo, hii *corporate tax* inalipwa baada ya kuwa Kampuni imeanza kutengeneza faida. Tulichokuwa tunakipigania kwenye sheria ni kuhakikisha tunapunguza ule muda mrefu wa *payback period,* waanze kulipa mapato mapema kuliko ule muda ambao ulikuwa umekisiwa kule awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini haya yote na mabadiliko ya mikataba, zile *MDAs* yanafanyika kwa mazungumzo na tumekwishakubaliana na haya

Makampuni kwamba, kuanzia mwezi Septemba, 2012 tunaanza kukaa mezani kujadili upya kupitia Mikataba yote ya Madini.

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika mchango wangu nilitaka kujua kwamba kulikuwa na sera ya kwamba sisi watumiaji wa umeme wa gesi tulipoanza kutumia umeme wa gesi miaka minne iliyopita, kulikuwa na ahadi kwamba atakayetumia umeme huo wataunganishiwa kwa gharama nafuu ya *flat rate* ya Sh. 70,000/= kwa kutumia Kampuni ya *Artumas*, bahati mbaya Kampuni ya *Artumas* sasa imefilisika na imekabidhi *TANESCO* na hiyo ahadi haijatekelezeka. Je, tukitaka kujua sasa *TANESCO* pia ahadi hiyo wataweza kuitekeleza? Siyo katika mradi huu wa bomba la gesi mpya, ni miaka minne iliyopita!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Murji tumekwishaongea naye mara kwa mara juu ya jambo hili. Lakini ni kweli kwamba Serikali inafanya mambo makubwa sana kule Mtwara na Lindi kwa sababu hata huo umeme wa gesi ambao wanautumia, Serikali inatoa fedha takriban Shilingi bilioni tano kila mwaka kufidia gharama za uzalishaji wa umeme wa gesi, kwa sababu hakuna namna yote ambayo wananchi wale kwa matumizi yale madogo madogo wanaweza wakalipa zile gharama.

Kwa hiyo, Serikali inafanya mambo makubwa sana na ziada ya hapo sasa tumepanga kwenda zaidi

ya pale. Kwa hiyo, hili analolisema la kupunguza gharama za umeme kwa Sh. 70,000/= ilikuwa ni ahadi ya wakati huo. Sasa tunakuja na mpango mkubwa ambao sasa utashirikisha na Serikali imeamua kweli kabisa kuhakikisha kwamba inaweka vizuri kule Kusini. Kwa hiyo, tuta-*accommodate* mambo mengi. Kwa hiyo, mimi nadhani hili liwe ni sehemu ya mazungumzo yetu tutakayoyazungumza Jumatatu, niliyoomba kukutana na Waheshimiwa Wabunge wa Lindi na Mtwara.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi kwenye mchango wangu wa maandishi nilikuwa nimemweleza kwanza kwa kumpongeza kwa maonyesho yale makubwa ya vito vya thamani yaliyofanyika Arusha na kwamba Wizara ilialika wanunuzi vito vya thamani kutoka sehemu mbalimbali duniani, na walikuwepo pale wanaliuza na hatimaye wanunuzi wengine walirudi na fedha zao. Sasa je, Sera inasemaje kuhusu kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo hasa wale wa vito vya thamani ambao wamekuwa wakitembea na mawe mfukoni bila kujua thamani yao ili waweze kupata soko? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria inaelekeza kwamba madini ya vito ni lazima kwanza yachimbwe na wazawa. Lakini Arusha hasa kwenye *Tanzanite one,* kuna tatizo kubwa la utoroshaji wa *Tanzanite* na hii inafanyika baada ya wale wanunuzi wa zamani waliokuwa wakitoka India, wamegeuka kuwa sasa ni ma-*broker.* Sasa hawa watu wetu Waswahili wamekwishakosa biashara sasa hivi. Kwa

hiyo, nilikuwa Arusha kule na nimeshaagiza wale wageni wote ambao wanajihusisha na biashara ya vito kama ma-*broker,* waondoke haraka. Niliwapa siku 14 na nikaagiza kabisa vyombo vya Ulinzi na Usalama vifanye msako baada ya siku 14, kama kuna wanunuzi toka nje wanaofanya kazi ya u-*broker* waondoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tumeweka mkakati kama Wizara kuhakikisha tunaifanya Arusha kuwa *John stone Center* ya Afrika na hilo tutalifanya kwa kujenga jengo maalum *Centre* na wafanyabiashara vijana wa Arusha wanaotembea Mitaani wawe na sehemu ambayo mnunuzi akija anawakuta na siyo kwenye vichochoro vya Arusha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Diana Chilolo.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi nilifarijika sana kusikia maelezo ya Mheshimiwa Waziri kwamba ataharakisha kuleta Sera na Sheria pamoja na Mpango wa Gesi hapa Bungeni ili aweze kusimamia mapato makubwa yatakayotokana na gesi. Sasa nikawa nimemshauri Mheshimiwa Waziri kwamba, anaonaje hayo mapato makubwa yaliyotokana na gesi atengeneze mfuko wa mapato pekee yake wa gesi ili Watanzania tuwe na historia kutokana na gesi tu, tumenufaika kiasi gani? Tumepata mapato gani? Tumefanya nini kutokana na fedha hizo?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo wazo, mbali na kwamba ameliuliza na

Kamati amependekeza, na sisi tunalo wakati tunatengeneza sera. Sera itakapokuja mbele yenu na baada ya kupitiwa na watu wengi sana, ni lazima fedha zinazopatikana kutokana na gesi au mafuta ziende kuzamishwa kwenye Mfuko wa Hazina, hatutajua zinatumikaje. Kwa hiyo, tutaweka *Special Fund,* tutafuta jina lake kama ambavyo nchi nyingine wanafanya mfano, Norway na sehemu nyingine. Ni wazo zuri sana, tumelichukua na sisi tunalo. *(Makofi)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kumekuwa na malalamiko mengi sana kwa vijana wenzangu ambao wanafanya kazi kwenye Makampuni ya migodi, mbali ya kwamba wanakosa kazi zenye staha ambazo wengi wao wanapata wageni. Lakini malalamiko haya yamekwenda mbele zaidi na kudhalilishwa na wengi hata kuvuliwa nguo kwa kisingizio cha kuondoa na mawe. Mimi nimefarijika kwamba kwenye hii Wizara, pia wapo Mawaziri vijana akiwemo Mjumbe wa Baraza Kuu. Mwenzangu, Mheshimiwa Stephen Masele: Sasa je, mmejipanga vipi kuhakikisha vijana hawa wa Kitanzania wanaondokana na manyanyaso hayo ambayo wamekuwa wakiyapata kwa muda mrefu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa swali la Mheshimiwa Ester Bulaya. Ni kweli kumekuwa na kesi nyingi zinaripotiwa za manyanyaso, tumepokea kesi kutoka Arusha kwenye Mgodi wa *Tanzanite One* kwamba vijana wetu wengi wanapopita pale wanapita kwenye *scanner* na wanahisi kwamba ile *scanner* inaweza ikawa na

madhara kiafya. Lakini nilipozungumza na uongozi wa Menejimenti ya mgodi ule wa *Tanzania One* wakasema kwamba ile inawasaidia wao kujua vilivyomo mle ndani. Lakini tukazungumza kwamba *scanner* zile au kuwapekua kwa njia ya *physical* kwa akinamama inakuwa shida kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni suala ambalo kwa kweli linahitaji majadiliano ya mara kwa mara baina ya Serikali na migodi hii kuhakikishia kwamba taratibu za kazi zinasimamiwa bila kunyanyasa jinsia ama Utaifa. *(Makofi)*

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri pale alipoishia Mheshimiwa Machali, naendelea kidogo, kwamba; kutokana na *message* zilizotumwa hapa Bungeni za kutisha, Waziri na Katibu Mkuu watashindwa kufanya kazi inavyotakiwa. Tumetumiwa *message* karibu nusu ya Waheshimiwa Wabunge hapa, wanamtisha na kwamba watamwondoa kwa vyovyote vile na watapambana naye mpaka mwisho, na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walimdai Katibu Mkuu rushwa Shilingi milioni 50 ili wakagawane kwenye Kamati zao. Huu ni ushahidi tosha na sisi tukienda kule nje tunadharauliwa Waheshimiwa Wabunge wote, kwamba Wabunge ni wala rushwa. Kwa hiyo, wametuchafua Wabunge wote humu ndani. Kwa hiyo, naomba majina yatajwe bila huruma yoyote, wanajulikana. Kwa nini tunaogopa kuwataja? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy, ahsante, hilo limekwishajibiwa. Tunaendelea.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, katika ukurasa wa 10, niliishauri Serikali kutokana na Taarifa za Serikali kwamba kuanzia mwezi Januari, mwaka 2012, mpaka mwezi Machi, mafuta, jamii ya *petrol gasoline* yenye thamani ya *dollar* 210 yaliingia nchini. Taarifa za Mkemia Mkuu wa Serikali zikasema *ethanol in essence* zaidi ya asilimia 10 ilikuwa imeongezwa kiasi ambacho kiliwapiga changa la macho Watanzania kwa hasara ya karibu *dollar* 20. Nikamwomba Mheshimiwa Waziri atoe msimamo wa Serikali, na kama hana la kufanya, awaombe msamaha Watanzania ambao waliuziwa kitu chenye thamani ndogo kwa bei ya thamani kubwa, yaani kwa kutumia *quotation* za *Mediteranian* wakati ndani kuna *ethanol* nyingi sana ambayo kwenye Soko la Dunia inauzwa *dollar* 200 wakati ukweli wenyewe sisi tumechanjiwa *Dollar* 1000 kwa tani.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mwijage, anafanya kazi nzuri sana kwenye Kamati, ameisaidia Kamati pamoja na Serikali kwa sababu yeye ni mtalaam wa masuala haya. Lakini pia nimpongeze kwa mchango wake katika *page* ya 10 zilizoandikwa mbele na nyuma, kwa hiyo, ni *page* 10 za maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kulitokea malalamiko ya mafuta mabaya ambayo ilibainika baadaye kwamba ni *ethanol* ilikuwa imezidi na *ethanol* ina bei ndogo. Kwa hiyo, sisi tunafikiria uchakachuaji

huku kwenye mafuta yakishashuka kumbe uchakachuaji unafanyika hata huko huko kabla hajafika hapa nchini. Hili tumelipokea na tunalifanyia kazi na bado tunahitaji ushirikiano mkubwa kutoka kwa Mheshimiwa Mwijage. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kilufi hayupo, Mheshimiwa Lugola.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka kujua, kama Wizara ya Nishati na Madini inayo sera ya *double standards* katika kuwataarifu watanzania juu ya kinachoendelea hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Waziri anafanya majumuisho, aliweza kuwa na ujasiri wa kuwataja wale ambao wamehusika na kuihujumu *TANESCO,* akataja Eva kama Mke wa William Mhando kwa Watanzania, akamtaja Fred kwa Watanzania, akataja Makampuni yakiwemo na Shule za St. Mary's na mengine kwa Watanzania wakawajua wanaiba umeme wa Tanzania, baadaye akaenda kwenye eneo la Wabunge ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini na akasema kwamba wamejihusisha na kuuza matairi mabovu na wamejihusisha na kupandisha bei ya matairi. Kwa maana hiyo, alikuwa anawataja watu ambao wanaihujumu *TANESCO*. Nataka maelezo ni sera ya *double standards* kwa Wizara hii kutaja baadhi ya Watanzania mbele wa Watanzania, na wengine kutowataja hapa Bungeni, ni sera ya *double standards*? Naomba majibu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge hakuna cha *double standards* hao wengine wana utaratibu mwingine wa kushughulikiwa. Mheshimiwa Zainab Kawawa.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kwamba mwanzoni mwa mwaka 2011 kwa maana ya mwishoni mwa mwaka wa fedha uliopita, *TANESCO* iliongeza bei ya umeme kwa asilimia 41. Ongezeko hili tunajua athari zake limechangia pia wizi wa umeme, ongezeko hili limechangia ugumu wa maisha, lakini kisingizio cha ongezeko la umeme huu ni kutokana na gharama za mgao wa umeme. Sasa naiomba Wizara itueleze hapa, kutokana na udharura ule ule wa kuongeza asilimia 41 ya gharama ya umeme, ni lini sasa itaishusha asilimia hiyo 41 ya gharama ya umeme kwa udhararu huo huo kwa kuwa sasa imekwishapunguza gharama ya mafuta ya kuendeshea mitambo ya umeme kwa Shilingi bilioni sita kwa mwezi, lakini pia imepunguza gharama ya kuunganisha umeme majumbani? Sasa ninaomba, sambamba na hayo, ituambie ni lini kwa dharura itapunguza hii asilimia 41 ili Watanzania turudi kule kule kulipa umeme kwa gharama nafuu ambazo tulikuwa tunalipa siku zote? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri naomba kwa kifupi sana.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Mbunge akumbuke historia ya nchi yetu, wakati tulikuwa na hoteli chache kule Arusha, Mwanza, hoteli zilikuwa za bei ya juu sana. Sasa hivi ukienda Kongo *DRC* hoteli ni chache, bei ya kule wakikupatia hoteli ya Dola 500 huwezi kuamini. Hapa siri ni kwamba Watanzania watumiaji wakiwa wengi bei itapungua. Kwa sasa hivi ni karibu asilimia 18 ya Watanzania ambao wanatumia umeme ukilinganisha na Kisiwa kidogo cha Mauritius ambacho ni karibu asilimia 99.8 ambacho raia wake wana umeme. Afrika Kusini ambaye *economically* ndiyo *giant* ya Afrika mwenye *GDP* ya zaidi ya Dola bilioni 500, asilimia 75 ya raia wake wana umeme.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge dhamira yetu ni kushusha umeme na ndiyo maana tunakuja na mikakati mingi sana ya uzalishali umeme na usambazaji wa umeme kusudi watu wakiongezeka, tukifika angalau asilimia 50 na ile bei itapungua.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri imeainisha migodi nane mikubwa ambayo inawasilisha mipango ya kufunga migodi *closure plans,* na hii italeta athari kubwa sana kwa ajira hapa nchini. Je, Serikali ina mpango gani licha ya mradi wa gesi na *Urani* na *Nickel*, ina mpango wowote wa kufunga migodi mingine mipya ya dhahabu au madini mengine?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELLE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ile *mining closure plan* haimaanishi kwamba migodi yote itafungwa kwa mara moja. Kila mgodi una maisha

yake. Kwa mfano, Bulyankhulu wanakwenda mpaka miaka 25, wapo wanaokwenda mpaka miaka 15. Kwa hiyo, ina uhai tofauti. Kwa hiyo, kilichopo pale ni matakwa ya sheria kwamba kila mgodi lazima uwe na *plan* watakapokuwa wanataka kufunga, mambo gani watayafanya kwa ajili ya utunzaji wa mazingira na mambo mengine mbalimbali. Kwa hiyo, zile ni hatua ambazo Wizara inazichukua kuhakikisha kwamba inatimiza matakwa ya sheria. Lakini pia ipo migodi mipya mingine ambayo ipo kwenye utaratibu wa kuanzishwa kama Mheshimiwa Waziri alizungumzia *Kabanga Nickel* kule Ngara, kuna Bariadi, kule kuna *Shanta mining* Chunya na Singida pale kuna *Shanta*. Kwa hiyo, ipo migodi mingi ambayo ipo kwenye *process* za mwisho katika utafiti na ipo njiani kuanzishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tatizo la ajira halitajitokeza sana kwa sababu bado kuna gunduzi nyingi zinaendelea kufanyika.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa, Taasisi za Serikali, Majeshi, Polisi, na Hospitali zimekuwa na matatizo makubwa sana kulipa bili za umeme. Huku Serikali na Bunge wakiwaidhinishia hizo bajeti za umeme kwenye bajeti zao: Je, ni lini sera ya kuchukua fedha zote zinazopelekwa kwenye Taasisi zikapelekwa moja kwa moja na Wizara? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri tu kwamba maswali mengine ni magumu. Lakini

hili kwa kweli jibu lake ni jepesi. Ni kweli kama fedha imetengwa kwa ajili ya umeme katika Wizara, inakuwaje ngumu tena isilipwe. Lakini niseme basi kwamba, kila Wizara itaangalia utaratibu wake, ila sisi Wizara ya Nishati na Madini tutaamua kwa zile Taasisi zetu zote kupeleka hela kama moja kwa moja au namna gani, kwa sababu mchakato unavyokwenda huko pengine ndiyo inayopelekea pengine zisilipwe bili, lakini zinaonekana kwenye vitabu vya bajeti.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa muda uliobaki unaniruhusu kutumia *guillotine* ni dakika kumi. Katibu.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipilitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* … Shs.1,812,553,000/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning* … Shs.1,726,723,000/=
Kif. 1004 - *Internal Audit Unit* … Shs. 845,173,000/=
Kif. 1005 - *Legal Services*… … … Shs.4,825,302,000/=
Kif. 1006 - *Government Communication Unit* … … … … … … … … Shs. 1,399,847,000/=
Kif. 1007 - *Procurement Management Unit*... … … … … … … … Shs. 800,614,000/=
Kif. 1008 - *Environment Management Unit* … … … … … … … … Shs. 587,358,000/=
Kif. 1009 - *Management Information System*.. ... ... ... ... ... ... ... .. Shs. 2,483,014,000/=
Kif. 2001 - *Minerals* … … … … … Shs.32,655,213,000/=
Kif. 2002 - *Madini Institute* … … Shs. 0
Kif. 2004 - *Tanzania Diamond Sorting Agency*

*(Tansort) ... ...* Shs. 1,966,898,000/=
Kif. 2005 - *Eastern Zone ...* Shs. 1,141,724,000/=
Kif. 2006 - *Western Zone ...* Shs. 670,899,000/=
Kif. 2007 - *Lake zone ... ...* Shs. 1,122,750,000/=
Kif. 2008 - *Northern Zone ...* Shs. 969,475,000/=
Kif. 2009 - *Southern Zone ...* Shs. 808,695,000/=
Kif. 2010 - *Central Western Zone* Shs. 1,039,656,000/=
Kif. 2011- *Central Zone ... ... ...* Shs. 729,942,000/=
Kif. 2012 - *Southern Western Zone* Shs. 943,308,000/=
Kif. 3001 - *Energy and petroleum* Shs. 45,495,170,000/=

*(vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipilitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**FUNGU 58 - WIZARA YA NISHATI NA MADINI**

Kif. 1003 - *Policy and Planning ...* Shs.700,000,000/=
Kif. 1008 - *Environment Management Unit ... ... ... ... ... ... ...* Shs.871,000,000/=
Kif. 2001 - *Minerals ... ... .... ...* Shs. 66,240,000,000/=
Kif. 2002 - *Madini Institute ... ...* Shs. 3,500,000,000/=
Kif. 2003 - *Research and Laboratory Services ... ... ... ... ... ...* Shs. 1,500,000,000/=
Kif. 3001 - *Energy and Petroleum* Shs. 458,379,861,000/=

*(vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipilitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia Makadirio ya Matumizi ya fedha za Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2012/2013 na kupitia vifungu vyote kwa pamoja na kuvipitisha bila ya mabadiliko yoyote. Hivyo basi, naliomba Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2012/2013 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Kwa hiyo, kwanza kabisa, naomba nichukue nafasi hii kukupongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu Waziri wako na Katibu Mkuu kwamba Wizara mmeichukua siku za karibuni, lakini tunaona kabisa ushujaa ulioko kule.

Kwa hiyo, tunawapongeza wafanyakazi na Wakurugenzi wote walioko chini ya Wizara hiyo kwamba tunawahitaji sana kurudisha uadilifu katika nchi katika eneo linalohusika na sisi tunawaombea kheri tuweze kufanikiwa. Kwa hiyo, sasa nitamwita Mheshimiwa Vita Kawawa.

**MHE. VITA M. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii sasa niwasilishe hoja yangu kuhusu Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge (Kanuni ya 53(2), natumia pia kifungu kidogo cha 55(3)(f).

Mheshimiwa Spika, katika michango iliyokuwa mingi ya Waheshimiwa Wabunge kwenye Wizara ya Nishati na Madini, imeonyesha kwamba, baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini na baadhi ya Wabunge kuwa wamejihusisha na vitendo vya rushwa. Kwa kuwa suala hili na tuhuma hizi ni suala linalohusu Maadili, na suala hili la Maadili linahusu pia haki, kinga na madaraka ya Bunge, kwa kutumia Kanuni ya 53(2) na Kanuni ya 55(3)(f) naomba kutoa hoja kwamba, kwa kuwa tuhuma hizi ni nzito, zinagusa Bunge lako Tukufu, na hivyo kulidhalilisha kwa ujumla wake, na kwa kuwa tuhuma hizo ni nzito na vigumu kuzithibitisha, naomba utumie Mamlaka yako yaliyoainishwa katika Kanuni ya 5(1), hivyo niombe Bunge lako likubali kwa mujibu wa Kanuni ya 5(1) naomba niisome na nanukuu, Mamlaka ya Spika, kifungu cha 5(1):

"Katika kutekeleza majukumu yake yaliyotajwa katika Ibara ya 84 ya Katiba, Spika ataongozwa na Kanuni hizi na pale ambapo Kanuni hazitokuwa na mwongozo, basi Spika atafanya kazi kwa kuzingatia Katiba, Sheria nyingine za nchi, Kanuni nyingine zilizopo, maamuzi ya awali ya Maspika wa Bunge pamoja na mila na desturi za Mabunge mengine yenye utaratibu

wa Kibunge unaofanana na utaratibu wa Bunge la Tanzania.”

Hivyo kwa mamlaka uliyonayo, naomba kwanza ukubali kuivunja na kuiunda upya Kamati ya Nishati na Madini na Kamati nyingine zilizopata kutuhumiwa kuhusiana na rushwa. Pili, naomba jambo hili lililolalamikiwa sana katika hotuba hii ya Nishati na Madini lifanyiwe uchunguzi na Kamati ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge ili ukweli wake ukibainika na hatua ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naona hoja hiyo imeungwa mkono, halafu iko wazi, haina ubishi mwingine. Kwa hiyo, kwa madhumuni hayo na pia ametumia kifungu sahihi cha ile 55(3)(f) ambayo ni Haki na Kinga za Wabunge, hii haitolewi taarifa. Kwa maana hiyo basi, Waheshimiwa Wabunge, sio tu kwa hoja hii, kwa siku zilivyokuwa zinakwenda, tabia ya Waheshimiwa Wabunge kwa maelezo haya imebadilika. Nimeagiza Kamati yangu ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge tutengeneze *code of ethics* na mtu yeyote atakayetuhumiwa katika mazingira hayo, lazima sisi tuchukue hatua inayostahili, tena kubwa. Pia tunataka siyo kwa yule Mbunge anayehusika tu,

tutakwenda na kwa yule mtu anayehusika. Kwa sababu imejitokeza sasa hivi utakuta Mbunge hapa anatoka jasho kweli kweli, anatoa hoja, kumbe anafanya kazi ya mtu fulani.

**WABUNGE FULANI:** Waambie!

**SPIKA:** Ni imani yangu kabisa kwamba Serikali yetu na nchi yetu kwa ujumla inapita katika kipindi cha mpito kama huo mpito wa Bunge, kama hamtakuwa imara na kuwa na msimamo wa kuweza kuisimamia Serikali, kwa ukweli hatutaweza kwenda, na matumaini ya wananchi ni wapi kama siyo Bunge? Mimi nasema kwa dhati kabisa, kitendo hiki kwa kweli hakikubaliki ndani ya Bunge hili. (*Makofi/Kicheko)*

Hatuwezi kuisimamia Serikali huku tunapokeapokea, mnaisimamiaje Serikali kwa mtindo huu? Kwa hiyo, naamini kabisa Wabunge mkikaa vizuri na tukafanya kazi yetu vizuri, mabadiliko makubwa katika uendeshaji wa Serikali yatatokea. Lakini wenzetu mara wanakwenda huku, mara wajipendekeze, mara waombe hiki, mara waombe hiki, hatuwezi kwenda hivyo. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, kwa maamuzi haya, kwanza kwa kutumia Kanuni hiyo ya 53, nalipeleka suala hili kwenye Kamati ya Haki, Kinga na Maadili ya Bunge ili walifanyie uchunguzi na kuleta taarifa hapa. Sasa hao mliokuwa mnawataka watajwe, sasa hiyo Kamati itafanya kazi hiyo. *(Makofi/Kicheko)*

Pili, kwa kutumia mamlaka niliyopewa na Kanuni ya 113(3) na baada ya Wabunge kuunga mkono hoja

ya Mheshimiwa Vita Kawawa, naridhia ombi hilo. Hivyo nitaivunja Kamati hiyo na nyingine ambazo zitaonekana zina tabia hiyo.

**MBUNGE FULANI:** Safi! Wakae bila Kamati hao. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa, niwashukuru sana kwa kazi mliyoifanya sana wiki hii na kwa ushujaa ambao mmeufanya kabisa katika kipindi hiki na kwa hiyo, natoa tangazo pia kwamba kuna mchezo wa Kirafiki na *NMB* wanaohusika mwende mkacheze kwa ari mpya na nguvu mpya mtuletee ushindi kama kawaida na ile Klabu ya Kulenga shabaha kesho waende. Vinginevyo, nataka nawatakia *week-end* njema, naahirisha Kikao cha Bunge mpaka siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi.

*(Saa 8.33 mchana Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 30 Julai, 2012 Saa Tatu Asubuhi)*